IDARA YA FAT-WA

Wizara ya Awqaf na
Mambo ya Kiislam

# MWONGOZO WENYE FAIDA WA SHERIA ZA KIISLAMU KWA MUISLAMU MPYA

*KIMETUNGWA NA*

*KITENGO CHA UTAFITI WA KISAYANSI,*

*IDARA YA FAT-WA.*

WIZARA YA AWQAF NA
MAMBO YA KIILAM

IDARA YA FAT-WA

# MWONGOZO WENYE FAIDA
# WA
# SHERIA ZA KIISLAMU
# KWA MUISLAMU MPYA

KIMETUNGWA NA

*KITENGO CHA UTAFITI WA KISAYANSI,*

*IDARA YA FAT-WA.*

## MALENGO YETU

- Kubainisha hukumu za kisheria kwa kila jambo linalojitokeza kwa Muislamu na matukio mbali mbali yakiwemo matukio na masuala mapya.
- Kueneza utamaduni wa msingi wa fiqhi baina ya wanajamii.
- Kueneza msimamo wa wastani baina ya wanajamii kwa kuchukua kadhia mbali mbali za Kiislamu kwa namna inayo-kubaliana na roho ya Uislamu na utu-kufu wake.
- Kuhuisha urithi wetu wa Kisheria (Fiq-hi) uliosheheni mazuri na uliojengeka juu ya misingi tofauti ya Ijtihad juu ya mtazamo katika mambo mbali mbali.
- Kuwapa Maimamu na Makhatwibu (Wahutubu Misikitini) maarifa ya kina katika Fiqhi yatakayowawezesha kujibu maswali ya watu.
- Kuishirikisha jamii Kifiq-hi katika misimu na minasaba mbali mbali kwa kutoa vipeperushi na nyenzo nyingine ambazo zinazungumzia minasaba hii kwa mta-zamo wa Kisharia.
- Kutoa vipeperushi katika kadhia ambazo zinajitokeza ulimwenguni, ambazo ni muhimu na zinaishughulisha jamii na kuna haja ya kuwa na uwelewa na kujua hukumu za Kisharia katika kadhia hizo.
- Kuwajali Waislamu wapya kwa kut-angaza Uislamu wao na kuwapa vitabu vyenye manufaa kwa lugha zao.

**IDARA YA FAT-WA**

**HAKI ZA UCHAPAJI ZIMEHIFADHIWA**

**CHAPA YA KWANZA**

**2017/1438**

**Tovuti ya Idara**

**www.islam.gov.kw/eftaa**

**: إدارة الإفتاء**

**: @efta_kw**

**: eftakw**

Kwa mawasiliano: Wizara ya Wakfu na Mambo ya Kiislamu, Kuwait.
P.O.Box 13, Safat 13011, Nukushi: 22418723, Baruapepe: eftaa@islam.gov.kw
Mawasilano yote yatumwe kwa: Mkurugenzi wa Idara ya Fat-wa

بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

## TAMKO LA IDARA

Shukrani zote ni kwa Mola wa viumbe, aliyeteremsha ukumbusho wenye hekima. Nakiri kwamba hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Allah tu asiyekuwa na mshirika, mwenye kusema katika kitabu chake kitukufu kwamba:

﴿أَفَمَن شَرَحَ ٱللَّهُ صَدۡرَهُۥ لِلۡإِسۡلَٰمِ فَهُوَ عَلَىٰ نُورٖ مِّن رَّبِّهِۦۚ فَوَيۡلٞ لِّلۡقَٰسِيَةِ قُلُوبُهُم مِّن ذِكۡرِ ٱللَّهِۚ أُوْلَٰٓئِكَ فِي ضَلَٰلٖ مُّبِينٍ﴾ الزمر: ٢٢

"***Je, mtu ambaye Allah amemfungulia kifua chake kuukubali Uislamu, akawa yuko katika nuru itokayo kwa Mola wake (ni sawa na mwenye moyo mgumu)? Basi, adhabu kali itawathibitikia wale wenye nyoyo ngumu. Hao wamo kwenye upotovu ulio wazi".*** Sura Azzumar: 22. Sala na salamu zimfikie Kiongozi, Muaminifu aliyesema kuwa: ***"Nimetumwa kwa dini iliyo safi, nyepesi".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad. Maana ni kwamba, nimetumwa kwa dini iliyosimama katika Tawhiid (kumpwekesha Allah), rehema na wepesi. Pia Mtume amesema kuwa: ***"Uislamu unafuta yaliyopita".*** Ameipokea Hadithi hii Muslim. Maana ni kwamba, Uislamu unafuta dhambi zilizofanywa kabla ya Uislamu.

Baada ya hayo:

Idara ya Fat-wa katika nchi ya Kuwait inayo furaha kuwapongeza na kuwatakia kheri wale walioingia katika Uislamu, bustani iliyonawiri ambayo bila shaka watapata matunda yake ndani ya nafsi zao, matunda ambayo ni kukunjuka kifua, ufahamu mzuri na kuondokana na itikadi tata katika nafsi zao. Pia watapata raha ya kweli katika

maisha yao. Raha hii haina maana kwamba hakutakuwepo baadhi ya vikwazo katika maisha au matatizo yanayokera na ambayo ni utakaso utokao kwa Allah kwa waja wake kwa kuthibitisha kauli yake isemayo kuwa:

﴿الٓمٓ ۝١ أَحَسِبَ ٱلنَّاسُ أَن يُتۡرَكُوٓاْ أَن يَقُولُوٓاْ ءَامَنَّا وَهُمۡ لَا يُفۡتَنُونَ﴾ العنكبوت: ١ – ٢

***"Alif laam Miim. Je, watu wanadhani wataachwa (wasitiwe katika misukosuko) kwa kuwa wanasema: Tumeamini? Basi ndio wasijaribiwe?".*** Sura Ankabut: 2-3. Lakini sisi tuna yakini kwamba, wewe ndiye mnufaikaji wa kweli katika uchaguzi huu sahihi, Allah akipenda. Hivyo tunakupa zawadi ya kitabu hiki kinachoitwa ***"Mwongozo Wenye Faida Wa Sheria Za Kiislamu Kwa Muislamu Mpya"*** kilichoandaliwa na kundi la watafiti katika Idara ya Fat-wa linaloundwa na:

1- Shekh Turkiy Issa Al-mutiiriy (Mwenyekiti).

2- Dr. Ayman Mohammad Al-omar (Mjumbe)

3- Shekh Nourdin Abdulsalam Musaiy (Mjumbe)

4- Shekh Ahmad Abdulwahab Salim (Mjumbe)

Tunamuomba Allah, kwa kitabu hiki, anawirishe njia yenu ya kuelekea kwenye pepo ya kudumu. Hakika, hiki ni kitabu kizuri kilichosheheni masuala mbalimbali ambayo Muislamu analazimika kuyajua katika dini.

**Tunamuomba Allah atuwezeshe na kutuongoza.**

**Idara ya Fat-wa**.

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Shukurani zote ni za Allah Mola wa viumbe, na nakiri kwamba hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Allah pekee, asiye na mshirika, kipenzi cha watu wema. Na nakiri kwamba Muhammad ni mja wake na ni Mtume wake. Tunaomba rehema na amani zimfikie yeye, Familia yake na Swahaba wake wote.

Ama baada ya haya:

Hakika, neema za Allah kwa mwanadamu ni nyingi na kubwa. Hazihesabiki na hazidhibitiki. Allah anasema kuwa:

﴿وَإِن تَعُدُّوا۟ نِعْمَةَ ٱللَّهِ لَا تُحْصُوهَآ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾ النحل: ١٨

***“Na mkihesabu neema za Allah hamtaweza kuzidhibiti. Hakika, Allah ni mwingi wa kusamehe (na) mwingi wa kurehemu”.*** Sura Annahl:18.

Neema kubwa na adhimu kabisa miongoni mwa neema za Allah ni kumuwezesha mja kufuata njia yake iliyonyooka, dini yake ya haki ambayo ameiridhia na kuwaamrisha watu kuifuata. Allah amesema kuwa:

﴿ٱلْيَوْمَ يَئِسَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ مِن دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَٱخْشَوْنِ ۚ ٱلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِى
وَرَضِيتُ لَكُمُ ٱلْإِسْلَٰمَ دِينًا﴾ المائدة: ٣

***“Leo nimekukamilishieni dini yenu na kukutimizieni neema yangu, na nimeridhia kwenu Uislamu uwe ndio dini yenu”.*** Sura Almaida: 3.

Hakika, hiyo ni neema kubwa na zawadi kubwa ambayo mwanadamu ameneemeshwa. Kwa neema hiyo, inapatikana raha na wema duniani na inapatikana nusura na kufaulu kukubwa Akhera. Allah amesesema kuwa:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ كَانَتۡ لَهُمۡ جَنَّٰتُ ٱلۡفِرۡدَوۡسِ نُزُلًا ١٠٧ خَٰلِدِينَ فِيهَا لَا يَبۡغُونَ عَنۡهَا حِوَلٗا﴾

الكهف: ١٠٧ – ١٠٨

"***Kwa yakini, walioamini na kufanya vitendo vizuri makazi yao yatakuwa pepo za Firdausi wakikaa milele humo. Hawatataka kuondoka katika makazi hayo".*** Sura Al- kahf: 107-108.

Kwa kuwa Uislamu ndio dini ya Allah ambayo hakuna dini nyingine inayokubalika zaidi ya hiyo, na hakuna ukweli usiokuwa huo, dini ya maumbile sahihi ambayo Allah amewaumbia wanadamu kwa maumbile hayo, dini ya Mitume na Manabii wote, dini ambayo imesimama juu ya msingi wa Tawhiid (kumpwekesha Allah), na kufanya ibada kwa ajili ya Allah tu, kutii na kufuata sheria zake, Allah Mtukufu hatakubali kwa watu Akhera dini isiyokuwa hiyo. Allah amesema kuwa:

﴿وَمَن يَبۡتَغِ غَيۡرَ ٱلۡإِسۡلَٰمِ دِينٗا فَلَن يُقۡبَلَ مِنۡهُ وَهُوَ فِي ٱلۡأٓخِرَةِ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ﴾ آل عمران: ٨٥

***"Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu haitakubaliwa kwake, Naye Akhera atakuwa katika wenye hasara".*** Sura Al-imraan: 85.

Uislamu ndio njia pekee ya wema na ufaulu wa duniani na Akhera.

Mtume (s.a.w.) alifanya bidii kubwa ya kuwalingania (kuwahubiria) watu wote kuingia katika Uislamu na kuwaongoza katika kumpwekesha Mola wa mbingu na ardhi. Hakuacha njia yoyote inayokubalika kisheria katika kuwalingania watu na kuwaongoza waingie katika Uislamu isipokuwa kwamba aliifuata. Yote hayo ni kwa kuonesha bidii ya kutaka wema wao na kutaraji mafanikio yao, kiasi kwamba Allah alimwambia kuwa:

﴿لَعَلَّكَ بَٰخِعٞ نَّفۡسَكَ أَلَّا يَكُونُواْ مُؤۡمِنِينَ﴾ الشعراء: ٣

***"Huenda (wewe Nabii Muhammad) ukaiangamiza nafsi yako kwa sababu hawawi Waislamu".*** Sura Ash-shuaraa: 3. Maana ni kwamba, huenda ukaidhuru nafsi yako kutokana na kusononeka na kukereka kwa sababu ya kutoamini kwao na kuto ongoka kwao.

Kama ambavyo bidii ya Mtume (s.a.w.) ilikuwa kubwa katika kulingania watu wawe Waislamu, furaha yake na faraja yake pia ilikuwa kubwa kwa wale wanaoingia katika Uislamu. Mtume alikuwa ni mtu mwenye kufahamu sana utukufu na hadhi ya neema hii, pia wema na neema za kudumu zinazopatikana kwa sababu yake. Allah amesema kweli alipomsifu Mtume wake kuwa:

﴿لَقَدْ جَآءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُم بِٱلْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ﴾ التوبة: ١٢٨

***"Kwa yakini kabisa, amekufikieni Mtume aliye jinsi moja na nyinyi. Yanamuhuzunisha yanayokutaabisheni. Anakuhangaikieni. Kwa walioamini ni mpole, mwenye huruma***". Sura Attawba: 128.

Kwa kuwa na wewe Muislamu mpya ni miongoni mwa waliopata neema hii kubwa ya Allah, hakika nawe ni mwenye mahitajio makubwa ya kujua sheria za dini yako, mafundisho yake na misingi yake kwa namna ambayo itakuhakikishia usalama wa itikiadi yako, usahihi wa utekelezaji wa ibada zako na misingi ya kuishi na jamii inayokuzunguka, hasa wale watu ambao bado sio Waislamu. Kwa sababu hii, tumekukusanyia sheria na masuala muhimu sana ambayo unahitaji kuyajua katika kitabu kimoja tulichokiita:

***Mwongozo Wenye Faida Wa Sheria Za Kiislamu Kwa Muislamu Mpya.***

Tunataraji kwa Allah kuwa ametuwafikisha katika kuchagua maudhui zake vyema na kuhakiki masuala yake.

Tunapenda kutanabahisha hapa kwamba, dini ya Kiislamu ni dini ya Allah na sheria ya mbinguni, imehifadhiwa dhidi ya makosa na upotoshaji. Ama wanadamu bado wanaendelea kujitahidi katika elimu na kufahamu. Hivyo, wengine wanakosea na wengine wanapatia. Wako hivyo mpaka mwisho wa dunia. Hizi ni jitihada zetu. Pale ambapo tumepatia hiyo inatokana na Allah, na pale ambapo tumekosea au kuteleza hiyo inatokana na nafsi zetu na shetani; ama Allah na Mtume wake hawahusiki na makosa au kuteleza huko.

## ❖ UTARATIBU WETU KWENYE KITABU HIKI

Kazi kwenye kitabu hiki imefuata misingi ifuatayo:-

(1) Imefanyika bidii ya kukitayarisha kitabu hiki kwa silabi rahisi na lugha nyepesi ambayo ni rahisi kwa Muislamu mpya kuifahamu, kuielewa na hatimae kufuata na kutekeleza.

(2) Kitabu kimefungika katika kutaja masuala muhimu ambayo yatampa Muislamu mpya mwanga wa kufahamu masuala ambayo yanamlazimu katika itikadi ya Kiislamu, pia sheria za ibada za lazima za vitendo ambazo hatakiwi kuziacha.

(3) Tumeegemea kwenye madhehebu ya Jumhuur ya Maulamaa (Kundi kubwa la wanazuoni) katika masuala yote ya Kifiq-hi pamoja

na kuzingatia Fat-wa zilizotolewa na Idara ya Fat-wa ya Wizara ya Wakfu na Mambo ya Kiislamu na kamati zake. Pia tumejihimu kutaja baadhi ya hoja za Qur'ani na Hadithi sahihi bila ya kurefusha na kuchepuka, kwa lengo la kuchunga wepesi na ufupishaji kwa kuangalia hali ya Muislamu mpya.

(4) Mada za kitabu hiki zimegawanywa katika milango minne.

- **Mlango wa mwanzo**: Umeitambulisha kiujumla dini ya Kiislamu.
- **Mlango wa pili**: Umeelezea masuala muhimu ya itikadi na Tawhidi.
- **Mlango wa tatu**: Umefafanua sheria nyingi za Kifiqhi na ibada za wajibu ambazo Muisalmu analazimika kuzijua.
- **Mlango wa nne na wa mwisho**: Umebainisha sheria na mahusiano ya kijamii na miamala ya kifedha ya Muislamu.

Mwisho, hatuna budi kuelekea kwa Allah na kumuomba atukubalie kazi yetu hii, aifanye iwe njema na halisi kwa ajili yake yeye, anufaishe kwayo na abariki kwayo. Yeye kwa kila jambo zuri ni mdhamini, naye ndiye mtegemewa bora, naye ndiye anayetutosha. Tunamuomba amfikishe rehema na amani na ambariki Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad, Familia yake na Swahaba wake wote.

**Kitengo cha Utafiti Wa Kisayansi**

**Katika Idara Ya Fat-wa**

# KITABU KILICHOPO MIKONONI MWETU

Miongoni mwa sifa kubwa ya dini ya Kiislamu ni kwamba, ni dini nyepesi na rahisi kwa kila mtu, kwa sababu mahusiano ya mwanadamu na Mola wake ni mahusiano ya moja kwa moja yasiohitaji kuwepo mkaa kati. Popote mwanadamu alipo anaweza kuwasiliana na Mola na Muumba wake na kumtangazia hamu yake ya kuingia katika Uislamu; akiwa nyumbani kwake, kazini kwake au hata bustanini kwake. Allah amesema kuwa:

﴿وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ﴾ البقرة: ١٨٦

***"Na waja wangu watakapokuuliza kuhusu mimi, (waambie kuwa) mimi niko karibu. Najibu maombi ya muombaji anaponiomba. Kwa hiyo, waniitikie na waniamini ili wapate kuongoka ".*** Sura Albaqara: 186.

Ewe ndugu yangu Muislamu mpya, uliyependelea kuingia katika Uislamu, hakika umeona na umegundua kwamba kuingia katika Uislamu hakukulazimu kuwepo kwa mtu wa kati wala kupata ridhaa yake juu ya hilo. Kubwa ulilolifanya ni kutikisa midomo yako na ulimi wako ukatamka Shahada (Ash-hadu Allaa Ilaaha Illallaah, Wa-ash-hadu Anna Muhammadan Rasuulu –llah = Ninakiri kuwa hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Allah tu na ninakiri kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah). Umetamka hayo kwa kuyakubali na kuyasadikisha maana yaliyomo ndani ya neno hili. Maana hayo ni:

**a.** Kukubali utumishi kwa Allah pekee, asiye na mshirika wala

mwenza wala mfano. Pia kuwa na unyenyekevu na kufuata maamrisho yake na kuacha aliyokataza.

**b.** Kukubali kwamba Muhammad ni mja wa Allah na Mtume wake. Ni Nabii na Mtume wa mwisho. Allah amemtuma kwa watu wote. Ni wajibu kumfuata katika kila alililoliamrisha na kuacha kila alililolikataza, na kusadikisha kila aliloeleza kwamba ni la kweli.

Maana hii ikijengeka ndani ya moyo wako, na ukatamka shahada mbili, utakuwa Muislamu wa kweli, na una haki kama walizo nazo Waislamu wengine, na utakuwa na wajibu kama walio nao. Yote hayo tutayabainisha katika kurasa za kitabu hiki, ili umuabudu Allah ukiwa na mwanga, na ujitahidi kufikia daraja za juu za imani.

Tunamuomba Allah akubariki katika Uislamu wako na imani yako, auimarishe moyo wako katika uongofu, akupe tawfiki (uwezeshaji wa kutenda) na usahihi katika matendo yako na ibada zako. Hakika, Allah yu karibu, mwenye kusikia na mwenye kujibu.

WIZARA YA AWQAF NA
MAMBO YA KIILAM

IDARA YA FAT-WA

# MWONGOZO WENYE FAIDA

# WA

# SHERIA ZA KIISLAMU

# KWA MUISLAMU MPYA

**KIMETUNGWA NA**

***KITENGO CHA UTAFITI WA KISAYANSI,***

***IDARA YA FAT-WA.***

# MLANGO WA KWANZA

## HAKIKA YA DINI
## KWA ALLAH NI UISLAMU

## HAKIKA YA DINI KWA ALLAH NI UISLAMU

Allah (s.w.) amemtuma Mtume wake Muhammad (s.a.w.) kwa dini ambayo amehitimisha kwayo dini zote, ameifanya kuwa ndio dini inayozitawala dini hizo na yenye kufuta sheria zake. Amechukua dhamana ya kuilinda na kuihifadhi isipotoshwe au kubadilishwa na kuisifu kuwa ni njia iliyonyooka ambayo mwenye kuifuata ataokoka duniani na Akhera. Yeyote atakayeiacha na kufuata njia nyingine atapotea na kuangamia, kwa sababu mtu kuikataa njia hiyo ni kutoka katika maumbile yake ambayo aliyoumbwa na Allah. Allah mtukufu amesema kuwa:

﴿ فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا ۚ فِطْرَتَ ٱللَّهِ ٱلَّتِى فَطَرَ ٱلنَّاسَ عَلَيْهَا ۚ لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ ٱللَّهِ ۚ ذَٰلِكَ ٱلدِّينُ ٱلْقَيِّمُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴾ الروم: ٣٠

***"Basi elekeza uso wako katika dini (sahihi) ukiacha dini potovu. (Hilo) Ndio umbile Allah alilowaumbia watu; (yaani dini ya Kiislamu inayowafikiana barabara na umbo la binadamu). Hakuna mabadiliko katika kuumba kwa Allah. Hiyo ndio dini ya sawa, na lakini watu wengi hawajui".*** Sura Ar-ruum: 30.

### KWANZA: UISLAMU NI DINI YA MAUMBILE

Kwa hakika Allah ameiumba nafsi ya mwanadamu katika hali ya kuelekea katika kila lenye kheri na manufaa, na kulikimbia kila lenye shari, uharibifu na madhara. Wewe utamuona mwanadamu, kwa maumbile yake, anapenda chakula na kinywaji kizuri, chenye faida na kukikataa chakula au kinywaji hicho kama ni kibaya, chenye madhara. Utamuona anapenda kufanya urafiki na mtu mwenye tabia nzuri na sifa njema, na kuepukana na mtu mwenye hulka mbaya na tabia chafu. Yeye humpenda, kumuheshimu na kumtukuza mtu mwenye sifa ya tabia njema na, kwa sababu hiyo, humpa kila aina ya heshima, hadhi na taadhima wakati ambapo hampi heshima, hadhi na taadhima hii mtu mwenye sifa ya kasoro, uzembe na udhaifu.

Haya ndio maumbile ambayo Allah ameyaumba katika nafsi ya mwanadamu na moyo wake. Amezifanya nyoyo kuwa tayari kukubali haki kama ambavyo ameyaumba macho kuwa na uwezo wa kuona na kuyaumba masikio kuwa na uwezo wa kusikia. Madamu nyoyo hizi zipo katika hali ya kukubali haki, zinaigundua haki hiyo na kuifuata na zinapobadilika kwa sababu ya mapenzi ya nafsi na matamanio zinaiacha haki na kuifuata batili. Imenukuliwa kwa Iyaadh, Allah amuwiye radhi, kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***“Allah anasema kwamba: Hakika, nimewaumba waja wangu wakiwa katika hali ya maumbile safi ya kukubali haki. Wakapitiwa na mashetani na kuwahalalishia yale niliyowaharamishia na wakawaamrisha wanishirikishe na vitu ambavyo sikuviteremshia hoja.”*** Hadithi hii imesimuliwa na Musilim.

Mtume (s.a.w.) ametupa habari kwamba, mwanadamu huzaliwa akiwa katika maumbile halisi ambayo Allah kamuumba nayo. Habadiliki mpaka apate viathiri kutoka nje vinavyobadilisha maumbile haya. Kapokea Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, kwamba Mtume amesema kuwa: ***“Kila mtoto anazaliwa akiwa katika maumbile safi. Wazazi wake ndio wanaomfanya awe Myahudi au Mkristo au Mmajusi, kama mnyama anavyozaa mnyama akatimia maumbo yake. Je, umemuona kukatwa popote? Kisha akasema Abuhuraira kwamba: Someni (aya hii) mkitaka: Ndio umbile Allah alilowaumbia watu. Hakuna mabadiliko katika maumbile ya Allah. Sura Arrum: 30".*** Hadithi hii imesimuliwa na Bukhari na Muslim.

Mtume (s.a.w.) anatueleza kuwa maumbile safi ni kufuata dini ya Kiislamu na sio kufuata dini nyingine zilizobadilishwa au mila ambazo Allah hajaziamrisha wala hajazifanya kuwa sheria. Hivi huoni kwamba, Mtume katika ile Hadithi hakusema kuwa: ***"Wazazi wake ndio wanaomfanya awe Myahudi au Mkristo au Mmajusi au Muislamu"***? ili atuoneshe ushahidi kwamba Uislamu ni dini ya maumbile halisi. Miongoni mwa yanayotia nguvu kwamba Uislamu ni dini ya maumbile safi ni nukuu nyingine ya Hadithi iliyotangulia inayosema wazi kwamba: ***"Kila mtoto huzaliwa katika mila hii mpaka ulimi wake umbainishe".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Mwenye kujifunza taaluma za Kiislamu atagundua kuwa Uislamu ndio haki inayomlazimu kuifuata, kwa sababu mafunzo yake yanachunga maumbile salama na kuyaenzi wala hayakinzani. Mafunzo ya Uislamu:

**1.** Yanaamrisha kumuabudu Allah pekee asiyekuwa na mshirika, Muumba ulimwengu wote, ufalme wote uko mkononi mwake, na yeye anaweza kila kitu. Muktadha wa maumbile salama ni kwamba, mwenye sifa za ukamilifu ndiye anayestahiki heshima na taadhima seuze Yule ambaye ukamilifu wake hauna ukomo wala mipaka!

**2.** Mafunzo ya sharia yamehalalisha mambo mazuri na kuharamisha mabaya, kwa sababu maumbile salama yanapenda kila kitu kizuri na kukikataa kila kibaya.

**3.** Mafunzo ya Uislamu yamehimiza maadili mema na tabia nzuri na kukataza maadili machafu na tabia mbaya, kwa sababu nafsi zilizo sawa zinapenda mema na zinakataa mabaya. Imepokewa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa, mjumbe wa Allah alisema kwamba: ***"Kisha nikaletewa vyombo viwili. Kimoja kina maziwa na kingine kina ulevi. (Malaika) Akasema: Kunywa unachotaka katika hivi vinywaji viwili. Mimi nikachukua maziwa nikayanywa. Nikaambiwa: Umechukua maumbile halisi. Kama ungechukua ulevi, umma wako ungepotoka".*** Hadithi hii imesimuliwa na Bukhari na Muslim.

## PILI: UISLAMU NI NINI?

Kila dini hapa ulimwenguni chanzo chake huhusishwa kwa mtu maalumu au kwa taifa fulani. Kwa mfano, dini ya Uyahudi hunasibishwa kwa Yuda na dini ya Kikristo hunasibishwa kwa Yesu Kristo na dini ya Budha hunasibishwa kwa Budha.

Ama Uislamu chanzo chake kinahusishwa na sifa maalumu ambayo imo ndani ya jina lake. Sifa hii ni kujisalimisha, kunyenyekea, kutekeleza na kufuata amri za mwenye kuleta dini hii ambaye ni Allah Mtukufu. Allah ameiita dini yake kuwa ni Uislamu, kwa sababu Muislamu ni lazima ajisalimishe kwake kwa kumpwekesha, kumuamini, kutekeleza amri zake, kuacha makatazo yake na kumtii bila ya ukaidi au kupinga.

Kwa maana hiyo, inaonekana wazi kuwa neno Uislamu linaonesha kwamba dini hii haikubuniwa na mtu yeyote wala hailihusu taifa maalumu. Makusudio yake ni watu wote wawe katika sifa yake inayoitafautisha na dini nyingine.

Uislamu kwa tafsiri yake maalumu kwamba ni dini aliyokuja nayo Muhammad haina maana kwamba inatika katika sifa hii ambayo inabeba jina la Uislamu. Mahubiri yake yamesimama katika kuwatoa watu katika utumwa wa kuwatumikia viumbe, mapenzi ya nafsi na matamanio, na kuwapeleka kwenye utumwa halisi wa kumtumikia Allah Mtukufu, kumnyenyekea, kumfuata na kumtii katika kila analoliamrisha na kuacha kila analolikataza.

Kwa hiyo, Uislamu ni kujisalimisha kwa Allah kwa kumpwekesha na kumfuata kwa utiifu mpaka yatulie mapenzi yake katika moyo wa Muislamu. Uislamu ni kuusafisha moyo usiwe na shirki na ukafiri kwa namna na maana zake zote mpaka uchafu wake utoke katika moyo wa Muislamu. Mtume (s.w.a.) ametuelekeza hayo pale aliposema kuwa: "***Na achukie kurejea katika ukafiri kama anavochukia kutumbukizwa katika moto".*** Hadithi hii Imesimuliwa na Bukhari na Muslim.

## TATU: UISLAMU NI DINI YA MITUME WOTE

Kila mtu hapa duniani inamlazimu ajisalimishe kwa Allah Mtukufu, amnyenyekee, atii amri zake na ajiepushe na makatazo yake bila ya kujali utafauti wa zama au mahali. Lakini watu walipobadilisha dini zao na wakafuata mapenzi ya nafsi zao na matamanio waliikosa njia ya haki na wakafuata batili. Hapo Allah Mtukufu alipeleka wajumbe wawaongoze watu katika njia ya uongofu, kufuata haki na kuwarejesha katika Tauhidi na kumuabudu yeye. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَا مِن قَبۡلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِيٓ إِلَيۡهِ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدُونِ﴾ الأنبياء: ٢٥

***"Na hatukumtuma Mtume yeyote kabla yako ila tulimfunulia ya kwamba: Hakuna anayestahiki kuabudiwa ila mimi. Basi, niabuduni".*** Sura Al-Anbiyaa: 25. Atakaye wakubalia Mitume anastahiki kupewa sifa ya kuitwa Muislamu, sifa ambayo Allah amewapa waja wake

wanaompwekesha. Allah Mtukufu kasema kuwa:

﴿هُوَ سَمَّىٰكُمُ ٱلۡمُسۡلِمِينَ مِن قَبۡلُ﴾ الحج: ٧٨

***"Yeye (Allah) alikuiteni Waislamu tangu (katika vitabu vya zamani huko".*** Sura Al-Hajj: 78.

Qur-an tukufu imetupa habari kuwa mahubiri (Daawa) ya Mitume wote yalikuwa ni mahubiri ya kuwaita watu kuingia katika Uislamu na kwamba mwenye kuwafuata Mitume anakuwa miongoni mwa Waislamu. Qur-an imesema kuhusu Mtume Nuhu kwamba:

﴿وَأُمِرۡتُ أَنۡ أَكُونَ مِنَ ٱلۡمُسۡلِمِينَ﴾ يونس: ٧٢

***"Na nimeamrishwa niwe miongoni mwa Waisalamu".*** Sura Yunus: 72.

Na Qur'ani imesema kuhusu Nabii Ibrahim na Ismail kuwa:

﴿رَبَّنَا وَٱجۡعَلۡنَا مُسۡلِمَيۡنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَآ أُمَّةٗ مُّسۡلِمَةٗ لَّكَ﴾ البقرة: ١٢٨

***"Ewe Mola wetu, tufanye tuwe Waislamu (wanyenyekevu) kwako na miongoni mwa kizazi chetu (pia ufanye) umma wa Kiislamu (mnyenyekevu) kwako".*** Sura Albaqara: 128.

Na Qur'ani imesema pia katika wasia wa Nabii Yakubu kwa watoto wake kwamba:

﴿أَمۡ كُنتُمۡ شُهَدَآءَ إِذۡ حَضَرَ يَعۡقُوبَ ٱلۡمَوۡتُ إِذۡ قَالَ لِبَنِيهِ مَا تَعۡبُدُونَ مِنۢ بَعۡدِيۖ قَالُواْ نَعۡبُدُ إِلَٰهَكَ وَإِلَٰهَ ءَابَآئِكَ إِبۡرَٰهِـۧمَ وَإِسۡمَٰعِيلَ وَإِسۡحَٰقَ إِلَٰهٗا وَٰحِدٗا وَنَحۡنُ لَهُۥ مُسۡلِمُونَ﴾ البقرة: ١٣٣

***"Je, (Nyinyi Wayahudi na Wakristo) mlikuwepo yalipomfika Yakubu mauti pale alipowaambia wanawe kuwa: Je, mtaabudu nini baada yangu? Wakasema: Tutamuabudu Mungu wako na Mungu wa wazazi wako Ibrahim na Ismail na Is-haka Mungu mmoja tu. Na sisi tumesilimu (tumenyenyekea) kwake".*** Sura Albaqara: 133.

Na Qur-an pia imesema kuhusu Nabii Mussa kwamba:

﴿إِن كُنتُمۡ ءَامَنتُم بِٱللَّهِ فَعَلَيۡهِ تَوَكَّلُوٓاْ إِن كُنتُم مُّسۡلِمِينَ﴾ يونس: ٨٤

***"Ikiwa nyinyi mmemuamini Allah basi mtegemeeni yeye ikiwa nyinyi ni Waislamu (wa kweli)".*** Sura Yunus: 84.

Na Qur'ani imesema kuhusu Nabii Yussuf kwamba:

﴿تَوَفَّنِي مُسْلِمًا وَأَلْحِقْنِي بِالصَّالِحِينَ﴾ يوسف: ١٠١

***"Nifishe nikiwa Muislamu na nichanganyishe na watendao mema"***. Sura Yusuf: 101. Pia Qur-an imesema kuhusu Nabii Suleiman kwamba:

﴿أَلَّا تَعْلُوا عَلَيَّ وَأْتُونِي مُسْلِمِينَ﴾ النمل: ٣١

***"Msinifanyie jeuri. Na fikeni kwangu hali ya kuwa mmeshakuwa Waislamu". Sura Annamli: 31***. Na Qur'ani imesema kuhusu Nabii Lut kuwa:

﴿فَمَا وَجَدْنَا فِيهَا غَيْرَ بَيْتٍ مِّنَ الْمُسْلِمِينَ﴾ الذاريات: ٣٦

***"Hatukupata humo ila tu nyumba moja yenye Waislamu".*** Sura Adh-haariyat: 36. Na ikasema pia kuhusu wanafunzi wa Nabii Issa kwamba:

﴿فَلَمَّا أَحَسَّ عِيسَىٰ مِنْهُمُ الْكُفْرَ قَالَ مَنْ أَنصَارِي إِلَى اللَّهِ ۖ قَالَ الْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنصَارُ اللَّهِ آمَنَّا
بِاللَّهِ وَاشْهَدْ بِأَنَّا مُسْلِمُونَ﴾ آل عمران: ٥٢

***"Issa alipohisi ukaidi wao (umeshitadi) alisema: Nani watakuwa wasaidizi wangu kuendea (katika kuitangaza dini ya Allah? Wanafunzi (wake) wakasema: Sisi ni wasaidizi wa (kutangaza dini ya) Allah. Tumemuamini Allah na shuhudia kwamba sisi ni Waislamu (tumejisalimisha kwa Allah)".*** Sura Al-Imran: 52.

Kwa hivyo mahubiri ya Mitume wote ni mahubiri mamoja yanayowaita watu kwenda katika Uislamu, kwa sababu Mungu wao ni mmoja na dini yao ni moja, hata kama sharia zitatofautiana kama tutakavyokuja kueleza baadae. Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Manabii (wote) ni ndugu wa matumbo mbali mbali. Mama zao tofauti na dini yao ni moja".*** Hadithi hii imesimuliwa na Bukhari na Muslim. Ndugu wa matumbo tofauti ni ndugu wa baba mmoja na mama mbali mbali.

Kwa hiyo, dini ya Allah aliyokuja nayo kila Mtume ni Uislamu. Kasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلْإِسْلَٰمُ﴾ آل عمران: ١٩

***"Bila ya shaka, dini ya (haki) mbele ya Allah ni Uislamu".*** Sura Al-Imran: 19. Na Allah hakubali kwa viumbe dini yoyote isipokuwa Uislamu, kama alivyosema kuwa:

﴿وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ ٱلْإِسْلَٰمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِى ٱلْءَاخِرَةِ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ﴾ آل عمران: ٨٥

***"Na atakayetaka dini isiyokuwa Uislamu basi haitakubaliwa kwake. Na yeye Akhera atakuwa katika wenye hasara (kubwa kabisa).*** Sura Al-Imran: 85.

## NNE: NGUZO ZA UISLAMU

Uislamu ni jengo kubwa lilokusanya pande mbali mbali za maisha ya mwanadamu. Ni lazima jengo hili liwe na misingi na nguzo imara inayolibeba. Misingi na nguzo hizo amezibainisha Mtume (s.a.w.) katika kauli yake isemayo kuwa: ***"Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano. Kukubali na kukiri kuwa hapana menye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah tu na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allah, na kusimamisha sala, na kutoa zaka na kuhiji, na kufunga Ramadhani".*** Hadithi hii imesimuliwa na Bukhari na Muslim.

**NGUZO YA KWANZA:** Kukubali kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah tu na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allah. Kukubali huku ndio kielelezo cha kuingia katika Uislamu. Hapana budi kwa mwenye kutaka kuingia katika Uislamu atamke kukubali huku (ambako kunaitwa Shahada). Kukubali huku kumejengeka katika nguzo mbili.

**Ya kwanza ni: Hapana mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah tu**.

Hii inamaanisha kwamba, katika huu ulimwengu hakuna muabudiwa ambaye ana haki ya kuabudiwa huko isipokuwa Allah (s.w.) tu. Shahada hii inakataa kuabudiwa kwa asiyekuwa Allah, kama ni Malaika,

Mitume, watu wema, Mawalii, miti, jua, mwezi, mawe au makaburi, kwa sababu vitu vyote hivi vimeumbwa na Allah Mola wa viumbe vyote. Sasa vipi mtu ambaye ameumbwa aabudu kiumbe mfano wake na aache kumuabudu Muumba? Kwa maana hiyo, kuabudu hakuwi sahihi isipokuwa tu kumuabudu Allah ambaye ulimwengu wote na vilivyomo ndani yake vinamnyenyekea yeye. Allah (s.w.) amesema kuwa:

﴿ شَهِدَ ٱللَّهُ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَأُو۟لُوا۟ ٱلْعِلْمِ قَآئِمًۢا بِٱلْقِسْطِ ۚ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ ﴾ آل عمران: ١٨

"***Allah ameshuhudia ya kwamba hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila yeye tu, na Malaika na wenye elimu (pia wameshuhudia)*, *akiwa ni mwenye kusimamia uadilifu. Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila yeye tu, mwenye nguvu, mwenye hekima".*** Sura Al-Imran: 18.

Kwa ajili hii, ndio neno hili la **لا إله إلاّ الله** likawa ndio nembo ya Uislamu, anuani yake na ufunguo wa kuingilia humo, kwa sababu linamaanisha kwamba mwanadamu anakiri utiifu wake na ufuasi wake wa kumuabudu Allah na kujitenga na kuabudu asiyekuwa Allah au kuabudu mwengine pamoja na Allah.

**Ya pili ni: Muhammad ni mjumbe wa Allah**. Kukubali huku kunakusanya mambo matatu muhimu, nayo ni haya yafuatayo:-

**1)** Kukiri kwamba, kwa haki, Allah amemtuma Muhammad (s.a.w.) kwa watu wote; Waarabu na Wasiokuwa Waarabu, weupe na weusi kuja kutoa habari njema na kutoa habari za maonyo. Amemtuma awaite watu katika kumuabudu Allah peke yake na waache ushirikina na ukafiri. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ وَمَآ أَرْسَلْنَٰكَ إِلَّا كَآفَّةً لِّلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا ﴾ سبأ: ٢٨

***"Na hatukukutuma (wewe Muhammad) ila tu (ukawe Mtume) kwa watu wote ukiwa mtoaji wa habari nzuri na muonyaji".*** Sura Sabai: 28.

**2)** Wajibu wa kumsadiki Mtume Muhammad (s.a.w.) kwa kila anachoeleza, kwa sababu hayo anayoyaeleza ni Wahyi (ufunuo)

utokao kwa Allah. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلْهَوَىٰٓ ۝٣ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْىٌ يُوحَىٰ﴾ النجم: ٣-٤

***"Wala (Mtume Muhammad) hasemi kwa mapenzi ya nafsi (yake). Hayakuwa haya (anayosema) ila tu ni Wahyi (ufunuo) uliofunuliwa (kwake)".*** Sura Annajm: 3-4.

**3)** Wajibu wa kumtii Mtume Muhammad (s.a.w.) katika kila alichoamrisha na kujiepusha na kila alichokataza na kukikemea, kwa sababu yeye ni mfikishaji ujumbe wa Allah, na Allah ameamrisha kumtii. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَمَآ ءَاتَىٰكُمُ ٱلرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَىٰكُمْ عَنْهُ فَٱنتَهُوا۟﴾ الحشر: ٧

***"Na alichokupeni Mtume kipokeeni na alichokukatazeni jiepusheni nacho".*** Sura Al-hashr: 7.

**NGUZO YA PILI:** Kusimamisha sala:

Sala ni ibada yenye matamshi na vitendo maalumu. Huanzwa kwa Takbira na kuhitimishwa kwa Salamu. Sala ndio nguzo kuu ya dini na ni jambo la mwanzo ambalo mja atahojiwa kwalo Siku ya Kiyama. Kwa sababu hii, ndio maana likawa jambo lililofaradhishwa na Allah Mtukufu:

﴿إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتْ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ كِتَٰبًا مَّوْقُوتًا﴾ النساء: ١٠٣

***"Kwa hakika, sala kwa Waislamu ni faradhi iliyowekewa nyakati maalumu".*** Sura Annisaa: 103. Kwa sababu ya utukufu wake na daraja yake, Allah ameifaradhisha mbinguni.

Kusimamisha sala ni kule kuitekeleza kwa Ikhlasi (nia safi na halisi ya utiifu kwa Allah) na unyenyekevu na kuhudhurisha moyo pamoja na kuchunga shuruti zake, nguzo zake, mambo yake ya wajibu na suna zake. Atakaye itekeleza kwa namna hii itakuwa ni nuru kwake, kama alivyosema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Na Sala ni Nuru".*** Hadithi hii Imesimuliwa na Muslim. Maana ni kwamba, sala

humuongoza mwenye kusali kwenye njia iliyo sawa, humuangazia njia ya uongofu, humzuia asifanye maasi na humkataza kufanya mambo maovu na machafu. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ﴾ العنكبوت: ٤٥

***"Bila shaka, sala (ikisaliwa ilivyo) huzuia (huyo mwenye kusali asifanye) mambo machafu na maovu".*** Sura Ankabut: 45.

**NGUZO YA TATU:** Kutoa Zaka:

Zaka ni kiwango cha lazima kukitoa katika mali inayokua na ambayo imefikia kiwango, na kuwapa wanaostahiki kwa masharti maalumu. Faradhi hii ni wajibu kwa matajiri wa Kiislamu kutoa katika mali zao na kuwapa ndugu zao wanaostahiki, wakiwemo fukara, masikini na wengine ambao Qur-ani imewataja. Allah (s.w.) amesema kuwa:

﴿إِنَّمَا ٱلصَّدَقَٰتُ لِلْفُقَرَآءِ وَٱلْمَسَٰكِينِ وَٱلْعَٰمِلِينَ عَلَيْهَا وَٱلْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِى ٱلرِّقَابِ وَٱلْغَٰرِمِينَ وَفِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱبْنِ ٱلسَّبِيلِ ۖ فَرِيضَةً مِّنَ ٱللَّهِ ۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ﴾ التوبة: ٦٠

"***Sadaka (Zaka)hupewa (watu hawa):- Fukara na masikini na watumishi wa Zaka na wanaotiwa nguvu nyoyo zao (kwa kuingia kwao katika Uislamu) na katika kuwapatia uhuru watumwa na katika kuwasaidia wenye madeni na katika (kutengeneza) mambo aliyoyaamrisha Allah na katika (Kupewa) wa safari (walioharibikiwa). Ni faradhi inayotoka kwa Allah. Na Alla ni Mjuzi, Mwenye hekima".*** Sura Attauba: 60.

Wote hao hupewa Zaka hiyo kwa kutekeleza amri ya Allah Mtukufu na kuwafanyia hisani waja wake. Kwa Zaka hiyo, Muislamu hujitakasa na madhambi na makosa na pia kujisafisha na ubahili. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿خُذْ مِنْ أَمْوَٰلِهِمْ صَدَقَةً تُطَهِّرُهُمْ وَتُزَكِّيهِم بِهَا﴾ التوبة: ١٠٣

***"Chukua kutoka katika mali zao sadaka (Zaka) uwasafishe na uwatakase kwayo".*** Sura Attauba: 103.

Zaka sio ufadhili wa mtu kwa mwenzake, bali ni haki ya Allah katika mali hii. Ndio maana Allah haikubali ila pale tu itakapo epukana na tabia mbaya kama vile kiburi, majivuno na masimbulizi kwa masikini. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ٱلَّذِينَ يُنفِقُونَ أَمۡوَٰلَهُمۡ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ ثُمَّ لَا يُتۡبِعُونَ مَآ أَنفَقُواْ مَنّٗا وَلَآ أَذٗى لَّهُمۡ أَجۡرُهُمۡ عِندَ رَبِّهِمۡ وَلَا
خَوۡفٌ عَلَيۡهِمۡ وَلَا هُمۡ يَحۡزَنُونَ ٢٦٢ ۞ قَوۡلٞ مَّعۡرُوفٞ وَمَغۡفِرَةٌ خَيۡرٞ مِّن صَدَقَةٖ يَتۡبَعُهَآ أَذٗىۗ وَٱللَّهُ غَنِيٌّ
حَلِيمٞ ٢٦٣ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تُبۡطِلُواْ صَدَقَٰتِكُم بِٱلۡمَنِّ وَٱلۡأَذَىٰ﴾ البقرة: ٢٦٢ - ٢٦٤

“***Wale wanaotoa mali zao katika njia ya Allah kisha hawafuatishi yale waliyoyatoa kwa masumbulizi wala udhia wao wana ujira wao kwa Mola wao, na hawatakuwa na hofu na wao hawatahuzunika. Kauli njema na kusamehe (anayekukosa) ni bora kuliko sadaka inayofuatishwa na udhia. Na Allah ndiye Mkwasi, Mpole. Enyi mlioamini, msiharibu sadaka (Zaka) zenu kwa masimbulizi na udhia”. Sura Al-baqara: 262-264***.

Kwa faradhi hii tukufu hupatikana hali ya jamii ya Kiislamu kuhurumiana, kushikamana na kwa sababu inalinda umoja wake, mshikamano wake na mapenzi yake.

**NGUZO YA NNE:** Kufunga Ramadhani

Ni kujizuia kula, kunywa na kujamiiana (kuingiliana kimwili mume na mke) katika mwezi wa Ramadhani kuanzia alfajiri mpaka kuzama kwa jua, kwa nia ya kumuabudu Allah Mtukufu. Funga ni ibada inayomnyanyua Muislamu na kurekebisha tabia zake. Inakuza uchamungu kwa Muislamu na kujiepusha na yaliyokatazwa. Inamzoesha kudhibiti utashi wake usijiachie katika kujitumbukiza katika matamanio yake. Hii ndio maana ya kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُتِبَ عَلَيۡكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ﴾
البقرة: ١٨٣

***“Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga (saumu) kama walivyo lazimishwa waliokuwepo kabla yenu ili mpate kumcha Mungu”.*** Sura Albaqara:183. Ama mfungaji ambaye huukosesha mwili wake kula na kunywa na akaruhusu ulimi wake na viungo vyake kufanya maasi na madhambi, mtu kama huyo Allah hana haja na funga yake. Mjumbe wa Allah (s.w.) amesema kuwa: ***"Yule asiye acha kusema uzushi na kuutumia basi Allah hana haja ya kuacha chakula chake na kinywaji chake".*** Hadithi hii imesimuliwa na Bukhari.

Katika funga, Muislamu hujifunza jinsi gani apate hisia za tabu wanazozipata ndugu zake masikini na mafukara ambao hawapati cha kuondoshea njaa zao na kuzima kiu. Mwenye kufunga hupata hisia za ugumu wa njaa na kiu pamoja kwamba ana uwezo wa kula na kunywa na, kwa sababu hiyo, huhisi jinsi gani ndugu zake wanapata shida na kuteseka na huku hawapati cha kuondoshea njaa zao. Hapo Muislamu hukimbilia kutoa na kuwasaidia.

**NGUZO YA TANO:** Kuhiji nyumba takatifu ya Allah.

Hija ni kwenda Makka katika miezi maalumu na kufanya vitendo maalumu.

Hija ni ibada ya kiwiliwili ambayo Allah kaifaradhisha mara moja katika umri wa mtu. Ibada hii imekuja ili kutekeleza amri ya Allah aliyomuamrisha Nabii Ibrahim isemayo kuwa:

﴿وَأَذِّن فِي ٱلنَّاسِ بِٱلۡحَجِّ يَأۡتُوكَ رِجَالٗا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٖ يَأۡتِينَ مِن كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٖ﴾ الحج: ٢٧

***"Na (tukamwambia kuwa:) Tangaza kwa watu habari za Hija, watakuja (wengine) kwa miguu na (wengine) juu ya kila mnyama aliyekonda (kwa kuchoka) wakija kutoka katika kila njia ya mbali".*** Sura Al-hajj: 27.

Katika hija zinaonekana hali za unyenyekevu kwa Allah na kumpwekesha kulikotimia pale Waislamu wanapotufu katika nyumba ya Allah wakiwa wameacha mapambo ya kidunia ili kuonesha unyenyekevu na utiifu wao kwa Allah. Wote kwa pamoja wanatamka kauli mbiu ya Tawhidi:

(لبّيك لا شريك لك لبّيك)

**"Tumekuitika ewe usiye na mshirika, tumekuitika"**

Katika hija hudhihiri hali ya usawa na umoja baina ya Waislamu wote kwa kauli mbiu yao moja (Talbiya), mavazi yao ya aina moja na mahala pao pamoja pamoja na tofauti za rangi zao, utaifa wao na hali zao.

Huu ndio Uislamu na hizi ndio nguzo zake kuu. Atakayezitekeleza ipasavyo ataonja utamu wa imani na atastahiki kupata msamaha wa Rahmani. Mtume (s.w.) amesema kuwa: ***"Ataonja utamu wa imani atakayeridhia kuwa Allah ni Mola (wake) na Uislamu ndio dini (yake) na Muhammad ni Mtume (wake)"***. Hadithi hii imesimuliwa na Muslim. Pia Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Atakayeridhia kuwa Allah ndiye Mola (wake) na Uislamu ndio dini (yake) na Muhammad ndiye Nabii (wake) ni wajibu yeye kupata pepo"***. Hadithi hii imesimuliwa na Muslim.

## TANO: UHUSIANO BAINA YA UISLAMU NA DINI NYINGINE ZA MBINGUNI ZILIZOTANGULIA

Kwakuwa dini zote za mbinguni zimeteremshwa kutoka kwa Allah Mtukufu tunakuta kwamba zinakubaliana katika misingi yake na madhumuni yake, kama Qur-ani Tukufu ilivyoliashiria hilo pale Allah Mtukufu aliposema kuwa:

﴿شَرَعَ لَكُم مِّنَ ٱلدِّينِ مَا وَصَّىٰ بِهِۦ نُوحًا وَٱلَّذِىٓ أَوْحَيْنَآ إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِۦٓ إِبْرَٰهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَىٰٓ ۖ أَنْ أَقِيمُوا۟ ٱلدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا۟ فِيهِ﴾ الشورى: ١٣

***"Amekupeni sharia ya dini ile ile aliyomuusia Nuhu na tuliokufunulia wewe na tuliowausia Ibrahimu na Mussa na Issa kwamba, simamisheni dini wala msifarakane ndani yake". Sura Ash- shuuraa: 13.***

**1)** Dini zote za mbinguni zinahubiri msingi mmoja ambao ni kumuamini Allah Mtukufu, kumpwekesha na kuachana na kuabudu asiyekuwa yeye.

**2)** Dini zote za mbinguni zinakubaliana juu ya kutenda yale mambo yote ambayo yanampeleka mwanadamu katika kheri na kuyaacha yale yote yanayompeleka katika shari.

**3)** Dini zote za mbinguni zinahubiri kushikamana na maadili mazuri na tabia njema.

Ama sheria na kanuni za utekelezaji, dini za mbinguni zinatofautiana katika mfumo na utekelezaji, kama Allah (s.w.) alivyosema kuwa:

﴿لِكُلّٖ جَعَلۡنَا مِنكُمۡ شِرۡعَةٗ وَمِنۡهَاجٗاۚ﴾ المائدة: ٤٨

"***Kila (umma) mmoja katika nyinyi (binadamu) tumeuwekea sharia (yake) na mfumo (wake)".*** Sura Almaida: 48.

Marejeo ya tofauti hii ni kutofautiana kwa tabia za mataifa, mahitaji yao, hali zao, zama zao na sehemu wanazotoka. Kwa mfano, sala imeamrishwa katika dini zote, lakini namna ya utekelezaji wake unatofautiana kutoka dini hadi dini nyingine. Funga imeamrishwa na dini zote, lakini namna yake inatofautiana kutoka dini na dini nyingine.

Hapa pana suala muhimu ambalo ni lazima kulizingatia. Suala lenyewe ni kwamba, Allah (s.w.) aliyapa mataifa yaliyopita jukumu la kulinda vitabu vyake ambavyo kawateremshia na kuwataka wao ndio wavitunze. Allah *Mtukufu* amesema kuwa:

﴿إِنَّآ أَنزَلۡنَا ٱلتَّوۡرَىٰةَ فِيهَا هُدٗى وَنُورٞۚ يَحۡكُمُ بِهَا ٱلنَّبِيُّونَ ٱلَّذِينَ أَسۡلَمُواْ لِلَّذِينَ هَادُواْ وَٱلرَّبَّٰنِيُّونَ وَٱلۡأَحۡبَارُ بِمَا ٱسۡتُحۡفِظُواْ مِن كِتَٰبِ ٱللَّهِ وَكَانُواْ عَلَيۡهِ شُهَدَآءَۚ﴾ المائدة: ٤٤

***"Hakika tuliteremsha Taurati yenye mwongozo na nuru. Manabii waliojisalimisha (kwa Allah walikuwa) wanawahukumu Wayahudi kwayo, na watawa na wanazuoni (pia walihukumu kwa Taurati hiyo) kwa sababu walitakiwa kukilinda kitabu cha Allah, na walikuwa mashahidi juu ya hilo".*** Sura Almaida: 44.

Kilichotokea kwao ni mapenzi ya nafsi na kupenda kwao dunia kuwatawala na, kwa sababu hiyo, wakathubutu kuvigusa vitabu hivyo na kubadilisha na kupotosha aya zake tukufu kwa mikono yao

kwa namna ambayo inaendana na mapenzi ya nafsi zao na utashi wao, kiasi kwamba aya hizo zikawa haziwasilishi madhumuni ya Alla. Kwa sababu hiyo, vitabu hivyo vimekuwa sio salama na haviaminiki. Qur'ani imetupa habari ya hujuma hii dhidi ya vitabu vya mbinguni pale Allah Mtukufu aliposema kuwa:

﴿يَٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ قَدۡ جَآءَكُمۡ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمۡ كَثِيرٗا مِّمَّا كُنتُمۡ تُخۡفُونَ مِنَ ٱلۡكِتَٰبِ﴾ المائدة: ١٥

***"Enyi watu wa kitabu, amekwisha kufikieni Mtume wetu anayekudhihirishieni mengi mliyokuwa mkiyaficha katika kitabu".*** Sura Almaida: 15. Na akasema pia kwamba:

﴿مِّنَ ٱلَّذِينَ هَادُواْ يُحَرِّفُونَ ٱلۡكَلِمَ عَن مَّوَاضِعِهِۦ﴾ النساء: ٤٦

''***Miongoni mwa Wayahudi (ambao) wanabadilisha maneno kuyatoa mahali pake".*** Sura Annisai: 46. Na akasema pia kwamba:

﴿فَوَيۡلٞ لِّلَّذِينَ يَكۡتُبُونَ ٱلۡكِتَٰبَ بِأَيۡدِيهِمۡ ثُمَّ يَقُولُونَ هَٰذَا مِنۡ عِندِ ٱللَّهِ لِيَشۡتَرُواْ بِهِۦ ثَمَنٗا قَلِيلٗاۖ فَوَيۡلٞ لَّهُم مِّمَّا كَتَبَتۡ أَيۡدِيهِمۡ وَوَيۡلٞ لَّهُم مِّمَّا يَكۡسِبُونَ﴾ البقرة: ٧٩

***''Basi adhabu kali itawafika wanaoandika kitabu kwa mikono yao kisha wakasema: Haya yametoka kwa Allah. (Wamesema uwongo huo) ili wachukue thamani ndogo ya kiulimwengu. Basi ole wao kwa yale waliyoyaandika kwa mikono yao (wakasingizia kuwa ya Mungu). Na ole wao kwa yale wanayoyachuma".*** Sura Albaqara:79.

Kwa vile dini ya Kiislamu aliyokuja nayo Muhammad (s.a.w.) ndio hitimisho la dini, Allah Mtukufu ameifanya Qur'ani kuwa ndio kitabu tawala kwa vitabu vya mbinguni vilivyotangulia. Qur-ani inatoa ushahidi wa kuyakiri na kuyakubali yale ya kweli na ya msingi yaliyomo katika vitabu hivyo na kuyabatilisha yale ambayo wapotoshaji wameyahusisha kwenye vitabu hivyo na kughushi kwa mikono yao.

Qur'ani ni kitabu kilicho juu ya vitabu vya mbinguni; kwa maana kwamba, Qur'ani inatoa ushahidi, inatoa habari za kweli, ni salama na inaaminika. Kwa ajili hiyo, Allah amechukua dhamana ya kuilinda dini hii isije ikapata mabadiliko na upotoshaji mpaka kitasimama

Kiyama. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ إِنَّا نَحۡنُ نَزَّلۡنَا ٱلذِّكۡرَ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَٰفِظُونَ ﴾ الحجر: ٩

***“Hakika, sisi ndio tulioteremsha mawaidha (haya ya Qur-ani), na hakika sisi ndio tutakaoyalinda”.*** Sura Alhijri: 9. Hakuna kitabu kitakachoteremshwa baada ya Qur'ani, na wala hakuna Mtume atakayeletwa baada ya Muhammad. Lau kama Allah asingeulinda Uislamu basi dini yake yote ingepotea kwa sababu ya mikono michafu.

Kwa sababu hii, ni wajibu kwa kila atakayesikia kuhusu Uislamu na kuujua auamini, hata kama yeye ni mfuasi wa dini nyingine. Ambaye hauamini Uislamu na haufuati hana sifa ya kuitwa **Muislamu**. Mtume Muhammad amebainisha jambo hili kwa kauli yake isemayo kuwa: ***“Naapa kwa yule ambaye nafsi ya Muhammad ipo mkononi mwake kwamba, hakuna yeyote katika umma huu atakayesikia kuhusu mimi; awe Myahudi au Mkristo halafu akafa bila ya kuyaamini yale niliyokuja nayo isipokuwa kwamba atakuwa katika watu wa motoni”***. Hadithi hii imesimuliwa na Muslim.

# MLANGO WA PILI

# ITIKADI YA MUISLAMU

## KUZIFUNGAMANISHA NYOYO KWA ALLAH

Moyo wa muumini unatamani sana raha ya dunia na akhera. Lakini raha hii ya moyo na utamu wa kweli haupatikani isipokuwa tu kwa kumtambua Allah, kumpenda, kujiweka karibu naye kwa kutenda yale anayoyapenda na kuyaridhia na pia kujiepusha na yote anayoyachukia na kumfanya akasirike.

### KWANZA: MOYO WA MUISLAMU BAINA YA HOFU, MATARAJIO NA KUPENDA

Nyoyo hizi zinahitaji zifungamanishwe na Mlezi wake na Muumbaji wake ili ipatikane dhamana kwamba zinakwenda katika njia ambayo Allah ameziwekea. Jambo muhimu sana linalomsukuma mja kutenda, kumrahisishia mwendo wake wa kwenda kwa Allah na kumfanya awe na bidii ya kufanya ibada ni amali za moyoni. Amali kubwa kabisa kati ya amali hizi ni kumpenda Allah, kutaraji mema kwake na kumuogopa.

Mja Muislamu hana katika moyo wake isipokuwa tu kumpenda Allah, kumpenda Mtume wake na kupenda anayoyapenda Allah na Mtume wake. Muislamu anapenda kufanya ibada na anawapenda waja wa Allah wafanyao ibada. Imepokewa kwa Annas, Allah amuwiye radhi, akimnukuu Mtume kuwa amesema kwamba: ***"Sifa tatu atakayekuwa nazo atapata utamu wa imani. Allah na Mtume wake wawe ndio anaowapenda zaidi kuliko kitu chochote, na ampende mtu kwa ajili ya Allah tu, na achukie kurudi katika ukafiri kama anavyochukia kutumbukizwa katika moto"***. Hadithi hii imesimuliwa na Bukhari na Muslim.

Moyoni mwa mja Muislamu kuna hofu ya kumuogopa Allah; hofu inayoufanya moyo kutetemeka kwa kuogopa kutokea hasira za Allah na adhabu yake kali iwapo atafanya jambo aliloliharamisha Allah au akazembea katika kutekeleza wajibu aliotakiwa kuufanya. Hofu hii inakuwa kinga kwa Muislamu dhidi ya kufuata mapenzi ya nafsi

yake na kujiachia katika matamanio yake. Pia hofu hii inamhimiza Muislamu awe imara katika kumtii Allah na kufuata amri zake.

Moyoni mwa mja Muislam kuna matarajio ya kupata rehema za Allah, radhi zake, mapenzi yake, thawabu na neema zake za duniani na akhera. Matarajio hayo humfanya Muislamu adumu katika kumtii Allah na ashindane katika kufanya kheri, kwa sababu moyo wake umefungamanishwa na rehema za Allah na yale ambayo Allah amewaandalia waja wake wachamungu na watiifu. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَٱلَّذِينَ هَاجَرُواْ وَجَٰهَدُواْ فِي سَبِيلِ ٱللَّهِ أُوْلَٰٓئِكَ يَرۡجُونَ رَحۡمَتَ ٱللَّهِۚ وَٱللَّهُ غَفُورٞ رَّحِيمٞ ﴾ البقرة: ٢١٨.

***"Hakika, wale walioamini na wale waliohama (kutoka Makka kuja Madina) na wakapigana Jihadi katika dini ya Allah, hao wanataraji rehema za Allah, na Allah ni mwingi wa kusamehe, mwingi wa kurehemu".*** Sura Albaqara: 218.

Moyo wa Muislamu katika mwendo wake wa kuelekea kwa Allah unapaswa uwe katika uwiano sawa baina ya mambo haya matatu, kwa sababu upande mmoja ukiuzidi mwingine moyo utapotoka katika ibada zake na utatoka katika njia iliyonyooka. Ibnulqayyim, Allah amrehemu, amesema kuwa: ***"Moyo katika kuelekea kwake kwa Allah ni kama ndege. Mapenzi ni kichwa chake na hofu na matarajio ni mbawa zake".*** (Madaarij Assaalikiin:1/517).

Hebu fikiria ndugu yangu Muislamu: Nini kitamkumba ndege huyo iwapo atakosa moja ya mbawa zake au kukosa kichwa chake? Bila shaka atakuwa ni ngawira ya kila muwindaji.

Muislamu ambaye anatekeleza ibada alizoamrishwa na Allah anapaswa azitekeleze kwa mapenzi na hamu ya kutaka kuwa karibu na Mola wake; akitaraji ibada hizo kukubaliwa na Allah, kuwa na matumaini ya kupata thawabu zake, neema zake na pepo yake. Pia anatakiwa kuwa na bidii ya kuzifanya ibada hizo kama Allah alivyoamrisha kwa hofu ya kurejeshewa mwenyewe na kutokubaliwa. Pia awe na hofu ya kuogopa adhabu ya Allah na hasira zake iwapo

atafanya uzembe.

Tambua ndugu Muislamu, Allah akurehemu, kwamba uwiano huu baina ya haya mambo matatu ndio njia ya Mitume. Allah Mtukufu ameeleza katika Qur-an kuhusu hali zao kwamba:

﴿ إِنَّهُمْ كَانُوا۟ يُسَٰرِعُونَ فِى ٱلْخَيْرَٰتِ وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا ۖ وَكَانُوا۟ لَنَا خَٰشِعِينَ ﴾
الأنبياء: ٩٠

***"Bila shaka, wao walikuwa wepesi katika kufanya mema na wakituomba kwa shauku (ya kupata thawabu) na hofu (ya kupata adhabu). Nao walikuwa wakitunyenyekea".*** Sura Al-anbiyaa: 90.

## PILI: MOYO WA MUISLAMU NA HISIA ZA UTUKUFU WA ALLAH (S.W.)

Miongoni mwa mambo makubwa na muhimu sana yanayopaswa kuwemo katika moyo wa Muislamu ni kuhisi utukufu wa Allah Mtukufu, kwa sababu kuhisi utukufu huu kunaufanya moyo huo uwe makini na ulioamka; anamkumbuka Allah katika kauli na vitendo vyake vyote. Haendi kufanya yanayomkasirisha Allah, na anafanya bidii ya kutekeleza amri zake.

Qur'ani imetupa habari kwamba, washirikina walithubutu kuingia katika ushirikina na ukafiri kwa sababu walikosa hisia za utukufu wa Allah. Kwa sababu hiyo, nyoyo zao zikawa susuwavu na ngumu, na wakafanya sawa viumbe na muumbuaji.  Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ وَمَا قَدَرُوا۟ ٱللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِۦ وَٱلْأَرْضُ جَمِيعًا قَبْضَتُهُۥ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ وَٱلسَّمَٰوَٰتُ مَطْوِيَّٰتٌۢ بِيَمِينِهِۦ ۚ سُبْحَٰنَهُۥ وَتَعَٰلَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴾ الزمر: ٦٧

"***Na hawakumheshimu Allah heshima ipasayo. Na (Siku ya Kiyama) ardhi yote itakuwa mkononi mwake. Na mbingu zitakunjwakunjwa katika mkono wake wa kulia. Ametukuka na ametakasika na yale wanayomshirikisha".*** Sura Azzumar: 67.

Allah amewashutumu wale ambao hofu ya kumuogopa Allah imedhoofika katika nyoyo zao. Amesema kuwa:

﴿مَّا لَكُمْ لَا تَرْجُونَ لِلَّهِ وَقَارًا﴾ نوح: ١٣

"***Mmekuwaje, hamuweki heshima kwa Allah?".*** Sura Nuhu: 13. Wafasiri wametafsiri kuwa: Kwa nini nyinyi hamumheshimu Allah ipasavyo?

Ndugu yangu Muislamu, unaweza kuuliza kuwa: *Nawezaje kuhisi utukufu wa Allah moyoni mwangu?* Qur'ani imetuelekeza njia na namna Muislamu anavyoweza kupata hisia na utukufu wa Allah moyoni mwake. Njia hizo ni hizi zifuatazo:-

**1) KUTAFAKARI UFALME WA ALLAH NA MAMBO MAKUBWA ALIYOYAUMBA.**

Muislamu kila anapoangalia na kutafakari huu ufalme mkubwa na mpana, hali hiyo humzidishia kumtukuza aliyeuumba na kuuanzisha. Ni kwa sababu hii, Allah amewataka wenye akili salama wawe na tafakari na mazingatio haya ili, kwa kufanya hivyo, waweze kupata hoja ya kufahamu utukufu wa Allah, uwezo wake na ulezi wake. Pia iwe mwongozo kwao wa kutambua kwamba yeye ndiye Mola na, yeye pekee bila ya kuwa na mshirika, ndiye anayestahiki kuabudiwa. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿إِنَّ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَاخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ۝١٩٠ الَّذِينَ يَذْكُرُونَ اللَّهَ قِيَامًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ وَيَتَفَكَّرُونَ فِي خَلْقِ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ رَبَّنَا مَا خَلَقْتَ هَٰذَا بَاطِلًا سُبْحَانَكَ فَقِنَا عَذَابَ النَّارِ﴾ آل عمران: ١٩٠-١٩١.

***"Kwa yakini kabisa, katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi na kupishana kwa usiku na mchana, ziko hoja (za kuonesha kuwepo kwa Allah mmoja), kwa wenye akili. Ambao humkumbuka Allah wakiwa wamesimama wima na wakiwa wamekaa na wakiwa wamejilaza. Na wanatafakari kuumbwa kwa mbingu na ardhi. (Wanasema): Ewe Mola wetu, hukuviumba vitu hivi bure. Utukufu ni wako. Basi tuepushe na adhabu ya moto".*** Sura Al-imran: 190-191. Zilipoteremka aya hizi Mtume (s.a.w.) alisema kuwa: ***"Adhabu kali impate yule atakaezisoma aya hizo kisha asizitafakari".*** Hadithi hii Imepokewa na Ibnihibban.

Pia Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿أَفَلَا يَنظُرُونَ إِلَى ٱلْإِبِلِ كَيْفَ خُلِقَتْ ﴿١٧﴾ وَإِلَى ٱلسَّمَآءِ كَيْفَ رُفِعَتْ ﴿١٨﴾ وَإِلَى ٱلْجِبَالِ كَيْفَ نُصِبَتْ ﴿١٩﴾ وَإِلَى ٱلْأَرْضِ كَيْفَ سُطِحَتْ﴾ الغاشية: ١٧-٢٠.

***"Hivi hawamtazami ngamia jinsi alivyoumbwa? Na mbingu jinsi ilivyoinuliwa? Na milima jinsi ilivyothabitishwa (ilivyoimarishwa)? Na ardhi jinsi ilivyotandazwa?".*** Sura Al-ghashiya: 17-20.

Angalia mbingu juu yako na tafakari usafi wake na mn'garo wa nyota zake ili upate kutambua uzuri wa umbile lake na utukufu wa muumbaji wake. Tafakari kubadilika kwa hali zake; usiku na mchana, hali ya kuwepo kwa mawingu na hali ya anga safi, kupatwa kwa jua na kupatwa kwa mwezi ili heshima na taadhima kwa aliyeumba hayo na kuyapanga izidi kuongezeka katika moyo wako. Allah ameyafanya hayo yawe hoja kwa mwenye kuogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake na kuogopa maonyo.

Angalia kwa mazingatio upana wa mbingu, ukubwa wa umbile lake na zilivyoumbwa kwa umakini mkubwa ili upate kutambua utukufu wa muumbaji wake. Imenukuliwa kwa Ibnimasoud, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***"Baina ya mbingu ya dunia na ile inayofuatia ni miaka mia tano, na baina ya mbingu na mbingu nyingine ni miaka mia tano, na baina ya mbingu ya saba na Kursiy ni miaka mia tano, na baina ya Kursiy na maji ni miaka mia tano, na Arshi iko juu ya maji, na Allah yupo juu ya Arshi. Kwake hakijifichi chochote katika vitendo vyenu".*** Athar hii imesimuliwa na Addaarimiy katika kitabu cha 'Arrad Alaljahmiyya', pia Ibnukhuzaima katika kitabu cha 'Tauhiid' na Ibnumajah katika kitabu cha 'Al-iimaan'.

Kama ni kustaajabu basi zistaajabu hizi mbingu ambazo, pamoja na ukubwa wake na upana wake uliokwenda juu sana, lakini hazina nguzo zinazozishikila. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ٱللَّهُ ٱلَّذِى رَفَعَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ بِغَيْرِ عَمَدٍ تَرَوْنَهَا﴾ الرعد: ٢

***"Allah ambaye ameziinua mbingu bila ya nguzo mnazoziona".*** Sura Arraad: 2.

Tafakari kupishana kwa usiku na mchana ili upate kugundua ukubwa wa fadhila za Allah kwa waja wake. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ قُلْ أَرَءَيْتُمْ إِن جَعَلَ ٱللَّهُ عَلَيْكُمُ ٱلَّيْلَ سَرْمَدًا إِلَىٰ يَوْمِ ٱلْقِيَٰمَةِ مَنْ إِلَٰهٌ غَيْرُ ٱللَّهِ يَأْتِيكُم
بِضِيَآءٍ ۖ أَفَلَا تَسْمَعُونَ ﴿٧١﴾ قُلْ أَرَءَيْتُمْ إِن جَعَلَ ٱللَّهُ عَلَيْكُمُ ٱلنَّهَارَ سَرْمَدًا إِلَىٰ يَوْمِ ٱلْقِيَٰمَةِ مَنْ إِلَٰهٌ
غَيْرُ ٱللَّهِ يَأْتِيكُم بِلَيْلٍ تَسْكُنُونَ فِيهِ ۖ أَفَلَا تُبْصِرُونَ ﴾ القصص: ٧١-٧٢.

***'Sema: Niambieni, kama Allah angeufanya usiku ukawa wa kudumu mpaka Siku ya Kiyama. Ni Mungu gani asiyekuwa Allah atakuleteeni mwanga? Basi je, hamsikii?. Sema: Niambieni, kama Allah angeufanya mchana ukawa wa kudumu mpaka Siku ya Kiyama, ni mungu gani asiyekuwa Allah atakuleteeni usiku mkapumzika humo? Basi je, hamuoni?".*** Sura Al-qasas: 71-72.

Viumbe wataweza kufanya nini kama jua halijatoka? Na wataweza kufanya nini kama mwezi haukutoka? Watafanya kazi vipi? Watalima vipi? Watalala vipi? Vipi, vipi, vipi...?

Uangalie kwa mazingatio huu mwezi muandamo ambao Allah kaufanya ni alama miongoni mwa alama zake za kustaajabisha, pale unapojitokeza kama uzi mwembamba halafu nuru yake inaongezeka hadi kufikia kiwango cha kuwa mwezi duara kamili. Halafu unaanza kupungua mpaka ukarejea katika hali yake ya awali. Allah ameuumba mwezi kuwa katika hali ili uwe kipimo cha wakati kwa watu katika maisha yao na ibada zao, na wakati huo huo uwe kielelezo cha nuru na uzuri ambao washairi wanautungia mashairi yao. Yote hayo yawe ni dalili ya utukufu wa Muumbaji wake.

Na utakapoiangalia ardhi ambayo unaishi juu yake na kutembea katika njia zake namna Allah alivyoitandaza na kuingiza ndani yake riziki za watu, vyakula vyao na akaiimarisha kwa milima mirefu, utaona humo maajabu ya mimea na matunda. Ardhi inatoa mimea yenye rangi tofauti na mazao yenye ladha tofauti wakati ardhi ni ile ile!

Ewe Muislamu, hebu iangalie milima mikubwa ambayo mwanadamu hupigwa butwaa kuona ukubwa wake na jinsi ilivyopanda juu, ili upate

hisia za kitu katika utukufu wa Allah ambaye ameiumba. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَمِنَ ٱلۡجِبَالِ جُدَدُۢ بِيضٞ وَحُمۡرٞ مُّخۡتَلِفٌ أَلۡوَٰنُهَا وَغَرَابِيبُ سُودٞ﴾ فاطر: ٢٧

***"Na katika milima zimo njia (tabaka) nyeupe na nyekundu na zenye rangi mbali mbali. Na milima (mingine) meusi sana".*** Sura Fatir: 27.

Allah ataiporomosha milima hii, ataivunja vipande vipande na kuifanya tambarare. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَيَسۡـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلۡجِبَالِ فَقُلۡ يَنسِفُهَا رَبِّي نَسۡفٗا ١٠٥ فَيَذَرُهَا قَاعٗا صَفۡصَفٗا ١٠٦ لَّا تَرَىٰ فِيهَا عِوَجٗا وَلَآ أَمۡتٗا﴾ طه: ١٠٥-١٠٧.

***"Na wanakuuliza kuhusu milima (itakuwaje Siku ya Kiyama?). Waambie: Mola wangu ataivunja vunja. Na ataiacha ikiwa uwanja uliokaa sawasawa (tambarare). Hutaona humo mdidimio wala muinuko".*** Sura Twaha: 105 -107.

Allah Mtukufu amesema pia kwamba:

﴿وَتَكُونُ ٱلۡجِبَالُ كَٱلۡعِهۡنِ ٱلۡمَنفُوشِ﴾ القارعة: ٥

***"Na milima itakuwa kama sufi zilizochambuliwa (zikawa zinapeperuka".*** Sura Al-qaria: 5.

## 2) KUITAFAKARI NAFSI YA MWANADAMU NA UMBO LAKE MARIDHAWA

Ewe Muislamu, ukitaka kujua zaidi uwezo mkubwa wa Allah na utukufu wake ili moyo wako uweze kumpenda, unachotakiwa kufanya ni kukaa karibu sana na nafsi yako uitafakari jinsi ilivyoumbwa na kuundwa. Tafakari uhodari na umakini wa Allah uliopo katika kuiumba nafsi ya mwanadamu, kuanzia kuumbwa hadi kufa! Allah anakupa picha ya kina na ya upembuzi wa hatua za kiumbe huyu mwanadamu alizozipitia. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِن كُنتُمْ فِى رَيْبٍ مِّنَ ٱلْبَعْثِ فَإِنَّا خَلَقْنَـٰكُم مِّن تُرَابٍ ثُمَّ مِن نُّطْفَةٍ ثُمَّ مِنْ عَلَقَةٍ ثُمَّ مِن مُّضْغَةٍ مُّخَلَّقَةٍ وَغَيْرِ مُخَلَّقَةٍ لِّنُبَيِّنَ لَكُمْ ۚ وَنُقِرُّ فِى ٱلْأَرْحَامِ مَا نَشَآءُ إِلَىٰٓ أَجَلٍ مُّسَمًّى ثُمَّ نُخْرِجُكُمْ طِفْلًا ثُمَّ لِتَبْلُغُوٓا۟ أَشُدَّكُمْ ۖ وَمِنكُم مَّن يُتَوَفَّىٰ وَمِنكُم مَّن يُرَدُّ إِلَىٰٓ أَرْذَلِ ٱلْعُمُرِ لِكَيْلَا يَعْلَمَ مِنۢ بَعْدِ عِلْمٍ شَيْـًٔا ۚ وَتَرَى ٱلْأَرْضَ هَامِدَةً فَإِذَآ أَنزَلْنَا عَلَيْهَا ٱلْمَآءَ ٱهْتَزَّتْ وَرَبَتْ وَأَنۢبَتَتْ مِن كُلِّ زَوْجٍۭ بَهِيجٍ﴾ الحج: ٥.

***"Enyi watu, kama nyinyi mmo katika shaka ya kufufuliwa, (mnaona haiwezekani kufufuliwa), basi kwa hakika sisi tulikuumbeni kwa udongo (Mzee wenu Nabii Adamu), kisha (tukawa tunakuumbeni nyinyi) kwa manii (mbegu ya uzazi), kisha (yanageuka) kuwa kipande cha damu, kisha kuwa kipande cha nyama kilichoumbika (kinachofanyika sura) na kisichoumbika ili tukubainishieni (uwezo wetu). Nasi tunakiwezesha kukaa tumboni tunachokitaka mpaka muda maalumu. Kisha tunakutoeni mkiwa watoto. Kisha (tunakuleeni) ili mfikie balehe yenu. Na miongoni mwenu kuna wanaokufa (kabla ya kufikia hali hii). Na miongoni mwenu kuna wanaofikishwa umri dhalili (ukongwe) ili (mkongwe huyo) asijue chochote baada ya kujua (kwake). Na unaiona ardhi imetulia kimya (imekuwa kame), lakini tunapoteremsha maji (mvua) juu yake, inatikisika na kufunguka na kuotesha kila namna ya mmea wenye kupendeza".*** Sura Al-hajj: 5.

Na anasema Allah Mtukufu kwamba:

﴿وَلَقَدْ خَلَقْنَا ٱلْإِنسَـٰنَ مِن سُلَـٰلَةٍ مِّن طِينٍ ﴿١٢﴾ ثُمَّ جَعَلْنَـٰهُ نُطْفَةً فِى قَرَارٍ مَّكِينٍ ﴿١٣﴾ ثُمَّ خَلَقْنَا ٱلنُّطْفَةَ عَلَقَةً فَخَلَقْنَا ٱلْعَلَقَةَ مُضْغَةً فَخَلَقْنَا ٱلْمُضْغَةَ عِظَـٰمًا فَكَسَوْنَا ٱلْعِظَـٰمَ لَحْمًا ثُمَّ أَنشَأْنَـٰهُ خَلْقًا ءَاخَرَ ۚ فَتَبَارَكَ ٱللَّهُ أَحْسَنُ ٱلْخَـٰلِقِينَ﴾ المؤمنون: ١٢-١٤.

***"Na kwa yakini, tulimuumba mwanadamu kutokana na udongo ulio safi. Kisha tukamfanya tone la manii (mbegu ya uzazi iliyowekwa) katika mahali palipohifadhiwa vizuri. Kisha tukalifanya tone hilo likawa donge la damu. Tukalifanya donge la damu hilo kuwa pande la nyama. Kisha pande hilo la nyama tukalifanya mifupa, na mifupa tukaivalisha nyama. Kisha Tukamfanya kiumbe chengine. Basi ametukuka Allah Mzuri zaidi wa waumbaji".*** Sura Al-muuminuna: 12-14

Hebu litafakari hili umbo la ndani la mwanadamu namna Allah alivyoweka humo mifumo na vifaa (viungo) ambavyo mwanadamu hawezi kupata picha ya namna vilivyoumbwa na umakini wa vinavyofanya kazi. Moyo unafanya kazi usiku na mchana bila ya kusimama. Viungo vya hisia vinatambua yaliyopo pembeni mwake, yawe ni ya kuona au ya kusikia au ya kuhisi. Ubongo unaendesha harakati zote za mwanadamu; furaha, huzuni, kucheka, kulia, kusimama, kukaa kitako, kulala na kuamka.

Ewe Muislamu, itafakari vyema nafsi yako ili kumheshimu Allah, kumpenda na kumtukuza kuwe imara katika moyo wako. Tafakari kwa makini hekima iliopo katika kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿وَفِىٓ أَنفُسِكُمْۚ أَفَلَا تُبْصِرُونَ﴾ الذاريات: ٢١

“***Na katika nafsi zenu (pia zimo alama za kuonesha utukufu wa Allah). Je, hamzioni?”.*** Sura Al-dhariyat: 21.

Wito huu wa Allah juu ya kutafakari ni wako wewe Muislam na pia ni wa watu wote kwa jumla ili yatulizane katika nyoyo mapenzi ya kumpenda Allah, kumtukuza na kumpwekesha na, kwa sababu hiyo, nyoyo zipate kufungamana na Mola wake, Muumba wake, anayezipa riziki na mwenye kusimamia mambo yake.

### 3) KUDUMU KUSOMA QUR'ANI

Qur-an Tukufu ni kitabu kitakatifu na ni ujumbe kwa watu wote. Ndani ya Qur'ani mna habari za watu waliokuwepo kabla yetu na pia habari za watu wa baada yetu. Maajabu yake hayamaliziki na miujiza yake haina mwisho. Allah Mtukufu ameifanya Qur'ani nuru na mwongozo kwa watu wote. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ذَٰلِكَ ٱلْكِتَٰبُ لَا رَيْبَۛ فِيهِۛ هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ﴾ البقرة: ٢.

***“Hiki ni kitabu kisichokuwa na shaka. Ni mwongozo kwa wamchao Allah”.*** Sura Albaqara: 2. Na amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿إِنَّ هَٰذَا ٱلْقُرْءَانَ يَهْدِى لِلَّتِى هِىَ أَقْوَمُ﴾ الإسراء: ٩.

***“Hakika, hii Qur'ani inaongoza (waja kuelekea) katika njia***

***iliyonyooka kabisa”.*** Sura Al-israa: 9.

Kwa hakika, kuzitafakari aya za Qur-an Tukufu ni katika mambo makubwa yanayoufanya moyo kuwa hai na kuufungamanisha na Mola wake. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿أَفَلَا يَتَدَبَّرُونَ ٱلْقُرْءَانَ أَمْ عَلَىٰ قُلُوبٍ أَقْفَالُهَآ﴾ محمد: ٢٤.

“***Je, hawaizingatii Qur-ani? Au katika nyoyo (zao) kuna kufuli?”.*** Sura Muhammad: 24.

Allah Mtukufu ameiteremsha hii Qur-an na kuifanya tiba ya nyoyo na viwiliwili. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَنُنَزِّلُ مِنَ ٱلْقُرْءَانِ مَا هُوَ شِفَآءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ﴾ الإسراء: ٨٢.

***“Na tunateremsha katika Qur-an (mafundisho yake) ambayo ni tiba na rehema kwa wanaoamini”***. Sura Al-israa: 82. Ni kwanini nyoyo laini haziwi nyenyekevu na kusikiliza maneno ya Mola wake, wakati ambapo vitu vigumu visivyokuwa na uhai vinamnyenyekea Mola? Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿لَوْ أَنزَلْنَا هَٰذَا ٱلْقُرْءَانَ عَلَىٰ جَبَلٍ لَّرَأَيْتَهُۥ خَٰشِعًا مُّتَصَدِّعًا مِّنْ خَشْيَةِ ٱللَّهِ ۚ وَتِلْكَ ٱلْأَمْثَٰلُ نَضْرِبُهَا لِلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُونَ﴾ الحشر: ٢١.

***“Lau kama tungeliiteremsha hii Qur-ani juu ya mlima, ungeliuona unanyenyekea, unapasukapasuka kwa sababu ya kumuogopa Allah. Na hii ni mifano tunawapigia (tunawaeleza) watu ili wafikiri”.*** Sura Alhashr: 21.

Hakika, mwenye kupenda kitu na moyo wake ukafungamana nacho hukikumbuka sana na kukitaja sana. Atakayedumu kuisoma Qur-ani ambayo ni maneno ya Allah (s.w.) hiyo inakuwa alama ya usafi wa moyo wake na kufungamanika kwa hisia zake na Allah (s.w.), na kwamba yeye anampenda Allah (S.W) mpaka amekuwa hachoki kuisoma Qur-an na kuizingatia. Imepokewa kwa Othman, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***“Lau kama nyoyo zenu zingekuwa safi, basi zisingelishiba maneno ya Mola wenu”.*** Athar

hii imesimuliwa na Abdallah bin Ahmad katika kitabu cha Azzuhd.

### 4) KUMJUA ALLAH KWA MAJINA YAKE NA SIFA ZAKE

Kwa hakika, Muislamu ambaye anasoma kitabu cha Allah, anagundua kwamba, hakuna aya miongoni mwa aya za kitabu hiki kitukufu ambayo haitaji jina katika majina ya Allah Mtukufu au sifa zake tukufu. Bali vitendo, majina sifa zake alizozitaja ni kubwa na nyingi zaidi kuliko mambo mengine ambayo watu wanayahitaji katika dunia yao na maisha. Ibnutaymiya amesema kuwa: ***"Katika Qur-ani yametajwa humo majina ya Allah na sifa zake na vitendo vyake zaidi ya yalivyotajwa masuala ya kula, kunywa na ndoa katika pepo".*** Dar-u Taarudhil-aqli Wannaqli 3/61. Hii inaonesha umuhimu wa Muislamu kujua sifa na majina haya, kwa sababu kuyajua kunaurithisha moyo kumtukuza Allah (s.w.) na kumpenda.

Wakati kujua majina na sifa za Allah kunarithisha heshima na hofu kumuogopa Allah, hiyo ni kwa sababu Muislamu anakuwa na itikadi kwamba Allah anayaona matendo ya waja na kauli zao, na hakuna kinachojificha kwake katika yale yaliyomo ndani ya nyoyo zao. Al-izzu Bin Abdissalam, Allah amrehemu, amesema kuwa: ***"Kufahamu maana ya majina ya Allah ni nyenzo ya kumkabili Allah kwa kutumia faida za maana hayo na ambazo ni hofu, matarajio mema, heshima, kupenda, kutegemea na faida nyingine miongoni mwa faida za kufahamu sifa za Allah".*** Shajaratul-maarif Wal-ahwaal. Uk. 1.

Kumjua Allah kwa majina yake na sifa zake huzifanya nyoyo ziwe na imani zaidi na imani hiyo kuwa madhubuti. Sheikh Abdulrahman Alsaad, Allah amrehemu amesema kuwa: "***Na kwa kadiri ya mja anavyomjua Mola wake ndivyo imani yake inavyokuwa. Kila maarifa yake ya kumjua Mola wake yanapoongezeka na imani yake inaongezeka, na Imani yake inapungua kila maarifa yake hayo ya kumjua Mola wake yanapopungua. Njia ya karibu zaidi ya kumfikisha kwenye hayo ni kutafakari majina ya Allah na sifa zake katika Qur-ani".*** Taisiirul-kariimir-rahman 1/35.

Sasa ni kitu gani kinampasa Muislamu akijue katika majina na sifa

za Allah ili avune matunda, apate faida na ili moyo wake ufungamane na Allah Mmoja Ambaye hakuna wa kufanana naye?

Kumjua Allah kwa majina yake na sifa zake kunapatikana kwa kupitia misingi ifuatayo:-

**a. MAJINA YOTE YA ALLAH NI MAZURI NA SIFA ZAKE ZOTE NI TUKUFU.**

Miongoni mwa heshima ya mja Muislamu kwa Mola wake ni kuwa na itikadi kwamba, majina yote ya Allah ni mazuri, na sifa zake zote ambazo amejisifia ni tukufu. Hii ni kusadikisha yale aliyoyaeleza Allah katika kitabu chake kitukufu kwamba:

﴿وَلِلَّهِ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ فَٱدۡعُوهُ بِهَا﴾ الأعراف: ١٨٠.

***"Na Allah ana majina mazuri, basi muombeni kwayo".*** Sura Al-aaraf: 180**.** Pia Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿قُلِ ٱدۡعُواْ ٱللَّهَ أَوِ ٱدۡعُواْ ٱلرَّحۡمَٰنَۖ أَيّٗا مَّا تَدۡعُواْ فَلَهُ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ﴾ الإسراء: ١١٠.

"***Sema: Muombeni Allah kwa jina la Allah au muombeni kwa jina la Rahman (Mwingi wa rehema). Kwa jina lolote mnalomwita (katika majina haya itafaa), kwani yeye ana majina mazuri".*** Sura AI-israa: 110. Na pia Allah amesema kuwa:

﴿ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَۖ لَهُ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ﴾ طه: ٨.

***"Allah, hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa yeye tu. Yeye tu ndiye mwenye majina mazuri".*** Sura Twaha: 8. Na pia amesema kuwa:

﴿هُوَ ٱللَّهُ ٱلۡخَٰلِقُ ٱلۡبَارِئُ ٱلۡمُصَوِّرُۖ لَهُ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ﴾ الحشر: ٢٤.

***"Yeye ndiye Allah, Muumbaji, Mtengenezaji, Mfanyaji wa sura (za viumbe). Yeye tu ndiye mwenye majina mazuri".*** Sura Al-hashr: 24.

Maana ya majina ya Allah kuwa mazuri ni kwamba, majina hayo yapo katika kiwango cha juu cha ukamilifu na hayana kasoro kwa namna yoyote ile. Majina yake ni mazuri na hakuna majina mazuri zaidi

wala kamilifu zaidi wala yanayopendeza zaidi wala yaliyotukuka zaidi kuliko majina yake hayo. Hii ni kwa sababu majina hayo yana maana nzuri, zilizotukuka na yana sifa maridhawa ambazo zinaonesha ukubwa na utukufu wa Allah ambaye amejipa majina hayo.

### b. NJIA YA KUJUA MAJINA YA ALLAH NA SIFA ZAKE

Haiwezekani kwa Muislamu kupata njia nzuri zaidi, kamilifu zaidi na salama zaidi ya majina ya Allah na sifa zake kuliko njia ya kitabu cha Allah na Hadithi za Mtume wake (s.w.), kwa sababu Allah Mtukufu ndiye, yeye mwenyewe, aliyejipa majina haya na sifa hizi. Yeye Allah Mtukufu ndiye anayeijua zaidi nafsi yake kuliko viumbe wake wote.

Iwapo tumefahamu kwamba Qur-ani tukufu ni kitabu cha Allah kwa viumbe wake na kwamba ndani yake kuna uongofu, nuru na haki, tutajua kwamba chanzo kikuu cha kujua majina ya Allah na sifa zake ni Qur-an Tukufu ambayo haiharibiwi toka zamani na siku zinazokuja. Ni uteremsho utokao kwa Allah Mwenye hekima na Mwenye kutajwa kwa kila sifa njema.

Na iwapo tumefahamu kwamba Mtume (s.a.w.) ni Mjumbe wa Allah na kwamba yeye hatamki kitu kwa matakwa yake, na kwamba Allah amempa jukumu la kuwatambulisha watu Mola wao na kuwafikishia dini yake ambayo ameiridhia kwayo, basi tutajua kuwa Hadithi sahihi za Mtume (s.a.w.) ndio njia nyingine ya kujua majina ya Allah na sifa zake, kwa sababu hakuna anayemjua Allah zaidi baada yeye mwenyewe kuliko Mtume (s.a.w.) alieyaminika. Amesema Imam Ahmad, Allah amrehemu, kuwa: ***"Allah hasifiwi ila tu kwa sifa ile aliyojipa yeye mwenyewe au kwa sifa aliyopewa na Mjumbe wake. Isivuke Qur-ani na Hadithi".*** Majmuul-fatawa 5/26.

### c. MSIMAMO WA MUISLAMU JUU YA MAJINA YA ALLAH NA SIFA ZAKE

Inampasa Muislamu anayeamini majina ya Allah na sifa zake ajilazimishe kufuata msimamo wa haki na njia sahihi ya kuamini majina ya Allah na sifa zake. Jambo hilo litawezekana tu kwa njia zifuatazo:-

**(1)** Kumthibitishia Allah majina na sifa alizojithibitishia yeye mwenyewe au kuthibitishiwa na Mtume wake. Pia kukanusha zile sifa ambazo amekanusha kuwa hahusiki nazo au ambazo Mtume wake (s.a.w.) amekanusha, kwa sababu hakuna anayemjua Allah zaidi kuliko yeye mwenyewe. Allah amesema kuwa:

﴿قُلْ ءَأَنتُمْ أَعْلَمُ أَمِ ٱللَّهُ﴾ البقرة: ١٤٠.

***(Sema: Hivi nyinyi ndio mjuao zaidi au Allah (ndiye ajuae zaidi)?".*** Sura Albaqara: 140. Vile vile hakuna anayemjua zaidi Allah baada yeye mwenyewe kuliko Mjumbe wake ambaye Allah kamuelezea kuwa:

﴿وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلْهَوَىٰٓ ۝٣ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ﴾ النجم: ٣–٤.

***'Wala hasemi kwa mapenzi ya nafsi (yake). Hayakuwa haya (anayoyasema) ila tu ni wahyi (ufunuo) uliofunuliwa (kwake)".*** Sura Annajm: 3 – 4.

**(2)** Kumtakasa Allah na kufanana na viumbe vyake. Amesema Allah kuwa:

﴿لَيْسَ كَمِثْلِهِۦ شَىْءٌ ۖ وَهُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْبَصِيرُ﴾ الشورى: ١١.

***'Hakuna chochote kinachofanana na yeye. Na yeye tu ndiye mwenye kusikia, mwenye kuona***". Sura Ash-shuura: 11**.**

Allah hafanani na chochote na wala hakuna kiumbe chake chochote kinachofanana na yeye. Yeye (s.w.) anasifika kwa sifa za ukamilifu na utukufu ambazo hazimpasi yeyeote kusifika kwazo isipokuwa yeye peke yake.

**(3)** Kutokuwa na tamaa ya kutaka kujua namna ya sifa za Allah zilivyo, kwa sababu hiyo ni katika elimu ya Ghaibu (masuala ya itikadi yasiyo onekana kwa macho) ambayo Allah peke yake amejipendelea kuijua. Akili haina uwezo wa kujua mambo ya Ghaibu. Amesema Allah (s.w.) kuwa:

﴿وَلَا يُحِيطُونَ بِهِۦ عِلْمًا﴾ طه: ١١٠.

***"Na (wao) hawawezi kumjua (Allah) vilivyo".*** Sura Taha: 110.

Pia Allah amesema kuwa:

﴿هَلۡ تَعۡلَمُ لَهُۥ سَمِيّٗا﴾ مريم: ٦٥.

*"**Je, unamjua (mwengine) mwenye jina (na sifa) lake**?".* Sura Maryam: 65.

**d. KUMTUKUZA ALLAH KWA MAJINA YAKE NA SIFA ZAKE**

Miongoni mwa dalili kubwa za kuonesha mja anamtukuza Mola wake na moyo wake kufungamana naye ni kuonekana dhahiri kwa athari ya kuamini majina ya Allah na sifa zake katika maisha yake na katika tabia zake. Muislamu mwenye moyo mkweli ni yule ambaye anamuabudu Allah kwa majina yake na sifa zake. Mifano ya suala hilo ni hii:

**(1) Kumuomba Allah kwa majina yake na sifa zake**:

**Ni** katika kumtukuza Allah mja Muislam kumuelekea na kumuomba kwa moyo wake na viungo vyake ili kutii amri yake. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَلِلَّهِ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ فَٱدۡعُوهُ بِهَاۖ وَذَرُواْ ٱلَّذِينَ يُلۡحِدُونَ فِيٓ أَسۡمَٰٓئِهِۦ﴾ الأعراف: ١٨٠.

***"Na Allah ana majina mazuri. Basi muombeni kwayo, na waacheni wale wanaoharibu utakatifu wa majina yake".*** Sura Al-raaf: 180.

Kumuomba Allah kwa majina yake na sifa zake kuko kwa aina mbili:-

<u>**Aina ya kwanza**</u>**: Dua ya ibada**. Maana yake ni mtu kumuabudu Allah Mtukufu kwa ibada za moyoni kama vile kuogopa, kutaraji mema, kupenda na kutegemea, au kwa ibada za viungo kama vile sala, funga, Hija, kusoma Qur-ani, kusabihi na dhikiri (kumtaja Allah), au kwa ibada za mali kama vile Zaka, sadaka na Udh-hiya (kuchinja mnyama siku ya sikukuu ya Id-el-haj).

Aidha ni katika dua za ibada kumtaja Allah (s.w.), kumsifu, kumtukuza na kumsabihi (kumtakasa) kwa majina na sifa zake zinazomstahiki ambazo ametufundisha. Muislamu anaposema:

Subhaanallah (Ametakasika Allah), Alhamdulillah (Shukurani ni za Allah), Laa Ilaaha illall-allah (Hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Allah tu), Allahu Akbar (Allah ni mkubwa zaidi), yote hayo ni katika kumtukuza Allah, kumsifu na ni katika kumuomba Allah (s.w.) kwa majina yake na sifa zake kwa njia ya kumuabudu. Dua ya ibada haina maombi. Lengo lake kuu ni kumuomba Allah kwa kumsifu na kusikia burudani kutaja majina yake na sifa zake.

**<u>Aina ya pili</u>**: **Dua ya kuomba**. Dua hii ni mja kumuomba Mola wake ampe jambo lenye manufaa na yeye au kumuomba amuepushe na jambo lenye madhara kwake, katika mambo ya dunia na ya akhera, kama kumuomba Allah amsamehe madhambi yake au kumuomba rehema au uongofu au Taufiq (kuwezeshwa kufanya mambo ya kheri) au kupata pepo au kuepushwa na moto na mengineyo.

Aina hizi mbili za dua, ile ya ibada na ile ya kuomba, zinakuwa pamoja. Kila muombaji anayemuomba Allah (s.w.) anamuomba kwa ikhlas (nia safi), hofu, matarajio na kupenda. Hii ni ibada. Mwenye kumtaja Allah kwa, maana halisi, anamuomba Allah na kumtaka amnyanyue daraja, amzidishie mambo mazuri na amsamehe makosa yake. Hii ni dua ya kuomba.

**(2) Kumuomba Allah kwa jina lake tukufu zaidi:**

Miongoni mwa fadhila kubwa za Allah kwa waja wake Waislamu ni kuwawekea jina mahususi katika majina yake mazuri, ambalo mja Muislamu haombi kwalo ila tu Allah humjibu dua yake na kumpa maombi yake. Bila shaka, Muislamu kuwa na hima ya kumuomba Allah kwa kutumia jina hili ni miongoni mwa mambo makubwa ambayo yanaufungamanisha moyo wa Muislamu na Mola wake. Imepokewa kwa Abdallah Ibniburaida akimnukuu baba yake ***"Kwamba Mtume wa Allah alimsikia mtu mmoja akisema kuwa:***

**اللَّهمَّ إنِّي أسألك بأنّي أشهد أنّك أنت اللَّه الّذي لا إله إلاّ أنت، الأحد الصّمد، الّذي لم يلد ولم يولد، ولم يكن له كفواً أحد. فقال النبيّ ﷺ: «والذي نفس محمّد بيده، لقد سأل اللَّه عليه باسمه الأعظم الذي إذا سُئل به أعطى، وإن دُعي به أجاب».**

***Ewe Mola wangu, kwa yakini mimi ninakuomba kwa sababu***

***mimi ninakri kuwa wewe ni Allah ambaye hakuna anayestahiki kuabudiwa ila wewe tu, wa pekee, mwenye kukusudiwa katika kutatua mahitaji ya waja, ambaye hakuzaa na hakuzaliwa, na hakuna yeyote wa kufanana naye. Mtume akasema kuwa: Nina'apa kwa (Allah) ambaye nafsi ya Muhammad iko mkononi mwake kwamba, (mtu huyu) amemuomba Allah kwa kutumia jina lake tukufu zaidi ambalo akiombwa kwalo anatoa na akiombwa kwalo anajibu".***

Hadithi hii imesimuliwa na Ahmad, Tirmidhiy, Ibnimaajah na Annasai katika kitabu cha Assunan Alkubraa.

Imenukuliwa kwa Anas Bin Malik, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa ***"Alikuwa pamoja na Mtume (S.A.W) akiwa amekaa kitako na kukawa kuna mtu mmoja anasali halafu akaomba dua hii:***

«اللَّهمَّ إنِّي أسألك بأنَّ لك الحمد، لا إله إلاَّ أنت المنّان، بديع السماوات والأرض يا ذا الجلال والإكرام، يا حيّ يا قيّوم».

***Ewe Mola wangu, ninakuomba kwa sababu wewe tu unastahiki shukurani. Hakuna anayestahiki kuabudiwa ila wewe tu mwingi wa kutoa, mbunifu wa mbingu na ardhi, ewe mwenye utukufu na ukarimu, ewe uliye hai, mwenye kusimamia mambo ya waja. Akasema Mtume kuwa: (Huyu mtu) amemuomba Allah kwa kwa jina lake kuu ambalo akiombwa kwalo hujibu na akiombwa kwalo hutoa".*** Hadithi hii imesimuliwa na Abudaud, Attirmidhiy, Annasai na Ibnimaajah.

Tia akilini mwako ewe Muislamu kwamba, unapomuomba Allah kwa kutumia dua hizi mbili tukufu unakuwa unamsifu Allah, unamtaja, unamtukuza na unamuomba kwa majina yake mazuri mazuri na sifa zake tukufu, bali unamuomba kwa jina lake tukufu zaidi, ukitaraji kupata majibu ya dua yako na kupata unachokiomba. Tambua kwamba umeshaahidiwa kujibiwa. Ni utukufu ulioje kama moyo wako utakuwa umefungamana na Mola wake na ulimi wako ukiwa laini kwa sababu ya kumtaja, kumsifu na kumuomba kwa kutumia majina yake na sifa zake anazostahiki.

### (3) Kujipamba kwa sifa anazozipenda Allah (s.w.)

Ni miongoni mwa muktadha wa kuamini majina ya Allah na sifa

zake Muislamu kujipamba kwa sifa anazozipenda Allah (s.w.) kama vile kusifika kwa elimu, uadilifu, huruma, upole, usamehevu, na kwa upande mwengine kujiepusha na sifa zinazomkasirisha Allah na ambazo hazimstahiki isipokuwa yeye tu, kama vile kiburi, utukufu, ujabari (utumiaji maamuzi binafsi), kutenzanguvu (kushurutisha). Amesimulia Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akimnukuu Mtume (s.a.w.) kuwa amesema kwamba: ***"Allah Mtukufu amesema kuwa: Kiburi ni joho langu na utukufu ni msuli wangu (shuka yangu). Kwa hiyo, yeyote atakaye nyan'ganyiana na mimi (atakayenipora) mojawapo ya sifa mbili hizo nitamtia motoni".*** Hadithi Qudsiy hii imesimuliwa na Ahmad, Abudaud na Ibnimaajah.

Kwa hiyo, Muislam kujipamba kwa sifa zinazompendeza Allah (s.w.) na kujiepusha na sifa zinazomchukiza ni dalili ya kweli kwamba imani imekuwa madhubuti ndani ya moyo wake na kwamba moyo huo umefungamana na Allah kwa kumtukuza na kumsifu.

### e. MWENYE KUYAHIFADHI MAJINA NA SIFA ZA ALLAH ATAINGIA PEPONI

Kujua majina ya Allah Mtukufu ni miongoni mwa vyanzo vikubwa sana vya imani, kwa sababu kuyajua majina ya Allah ni sababu ya mja kuingia peponi. Kwa vile peponi hawaingii isipokuwa wenye kuamini tu, suala la mja kuyajua majina ya Allah limekuwa ni sababu ya imani inayopelekea kuingia peponi, na ni chemchemi ya yeye kupata nguvu na kuwa kwake imara. Amesimulia Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Allah ana majina 99; mia kasoro moja. Atakaye yahifadhi ataingia peponi".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Maana ya kuhifadhi sifa na majina ya Allah ni kuyaweka moyoni bila ya kusahau, kufahamu maana yake, kujua mafundisho yake, kutekeleza muktadha wake, kumtaja Allah na kumuomba kwayo na kujipamba kwa adabu zake na maadili yake. Mtu ambaye atayachukulia hivi majina na sifa za Allah, nafsi yake itatakasika, vitendo vyake vitakuwa vizuri, utiifu wake kwa Mola wake utakuwa mkubwa zaidi na pia kumheshimu Mola wake, kumuogopa na kumpenda kutaongezeka.

Hivi ndivyo Muislamu anavyotakiwa kutambua kwamba, Allah

yuko pamoja naye katika hali zake zote ili izalike katika moyo wake hali ya kumhofu na kumheshimu Allah, jambo ambalo litamkinga dhidi ya ushawishi wa shetani. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ إِنَّ ٱلَّذِينَ ٱتَّقَوۡاْ إِذَا مَسَّهُمۡ طَٰٓئِفٞ مِّنَ ٱلشَّيۡطَٰنِ تَذَكَّرُواْ فَإِذَا هُم مُّبۡصِرُونَ ﴾ الأعراف: ٢٠١.

***"Kwa yakini, wale wanaomuogopa (Allah) zinapowagusa pepesi za shetani (tukio lolote la ushawishi wa shetani na kwa sababu hiyo wakafanya maasi) hukumbuka (Allah na) tahamaki wamekwisha ona (haki na njia sahihi)".*** Sura Al-aaraf: 201.

Mwisho, ndugu Muislamu, wewe uko katika neema ambayo hakuna neema nyingine bora zaidi baada ya hiyo. Allah amekupa neema ya imani na uongofu, na amekuepusha kuingia katika moto wa wapotofu na waliopotea. Mshukuru Allah kwa neema zake na muombe akuzidishie fadhila zake. Tambua kwamba, furaha yako kwa neema hii haitimii isipokua tu pale moyo wako utakapokuwa umeuelekeza kwa Allah tu. Katika mazungumzo haya ya haraka umejifunza namna unavyoweza kuufungamanisha moyo wako kwa Allah. Kwa hiyo, jitahidi kuwa na Ikhlas (Nia safi) na jitahidi kufanya amali (njema) ili upate kuonja utamu wa imani na ladha ya utiifu.

# TAWHID NA AINA ZAKE

Wajibu wa mwanzo unaompasa Muislamu kuujua na kuutekeleza ni kumpwekesha Allah Mtukufu, jambo ambalo mja hawezi kusalimika mbele ya Allah isipokuwa tu kwa kulitekeleza na kuufanyia kazi muktadha wake kwa vitendo. Hilo ni jambo la mwanzo kabisa atakaloulizwa mja kaburini kwake, na Siku ya Kiyama atakapokutana na Mola wake. Kwa ajili hii, Allah ameteremsha vitabu na akatuma wajumbe (A.S) wote kwa ajili ya kulihubiri jambo hilo. Kasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَا مِن قَبۡلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِيٓ إِلَيۡهِ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدُونِ﴾ الأنبياء: ٢٥.

***"Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba, hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila mimi tu. Basi, niabuduni".*** Sura Al-anbiyaa: 25.

Katika mlango huu tutabainisha maana ya Tawhid, aina zake, fadhila zake, maana ya neno la Tawhid (لا إله إلاّ اللَّه) na shuruti zake. Pia tutazungumzia jambo linalokinzana na Tawhid na ambalo ni Shirki (ushirikishaji) na aina zake. Mwisho, tutabainisha madhambi makubwa (Kabaair) na tofauti baina yake na baina ya madhambi madogo. Pia tutabainisha hukumu ya mwenye kufanya madhambi makubwa duniani na akhera. Tunamuomba Allah Tawfiq (uwezeshaji).

## KWANZA: ALLAH NI NANI?

Allah ni Muabudiwa, Mmoja, wa pekee, hakuzaa na hakuzaliwa, mwenye sifa za ukamilifu na utukufu, ameepukana na kila kasoro na upungufu. Hafanani na yeyote katika viumbe vyake, na yeye ndiye muumbaji wa ulimwengu huu na muendeshaji wa mambo yake. Kwake hakijifichi kitu chochote katika ardhi yake na mbingu zake,

na hakuna kinachotokea ila tu kwa idhini yake. Yeye ndiye mwenye fadhila na neema kwa waja wake. Yeye tu ndiye anayestahiki kuabudiwa na si mwengine. Atawakusanya waja wake kwa ajili ya hesabu katika siku ambayo haina shaka.

## PILI: MAANA YA TAWHID

Tawhid ni kumpwekesha Allah katika Rububiya (utendaji wake) na katika Uluhiya (kustahiki kwake kuabudiwa) na katika majina na sifa zake kamilifu.

## TATU: AINA ZA TAWHID

Aina za Tawhid ni tatu: Tawhid Rububiya, Tawhid Uluhiya na Tawhid ya Majina na Sifa.

### AINA YA KWANZA: TAWHID RUBUBIYA

Maana ya Tawhid hii ni kumpwekesha Allah Mtukufu kwa kutenda kwake, kama vile kuumba, ufalme, kuendesha (mambo ya viumbe), na kusimamia (mambo ya viumbe) na kuwa na itikadi thabiti kwamba, Allah Mtukufu ndiye Mlezi wa kila kitu, mmiliki wake na kwamba yeye ndiye mwendeshaji wa ulimwengu huu na mwenye kusimamia mambo yake. Yeye ndiye muumbaji wa viumbe, mwenye kuwapa riziki, mwenye kuwapa uhai na mauti. Anasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿ ٱللَّهُ ٱلَّذِى خَلَقَكُمْ ثُمَّ رَزَقَكُمْ ثُمَّ يُمِيتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ ۖ هَلْ مِن شُرَكَآئِكُم مَّن يَفْعَلُ مِن ذَٰلِكُم مِّن شَىْءٍ ۚ
سُبْحَٰنَهُۥ وَتَعَٰلَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴾ الروم: ٤٠.

***‘Allah ndiye aliyekuumbeni, kisha akakupeni riziki, kisha akakufisheni, kisha akakupeni uhai. Je, miongoni mwa wale mnaowashirikisha na Mungu yuko awezaye kufanya lolote katika haya? Yeye (Allah) ameepukana na upungufu na ameepukana na wale wanaomshirikisha naye".*** Sura Arruum: 40.

Hakuna muumbaji wala mmiliki wala mtoaji riziki wala mpangaji wa mambo ya viumbe isipokuwa Allah Mtukufu tu. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿أَلَا لَهُ ٱلْخَلْقُ﴾ الأعراف: ٥٤.

"***Fahamuni, kuumba ni kwake yeye tu".*** Sura Al-aaraf: 54.

Na Alla amesema pia kwamba:

﴿أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ ٱللَّهَ لَهُۥ مُلْكُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ﴾ البقرة: ١٠٧

***"Hivi hujui kwamba Allah tu ndiye mwenye ufalme wa mbingu na ardhi?".*** Sura Albaqara: 107.

Makafiri, kwa jumla, katika zama za Mtume (s.a.w.) waliikubali aina hii ya Tawhid, na asilimia kubwa ya watu wa dini mbali mbali hawakuipinga. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ ٱلسَّمَآءِ وَٱلْأَرْضِ أَمَّن يَمْلِكُ ٱلسَّمْعَ وَٱلْأَبْصَٰرَ وَمَن يُخْرِجُ ٱلْحَيَّ مِنَ ٱلْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ ٱلْمَيِّتَ مِنَ ٱلْحَيِّ وَمَن يُدَبِّرُ ٱلْأَمْرَ ۚ فَسَيَقُولُونَ ٱللَّهُ ۚ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ﴾ يونس: ٣١.

***"Sema: Ni nani anayewapeni riziki kutoka mbinguni (kwa kuleta mvua), na katika ardhi (kwa kuotesha mimea)?. Au ni nani anayemiliki masikio (yenu) na macho (yenu)? Na ni nani amtoae mzima katika mfu na kumtoa mfu katika mzima?. Na ni nani atengenezaye mambo yote? Watasema: Ni Allah. Basi sema: Je, kwa nini hamuogopi?".*** Sura Yunus: 31.

Tawhid ya Rububiya peke yake haitoshi kumuingiza mtu katika Uislamu bila ya kupatikana kwa aina nyingine za Tawhid. Hii ni kwa sababu, yule ambaye ni muumbaji, mtoaji riziki, mwenye kumiliki kila kitu na mwenye kuendesha kila kitu ni lazima awe muabudiwa wa pekee, asiwe na mshirika na ibada zisifanywe ila kwa ajili yake tu. Ni kwa sababu hii, ndio maana makafiri wa Kiarabu haikuwatosha kuikubali kwao Tawhid ya Rububiya. Allah aliwaamrisha na kuwataka wampwekeshe katika ibada; jambo ambalo ndio Tawhid ya Uluhiya. Aliwabainishia kuwa, kukiri kwao kwamba Allah peke yake ndiye muumbaji, mmiliki, muendeshaji wa mambo ya viumbe na kumshirikisha mwengine katika kumuabudu, huko ni kukinzana. Anasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَلَئِن سَأَلۡتَهُم مَّنۡ خَلَقَهُمۡ لَيَقُولُنَّ ٱللَّهُۖ فَأَنَّىٰ يُؤۡفَكُونَ ﴾ الزخرف: ٨٧.

***"Na, kwa yakini kabisa, ukiwauliza: Ni nani aliyewaumba? Kwa yakini kabisa watasema: Ni Allah". Basi ni vipi wanageuzwa?".*** Sura Azzukhruf: 87. Maana ni kwamba: Vipi wanaondoshwa katika kumuabudu Allah peke yake?

## AINA YA PILI: TAWHID YA ULUHIYA

Tawhid hii huitwa pia Tawhid ya ibada. Maana yake ni kumpwekesha Allah katika ibada, kuwa na itikadi thabiti kwamba Allah ndiye mwenye haki ya kuabudiwa na kwamba kila kinachoabudiwa badala yake ni batili, Yeye aliyetakasika ndiye anayestahiki kuabudiwa, kunyenyekewa na kutiiwa kusikokuwa na mipaka, asishirikishwe na yeyote vyovyote awavyo; awe Issa, Allah amfikishie amani, au Mtume yeyote mwengine au Malaika Watukufu. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَٱعۡبُدُواْ ٱللَّهَ وَلَا تُشۡرِكُواْ بِهِۦ شَيۡـٔٗا﴾ النساء: ٣٦

***"Na mwabuduni Allah wala msikishirikishe naye kitu chochote".*** Sura Annisaa: 36.

Kwa hiyo, ibada zote zinatakiwa kufanywa kwa ajili ya Allah peke yake asiyekuwa na mshirika. Ni sawa ibada hizo ziwe za moyoni kama vile hofu, kutaraji na kutegemea, au za maneno kama vile sala, hija na funga.

Sisi hatutakiwi kuogopa, kutaraji, kutegemea, kuomba msaada, kuomba kinga, kusali, kufunga saumu na kuhiji ila kwa Allah Mtukufu peke yake. Kasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿قُلۡ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحۡيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ١٦٢ لَا شَرِيكَ لَهُۥۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرۡتُ وَأَنَا۠ أَوَّلُ ٱلۡمُسۡلِمِينَ﴾ الأنعام: ١٦٢ - ١٦٣

***"Sema: Hakika, sala yangu na ibada yangu (zote nyengine) na uzima wangu na kufa kwangu (yote hayo) ni kwa ajili ya Allah Mola wa walimwengu wote, hana mshirika. Na haya ndio niliyoamrishwa,***

***na mimi ni wa kwanza kabisa wa waliojisalimisha (kwa Allah kwa kuyatekeleza)".*** Sura Al-an-aam: 162-163.

Aina hii ya Tawhid ndio waliyoikana (waliyoikataa) makafiri hapo zamani na hata sasa. Amesema Allah Mtukufu katika kunukuu kauli yao ya kuikataa Tawhid hii kwamba:

﴿أَجَعَلَ ٱلْـَٔالِهَةَ إِلَٰهًا وَٰحِدًاۖ إِنَّ هَٰذَا لَشَيْءٌ عُجَابٌ﴾ ص: ٥

***"Oh! Amewafanya miungu (yote) kuwa Mungu mmoja tu! Bila shaka hili ni jambo la ajabu sana".*** Sura Swaad: 5.

Ni kwa sababu hii Allah ametuma wajumbe na akateremsha vitabu kwa ajili ya kuwaita (kuwalingania) watu na kuwarejesha katika kumpwekesha kumfanyia yeye tu ibada. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ ٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ وَٱجْتَنِبُوا۟ ٱلطَّٰغُوتَ﴾ النحل: ٣٦

"***Na bila shaka tulimpeleka Mtume katika kila umma ya kwamba muabuduni Allah na Muepukeni Taghuti".*** Sura Annahl: 36. Maana ya Taghuti ni kila anayeabudiwa badala ya Allah naye akawa radhi katika kuabudiwa huko.

## AINA YA TATU: TAWHID YA MAJINA NA SIFA

Tawhid hii ni kuamini majina na sifa ambazo yeye mwenyewe Allah amejithibitishia kuwa nazo ndani ya Qur-an au alizothibitishiwa na Mjumbe wake (s.a.w.) katika Hadithi sahihi. Pia ni kuwa na itakidi thabiti kwamba, Allah ana majina mazuri na ana sifa za juu na kwamba anasifika kwa sifa zote za ukamilifu na ametakasika na sifa zote za upungufu. Kwa maana hiyo, yeye yuko tofauti na viumbe vyote. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿لَيْسَ كَمِثْلِهِۦ شَيْءٌۖ وَهُوَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْبَصِيرُ﴾ الشورى: ١١.

***"Hakuna chochote mfano wake, naye ni mwenye kusikia, mwenye kuona".*** Sura Ash-shuura:11. Na amesema pia kwamba:

﴿قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ۝١ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ۝٢ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ﴾ الإخلاص: ١-٣.

***"Sema: Yeye Allah ni wa pekee. Allah tu ndiye anayestahiki kukusudiwa. Hakuzaa na hakuzaliwa. Na hana hata mmoja anayefanana naye".*** Sura Al-khlas: 1- 4.

## NNE: FADHILA ZA TAWHID

Kumpwekesha Allah kuna manufaa mengi. Katika hayo ni haya yafuatayo:-

1. Mwenye kumpwekesha Allah anapata uongofu kamili na amani iliyotimia, duniani na akhera. Allah Mtukufu anawaondoshea wenye Tawhid shari za dunia na akhera na anawapa neema ya maisha mazuri na utulivu.

2. Tawhid ni sababu ya kuingia peponi na kuokoka na moto. Hata kama mja ataadhibiwa kwa baadhi ya madhambi na maasi lakini hatokaa motoni milele kwa sababu ya kuwa na Tawhid.

3. Ni sababu ya kusamehewa madhambi makubwa na kufutiwa madhambi madogo madogo. Pia ni sababu ya kupata Shufaa (Maombezi) ya Mtume Siku ya Kiyama.

4. Ni sababu kubwa ya kuondoshewa matatizo ya dunia na akhera na kukingwa dhidi ya mateso yake.

5. Kauli na amali zote za dhahiri na za siri ili zikubaliwe, ziwe kamilifu na kulipwa zinategemea Tawhid. Kadiri Tawhid na ikhlas (nia safi ya kutenda kwa ajili ya Allah) zinavyokuwa na nguvu ndivyo mambo haya yanavyokuwa kamili na kutimia.

6. Tawhid inamkomboa mja asiwe mtumwa wa viumbe vyengine, kufungamana navyo, kuviogopa, kuvitaraji kumletea manufaa na kutenda kwa ajili yake. Hii ndio heshima ya kweli na ndio hadhi ya juu. Pamoja na hayo, mja anakuwa anamuabudu Allah, hamtaraji mwengine, hamuogopi yeyote isipokuwa yeye tu na hana marejeo ila kwake tu. Kwa kufanya hivyo, ndipo mafanikio yake yanapotimia kufaulu kwake kunakuwa kweli.

7. Allah Mtukufu amechukua dhamana kwa watu wa Tawhid

kwamba, hapa hapa duniani, atawapa ushindi, ukombozi, hadhi, heshima, mambo mazito kuwa mepesi, kuziweka hali zao vizuri na kuwawezesha kuwa na kauli na vitendo sahihi.

## TANO: MAANA YA TAMKO LA TAWHID

Tamko la Tawhid ni لا إله إلا اللهَّ (Laa ilaaha illa-llaah).

**Maana yake ni**: Hakuna wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah peke yake. Neno hili linakanusha asiyekuwa Allah Mtukufu kuitakidiwa kuwa ni mungu, na linathibitisha sifa ya mungu ni ya Allah peke yake, asiyekuwa na mshirika.

Neno "إله Ilaah" maana yake ni mungu muabudiwa. Kwa maana hiyo, atakayeabudu chochote atakuwa amekifanya kitu hicho mungu muabudiwa badala ya Allah. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿ذَٰلِكَ بِأَنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلۡحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدۡعُونَ مِن دُونِهِۦ هُوَ ٱلۡبَٰطِلُ وَأَنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلۡعَلِيُّ ٱلۡكَبِيرُ﴾ الحج: ٦٢.

***"Hayo ni kwa sababu Allah ni haki, na kwamba vile wanavyoviabudu badala yake ndio tu batili na kwamba Allah ndiye aliye juu, mkubwa".*** Sura Alhaj: 62.

**Ibada** ni kila kauli na matendo ya dhahiri na ya siri anayoyapenda Allah na kuridhia, kama vile kuomba (dua), kuogopa, kutegemea, sala, dhikiri (kumtaja Allah) na mengineyo.

Yote hayo ni lazima yawe kwa ajili ya Allah peke yake asiye na mshirika. Atakayefanya chochote kwa ajili ya asiyekuwa Allah atakuwa amefanya ushirika (Shirk). Kasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَمَن يَدۡعُ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ لَا بُرۡهَٰنَ لَهُۥ بِهِۦ فَإِنَّمَا حِسَابُهُۥ عِندَ رَبِّهِۦٓۚ إِنَّهُۥ لَا يُفۡلِحُ ٱلۡكَٰفِرُونَ﴾ المؤمنون: ١١٧

***"Na yeyote atakaye muomba (muabudu) mungu mwengine pamoja na Allah wakati hana ushahidi wa hilo, basi bila shaka hesabu yake iko kwa Mola wake. Kwa hakika, makafiri hawafanikiwi".*** Sura Al-muuminun:117.

## SITA: MASHARTI YA TAMKO LA TAWHID

Kukiri na kukubali kumpwekesha Allah hakumsaidii ila kwa kupatikana shuruti saba, nazo ni:-

**1)** Kujua maana Tamko la Tawhid inayokusudiwa kwa kukanusha na kuthibitisha. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿فَٱعۡلَمۡ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ﴾ محمد: ١٩.

***"Jua ya kwamba, hakuna aabudiwaye kwa haki ila Allah tu".*** Sura Muhammad: 19.

**2)** Iwepo yakini isiyokuwa na shaka kwamba, mtamkaji wa Tamko hilo ana imani na uhakika wa maana yake. Akiwa na shaka au wasiwasi kuhusu maana yake, tamko halitakuwa na manufaa na yeye. Kasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿إِنَّمَا ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ ثُمَّ لَمۡ يَرۡتَابُواْ﴾ الحجرات: ١٥.

***"Ilivyo ni kwamba, wenye kuamini kweli kweli ni wale waliomuamini Allah na Mtume wake kisha wakawa si wenye shaka".*** Sura Alhujuraat: 15.

**3)** Iwepo Ikhlas (Nia na dhamira safi) isiyokuwa na Shirki (ushirikishaji). Hili litapatikana kwa namna kwamba, mtamkaji wa Tamko hilo asiwe na lengo lolote la mambo ya kidunia. Kasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُواْ ٱللَّهَ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ﴾ البينة: ٥.

***"Na hawakuamrishwa ila tu kumuabudu Allah kwa kumtakasia yeye tu dini, wakiziacha dini za upotofu"***. Sura Albayyina: ***5***. Neno "Kuacha dini za upotofu" maana yake ni kuondoka katika Shirki (ushirikishaji) na kwenda katika Tawhid safi.

**4)** Uwepo ukweli usiokuwa na uongo kwa mtu kulitamka Tamko hili kwa ukweli kutoka ndani ya moyo wake. Mtume Muhammad (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Hakuna yeyote atakayekiri kuwa, hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila Allah tu na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allah ikiwa ni ukweli utokao ndani ya moyo wake,***

***isipokuwa kwamba Allah atamuharamishia moto mtu huyo (Yaani: kuingia motoni itakuwa ni haramu kwake)”.*** Hadithi hii imesimuliwa na Bukhari na Muslim, na matamshi yake ni ya Bukhari.

**5)** Kulipenda Tamko hili, kupenda muktadha wake na kuwapenda wanaoliamini na wanaolifanyia kazi. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَتَّخِذُ مِن دُونِ ٱللَّهِ أَندَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ ٱللَّهِ ۖ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَشَدُّ حُبًّا لِّلَّهِ﴾ البقرة: ١٦٥.

***“Na katika watu kuna wanaofanya miungu badala ya Allah; wanawapenda kama kumpenda Allah. Lakini walioamini wanampenda sana Allah”.*** Sura Albaqara:165. Na Mtume (s.a.w.) amesema kuwa:

***“Mambo matatu atakayekuwa nayo atapata utamu wa imani. Allah na Mjumbe wake wawe ndio anaowapenda zaidi kuliko chochote, na ampende mja kwa ajili ya Allah tu, na achukie kurejea katika ukafiri kama anavyochukia kutupwa motoni”***. Hadithi hii imesimuliwa na Bukhari na Muslim.

**6)** Kutii na kufuata madhumuni ya Tamko hili. Kasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَأَنِيبُوٓا۟ إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا۟ لَهُۥ﴾ الزمر: ٥٤.

***“Na rejeeni kwa Mola wenu na kuweni watiifu kwake”.*** Sura Azzumar: 54.

**7)** Kukubali kumuabudu Allah peke yake na kuacha kuabudu asiyekuwa yeye; jambo ambalo ndio dhamira ya Tamko hili. Atakaye litamka neno hili bila ya kukubali kumuabudu Allah peke yake atakuwa miongoni mwa wale Allah aliowaelezea kwamba:

﴿إِنَّهُمْ كَانُوٓا۟ إِذَا قِيلَ لَهُمْ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٣٥﴾ وَيَقُولُونَ أَئِنَّا لَتَارِكُوٓا۟ ءَالِهَتِنَا لِشَاعِرٍ مَّجْنُونٍ﴾ الصافات: ٣٥-٣٦.

“***Kwa yakini, wao walipokuwa wakiambiwa: Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah tu walikuwa wakifanya kiburi***

***(kwa kukataa) na wanasema kuwa: Oh! Tuiache miungu yetu kwa ajili ya (huyu) mtunzi wa mashairi, mwendawazimu?".*** Sura Asswaaffat: 35-36.

## SABA: MAMBO YANAYOTENGUA TAWHID

Tawhid inatenguka kwa kumfanyia Allah ushirika (Shirki).

Iwapo kumpwekesha Allah na kumfanyia yeye tu ibada ndio wajibu mkubwa na wa muhimu sana, basi Shirki ni maasi makubwa kabisa kwa Allah Mtukufu, kwa sababu hii ni dhambi pekee ambayo Allah hakubali kuisamehe. Kasema Allah mtukufu kuwa:

﴿ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِۦ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَآءُ ﴾ النساء: ١١٦.

***"Hakika, Allah hatoi msamaha (kwa dhambi ya) kushirikishwa, na anatoa msamaha (kwa) dhambi ya chini ya hiyo kwa amtakaye".*** Sura Annisaa: 116.

Mtume (s.a.w.) alipoulizwa kwamba: Ni ipi dhambi kubwa zaidi kwa Allah? Akasema: ***"Ni wewe kumfanyia Allah mwenza wakati yeye ndiye aliyekuumba"***. Hadithi hii imesimuliwa na Bukhari na Muslim.

Shirki inaharibu amali njema na inazibatilisha. Amali njema hazikubaliwi wala mja hapati thawabu juu ya amali hizo inapokuwepo Shirki. Hiyo ni kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿ وَلَوْ أَشْرَكُوا۟ لَحَبِطَ عَنْهُم مَّا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴾ الأنعام: ٨٨.

***"Na lau kama wangeshirikisha, bila shaka yangewaharibikia yale waliyokuwa wakiyatenda".*** Sura Al-an-aam: 88.

Shirki inamhakikishia mwenye kuwa nayo kukaa milele motoni iwapo atakufa nayo. Allah amesema kuwa:

﴿ إِنَّهُۥ مَن يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ ٱللَّهُ عَلَيْهِ ٱلْجَنَّةَ وَمَأْوَىٰهُ ٱلنَّارُ ﴾ المائدة: ٧٢.

***"Ilivyo ni kwamba, yeyote anayemfanyia Allah Shirki, hakika Allah amemharamishia Pepo, na makazi yake ya milele (yatakuwa) motoni".*** Sura Almaida: 72.

## NANE: AINA ZA SHIRKI

Shirki ni aina mbili. **Ya kwanza**: Ni Shirki kubwa ambayo inapingana kabisa na msingi wa Tawhidi, na inamtoa mja katika Uislamu. **Ya pili**: Ni Shirki ndogo inayokinzana na Tawhidi kamilifu inayotakiwa, lakini haimtoi mja katika Uislamu.

### AINA YA KWANZA: SHIRKI KUBWA

Shirki hii ni kufanya aina yoyote ya ibada kumfanyia asiyekuwa Allah, kama kumuomba asiyekuwa Allah jambo ambalo hakuna aliwezaye isipokuwa Allah tu, au kumtegemea asiyekuwa Allah[1], au kumsujudia asiyekuwa Allah kwa namna ya kuabudu. Kasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَلَا تَدۡعُ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَا لَا يَنفَعُكَ وَلَا يَضُرُّكَۖ فَإِن فَعَلۡتَ فَإِنَّكَ إِذٗا مِّنَ ٱلظَّٰلِمِينَ﴾ يونس: ١٠٦.

*"**Na usiombe, badala ya Allah, kisichoweza kukunufaisha na kisichoweza kukudhuru. Basi ukifanya (hivyo), wewe wakati huo utakuwa miongoni mwa madhalimu (wa nafsi zao)".*** Sura Yunus: 106.

Yaani: Utakuwa miongoni mwa wenye kufanya Shirki.

Pia amesema Allah (s.w.) kuwa:

﴿وَعَلَى ٱللَّهِ فَتَوَكَّلُوٓاْ إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ﴾ المائدة: ٢٣.

***"Na mtegemeeni Allah tu ikiwa nyinyi ni wenye kuamini".*** Sura Almaida: 23. Na amesema pia kwamba***:***

﴿فَٱسۡجُدُواْۤ لِلَّهِ وَٱعۡبُدُواْ۩﴾ النجم: ٦٢.

***"Basi msujudieni Allah na mumuabudu".*** Sura Annajm: 62.

Ikiwa kuomba, kutegemea na kusujudu ni katika ibada ambazo Allah kaamrisha afanyiwe yeye tu, basi atakayezifanya kwa ajili ya Allah atakuwa ni mwenye kumpwekesha, na atakayezifanya kwa

---

(1) Sio katika kumtegemea asiyekuwa Allah mja kutumia nyenzo au kuwaomba msaada baadhi ya watu katika mambo ambayo wanayaweza.

asiyekuwa Allah atakuwa amemshirikisha.

Inaingia katika aina hii ya Shirki kubwa Shirki ya utiifu katika kuhalalisha na kuharamisha. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿ ٱتَّخَذُوٓاْ أَحۡبَارَهُمۡ وَرُهۡبَٰنَهُمۡ أَرۡبَابٗا مِّن دُونِ ٱللَّهِ وَٱلۡمَسِيحَ ٱبۡنَ مَرۡيَمَ وَمَآ أُمِرُوٓاْ إِلَّا لِيَعۡبُدُوٓاْ إِلَٰهٗا وَٰحِدٗاۖ لَّآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَۚ سُبۡحَٰنَهُۥ عَمَّا يُشۡرِكُونَ ﴾ التوبة: ٣١.

***”Wamewafanya wanazuoni wao na watawa wao miungu badala ya Allah. Na (pia wamemfanya mungu) Masia mwana wa Mariamu na ilhali hawakuamrishwa isipokuwa tu kumuabudu mungu mmoja. Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila yeye tu. Ametakasika na yale wanayomshirikisha nayo".*** Sura Attawba: 31.

Aya hii iliwateremkia Wayahudi na Wakristo ambao waliwatii wanazuoni wao na watawa wao katika kuhalalisha aliyoharamisha Allah, na kuharamisha aliyohalalisha Allah. ***"Imenukuliwa kwa Adiyu bin Hatim, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: Nilikwenda kwa Mtume (s.a.w.) na shingoni mwangu kukiwa kuna msalaba wa dhahabu. Mtume akasema: Ewe Adiyu, ondoa sanamu hili shingoni mwako, na nikamsikia anasoma katika Sura Baraa-ah:***

﴿ ٱتَّخَذُوٓاْ أَحۡبَارَهُمۡ وَرُهۡبَٰنَهُمۡ أَرۡبَابٗا مِّن دُونِ ٱللَّهِ ﴾

***Wamewafanya wanazuoni wao na watawa wao miungu badala ya Allah.*** Sura Attawba: 31. ***Akasema Mtume: Ama wao (Wayahudi na Wakristo) walikuwa hawawaabudu (wanazuoni na watawa wao), lakini walikuwa wakiwahalalishia jambo basi nao wanalihalalisha, na wakiwaharamishia basi nao wanaliharamisha”***. Hadithi hii imesimuliwa na Tirmidhy.

## AINA YA PILI: SHIRKI NDOGO

Shirki hii ni nyenzo inayompeleka mja kwenye Shirki Kubwa. Shirki Ndogo ni aina mbili: Shirki ya wazi na shirki iliyojificha.

### 1) Shirki ya Wazi:

Shirki hii inapatikana kwa kutamka na kwa vitendo. Kutamka ni

kama vile kuapa kwa asiyekuwa Allah (mtu akasema: ***"Nina'apa kwa Mtume au Nina'apa kwa Masia".*** Au mtu akasema: ***"Akitaka Allah na wewe".*** Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Atakayeapa kwa asiyekuwa Allah, basi huyo ameshakufuru au ameshirikisha".*** Hadithi hii imesimuliwa na Tirmidhy.

Na Mtume alimjibu yule mtu aliyemwambia: ***"Ewe Mjumbe wa Allah, akitaka Allah na wewe"*** **alimjibu kwamba:** ***"Je, umenifanya mwenza wa Allah? Lakini (sema:) Akitaka Allah peke yake".*** Hadithi hii imesimuliwa na Ahmad. Vitendo ni kama kuvaa hirizi au uzi kwa ajili ya kuondosha balaa, na kuwa na itikaidi kwamba hirizi na uzi huo ni sababu ya kuondosha balaa.

**2) Shirki Iliyojificha**:

Hii ni shirki ya nia na utashi, kama kufanya kwa kutaka uonekane au kujitangazia. Hali hii itapatikana kwa mtu kutomkusudia Allah katika amali yake, bali anakusudia asifiwe na watu na wamtaje vizuri. Kwa mfano: Mtu anasali na kufunga ili watu waseme kuwa: Amekuwa imara katika dini na amekuwa Muislamu mzuri. Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Jambo kubwa ninalolihofia sana kwenu ni Shirki Ndogo. (Swahaba) Wakasema: Shirki Ndogo ni ipi ewe Mjumbe wa Allah? Mtume akasema: Ni Ria (kufanya kwa kujionesha). Allah atawaambia wafanyao Shirki hii pale watu watakapopewa malipo ya amali zao Siku ya Kiyama kwamba: Nendeni kwa wale mliokuwa mkiwaonesha (amali zenu) duniani. Angalieni: Je, mtapata malipo yoyote kwao?".*** Hadithi hii imesimuliwa na Ahmad.

## TISA: UTAMBULISHO WA DHAMBI KUBWA NA TOFAUTI BAINA YAKE NA BAINA YA DHAMBI NDOGO

Madhambi na maasi yafanywayo na Muislamu yamegawika katika Madhambi Makubwa (Kabaair) na Madhambi Madogo (Swaghaair). Anasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿إِن تَجْتَنِبُوا۟ كَبَآئِرَ مَا تُنْهَوْنَ عَنْهُ نُكَفِّرْ عَنكُمْ سَيِّـَٔاتِكُمْ وَنُدْخِلْكُم مُّدْخَلًا كَرِيمًا﴾

النساء: ٣١.

"***Kama mtajiepusha na maovu makubwa mnayokatazwa,***

***tutakufutieni makosa yenu (madogo) na tutakuingizeni mahali patukufu (kabisa, napo ni Pepo)".*** Sura Annisaa: 31.

Neno (كبائر Kabaair) ni wingi wa neno Kabira (كبيرة) ambalo maana yake ni: **Kila dhambi iliyopangiwa adhabu duniani au tishio maalumu kali huko akhera.** Maana ya adhabu za duniani ni: Zile adhabu maalumu zilizowekwa. Kwa mfano: Kuuliwa kwa mwenye kuua, kumkata mkono mwizi na kumpiga bakora mzinifu. Maana ya tishio maalumu kali huko akhera ni: Tishio la kuingizwa motoni au kulaaniwa au kukasirikiwa au kuzuiwa kuingia peponi au kwamba hatopata hata harufu yake au kumuondoshea sifa ya imani na kwamba yeye si katika Waislamu, na mfano wa hayo.

Dhambi ndogo ni ile ambayo haikuwekewa adhabu maalumu hapa duniani wala tishio kali maalumu huko akhera.

## KUMI: HUKUMU YA MWENYE KUFANYA DHAMBI KUBWA

Mwenye kufanya Dhambi Kubwa, isiyokuwa Shirki au ukafiri, hatoki katika Uislamu kwa dhambi hiyo. Hapa duniani anakuwa Muislamu mwenye imani pungufu. Ni Muislamu kwa imani yake na ni fasiki (muovu) kwa dhambi yake kubwa, na huko akhera atakuwa katika utashi wa Allah. Akitaka atamsamehe na akitaka atamuadhibu. Akiadhibiwa hatokaa milele motoni, bali atatoka motoni humo kwa ile imani aliyonayo, hata kama ni chembe ndogo kabisa. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w) isemayo kuwa: ***"Atatoka motoni yeyote aliyetamka لا إله إلا الله = Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah tu na ilhali moyoni mwake kuna kheri japo kama uzito wa punje ya shairi. Na atatoka motoni yeyote aliyetamka لا إله إلا الله = Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah tu na ilhali moyoni mwake kuna kheri japo kama uzito wa punje ya ngano. Na atatoka katika moto yeyote aliyetamka لا إله إلا الله = Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah tu na ilhali moyoni mwake kuna kheri japo yenye uzito wa chembe ndogo kabisa".*** Hadithi hii imesimuliwa na Bukhari na Muslim.

## NGUZO YA PILI

## KUAMINI MALAIKA

Miongoni mwa nguzo za imani ambazo ni wajibu kwa Muislamu kuwa na itakidi nazo na imani yake haiwi sahihi isipokuwa tu kwa kuzikubali ni kuamini Malaika Watukufu. Allah anasema kuwa:

﴿لَّيْسَ ٱلْبِرَّ أَن تُوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ قِبَلَ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ وَلَٰكِنَّ ٱلْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةِ وَٱلْكِتَٰبِ وَٱلنَّبِيِّۦنَ﴾ البقرة: ١٧٧.

***"Wema sio (tu) kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi (katika kusali. Yako na mema mengine). Bali wema (hasa) ni (wa wale) wanaomuamini Allah na Siku ya Mwisho na Malaika na kitabu na Manabii".*** Sura Albaqarah: 177.

Katika mlango huu tutatoa utambulisho wa Malaika, wajibu wa kuwa na itikadi kwamba wapo, sifa zao za kimaumbile na za kimaadili, idadi yao, majina yao, nyadhifa zao, uhusiano wao na binadamu na manufaa ya kuwa na itikadi ya kuwepo kwao.

### KWANZA: UTAMBULISHO WA MALAIKA

Malaika ni viumbe miongoni mwa viumbe vya Allah. Wameumbwa kutokana na nuru, na wana uwezo wa kujibadilisha na kujigeuza. Allah amewaumba kwa ajili ya kumuabudu yeye na kutekeleza amri zake ulimwenguni. Hawamuasi Allah kwa aliyowaamrisha na wanafanya wanayoamrishwa.

Malaika ni miongoni mwa viumbe visivyoonekana kwa macho. Hatuwaoni lakini tunaamini imani thabiti isiyokuwa na shaka kwamba wapo, kwa sababu Allah ametueleza kuwepo kwao na vile vile Mtume (s.a.w.) ametueleza kuwepo kwao, jambo ambalo linatufanya tuwe na yakini ya kuwepo kwao.

### PILI: WAJIBU WA KUAMINI MALAIKA

Ni wajibu kwa Muislamu kuwa na itikadi thabiti kwamba Allah ameumba Malaika ambao ni viumbe katika viumbe vyake. Hawaendi

kinyume na amri zake na hawachoki na kumuabudu. Idadi yao ni kubwa na hakuna ajuwaye idadi yao kamili ila yeye Allah tu. Wengine wanajuilikana kwa majina na, kwa sababu hiyo, ni wajibu kuwaamini na pia kuamini majukumu yao kwa ufafanuzi. Wengine hawajuilikani kwa majina na, kwa sababu hiyo, ni wajibu kuwaamini kwa jumla. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ ءَامَنَ ٱلرَّسُولُ بِمَآ أُنزِلَ إِلَيۡهِ مِن رَّبِّهِۦ وَٱلۡمُؤۡمِنُونَۚ كُلٌّ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَمَلَٰٓئِكَتِهِۦ وَكُتُبِهِۦ وَرُسُلِهِۦ ﴾ البقرة: ٢٨٥.

“***Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake, na Waislamu (pia wameamini hayo). Wote wamemuamini Allah na Malaika wake na vitabu vyake na Mitume wake".*** Sura Albaqarah: 285.

Kuwaamini Malaika ni nguzo ya pili katika nguzo sita za Imani, kama ilivyokuja katika Hadithi ya Jibrili alipomuuliza Mtume (s.a.w.) kuhusu imani na Mtume akamjibu kwamba, imani ni: ***"Umuamini Allah na Malaika wake na vitabu vyake na Mitume wake na Siku ya Mwisho na uamini Qadari (mipango ya Allah); kheri yake na shari yake”.*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Kuamini Malaika kunabeba mambo manne:

**LA KWANZA:** Kuamini kwamba wapo.

**LA PILI:** Kuamini sifa zao, idadi yao, majina yao na kazi zao.

**LA TATU:** Kuwaweka katika daraja zao kwamba wao ni viumbe wa Allah, wanapewa amri, wanapewa majukumu, hawana uwezo wa kufanya jambo ila tu lile ambalo Allah amewawezesha kulifanya. Wao kufa ni jambo linalowezekana. Hawana sifa yoyote ya Umungu. Wao ni kama Allah alivyosema kuwa:

﴿ بَلۡ عِبَادٞ مُّكۡرَمُونَ ﴾ الأنبياء: ٢٦.

***“Bali (hao Malaika) ni waja wa Allah waliotukuzwa".*** Sura Al-anbiyaa: 26.

## TATU: SIFA ZA MALAIKA

**KWANZA: Sifa zao za kimaumbile.** Miongoni mwa sifa za kimaumbile za Malaika ni kwamba:

**1) Wameumbwa kutokana na nuru.** Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: “Wameumbwa Malaika kutokana na nuru”. Hadithi hii imepokewa na Muslim. Kwakuwa Malaika ni viumbe walioumbwa kutokana na nuru, wanadamu hawawezi kuwaona, hasa kwa sababu Allah hajayapa macho yetu uwezo wa kuona vitu vya namna hii.

**2) Maumbo yao ni makubwa:** Allah amewafanya Malaika kuwa tofauti na wanadamu na majini kwa kuwapa maumbo makubwa na yenye nguvu. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ قُوٓاْ أَنفُسَكُمۡ وَأَهۡلِيكُمۡ نَارٗا وَقُودُهَا ٱلنَّاسُ وَٱلۡحِجَارَةُ عَلَيۡهَا مَلَٰٓئِكَةٌ غِلَاظٞ شِدَادٞ لَّا يَعۡصُونَ ٱللَّهَ مَآ أَمَرَهُمۡ وَيَفۡعَلُونَ مَا يُؤۡمَرُونَ ﴾ التحريم: ٦.

***“Enyi mlioamini, jikingeni na (zikingeni) familia zenu dhidi ya moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia moto huo Malaika wakali, wenye nguvu. Hawamuasi Allah kwa amri zake na wanatenda wanayoamrishwa".*** Sura Attahrim: 6.

Na amesema Mtume (s.a.w.) kuhusu Malaika Jibrili alipomuona usiku wa Israi kwamba: ***"Nilimuona (Jibrili) alipokuwa akishuka kutoka mbinguni huku ukubwa wa umbo lake ukiwa umejaza sehemu iliopo baina ya mbingu na ardhi".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**3) UZURI WA MALAIKA:** Allah amewaumba Malaika katika sura za kupendeza. Allah amesema kuhusu Malaika Jibrili kwamba:

﴿ ذُو مِرَّةٖ فَٱسۡتَوَىٰ ﴾ النجم: ٦.

***"Mwenye umbo zuri na amekaa sawasawa".*** Sura Annajm: 6. Amesema Ibni abbas kwamba ***"Mwenye umbo zuri"*** maana ni ***"Mwenye sura nzuri".***

**4) UWEZO WA KUBADILIKA BADILIKA**. Allah amewaumba

Malaika wakiwa na uwezo wa kubadilika na kujigeuza katika sura ya binadamu, kama alivyojigeuza Jibrili alipokwenda kwa Maryam. Amesema Allah kuwa:

﴿فَأَرْسَلْنَا إِلَيْهَا رُوحَنَا فَتَمَثَّلَ لَهَا بَشَرًا سَوِيًّا﴾ مريم: ١٧.

***"Tukampelekea Malaika wetu (Jibrili) akajitokeza kwake (katika sura ya) binadamu aliye kamili".*** Sura Maryam: 17.

**5) WANA MBAWA**. Mbawa hizi zinatofautiana kwa ukubwa na idadi. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ فَاطِرِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ جَاعِلِ ٱلْمَلَٰٓئِكَةِ رُسُلًا أُو۟لِىٓ أَجْنِحَةٍ مَّثْنَىٰ وَثُلَٰثَ وَرُبَٰعَ ۚ يَزِيدُ فِى ٱلْخَلْقِ مَا يَشَآءُ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ﴾ فاطر: ١.

***"Sifa zote njema ni za Allah, muumba mbingu na ardhi, aliyewaumba Malaika kuwa wajumbe, wenye mbawa mbili mbili na (wenye mbawa) tatu tatu na (wenye mbawa) nne nne. Anazidisha katika kuumba apendavyo. Bila shaka, Allah ni mwenye uwezo wa kila kitu".*** Sura Faatir: 1.

Imenukuliwa kwa Abdallah bin Masoud, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa ***"Mtume (s.a.w.) alimuona Jibrili akiwa na mbawa mia sita"*** . Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**6) Malaika si wanawake na si wanaume.** Katika suala hili makafiri wa Kiarabu walipotoka pale walipodai kwamba Malaika ni wanawake. Allah aliwajibu kwa kauli yake isemayo kuwa:

﴿وَجَعَلُوا۟ ٱلْمَلَٰٓئِكَةَ ٱلَّذِينَ هُمْ عِبَٰدُ ٱلرَّحْمَٰنِ إِنَٰثًا ۚ أَشَهِدُوا۟ خَلْقَهُمْ ۚ سَتُكْتَبُ شَهَٰدَتُهُمْ وَيُسْـَٔلُونَ﴾ الزخرف: ١٩.

***"Na wamewafanya Malaika ambao ni waja wa (Allah) Mwingi wa rehema kuwa ni wanawake. Je, wameshuhudia kuumbwa kwao? Ushahidi wao utaandikwa na wataulizwa".*** Sura Azzukhruf: 19.

**7) Hawali, hawanywi, hawaowi na hawazaani.** Allah ametupa habari kwamba, Malaika walikwenda kwa (Mtume) Ibrahim wakiwa katika sura ya binadamu. Aliwapa chakula na wakakataa kula. Ibrahimu aliingiwa na hofu ya kuwaogopa nao wakamuekea wazi ukweli wao. Allah amesema kuwa:

﴿فَلَمَّا رَءَآ أَيۡدِيَهُمۡ لَا تَصِلُ إِلَيۡهِ نَكِرَهُمۡ وَأَوۡجَسَ مِنۡهُمۡ خِيفَةٗۚ قَالُواْ لَا تَخَفۡ إِنَّآ أُرۡسِلۡنَآ إِلَىٰ قَوۡمِ لُوطٖ﴾ هود: ٧٠.

***"(Ibrahimu) Alipo ona kuwa hawataki kula aliwashangaa na kuingiwa na hofu ya kuwaogopa. (Malaika) Walisema: Usiogope. Kwa yakini, sisi tumetumwa kwenda kwa watu wa Luti (ili kuwaangamiza) ".*** Sura Hud: 70.

Wanazuoni wamekubaliana kwamba Malaika hawaoani na hawazaani.

**8) Hawachoki na hawana uvivu.** Allah ametufahamisha kwamba Malaika wanamuabudu na kutekeleza amri zake bila ya kuchoka wala kuona uvivu. Katika hayo hawako kama walivyo binadamu. Allah Mtukufu amesema katika kutaja wasifu wao kwamba:

﴿يُسَبِّحُونَ ٱلَّيۡلَ وَٱلنَّهَارَ لَا يَفۡتُرُونَ﴾ الأنبياء: ٢٠.

***"Wanamtukuza (Allah) usiku na mchana. Hawanyong'onyei".*** Sura Al-anbiyaa: 20.

Na amesema Allah kuwa:

﴿فَإِنِ ٱسۡتَكۡبَرُواْ فَٱلَّذِينَ عِندَ رَبِّكَ يُسَبِّحُونَ لَهُۥ بِٱلَّيۡلِ وَٱلنَّهَارِ وَهُمۡ لَا يَسۡـَٔمُونَ﴾ فصلت: ٣٨.

"***Ikiwa watafanya kiburi, (basi Allah hana haja nao), kwani wale (Malaika watukufu) walioko kwa Mola wako wanamtukuza usiku na mchana nao hawafanyi kuchoka".*** Sura Fussilat: 38.

**9) Malaika wanakufa**. Hii ni katika hekima za Allah, ukamilifu wa sifa yake ya Mola, ukamilifu wa uhai wake na ukamilifu wa usimamizi wake wa kudumu wa kusimamia viumbe. Amesema Allah

Mtukufu kuwa:

﴿كُلُّ شَيۡءٍ هَالِكٌ إِلَّا وَجۡهَهُۥ﴾ القصص: ٨٨.

***"Kila kitu kitakufa isipokuwa yeye (Allah) tu".*** Sura Alqasas: 88.

Viumbe vyote vitapokufa Allah atatangaza:

﴿لِّمَنِ ٱلۡمُلۡكُ ٱلۡيَوۡمَ﴾ غافر: ١٦.

***"Ni wa nani ufalme hivi leo?".*** Atajibu:

﴿لِلَّهِ ٱلۡوَٰحِدِ ٱلۡقَهَّارِ﴾ غافر: ١٦.

***"Ni wa Allah, Mmoja, Mwenye nguvu isiyoshindwa".*** Sura Ghafir (Muumin): 16.

**PILI: Sifa zao za kitabia:** Miongoni wa sifa za malaika za kitabia ni hizi:

**1)** Wana kinga ya kutofanya dhambi. Amesema Allah kuwa:

﴿لَّا يَعۡصُونَ ٱللَّهَ مَآ أَمَرَهُمۡ وَيَفۡعَلُونَ مَا يُؤۡمَرُونَ﴾ التحريم: ٦.

***"Hawamuasi Allah kwa amri zake na wanatenda wanayoamrishwa".*** Sura Attahrim: 6.

**2)** Wanamuogopa Allah.

﴿وَيُسَبِّحُ ٱلرَّعۡدُ بِحَمۡدِهِۦ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ مِنۡ خِيفَتِهِۦ﴾ الرعد: ١٣.

***"Na radi inamtukuza (Allah) kwa kumshukuru na Malaika (pia) kwa kumuogopa".*** Sura Arrad: 13.

Allah amesema pia kuwa:

﴿وَهُم مِّنۡ خَشۡيَتِهِۦ مُشۡفِقُونَ﴾ الأنبياء: ٢٨.

***"Na wao (Malaika) kwa kumuogopa yeye (Allah) ni wanyenyekevu".*** Sura Al-anbiyaa: 28.

**3)** Hawachoki kumtaja Allah. Utajo wao mkubwa ni kutukuza.

Amesema Allah akiwaelezea Malaika kwamba:

﴿يُسَبِّحُونَ ٱلَّيۡلَ وَٱلنَّهَارَ لَا يَفۡتُرُونَ﴾ الأنبياء: ٢٠.

***"Wanatukuza usiku na mchana. Hawachoki".*** Sura Al-anbiyaa: 20.

**4)** Ni watukufu, wema. Amesema Allah kuwa:

﴿بِأَيۡدِي سَفَرَةٖ ١٥ كِرَامِۭ بَرَرَةٖ﴾ عبس: ١٥-١٦.

***"Zimo katika mikono ya mabalozi (wa Allah). Watukufu, wema".*** Sura Abasa: 15–16. Maana ya mabalozi ni kwamba, wanafikisha ujumbe wa Allah kwa Mitume wake. Maana ya watukufu na wema ni kwamba, maumbo yao ni mazuri na yenye heshima na pia tabia na maadili yao ni safi na bora.

**5) Ni wenye nidhamu katika mambo yao.** Ushahidi wa hilo ni namna walivyojipanga mstari mbele ya Mola wao. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿يَوۡمَ يَقُومُ ٱلرُّوحُ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةُ صَفّٗاۖ لَّا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنۡ أَذِنَ لَهُ ٱلرَّحۡمَٰنُ وَقَالَ صَوَابٗا﴾ النبأ: ٣٨.

***"Siku atakaposimama kwa mstari Roho na Malaika (wengine). Hawatasema (lolote) ila (tu atakayesema ni) yule ambaye (Allah) Mwingi wa rehema (amempa idhini ya kusema), na atasema yaliyo sawa”.*** Sura Annabai: 38. Roho ni Jibrili.

Imenukuliwa kwa Jabir bin Samura, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***“Kwa nini hamjipangi mstari kama wanavyojipanga Malaika? Tukasema (kumwambia Mtume kuwa): Ewe Mtume wa Allah, Malaika wanajipangaje mstari mbele ya Mola wao? (Mtume akasema): Wanakamilisha safu za mwanzo na wanashikamana katika safu"***. Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**6) Malaika wana tabia ya kuona haya.** Amesema Mtume (s.a.w.) akimuelezea Uthman bin Affan, Allah amuwiye radhi, kwamba: ***"Vipi nisimuonee haya mtu ambaye Malaika wanamuonea haya?".*** Hadithi hii imesimuliwa na Muslim.

## NNE: IDADI YA MALAIKA

Malaika ni viumbe wengi. Hakuna anayejua idadi yao isipokuwa Allah tu ambaye amewaumba. Amesema Allah kuwa:

﴿وَمَا يَعْلَمُ جُنُودَ رَبِّكَ إِلَّا هُوَ﴾ المدثر: ٣١.

***"Na hapana yeyote ajuwae majeshi ya Mola wako ila yeye tu".*** Sura Almuddath-thir: 31.

Miongoni mwa dalili zinazo onesha wingi wao ni kwamba, Malaika Jibrili, Allah amfikishie amani, alimwambia Mtume (s.a.w.) katika usiku wa Israi na Miraji pale walipopanda mbingu ya saba na kukuta huko Msikiti unaoitwa Baitul Maamur kwamba: "***Msikiti huu wa Baitul Maamur, wanasali ndani yake kila siku Malaika elfu sabini. Wakitoka hawarudi tena maisha yao"***. Hadithi hii imepokewa na Bukhariy na Muslim, na matamshi haya ni ya Bukhariy.

## TANO: MAJINA YA MALAIKA

Malaika wana majina. Majina yanayojuilikana ni machache sana. Haya hapa majina ya Malaika ambao majina yao yametajwa ndani ya Qur'ani Tukufu na ndani ya Hadithi Sahihi (Sunna) za Mtume (s.a.w.):

### 1,2) Jibrili na Mikaeli:

Amesema Allah kuwa:

﴿ قُلْ مَن كَانَ عَدُوًّا لِّجِبْرِيلَ فَإِنَّهُۥ نَزَّلَهُۥ عَلَىٰ قَلْبِكَ بِإِذْنِ ٱللَّهِ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَهُدًى وَبُشْرَىٰ لِلْمُؤْمِنِينَ ﴿٩٧﴾ مَن كَانَ عَدُوًّا لِّلَّهِ وَمَلَٰٓئِكَتِهِۦ وَرُسُلِهِۦ وَجِبْرِيلَ وَمِيكَىٰلَ فَإِنَّ ٱللَّهَ عَدُوٌّ لِّلْكَٰفِرِينَ ﴾ البقرة: ٩٧-٩٨.

***"Sema: Yeyote anayemfanyia uadui Jibrili, hakika yeye ameiteremsha (Qur'ani) moyoni mwako kwa idhini ya Allah (sio kafanya kwa kupendelea) inayosadikisha yale yaliyokuwa kabla yake, na ni mwongozo na habari njema kwa waumini. Yeyote anayemfanyia uadui Allah na Malaika wake na Mitume wake na Jibrili na Mikaeli, (anatafuta kuangamia) kwani Allah ni adui wa makafiri".*** Sura Albaqarah: 97-98.

**3) Israfil**:

Huyu ni Malaika mpulizaji parapanda.

Jibrili, Mikaeli na Israfil ni Malaika ambao Mtume (s.a.w.) alikuwa akiwataja katika dua yake anapoanza kusali sala zake za usiku. Imenukuliwa kwa Aisha, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa “Mtume alipokuwa anasimama usiku kuanza kusali alikuwa anafungua sala yake (kwa kusema kuwa):

(اللهمَّ ربَّ جبرائيل وميكائيل وإسرافيل، فاطرَ السموات والأرض، عالمَ الغيب والشهادة، أنت تحكم بين عبادك فيما كانوا فيه يختلفون، اهدني لما اختُلِفَ فيه من الحقِّ بإذنك، إنك تهدي من تشاء إلى صراط مستقيم)

***Ewe Mola wa Jibrili na Mikaeli na Israfil, Muumba wa mbingu na ardhi, Mjuzi wa Ghaibu (mambo yasiyo onekana kwa macho) 75ay a wazi. Wewe unahukumu baina ya waja wako katika yale waliyotofautiana. Kwa idhini yako, niongoze kwenye haki ambayo pamekuwepo tofauti kwa ajili yake. Kwa yakini, wewe unaongoza kwenye njia iliyonyooka".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**4) Malik:**

Ni msimamizi wa motoni. Amesema Allah Mtukufu kuhusu watu wa motoni kwamba:

﴿وَنَادَوۡاْ يَٰمَٰلِكُ لِيَقۡضِ عَلَيۡنَا رَبُّكَ﴾ الزخرف: ٧٧.

***"Na watapiga kelele (kumwambia ule Malaika (Malik) anayewaadhibu kwamba: Ewe Malik, hebu atumalize Mola wako (atupe mauti tufe ili tuepukane na haya mateso)".*** Sura Azzukhruf: 77.

**5,6) Munkar na Nakiir:**

Imethibiti katika Sunna sahihi kwamba, Malaika wawili ambao wanawauliza maiti katika makaburi yao wanaitwa Munkar na Nakiir.

**7,8) Haruti na Maruti:**

Na hao ndio aliowataja Allah SW katika kauli yake :

﴿وَٱتَّبَعُواْ مَا تَتۡلُواْ ٱلشَّيَٰطِينُ عَلَىٰ مُلۡكِ سُلَيۡمَٰنَۖ وَمَا كَفَرَ سُلَيۡمَٰنُ وَلَٰكِنَّ ٱلشَّيَٰطِينَ كَفَرُواْ

يُعَلِّمُونَ ٱلنَّاسَ ٱلسِّحْرَ وَمَآ أُنزِلَ عَلَى ٱلْمَلَكَيْنِ بِبَابِلَ هَٰرُوتَ وَمَٰرُوتَ ۚ وَمَا يُعَلِّمَانِ مِنْ أَحَدٍ حَتَّىٰ
يَقُولَآ إِنَّمَا نَحْنُ فِتْنَةٌ فَلَا تَكْفُرْ ﴾ البقرة: ١٠٢.

***"Walifuata yale mashetani walioyasimulia (wakidai kuwa yalikuwa) katika ufalme wa (Nabii) Suleiman. Na Suleiman hakukufuru, bali mashetani ndio walikufuru wakiwafundisha watu uchawi (waliokuwa wakiujua wenyewe tangu zamani), na (uchawi) uiloteremshwa kwa Malaika wawili Haruti na Maruti katika mji wa (Babil). Wala (malaika hao) hawakuwa wakimfundisha yeyote mpaka wamwambie: Hakika, sisi ni mtihani (wa kupima utiifu wenu), basi usikufuru".*** Sura Albaqara:102.

Katika muundo wa aya hii inaelekea kwamba Allah Mtukufu aliwatuma Malaika wawili hao wawe fitna (majaribu) kwa watu katika kipindi kati ya vipindi vya nyakati fulani. Kuna simulizi na hekaya nyingi zilizobuniwa kuhusu Malaika wawili hao, na lakini, hazikuthibiti kwenye Qur'ani na Sunna.

## SITA: KAZI ZA MALAIKA

Matamshi ya sheria yanaonesha kwamba Malaika wanatekeleza majukumu na kazi kubwa mbinguni na ardhini. Hakuna ajuae wingi wa kazi hizi ila Allah tu. Malaika kwa mujibu wa kazi walizopewa na Alla ni makundi mengi. Miongoni mwa makundi hayo ni hawa wafuatao:

**1) Malaika wenye kazi ya kubeba Arshi**. Arshi katika lugha ya Kiarabu ni kochi la mfalme. Vile vile lina maana ya paa la kitu. Neno hili limetolewa kutoka katika nomino "muinuko". Arshi imeitwa hivyo kwa sababu ya kuinuka kwake na kuweko kwake juu.

Makusudio yake hapa ni Arshi ya Rahmani ambayo ndio kiumbe kikubwa zaidi na kilicho juu zaidi. Arshi, ikiwa kama paa na Kuba la ulimwengu, imezizunguka mbingu na vilivyoko juu yake. Hakuna ajuae ilivyo zaidi ya Allah. Inabebwa na Malaika wanane. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَيَحۡمِلُ عَرۡشَ رَبِّكَ فَوۡقَهُمۡ يَوۡمَئِذٖ ثَمَٰنِيَةٞ﴾ الحاقة: ١٧.

*"Na Malaika wanane juu yao watabeba Arshi ya Mola wako siku hiyo"***.** Sura Alhaaqqa: 17.

**2) Malaika wenye kazi ya kufikisha Wahyi (Ufunuo).**

Wahyi ni vitabu na sheria alizoziteremsha Allah kwa Manabii na Mitume wake. Malaika mwenye jukumu hilo ni Jibrili, Allah amfikishie amani. Allah, akiielezea Qur'ani, amesema kuwa:

﴿نَزَلَ بِهِ ٱلرُّوحُ ٱلۡأَمِينُ ١٩٣ عَلَىٰ قَلۡبِكَ لِتَكُونَ مِنَ ٱلۡمُنذِرِينَ﴾ الشعراء: ١٩٣-١٩٤.

***"Ameiteremsha (hiyo Qur'ani) Malaika muaminifu (Jibrili). Juu ya moyo wako ili wewe uwe miongoni mwa waonyaji".*** Sura Ash-shuaraa: 193-194.

Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Allah Akitamka Wahyi viumbe wa mbinguni wanaisikia mbingu inatoa sauti mfano wa mnyororo unaobururwa kwenye sakafu. Hapo Malaika wanaghumiwa na kubaki katika hali hiyo mpaka anapowajia Jibrili. Akiwajia Jibrili wanazinduka na kusema: Ewe Jibrili, Mola wako kasemaje? Jibrili anajibu: (Kasema) Haki. Na wao wanasema: Haki, haki".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi.

**3) Malaika wenye kazi ya kusimamia pepo (Wasimamizi wa Pepo):**

Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَسِيقَ ٱلَّذِينَ ٱتَّقَوۡاْ رَبَّهُمۡ إِلَى ٱلۡجَنَّةِ زُمَرًاۖ حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءُوهَا وَفُتِحَتۡ أَبۡوَٰبُهَا وَقَالَ لَهُمۡ خَزَنَتُهَا سَلَٰمٌ عَلَيۡكُمۡ طِبۡتُمۡ فَٱدۡخُلُوهَا خَٰلِدِينَ﴾ الزمر: ٧٣.

***"Na waliomcha Mola wao watapelekwa peponi makundi makundi mpaka watakapoifikia (na kukuta) milango yake imekwishafunguliwa na wasimsmizi wake watawaambia: Amani iwe kwenu. Furahini, ingieni humu mkae milele".*** Sura Azzumar: 73.

**4) Malaika wenye kazi ya kusimamia moto wa Jahanamu (Wasimamizi wa Jahanamu):**

Amesema Allah kuwa:

﴿وَسِيقَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ إِلَىٰ جَهَنَّمَ زُمَرًاۖ حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءُوهَا فُتِحَتۡ أَبۡوَٰبُهَا وَقَالَ لَهُمۡ خَزَنَتُهَآ أَلَمۡ يَأۡتِكُمۡ رُسُلٞ مِّنكُمۡ يَتۡلُونَ عَلَيۡكُمۡ ءَايَٰتِ رَبِّكُمۡ وَيُنذِرُونَكُمۡ لِقَآءَ يَوۡمِكُمۡ هَٰذَاۚ قَالُواْ بَلَىٰ وَلَٰكِنۡ حَقَّتۡ كَلِمَةُ ٱلۡعَذَابِ عَلَى ٱلۡكَٰفِرِينَ﴾ الزمر: ٧١.

***"Na waliokufuru watapelekwa Jahanamu wakiwa makundi kwa makundi mpaka watakapoifikia itafunguliwa milango yake na wasimamizi wake watawaambia: Je, hawakukujieni Mitume miongoni mwenu wakikusomeeni aya za Mola wenu na kukuonyeni kukutana na siku yenu hii? Watasema: Kwa nini? (Ni kweli Mitume walitujia) ! Lakini limethibiti neno la adhabu kwa wale waliokanusha (Nao ndio sisi)”.*** Sura Azzumar 71.

**5) Malaika wenye jukumu la kuleta mvua, upepo na mawingu.**

Mwenye jukumu la mvua ni Mikaeli ambaye ana Malaika wengine wasaidizi. Allah amesema kuwa:

﴿فَٱلزَّٰجِرَٰتِ زَجۡرٗا﴾ الصافات: ٢.

***“Tena (Nina'apa) kwa wale (Malaika) wanaosukuma mawingu”.*** Sura Assaaffat: 2.

**6) Malaika mwenye kusimamia kupuliza baragumu.** Huyu ni Israfil.

Allah amesema kuwa:

﴿وَنُفِخَ فِي ٱلصُّورِ فَصَعِقَ مَن فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَن فِي ٱلۡأَرۡضِ إِلَّا مَن شَآءَ ٱللَّهُۖ ثُمَّ نُفِخَ فِيهِ أُخۡرَىٰ فَإِذَا هُمۡ قِيَامٞ يَنظُرُونَ﴾ الزمر: ٦٨.

***”Na litapigwa baragumu watoke roho waliomo mbinguni na waliomo ardhini ila yule amtakaye Allah. Tena litapigwa mara nyingine. Hapo, watasimama (watafufuka) wawe wanatazama (nini kitatokea”.*** Sura Azzumar: 68.

Na amesema Mtume (S.A.W.) kuwa: “***Vipi nitakuwa na raha na ilhali (Malaika) mwenye baragumu tayari ameliweka mdomoni***

***baragumu anasubiri idhini aamrishwe apulize?".*** Hadithi hii imepokewa na Tirmidhy.

**7) Malaika wa milima.**

Imethibiti katika Hadithi ya Bibi Aisha, Allah amuwiye radhi, katika kisa cha kutoka kwa Mtume (s.a.w.) kwenda Taif kuwalingania watu wake na wakayakataa mahubiri yake na kuwahamasisha watu wao waovu wamdhuru kwamba, Mtume (s.a.w.) alisema kuwa: "***Nikanyanyua juu kichwa changu ghafla nikajiona niko kwenye wingu lililonifunika. Nikatazama nikamuona Jibrili kwenye wingu lile. Aliniita na kuniambia: Hakika Allah amesikia kauli ya watu wako waliyokuambia na walivyokujibu, na Allah amemtuma Malaika wa milima kwako ili umuamrishe utakalo awafanye. Malaika wa milima aliniita, alinisalimia halafu akaniambia kuwa: Ewe Muhammad, kama utakavyo. Ukitaka niwabamize na milima miwili (mlima Abuqais na mlima Qaiqaan iliopo Makka). Alisema Mtume*** (s.a.w. kumwambia Malaika wa milima kuwa: usifanye hivyo kwa sababu) ***Nataraji Allah atoe katika migongo yao (vizazi vyao) wenye kumuabudu Allah pekee na wasikishirikishe naye kitu chochote".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

## SABA : UHUSIANO YA MWANADAMU NA MALAIKA

Uhusiano wa Malaika na binadamu ni mkubwa. Miongoni mwa Malaika kuna wenye kusimamia mambo ya mwanadamu akiwa katika tumbo la mama yake. Wengine wamepewa jukumu la kumlinda na kumkinga. Wengine wamepewa kazi ya kuandika matendo na mihangaiko yake. Wengine wana kazi ya kuamsha moyo wa kufanya mambo ya kheri katika nafsi yake na wengine wamepewa kazi ya kutoa roho yake wakati wa mauti yake ukifika. Ufuatao ni ufafanuzi wa hayo:

**1) Walipewa jukumu la kumsimamia mwanadamu katika tumbo la uzazi.** Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: "***Allah amempa jukumu Malaika katika mfuko wa uzazi. Anasema (Malaika wakati mbegu ya uzazi ikiingia katika mfuko wa uzazi kuwa:) Ewe Mola wangu, (sasa) ni mbegu ya uzazi. Ewe Mola wangu, (sasa) ni pande la damu. Ewe Mola wangu, (sasa) ni pande la nyama. Allah akitaka***

***kukamililsha kiumbe chake anasema Malaika kuwa: Ewe Mola wangu, (Je, awe) ni mwanaume au mwanamke? Ni mwema au muovu? Vipi riziki zake? Vipi mauti yake? Yote hayo yanaandikwa tumboni mwa mama yake".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**2) Waliopewa jukumu la kumkinga mwanadamu na kumlinda.**

Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿لَهُۥ مُعَقِّبَٰتٌ مِّنۢ بَيۡنِ يَدَيۡهِ وَمِنۡ خَلۡفِهِۦ يَحۡفَظُونَهُۥ مِنۡ أَمۡرِ ٱللَّهِ﴾ الرعد: ١١.

***"(Kila mtu) Ana (Malaika) wanaopokezana mbele yake na nyuma yake. Wanamlinda kwa amri ya Allah".*** Sura Arraad: 11. Mfasiri mkubwa wa Qur'an Abdallah Ibni abbas, Allah amuwiye radhi yeye na baba yake, amesema kwamba wanaopokezana ni Malaika wa Allah. Allah amewaweka ili kumlinda mwanadamu mbele yake na nyuma yake. Ikija Qadari (mipango) ya Allah ambayo amepanga kwamba jambo fulani limfike mwanadamu, basi Malaika hao humuacha.

**3) Waliopewa kazi ya kuhifadhi na kutunza amali za wanadamu**; kusajili amali njema na mbaya. Allah amesema kuwa:

﴿وَإِنَّ عَلَيۡكُمۡ لَحَٰفِظِينَ ١٠ كِرَامٗا كَٰتِبِينَ ١١ يَعۡلَمُونَ مَا تَفۡعَلُونَ﴾ الانفطار: ١٠-١٢.

***"Na kwa yakini kabisa, mnao wenye kutunza. Watukufu, wenye kuandika.Wanajua mnayoyatenda".*** Sura Al-infitar: 10 -12.

Allah amemuwekea kila mwanadamu Malaika wawili, wenye kuambatana na mwanadamu popote alipo, walio na jukumu la kuandika matendo na kauli zake. Allah amesema kuwa:

﴿إِذۡ يَتَلَقَّى ٱلۡمُتَلَقِّيَانِ عَنِ ٱلۡيَمِينِ وَعَنِ ٱلشِّمَالِ قَعِيدٞ ١٧ مَّا يَلۡفِظُ مِن قَوۡلٍ إِلَّا لَدَيۡهِ رَقِيبٌ عَتِيدٞ﴾ ق: ١٧-١٨.

***"Wakati wanapopokea wapokeaji (Malaika) wawili waliokaa (walioambata) kuliani (mwa mwanadamu) na kushotoni (kwake). Hatamki kauli yoyote isipokuwa tu karibu naye yupo mviziaji, aliye tayari (kuandika)".*** Sura Qaaf: 17-18. Maana ya mviziaji ni mfuatiliaji anayengojea kuandika. Maana ya waliotayari (kuandika) ni kwamba wako makini katika jukumu hilo la kuandika na hakuna neno

linalowaponyoka.

Usajili na uandishi wa Malaika wa amali za wanadamu ni jambo la uhakika na, kwa sababu hii, ndio maana amali hizo zinahifadhiwa na kutunzwa, halafu zitawasilishwa Siku ya Kiyama na kufunuliwa. Allah amesema kuwa:

﴿وَكُلَّ إِنسَٰنٍ أَلْزَمْنَٰهُ طَٰٓئِرَهُۥ فِى عُنُقِهِۦ ۖ وَنُخْرِجُ لَهُۥ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ كِتَٰبًا يَلْقَىٰهُ مَنشُورًا﴾ الإسراء: ١٣.

***"Na kila mwanadamu tumemfungia vitendo vyake shingoni mwake. Na tutamtolea Siku ya Kiyama daftari (lililoandikwa ndani yake kila jambo alilolifanya) atakalolikuta limefunuliwa. Ataambiwa:) Soma daftari lako. Nafsi yako inakutosha leo kukuhisabu (Yaani: Jipime mwenyewe na ujihukumu mwenyewe)".*** Sura Al-israa: 13-14.

**4) Wenye kuamsha vichocheo vya kutenda kheri katika nafsi za wanadamu**.

Allah amemuwekea kila mwanadamu mwambata Malaika mwenye jukumu la kumhamasisha na kumshawishi kufanya kheri. Pia amemewkea mwambata Jini mwenye jukumu la kumchochea na kumpambia kufanya maovu. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Hakuna yeyote miongoni mwenu ila amewekewa mwambata wake wa Malaika na mwambata wake wa Jini. (Swahaba) Wakasema: Hata wewe ewe Mjumbe wa Allah? (Mtume) Akasema: Hata mimi, lakini Allah amenisaidia kwenye hilo, na kwahiyo (yule mwambata Jini) amekuwa Muislamu na kwa sababu hiyo haniamrishi ila kheri tu".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**5) Waliopewa jukumu la kutoa roho za watu.**

Huyu ni Malaika wa mauti ambaye anafanya kazi ya kutoa roho za waja na baadae kuzikabidhi kwa Malaika wenzake ambao huzibeba roho hizo na kupanda nazo mbinguni kwa amri ya Allah. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿قُلْ يَتَوَفَّىٰكُم مَّلَكُ ٱلْمَوْتِ ٱلَّذِى وُكِّلَ بِكُمْ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ﴾ السجدة: ١١.

***"Sema: Anakufisheni Malaika wa mauti aliyewakilishwa kwenu, kisha mtarejeshwa kwa Mola wenu".*** Sura Assajda: 11.

Malaika wanatoa roho za makafiri na watu waovu kwa kuzing’oa na kuzivuta kwa nguvu kubwa. Ama waumini, Malaika wanatoa roho zao kwa upole na ulaini.

## NANE: MATUNDA NA FAIDA ZA KUAMINI MALAIKA

Kuamini Malaika kuna matunda na faida nyingi zikiwemo hizi zifuatazo:

**1)** Kujua utukufu wa aliyewaumba, nguvu na uwezo wake.

**2)** Kumshukuru Allah kwa kujali waja wake pale alipowawekea baadhi ya hawa Malaika wenye kuwalida, kuandika amali zao na maslahi yao mengine.

**3)** Kuwapenda Malaika na kuwaheshimu kwa sababu ya kumuabudu kwao Allah kwa njia ya ukamilifu sana na kwa sababu ya Malaika kuwaombea msamaha waumini.

## NGUZO YA TATU

## KUAMINI MITUME, Allah awafikishie amani

Hekima na rehema za Allah Mtukufu zimeamua kupeleka katika kila umma Mtume anayewabainishia sheria na njia yake, kuwaelekeza njia yake iliyonyooka. Wakati huo huo Mtume huyo akiwapa habari njema wenye kutii na kufuata njia sahihi kwamba watapata neema na thawabu nyingi, na kuwapa onyo wenye kuasi na kuiacha njia hii kwamba watapata adhabu yenye kuumiza. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَإِن مِّنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ﴾ فاطر: ٢٤.

*"Na hakuna taifa lolote ila alipita humo muonyaji".* Sura Fatir: 24.

Imekuwa hivyo kwa sababu Allah ni Hakimu Muadilifu, na ni miongoni mwa muktadha wa uadilifu wake kwamba hamuadhibu yeyote yule katika viumbe wake isipokuwa tu baada ya kumsimamishia hoja, njia kuwa bayana kwake, uongofu kuwa wazi kwake na akajua haki na batili na upotofu na uongofu. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿مَّنِ ٱهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِى لِنَفْسِهِۦ ۖ وَمَن ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۚ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا﴾ الإسراء: ١٥.

"***Anayeongoka, basi anaongoka kwa (maslahi) ya nafsi yake mwenyewe, na anayepotea, basi anapotea kwa (hasara ya) nafsi yake mwenyewe. Na nafsi haitabeba dhambi za nafsi nyengine. Na sisi si wenye kuadhibu (viumbe) mpaka tupeleke Mtume (awafahamishe yaliyo ya haki. Wakiyakataa ndipo wanapoadhibiwa)".*** Sura Al-israa: 15.

Haya yote hayatimii isipokuwa tu kwa kuletwa Mitume ambao ni mabalozi wa Allah kwa viumbe vyake, wenye kufikisha sharia za

Allah na mwongozo wake.

Kwa sababu hiyo, kuamini Mitume imekuwa wajibu mkubwa na nguzo kuu katika nguzo za imani. Imani ya mja bila ya nguzo hii haiwi sahihi.

Katika mlango huu tutajaribu kuangaza nguzo hii kubwa ambayo ni nguzo ya nne katika nguzo za kumuamini Allah. Kwa msaada wa Allah tunasema hivi:

## KWANZA: MAANA YA KUAMINI MITUME

Maana ya kuamini Mitume ni kuwa na itikadi thabiti kwamba Mitume wote wametumwa na Allah na kwamba Allah ametuma Mtume kwa kila umma atokanaye na wao akiwalingania (akiwahubiria) wamuadu Allah peke yake na kuacha kuabudu Miungu wengine. Amesema Allah kuwa:

﴿وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ﴾ النحل: ٣٦.

***"Na kwa yakini kabisa, tulimpeleka Mtume katika kila umma (akiwa na ujumbe) kwamba: Muabuduni Allah na muepukeni Taghuti".*** Sura Annahl: 36. Pia kuwa na itikadi kwamba Mitume na Manabii wote hawa ni wakweli, waadilifu, waongofu, watukufu, wachamungu, waaminifu na kwamba wamefikisha yote waliyotumwa na Allah kuyafikisha. Hawakuficha kitu, hawakubadilisha kitu, hawakupunguza herufi wala kuongeza kwa utashi wao na kwamba Mitume wako katika haki iliyo wazi.

## PILI: HUKUMU YA KUAMINI MITUME

Kuamini Mitume na Manabii wa Allah ni wajibu miongoni mwa wajibu wa dini hii na ni nguzo kubwa miongoni mwa nguzo za imani. Imani ya mja bila ya nguzo hii haiwi sahihi. Amesema Allah kuwa:

﴿آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِن رَّبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ ۚ كُلٌّ آمَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ﴾ البقرة: ٢٨٥.

***"Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola***

***wake, na Waislamu (pia wameamini hayo). Wote wamemuanini Allah na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume wake".*** Sura Albaqara: 285. Allah amefanya kuamini Mitume ni miongoni mwa nguzo za imani, ni miongoni mwa mambo mengi ambayo Mtume ameyaamini na waumini wote. Amebainisha kuwa waumini hawabaguwi Mitume kwa kuwaamini baadhi na kuacha kuwaamini wengine. Wanawaamini wote.

Allah amebainisha ndani ya kitabu chake ukafiri wa wale ambao hawaamini Manabii na Mitume, au kuwabagua kwa kuwaamini baadhi yao na kuwakataa wengine. Amesema Allah kuwa:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ يَكۡفُرُونَ بِٱللَّهِ وَرُسُلِهِۦ وَيُرِيدُونَ أَن يُفَرِّقُواْ بَيۡنَ ٱللَّهِ وَرُسُلِهِۦ وَيَقُولُونَ نُؤۡمِنُ بِبَعۡضٖ وَنَكۡفُرُ
بِبَعۡضٖ وَيُرِيدُونَ أَن يَتَّخِذُواْ بَيۡنَ ذَٰلِكَ سَبِيلًا ١٥٠ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡكَٰفِرُونَ حَقّٗاۚ﴾ النساء: ١٥٠-١٥١.

***"Hakika, wale waliomkufuru Allah na Mitume wake na wanataka kutenganisha baina ya Allah na Mitume wake na wanasema (kuwa): Wengine tunawaamini na wengine tunawakataa. Na wanataka kushika njia iliyo katikati ya hayo (si ya Kiislamu hasa wala ya kikafiri). Hao ndio makafiri wa kweli".*** Sura Annisaa: 150 -151.

Baada ya hapo Allah, akibainisha hali ya waumini, amesema kuwa:

﴿وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِٱللَّهِ وَرُسُلِهِۦ وَلَمۡ يُفَرِّقُواْ بَيۡنَ أَحَدٖ مِّنۡهُمۡ أُوْلَٰٓئِكَ سَوۡفَ يُؤۡتِيهِمۡ أُجُورَهُمۡۚ وَكَانَ
ٱللَّهُ غَفُورٗا رَّحِيمٗا﴾ النساء: ١٥٢.

***"Na wale waliomuamini Allah na Mitume wake na wasibague baina ya yeyote katika wao (bali wamewaamini wote), hao (Allah) atawapa ujira wao. Na Allah ni mwingi wa kusamehe (na) mwingi wa kurehemu".*** Sura Annisaa:152.

## TATU: IDADI YA MITUME NA MANABII

Mitume na Manabii wa Allah ni wengi. Miongoni mwao kuna ambao Allah ametutajia habari zao katika kitabu chake. Hao ni Adamu, Nuhu, Idrissa, Hudi, Saleh, Ibrahim, Ismail, Is-haq, Yakubu, Yusuf, Luti, Shuaibu, Yunus, Musa, Haroun, Iliasa, Zakariya, Yahya, Alyasaa, Dhulkifli, Daudi, Suleiman, Ayoub, Al-asbat (watoto wa Yakubu), Issa

na Muhammad ambaye ni wa mwisho wao wote. Allah awape rehema na amani wote.

Wengine hatukutajiwa habari zao. Allah amesema kuwa:

﴿وَرُسُلًا قَدۡ قَصَصۡنَٰهُمۡ عَلَيۡكَ مِن قَبۡلُ وَرُسُلًا لَّمۡ نَقۡصُصۡهُمۡ عَلَيۡكَ﴾ النساء: ١٦٤.

***"Na (tuliwapelekea wahyi) Mitume tuliokuhadithia (habari zao) zamani na Mitume ambao hatukukuhadithia (habari zao)".*** Sura Annisaa: 164.

## NNE: MANABII NA MITUME WA ALLAH NI BINADAMU

Manabii na Mitume wote hawa ni binadamu. Hawana sifa yoyote ya umungu. Kwa maana hiyo hawapaswi kuabudiwa. Hawana uwezo wa kujiletea manufaa wala madhara. Allah amesema kuhusu Mtume Nuhu kwamba:

﴿وَلَآ أَقُولُ لَكُمۡ عِندِي خَزَآئِنُ ٱللَّهِ وَلَآ أَعۡلَمُ ٱلۡغَيۡبَ وَلَآ أَقُولُ إِنِّي مَلَكٞ﴾ هود: ٣١.

***"Na (mimi) sikuambieni (kuwa) ninazo hazina za Allah, na (mimi) sijui Ghaibu, na sisemi kuwa mimi ni Malaika".*** Sura Hud: 31.

Allah amemuamrisha Mtume wake Muhammad aseme kuwa:

﴿قُل لَّآ أَمۡلِكُ لِنَفۡسِي نَفۡعٗا وَلَا ضَرًّا إِلَّا مَا شَآءَ ٱللَّهُ﴾ الأعراف: ١٨٨.

***"Sina mamlaka ya kujipa manufaa wala (kujiondolea) madhara ila tu atakapo Allah".*** Sura Al-aaraaf: 188.

Mitume na Manabii ni binadamu watukufu aliowateua Allah na kuwapa heshima ya kuwa wajumbe wake. Amesema Allah kuwa:

﴿قَالَتۡ لَهُمۡ رُسُلُهُمۡ إِن نَّحۡنُ إِلَّا بَشَرٞ مِّثۡلُكُمۡ وَلَٰكِنَّ ٱللَّهَ يَمُنُّ عَلَىٰ مَن يَشَآءُ مِنۡ عِبَادِهِۦ﴾ إبراهيم: ١١.

***"Mitume wao wakawaambia: Sisi ni binadamu kama nyinyi, na lakini, Allah anamshushia neema amtakaye katika waja wake".*** Sura Ibrahim: 11.

*** Kwa nini Mitume ni binadamu?**

Upinzani wa maadui wa Mitume wanaopinga binadamu kupewa utume ulikuwa mwingi sana. Jambo hili lilikuwa mojawapo ya sababu kubwa zilizowafanya watu wakatae kumuani Allah Mtukufu. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَمَا مَنَعَ ٱلنَّاسَ أَن يُؤْمِنُوٓا۟ إِذْ جَآءَهُمُ ٱلْهُدَىٰٓ إِلَّآ أَن قَالُوٓا۟ أَبَعَثَ ٱللَّهُ بَشَرًا رَّسُولًا﴾ الإسراء: ٩٤.

***"Na hakuna kilichowazuia watu kuamini pale mwongozo ulipowajia isipokuwa tu kule kusema: Hivi Allah amempa utume binadamu?".*** Sura Al-israa: 94.

Waliona kwamba kuwafuata Mitume, kwa sababu ni binadamu, ni jambo la aibu na ni hasara ya wazi. Amesema Allah kuwa:

﴿وَلَئِنْ أَطَعْتُم بَشَرًا مِّثْلَكُمْ إِنَّكُمْ إِذًا لَّخَٰسِرُونَ﴾ المؤمنون: ٣٤.

***"Na kama mkiwatii binadamu kama nyinyi basi wakati huo, kwa yakini, mtakuwa wenye hasara".*** Sura Almuuminuun: 34.

Wakati wa kutafakari na kuzingatia inadhihiri hekima ya Allah ya kuwafanya Mitume watokane na binadamu. Hili limefanyika kwa kuzingatia mambo mengi. Miongoni mwa mambo hayo ni haya yafuatayo:

1) Wanadamu wana uwezo mkubwa wa kuongoza na kuelekeza. Wao ndio wanaofaa kuigwa. Hekima hii inaonekana dhahiri kwa kila Mtume miongoni mwao.

2) Ugumu wa kuwaona Malaika. Hiyo inatokana na kutofautiana kwa maumbile ya Malaika na ya binadamu. Kuwasiliana na Malaika kuna shida na uzito mkubwa ambao binadamu wote hawawezi kuumudu. Imekuja katika Hadithi kwamba Mtume (s.a.w.) alikuwa anapata tabu mno wakati wa kuteremka Wahyi. Wahyi unapoteremka, rangi yake inambadilika, jasho linamtoka na mwili wake kutetemeka. Wale waliokuwa karibu naye walikuwa wakiyaona hayo. Kwa hiyo, binadamu kupewa utume imekuwa jambo la lazima ili iwe rahisi kuzungumza nao, kuwafahamu na kuchanganyika nao. Kama Allah angewapa utume Malaika hayo yasingeliwezekana.

3) Mtume haji kuleta ujumbe tu. Haji kuleta ujumbe fulani tu kutoka kwa Allah na kuondoka. Lakini anakaa na kuishi na watu ili kulea kundi la watu katika kufuata haki. Yeye mwenyewe anakuwa kigezo cha kivitendo kwa kundi hilo, na wao wanakuwa kwa upande wao ni kigezo kwa watu wengine. Ama endapo Mtume atakuwa Malaika lengo hili haliwezi kufikiwa, kwani watu watasema: *"Huyu ni Malaika na sisi ni binadamu; tuna miili, utashi na matamanio"*. Kwa sababu hiyo, watakataa kufuata maamrisho ya Mola wao na kutoa hoja kwamba binadamu hawana uwezo wa kuwafuata Malaika na kamwe hilo hawaliwezi. Hilo ni suala la Malaika ambao hawaishi katika ulimwengu huu, hawana hisia za utashi na matamanio kama walivyo binadamu. Hapa binadamu watasema: *"Vipi Allah atuletee Mtume Malaika na atutake tumfuate katika vitendo vyake? Kwa nini asitume Mtume mwanadamu kama sisi, anayehisi kama tunavyohisi, anayefikiri kama tunavyofikiri, anayehisi mahitaji yetu ya msingi na kwa mipaka ya uwezo wetu?"*. Kwa sababu hiyo, hekima za Allah zimeamua Mitume wawe binadamu.

## TANO: KUZIDIANA DARAJA BAINA YA MITUME

Mitume wanatofautiana daraja baina yao. Baadhi yao ni bora zaidi kwa Allah Mtukufu kuliko wengine. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿تِلْكَ ٱلرُّسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ﴾ البقرة: ٢٥٣.

***"Mitume hao tumewafanya bora baadhi yao kuliko wengine".*** Sura Albaqara: 253.

Mitume bora zaidi ni Nuhu, Ibrahim, Mussa, Issa na Muhammad Allah awape amani wote. Hao ndio waliotajwa ndani ya kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿وَإِذْ أَخَذْنَا مِنَ ٱلنَّبِيِّـۧنَ مِيثَٰقَهُمْ وَمِنكَ وَمِن نُّوحٍ وَإِبْرَٰهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَى ٱبْنِ مَرْيَمَ ۖ وَأَخَذْنَا مِنْهُم مِّيثَٰقًا غَلِيظًا﴾ الأحزاب: ٧.

***"Na (kumbuka) wakati tulipochukua kwa Mitume ahadi yao na kwako na kwa Nuhu na Ibrahimu na Musa na Isa Mwana wa Mariamu na tumechukua kwao ahadi nzito".*** Sura Al-ahzaab: 7.

Aliye bora zaidi kati ya Mitume hawa watano ni Muhammad na Ibrahimu, Allah awape amani. Na katika wawili hao bora zaidi ni Muhammad, Allah ampe amani. Amesema Mtume kuwa: ***"Mimi ni bora zaidi wa watoto wa Adamu Siku ya Kiyama".*** Ameipokea Hadithi hii Muslim.

## SITA: DINI YA MITUME NI MOJA NA SHERIA ZAO NI TOFAUTI

Dini ya Mitume wote ni moja ambayo ni Uislamu inayohubiri kumpwekesha Allah, kumuabudu yeye tu na kuacha kuabudu miungu wengine. Amesema Allah kuwa:

﴿وَلَقَدۡ بَعَثۡنَا فِي كُلِّ أُمَّةٖ رَّسُولًا أَنِ ٱعۡبُدُواْ ٱللَّهَ وَٱجۡتَنِبُواْ ٱلطَّٰغُوتَۖ فَمِنۡهُم مَّنۡ هَدَى ٱللَّهُ وَمِنۡهُم مَّنۡ حَقَّتۡ عَلَيۡهِ ٱلضَّلَٰلَةُۚ﴾ النحل: ٣٦.

***”Na bila shaka tulimpeleka Mtume katika kila umma (akiwa na ujumbe) kwamba: Muabuduni Allah na muepukeni Taghuti. Miongoni mwao wako ambao Allah amewaongoa, na miongoni mwao wako ambao upotofu (upotevu) umethibiti kwao".*** Sura Annahl: 36. Pia Allah amesema kuwa:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَا مِن قَبۡلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِيٓ إِلَيۡهِ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعۡبُدُونِ﴾ الأنبياء: ٢٥.

***"Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia kwamba hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila mimi tu. Basi niabuduni”.*** Sura Al-anbiyaa: 25.

Mitume wote wamekuja na dini ya Uislamu ambayo Allah hakubali dini yoyote badala yake. Amesema Allah kuwa:

﴿إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلۡإِسۡلَٰمُۗ﴾ آل عمران: ١٩.

***”Bila shaka dini (ya haki) mbele ya Allah ni Uislamu”.*** Sura Aal-imraan: 19. Kwa sababu hii, ni kosa baadhi ya watu kusema **(Dini za mbinguni)** kwakuwa dini ni moja tu, nayo ni Uislamu ambao unahubiri kumuabudu Allah pekee, na kwa Uislamu huo huo Manabii na Mitume wote wametumwa.

Tofauti baina ya Manabii na Mitume ipo katika sheria; kwa maana

ya masuala ya halali na haramu na maamrisho na makatazo. Jambo linaweza kuwa halali katika sheria ya Mtume fulani lakini likawa haramu katika sheria za Nabii mwengine. Pia jambo linaweza kukubalika katika sheria ya Nabii fulani lakini lisikubalike katika sheria ya Nabii mwengine na kadhalika.

Allah ameuwekea kila umma sheria inayowiana hali yake na wakati wake, na inayoufanya umma huo kuwa mwema na yenye dhamana ya kulinda maslahi yake. Ama itikadi ni moja tu kwa Mitume wote. Ndio maana Mtume (s.a.w.) akasema kuwa: ***"Mitume ni ndugu wa baba mmoja. Mama zao tofauti na dini yao ni moja".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Makusudio ni kwamba Manabii wote ni kama ndugu wa baba mmoja. Dini yao, ambayo ni kumpwekesha Allah, ni moja mama zao, ambao ni sheria zao, ni tofauti.

## SABA :KAZI NA MAJUKUMU YA MITUME

Mitume ni mabalozi wa Allah kwa waja wake na ni wabebaji wa Wahyi wake. Allah amewateua kwa ajili ya kazi maalumu zilizotajwa ndani ya Qur'ani na Sunna. Kazi hizo ni kama ifuatavyo:

### 1) Kufikisha ujumbe ulio wazi:

Kazi hii ndio Jukumu la msingi la Mitume. Allah amewapa utume ili kuwafikishia watu ujumbe ulioteremshwa kwao kutoka kwa Mola wao na kuufafanua kwa kauli na vitendo, kama Mtume (s.a.w.) alivyokuwa akifanya yeye na Swahaba wake. Katika Qur'ani kuna aya kumi na tatu zinazotamka kwamba jukumu la Mitume ni kufikisha ujumbe. Amesema Allah akimuamrisha Mtume wake kwamba:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلرَّسُولُ بَلِّغۡ مَآ أُنزِلَ إِلَيۡكَ مِن رَّبِّكَۖ وَإِن لَّمۡ تَفۡعَلۡ فَمَا بَلَّغۡتَ رِسَالَتَهُۥ﴾ المائدة: ٦٧.

***"Ewe Mtume, fikisha yale uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako. Na kama hutafanya, basi hukufikisha ujumbe wake".*** Sura Almaaida: 67.

### 2) Kumhubiri Allah:

Jukumu la Mitume haliishii kwenye kufikisha na kufafanua haki

peke yake. Zaidi ya hapo, Mitume wanawaita watu kukubali mahubiri yao, kuyafuata na kuyafanyia kazi kwa itikadi, kauli na vitendo. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ﴾ النحل: ٣٦.

***"Na kwa yakini kabisa, tulimpeleka Mtume katika kila umma (akiwa na ujumbe) kwamba: Muabuduni Allah na muepukeni Taghuti".*** Sura Annahl: 36. Kila Mtume aliwaambia watu wake kwamba:

﴿فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُونِ﴾ آل عمران: ٥٠.

***"Kwa hiyo, mcheni Allah na nitiini".*** Sura Aal-imraan: 50.

Mwenye kutafakari hali za Mitume na kaumu zao kama ilivyokuja ndani ya Qur'ani atatambua kiwango cha juhudi kubwa zilizofanywa na Mitume katika kulingania watu kwenye njia ya Allah. Katika hili, ikutoshe tu kusoma sura Nuh ili uone juhudi alizozifanya kwa kipindi cha miaka mia tisa na hamsini. Aliwalingania usiku na mchana, kwa siri na kwa dhahiri. Alitumia njia za kutamanisha na kuogofya, ahadi nzuri na makamio. Alijaribu kufungua akili zao na kuwaelekeza kuona dalili (za kuwepo kwa Allah) zilizomo katika ulimwengu, lakini walipinga na kukataa. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿قَالَ نُوحٌ رَّبِّ إِنَّهُمْ عَصَوْنِي وَاتَّبَعُوا مَن لَّمْ يَزِدْهُ مَالُهُ وَوَلَدُهُ إِلَّا خَسَارًا﴾ نوح: ٢١.

***"Nuhu akasema: Ewe Mola wangu, hakika wao wameniasi na wamewafuata amabo mali zao na watoto wao hawatawazidishia ila hasara tu".*** Sura Nuh: 21.

**3) Kutoa habari njema na kutoa habari za kuonya:**

Jukumu hili linafungamana na kumhubiri Allah. Mitume wanawahubiria watu kumuamini Allah na kumtii kwa kutekeleza amri zake na kuacha aliyokataza. Wakati huo huo wanawapa habari njema watiifu wafanyao ibada kwamba watapata mafanikio makubwa na maisha mazuri duniani na akhera. Pia wanawatahadhrisha wafanyao maasi na kuhalifu amri zake kwamba maisha ya dhiki duniani na

adhabu kali akhera. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَمَا نُرۡسِلُ ٱلۡمُرۡسَلِينَ إِلَّا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ﴾ الأنعام: ٤٨.

"***Na hatutumi Mitume ila tu huwa watoaji habari njema na waonyaji".*** Sura Al-an'aam: 48.

Ni katika ukamilifu wa rehema na uadilifu wa Allah kwamba amewabainishia watu aina mbali mbali za neema na aina za starehe ambazo ameziandaa kwa ajili ya waja wake wema, kama alivyobainisha aina za adhabu na maangamizo ambayo ameyandaa kwa ajili ya waja wake waasi na makafiri.

**4) Kusahihisha fikra potofu na itikadi batili:**

Allah ameumba waja wake katika maumbile salama wanaomuabudu Allah pekee bila ya kumshirikisha na kitu chochote. Lakini mashetani waliwajia, wakawapambia batili na kuwachochea fikra zenye utata upotofu mpaka wakapotea, wakenda tofauti na njia iliyonyooka na kwenda kinyume na haya maumbile salama ambayo walikuwa nayo. Kwa sababu hiyo, ikawa ni miongoni mwa rehema za Allah na fadhila zake kwamba kila inapotokea hivyo anatuma Mitume wake ili wawarudishe watu kwenye njia sahihi na iliyonyooka. Amesema Allah kuwa:

﴿كَانَ ٱلنَّاسُ أُمَّةً وَٰحِدَةً فَبَعَثَ ٱللَّهُ ٱلنَّبِيِّـۧنَ مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ﴾ البقرة: ٢١٣.

***"Watu (wote) walikuwa umma mmoja (katika dini moja ya haki aliyokuja nayo Nabii Adamu, halafu wakatofautiana). Basi Allah akawaleta Manabii wakitoa habari njema na wakitoa habari za onyo".*** Sura Albaqarah: 213. Maana ni kwamba watu walikuwa umma mmoja unaompwekesha Allah, kumuamini na kumuabudu yeye tu. Walitofautiana na hivyo Allah akatuma Mitume wenye kutoa habari njema na kuhadharisha.

Pamoja na kwamba kila Mitume alikuwa akiwahubiria watu wake kumpwekesha Allah na kuacha miungu wengine, kila Mtume alihusika na kurekebisha upotokaji uliotokea katika wakati wake na katika eneo lake. Hii ni kwa sababu upotokaji wa kuacha njia sahihi

unatofautiana kwa mujibu wa wakati na mahali. Mtume Nuhu, Allah ampe amani, aliwakataza watu wake kuabudu masanamu yaliyokuwa yameenea baina yao, na hivyo hivyo Mtume Ibrahimu. Mtume Hudi aliwakataza watu wake kujikweza na kufanya udikteta. Mtume Salehe alikataza na kupinga ufisadi katika ardhi na kuwakumbatia mafisadi. Mtume Luti ulawiti uliokuwa umeenea baina ya watu wake. Mtume Shuaibu alipambana na janga la ufisadi wa kiuchumi uliokuwa ukitendeka kwenye kupunja vipimo vya ujazo na uzito.

**5) Kuwasimamishia waja hoja:**

Allah ametuma Mitume na kuteremsha vitabu ili watu wasiwe na hoja wala udhuru Siku ya Kiyama. Amesema Allah kuwa:

﴿رُّسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى ٱللَّهِ حُجَّةُۢ بَعْدَ ٱلرُّسُلِۚ وَكَانَ ٱللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا﴾

النساء: ١٦٥.

***"Mitume watoao habari njema na watoa onyo ili watu wasiwe na hoja juu kwa Allah baada ya (kuletwa hawa) Mitume".*** Sura Annisaa: 165. Kama Allah asingepeleka Mitume kwa watu, wangekuja Siku ya Kiyama na kuzozana na Allah na kusema kuwa: Vipi unatuadhibu na kututia motoni wakati hukutuletea Mitume wa kutufikishia unayoyataka kwetu? Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَلَوْ أَنَّآ أَهْلَكْنَٰهُم بِعَذَابٍ مِّن قَبْلِهِۦ لَقَالُواْ رَبَّنَا لَوْلَآ أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولًا فَنَتَّبِعَ ءَايَٰتِكَ مِن قَبْلِ أَن نَّذِلَّ وَنَخْزَىٰ﴾ طه: ١٣٤.

***"Na lau kama tungaliwaangamiza kwa adhabu kabla ya kuja huyo (Mtume), wangesema: Ewe Mola wetu, kwanini usituletee Mtume tukazifuata aya zako kabla ya (sisi) kudhalilika hivi na kufedheheka?".*** Sura Taha: 134. Maana ni kwamba: Kama Allah angaliwaangamiza kwa adhabu, ikiwa ni malipo ya ukafiri wao, kabla ya kupelekewa Mtume wangalisema: Kwa nini hukutuletea Mtume ili tujue unachokitaka, tufuate aya zako na mfumo wa maisha uutakao? Allah, kwa rehema zake, alitaka isiwepo hoja wala udhuru kwa yeyote, ndio akatuma Mitume na kushusha vitabu. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Na hakuna yeyote anayependa udhuru zaidi***

***ya Allah. Kwa sababu hiyo, ametuma (Mitume) wenye kutoa habari njema na habari za onyo"***. Hadithi hii imepokwa na Bukhari na Muslim.

### 6) Kusimamia mambo yote ya umma na siasa zake:

Walioamini Mitume na kuwafuata wanakuwa kundi moja na umma mmoja. Umma hauwezi kusimama ila tu unapokuwa chini ya kiongozi ambaye utamtii, utampa majukumu ya kuendesha mambo yake na kuchunga maslahi yake na kuhakikisha kuwa malengo yake yanafikiwa. Mtume ndiye mtu mbora zaidi wa kutekeleza hayo. Yeye ni alama ya umma na ni kiongozi wake, katika mambo ya dini, anayeupa maelekezo ya kuelekea kwa Mola wake. Ni jambo muwafaka kwamba yeye pia awe kiongozi wa umma katika mambo ya kidunia kwa kuulinda umma dhidi ya mifarakano na kutumbia katika matatizo. Kwa hiyo, Mtume ni kiongozi bora wa kuuongoza umma na kusimamia mambo yake kwa mujibu wa mwongozo utokao kwa Allah. Anasema Allah Mtukufu kuwa:

﴿ إِنَّآ أَنزَلۡنَا ٱلتَّوۡرَىٰةَ فِيهَا هُدٗى وَنُورٞۚ يَحۡكُمُ بِهَا ٱلنَّبِيُّونَ ٱلَّذِينَ أَسۡلَمُواْ لِلَّذِينَ هَادُواْ ﴾

المائدة: ٤٤.

***"Hakika tuliteremsha Taurati yenye mwongozo na nuru. Manabii waliojisalimisha (kwa Allah walikuwa) wanawahukumu kwayo Wayahudi".*** Sura Almaida: 44. Pia amesema Allah kumwambia Mtume wake kwamba:

﴿وَأَنِ ٱحۡكُم بَيۡنَهُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ وَلَا تَتَّبِعۡ أَهۡوَآءَهُمۡ وَٱحۡذَرۡهُمۡ أَن يَفۡتِنُوكَ عَنۢ بَعۡضِ مَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ

إِلَيۡكَ﴾ المائدة: ٤٩.

***"Na hukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Allah. Na usifuate mapenzi yao ya nafsi. Na jihadhari nao wasije kukushawishi ukaacha baadhi ya yale aliyokuteremshia Allah".*** Sura Almaida: 49.

Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Wana wa Israili walikuwa wakipangiwa mambo yao na Manabii. Kila anapokufa Nabii alikuja badala yake Nabii mwengine".*** Hadithi hii imepokewa na

Bukhari na Muslim. Maana ya kupangiwa mambo yao na Mitume ni kwamba, Mitume ndio waliokuwa wakisimamia mambo yao kama viongozi na watawala wanavyofanya kwa raia.

## NANE: SIFA ZA MITUME:

Kwakuwa Mitume ni mabalozi wa Allah kwa waja wake, wakifanya kazi ya kuwafikishia ujumbe wa maamrisho na makatazo yake na Allah ndiye anayewasimamia na kuwakinga, imekuwa ni lazima wawe na sifa za kibinadamu zilzo kamilifu zinazowawezesha makusuduio ya jukumu lao kubwa la kuwaelekeza watu waelekee kwa Allah na kuwaongoza kwenye njia iliyo sawa. Mitume ni wenye sifa kamiifu za kibinadamu kwa kiwango cha juu sana. Allah mwenyewe, kwa ujuzi wake na hekima zake, amewateua. Kwa sababu hiyo, wamekuwa wenye nyoyo safi sana, tabia nzuri sana na akili kubwa sana. Allah amesema kuwa:

﴿ٱللَّهُ أَعۡلَمُ حَيۡثُ يَجۡعَلُ رِسَالَتَهُۥ﴾ الأنعام: ١٢٤.

***"Allah ndiye ajuaye zaidi mahali anapoweka ujumbe wake".*** Sura Al-an-aam: 124.

Kutokana na kwamba majukumu ya Mitume yanahitaji kuchanganyika na kujumuika na watu, wamekuwa na maumbo kamilifu sana na mazuri sana. Hakuna yeyote aliyekuwa na kasoro katika umbo lake.

Pia, kutokana na kwamba majukumu ya Mitume yanahitaji kuwa na mahusiano na tabia za wanadamu; mbaya na nzuri, wamekuwa na tabia zenye kiwango cha juu cha ukamilifu ili waweze kukabiliana na maudhi na matatizo yakatayowakuta wakati wa kutekeleza majukumu yao. Mwenye kuzingatia historia ya maisha ya Mtume (s.a.w.) atayakuta hayo yako wazi kabisa, hata pale mkewe, Aisha, Allah amuwiye radhi, alipoulizwa kuhusu tabia za Mtume alisema kuwa: ***"Tabia zake zilikuwa Qura'ni***". Hadithi hii imepokewa na Ahmad. Kadhalika Mitume wote, Allah awape amani, walikuwa ni mifano ya juu ya tabia njema.

Zaidi ya maumbo kamilifu na tabia njema za Mitume ni kwamba wao pia wanazo sifa nyingine muhimu ambazo majukumu yao

yanazihitaji kama binadamu waunganishi baina ya Allah na baina ya viumbe wake. Sifa hizi, kwa pamoja, lazima kila Mtume awe nazo. Sifa hizo ni hizi zifuatazo:

### 1) Ukweli:

Mtume lazima awe mkweli, kwa sababu yeye anafikisha ujumbe wa Allah wa dini yake na sheria zake kwa watu. Ikiwa hali halisi ni hiyo, itakuwa jambo lisilowezekana Allah kumpa utume mtu muongo. Kuna aya nyingi ndani ya Qur'ani zenye kuonesha ukweli wa Mitume, kama kauli ya Allah inayosema kuwa:

﴿وَٱذۡكُرۡ فِي ٱلۡكِتَٰبِ إِسۡمَٰعِيلَۚ إِنَّهُۥ كَانَ صَادِقَ ٱلۡوَعۡدِ وَكَانَ رَسُولٗا نَّبِيّٗا﴾ مريم: ٥٤.

'***Na mtaje katika kitabu (hiki) Ismaili. Bila shaka yeye alikuwa mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume, Nabii".*** Sura Maryam: 54. Na akasema Allah kuwa:

﴿وَٱذۡكُرۡ فِي ٱلۡكِتَٰبِ إِدۡرِيسَۚ إِنَّهُۥ كَانَ صِدِّيقٗا نَّبِيّٗا﴾ مريم: ٥٦.

***"Na mtaje Idriss katika kitabu (hiki). Bila shaka yeye alikuwa mkweli sana, Nabii".*** Sura Maryam: 56. Mtume (Muhammad) s.a.w. kabla ya kuwa Mtume alikuwa akijuilikana baina ya Waarabu kwa jina la heshima la *Mkweli Muaminifu*.

### 2) Uaminifu:

Sifa hii ni pacha wa sifa ya ukweli, kwa sababu muongo hawezi kuwa muamiinifu, kama ambavyo mtu asiyekuwa muaminifu hawezi kuwa mkweli. Ni lazima mkweli awe muaminifu na muaminifu awe mkweli. Kinyume cha uaminifu ni hiana. Ni muhali kwa Allah kumpa mtu asiyekuwa muaminifu amana ya kubeba ujumbe wake kwa watu, kwa sababu kama ingewezekana Mtume kuwa sio muaminifu angebadilisha sharia na kufanya hujuma katika sheria anazopewa na Allah. Kwa namna hiyo, yangepotea malengo ya ujumbe wa Allah, na ambayo ni kuweka hali nzuri na kutekeleza kwa vitendo maamrisho ya Allah pekee. Kwa sababu hiyo, Mitume wote wa Allah wamekuwa waaminifu.

### 3) Inteligensia:

Mtume anakuwa mtu mwenye inteligensia na busara anayetambua

kwa haraka mambo yanayojiri katika mazingira yake na kuyachukulia hatua kwa mujibu wa akili timamu na yenye busara inavyotaka. Busara na werevu ni lazima kwa Mtume ili awe na uwezo wa kuwaridhisha kwa hoja watu wenye misimamo ya wastani anaowalingania na ambao si wenye inda na inadi. Pia busara na werevu ni lazima kwa Mtume ili aweze kuondoa wasiwasi na shaka katika nafsi za anaowalingania.

**4) Kinga ya kukosea:**

Hii ni kinga ambayo Allah amewapa Mitume wake ili waepukane na kufanya makosa, shari na dhambi zisipate nafasi katika nafsi zao na ili wabaki salama na wasafi bila ya kuwa na kasoro na mapungufu tangu kupewa utume mpaka mwisho wa uhai wao. Allah amewapa kinga ya kutofanya dhambi na maasi na amewafanya wasafi. Kamwe hawafanyi dhambi kubwa, si kwa makusudi wala kwa kusahau. Pia hawakusudii kufanya dhambi ndogo. Kama itatokea kufanya dhambi ndogo wanatubu haraka bila ya kuchelewa, kwa sababu watu wameamrishwa kuwafuata na kuwaiga. Amesema Allah kuwa:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَا مِن رَّسُولٍ إِلَّا لِيُطَاعَ بِإِذۡنِ ٱللَّهِ﴾ النساء: ٦٤.

***"Na hatukumleta Mtume yeyote ila tu atiiwe kwa idhini ya Allah".*** Sura Annisaa: 64. Pia Allah amesema kuwa:

﴿لَّقَدۡ كَانَ لَكُمۡ فِي رَسُولِ ٱللَّهِ أُسۡوَةٌ حَسَنَةٞ لِّمَن كَانَ يَرۡجُواْ ٱللَّهَ وَٱلۡيَوۡمَ ٱلۡأٓخِرَ﴾ الأحزاب: ٢١.

***"Na bila shaka mnao mfano mwema (wa kuiga) kwa Mtume wa Allah kwa mwenye kumtaraji Allah na (kuitaraji) Siku ya Mwisho".*** Sura Al-ahzaab: 21. Kama ingekuwa inawezekana Mitume wafanye Dhambi Kubwa, suala la kuwaiga lisingekuwa na maana.

Pia Allah amewapa Mitume kinga ya kusahau katika kubeba ujumbe. Mitume hawasahau kitu katika yale waliyotumwa na Allah. Amesema Allah kumwambia Mtume wake Muhammad (s.a.w.) kuwa:

﴿سَنُقۡرِئُكَ فَلَا تَنسَىٰٓ﴾ الأعلى: ٦.

***"Tutakusomesha na hutasahau".*** Sura AL-aalaa: 6**.** Pia Allah amesema kuwa:

﴿وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلۡهَوَىٰٓ ۝٣ إِنۡ هُوَ إِلَّا وَحۡيٞ يُوحَىٰ﴾ النجم: ٣-٤.

***"Na hatamki kwa mapenzi ya nafsi (yake). Hayakuwa hayo (atamkayo) isipokuwa tu ni wahyi (ufunuo) unaofunuliwa (kwake)".*** Sura Annajmi: 3-4.

Pia Mitume wanayo kinga katika kufikisha ujumbe walioamrishwa na Allah kuufikisha. Wanafikisha ujumbe kama walivyoamrishwa na Allah bila ya kukosea au kuongeza au kupunguza.

## TISA: MIUJIZA YA MITUME:

Hii ni miujiza ambayo Allah ameipitisha kwa Mitume wake kwa lengo la kuthibitisha ukweli wao na hoja ya haki waliyo nayo. Kwa sababu hii Allah ameiita kwenye kitabu kuwa alama zinazo onesha ukweli wao.

Kitendo cha Allah kuwatia nguvu Mitume wake kwa miujiza kinatokana na ukamilifu wa uadilifu wake, huruma yake kwao, kupenda kwake udhuru na kusimamisha hoja kwa waja wake. Allah hakumtuma Mtume yeyote katika ila amekuja na muujiza unao onesha ukweli wake kwa yale aliyoyaeleza. Amesema Allah kuwa:

﴿لَقَدۡ أَرۡسَلۡنَا رُسُلَنَا بِٱلۡبَيِّنَٰتِ وَأَنزَلۡنَا مَعَهُمُ ٱلۡكِتَٰبَ وَٱلۡمِيزَانَ لِيَقُومَ ٱلنَّاسُ بِٱلۡقِسۡطِ﴾

الحديد: ٢٥.

***"Kwa hakika tuliwapeleka Mitume wetu kwa dalili waziwazi na tukateremsha vitabu na uadilifu pamoja nao".*** Sura Alhadid: 25**.** Na amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Hakuna Mtume yeyote katika Mitume isipokuwa tu katika miujiza amepewa miujiza ambayo mfano wake watu waliiamini. Na muujiza niliopewa mimi ni Wahyi (ufunuo) ulioshushwa na Allah kwangu. Na nataraji niwe na wafuasi wengi zaidi kuliko wao Siku ya Kiyama".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Na ni miongoni mwa hekima kubwa za Allah kwamba amefanya muujiza wa kila Mtume unaendana na mambo ya watu wake aliotumwa kwao na ambayo wameyabobea ili kuipa nguvu hoja wanayosimamishiwa na ili usiwepo udhuru. Kama muujiza wa

Mtume ungekuwa umewekwa katika jambo ambalo wale watu Mtume katumwa kwao hawalijui, huo ungekuwa udhuru kwao wa kutolitambua jambo wasilolijua. Nabii Mussa, Allah ampe amani, alipelekwa kwa watu ambao uchawi ulikuwa umeenea baina yao. Allah alimpa muujiza ambao ulizishinda nguvu za wachawi kufanya kama alivyofanya. Wachawi walipoona hali hiyo walitambua kuwa hayo sio matendo ya uchawi, bali ni muujiza wa Mungu ambao Allah amemtia nguvu kwao Nabii wake Mussa. Wachawi hawakuwa na la kufanya ila tu ni kuwa wanyenyekevu na kuamini.

Allah alipomtuma Nabii wake Issa, Allah ampe amani, kwa Bani Israili fani ya tiba ndiyo iliyokuwa imeenea baina yao. Hekima ya Allah ikawa ni kufanya miujiza yake mingi iwe katika fani ya tiba. Kupitia kwa Nabii Issa, Allah alitibu watu wenye mbalanga (barasi), vipofu na kufufua wafu. Mbalanga na upofu ni miongoni mwa maradhi sugu ambayo watu wa tiba wakati huo hawakuwa na uwezo wa kuyatibu. Allah alimpa Mtume Issa muujiza wa kuyatibu maradhi hayo kwa kugusa na dua, kwa lengo la kumpa nguvu, kusadikisha na kuwatangazia kwamba haya yanatoka kwa Allah.

Ni hivyo hivyo kwa Mtume Muhammad, Allah ampe rehema na amani. Yeye alitumwa kwa watu waliokuwa wamebobea katika lugha na fasihi, wakati yeye alikuwa hajui kusoma na kuandika. Allah alipompa utume aliuweka muujiza wake katika ufasaha wa lugha jambo ambalo Waarabu walilibobea. Allah alimpa Qur'ani na kuwapa changamoto Waarabu walete mfano wake wakashindwa. Halafu aliwapa changamoto walete sura kumi na wakashindwa. Halafu aliwapa changamoto ya kuleta mfano wa sura wakashindwa. Halafu aliwafahamisha kwamba hata kama watu wote na wakasaidiwa na majini wangekusanyika ili walete mfano wa Qur'ani hii wasingeweza kuleta mfano wake. Amesema Allah kuwa:

﴿ قُل لَّئِنِ ٱجْتَمَعَتِ ٱلْإِنسُ وَٱلْجِنُّ عَلَىٰٓ أَن يَأْتُوا۟ بِمِثْلِ هَٰذَا ٱلْقُرْءَانِ لَا يَأْتُونَ بِمِثْلِهِۦ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا ﴾ الإسراء: ٨٨.

***"Sema: Kwa yakini kabisa, kama watu (wote) na majini wangejumuika ili kuleta mfano wa hii Qur'ani basi hawataleta mfano wake hata kama watasaidiana".*** Sura Al-israa: 88.

## KUMI: WAHYI

Wahyi ni njia au namna ambayo kwayo Allah anawafikishia Mitume na Manabii wake yale anayotaka; anayoamuru na anayokataza. Haya yanafanyika kwa kupitia mambo kadhaa. Miongoni mwa mambo hayo ni haya yafuatayo:

### 1) Ndoto za usingizini:

Ndoto za Manabii ni haki na ni Wahyi utokao kwa Allah kwenda kwao. Imenukuliwa kwa Aisha, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***"Wahyi wa mwanzo kabisa ulioanza kwa Mtume ni ndoto njema ya usingizini. Alikuwa haoti ndoto ila inakuwa kweli na wazi mfano wa kupambazuka kwa asubuhi".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

### 2) Allah kuzungumza na Mitume wake nyuma ya pazia:

Hilo lilifanyika pale Allah alivyozungumza na Nabii wake Mussa, na Allah alivyozungumza na Mtume wetu Muhammad usiku wa Israi na Miraji.

### 3) Kumtumia mjumbe katika Malaika, na aghalabu ni Jibrili.

## KUMI NA MOJA: WAJIBU WETU KWA MITUME

Dini yetu tukufu imewajibisha kwa kila Muislamu haki kadhaa kuwatendea Manabii wa Allah ikiwa ni kutekeleza amri ya Allah ya kuwatukuza na kuwaheshimu, pia kukubali kwamba, kwa wao kupewa jukumu la utume na kuifafanua haki, Allah amewafanya bora zaidi kuliko viumbe wengine. Miongoni mwa haki hizo ni hizi zifuatazo:

**1) Kuwaamini Mitume wote bila ya kumbagua yeyote.** Ubaguzi unakuwa kwa kuwakubali baadhi na kuwakataa wengine, kama Wakristo walivyomuamini Issa na kumkataa Muhammad, na kama Wayahudi walivyomuamini Mussa na kamkataa Issa na Muhammad, Allah awape rehema na amani. Amesema Allah kuwa:

﴿قُولُوٓاْ ءَامَنَّا بِٱللَّهِ وَمَآ أُنزِلَ إِلَيۡنَا وَمَآ أُنزِلَ إِلَىٰٓ إِبۡرَٰهِـۧمَ وَإِسۡمَٰعِيلَ وَإِسۡحَٰقَ وَيَعۡقُوبَ وَٱلۡأَسۡبَاطِ وَمَآ أُوتِيَ مُوسَىٰ وَعِيسَىٰ وَمَآ أُوتِيَ ٱلنَّبِيُّونَ مِن رَّبِّهِمۡ لَا نُفَرِّقُ بَيۡنَ أَحَدٖ مِّنۡهُمۡ وَنَحۡنُ لَهُۥ مُسۡلِمُونَ﴾ البقرة: ١٣٦.

***"Semeni (nyinyi Waislamu kuwaambia Wayahudi na Wakristo kuwa): Tumemuamini Allah na yale yaliyoteremshwa kwetu na yale yaliyoteremshwa kwa Ibrahimu na Ismaili na Isihaka na Yakubu na kizazi (cha Yakubu) na (pia tumeamini yale) waliyopewa Mussa na Issa na pia yale waliyopewa Manabii (wengine) kutoka kwa Mola wao. Hatubagui yeyote katika hao. (Wote tunawaamini), na sisi tumenyenyekea kwake".*** Sura Albaqara: 136.

Linalopaswa kueleweka hapa ni kwamba, haifai kwa yeyote baina ya majini na wanadamu kufuata sheria za Mtume yeyote aliyepita baada ya kuletwa kwa Mtume Muhammad (s.a.w.) ambaye ametumwa kwa watu wote. Sheria za Mtume Muhammad zimekuja kuondoa na kufuta sheria zote za Manabii waliokuwepo kabla yake. Hakuna dini isipokuwa tu ile aliyotumwa kwayo Mtume Muhammad, na hakuna ufuasi isipokuwa tu wa kumfuata Mtume huyu Mtukufu. Allah amesema kuwa:

﴿وَمَن يَبۡتَغِ غَيۡرَ ٱلۡإِسۡلَٰمِ دِينٗا فَلَن يُقۡبَلَ مِنۡهُ وَهُوَ فِي ٱلۡأٓخِرَةِ مِنَ ٱلۡخَٰسِرِينَ﴾ آل عمران: ٨٥.

***"Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye hasara".*** Sura Aal-imran: 85.

Na Allah pia amesema kuwa:

﴿وَمَآ أَرۡسَلۡنَٰكَ إِلَّا كَآفَّةٗ لِّلنَّاسِ بَشِيرٗا وَنَذِيرٗا وَلَٰكِنَّ أَكۡثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعۡلَمُونَ﴾ سبأ: ٢٨.

***"Na hatukukutuma (wewe Muhammad) isipokuwa tu (ukawe Mtume) kwa watu wote, ukitoa habari nzuri na ukitoa habari za onyo, lakini watu wengi hawajui".*** Sura Sabai: 28.

**2) Kuwapenda wote, kuwaunga mkono, kuacha kuwachukia na**

**kuacha kuwafanyia uadui.** Yeyote **a**nayemchukia Nabii yeyote katika Manabii anakuwa kafiri. Amesema Allah kuwa:

﴿ مَن كَانَ عَدُوًّا لِّلَّهِ وَمَلَٰٓئِكَتِهِۦ وَرُسُلِهِۦ وَجِبۡرِيلَ وَمِيكَىٰلَ فَإِنَّ ٱللَّهَ عَدُوٌّ لِّلۡكَٰفِرِينَ ﴾ البقرة: ٩٨

*"Anayemfanyia uadui Allah na Malaika wake na Mitume wake na Jibrili na Mikaeli (anatafuta kuangamia kwani) Allah ni adui wa makafiri".* Sura Albaqara: 98.

**3) Kuwaheshimu**. Haifai kwa Muislamu kumdharau Mtume yeyote. Muislamu anapaswa kuwa na itikadi kwamba, Mitume wote wametekeleza wajibu wao na kufikisha ujumbe wa Allah kwa ukamilifu, na kwamba wamefikia daraja ya juu ya ukamilifu wa kibinadamu. Hakuna upungufu unaowatia dosari wala hakuna dosari inayowashushia hadhi. Allah, baada ya kutaja orodha ndefu ya Manabii na Mitume, amesema kuwa:

﴿ وَإِسۡمَٰعِيلَ وَٱلۡيَسَعَ وَيُونُسَ وَلُوطٗاۚ وَكُلّٗا فَضَّلۡنَا عَلَى ٱلۡعَٰلَمِينَ ﴾ الأنعام: ٨٦.

*"Na (tukamuongoa) Ismaili na Alyasaa (Elisha) na Yunusu na luti. Na wote tumewafanya bora kuliko walimwengu (wote)".* Sura Al-an-aam: 86.

**4) Kuukataa upitilizaji kiasi wa waliopitiliza kiasi katika kuwaamini Mitume**, kama Wakristo walivyopitiliza kiasi katika kumuani Masiya Issa Mwana Maryam pale walipodai kuwa yeye ni mwana wa mungu. Ilivyo ni kwamba yeye ni mja wa Allah na Mtume wake. Amesema Allah kuwa:

﴿ إِنَّمَا ٱلۡمَسِيحُ عِيسَى ٱبۡنُ مَرۡيَمَ رَسُولُ ٱللَّهِ وَكَلِمَتُهُۥٓ أَلۡقَىٰهَآ إِلَىٰ مَرۡيَمَ وَرُوحٞ مِّنۡهُ ﴾ النساء: ١٧١.

*"Ilivyo ni kwamba, Masiya Issa Mwana wa Mariyamu ni Mtume wa Allah na (ni kiumbe aliyeumbwa kwa) tamko lake alilompelekea Maryamu na ni roho iliyotoka kwake".* Sura Annisaa: 171.

**5) Kuwaombea rehema na amani.** Allah ametueleza kuwa

atabakisha sifa nzuri kwa Mitume wake na pia atabakisha kwa umma kuwaombea amani Mitume wao baada yao. Amesema Allah kuwa:

﴿وَتَرَكۡنَا عَلَيۡهِ فِي ٱلۡأٓخِرِينَ ٧٨ سَلَٰمٌ عَلَىٰ نُوحٖ فِي ٱلۡعَٰلَمِينَ﴾ الصافات: ٧٨-٧٩.

***"Na tukamuachia (sifa nzuri) kwa (watu wote) waliokuja baadaye. Amani iwe kwa Nuhu ulimwenguni kote”.*** Sura Assaaffaat: 78-79.

Allah amesema pia kuhusu Nabii Ibrahimu kwamba:

﴿وَتَرَكۡنَا عَلَيۡهِ فِي ٱلۡأٓخِرِينَ ١٠٨ سَلَٰمٌ عَلَىٰٓ إِبۡرَٰهِيمَ﴾ الصافات: ١٠٨-١٠٩.

***"Na tukamuachia (sifa nzuri) kwa (watu wote) waliokuja baadaye. Amani iwe kwa Ibrahimu”.*** Sura Assaaffaat: 108 – 109.

Na Allah amesema pia kwamba:

﴿وَسَلَٰمٌ عَلَى ٱلۡمُرۡسَلِينَ﴾ الصافات: ١٨١.

***"Na amani iwe kwa Mitume (wote)”.*** Sura Assaaffaat: 181.

**6) Kutolinganisha ubora baina yao**; iwapo hilo litafanyika kwa njia ya majigambo na kubeza haki yao. Hii ndio heshima, taadhima na itikadi kamilifu kwa Mitume. Mtume (s.a.w.) amekataza kulinganisha ubora baina ya Mitume kwa kusema kuwa: ***"Msilinganishe ubora baina ya Manabii wa Allah".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

## MUHAMMAD BIN ABDALLAH

(Allah ampe rehema na Amani)

## NABII WA MWISHO

Kumzungumzia Mtume wetu Muhammad (s.a.w.) sio kama kumzungumzia mtu mwengine. Kumzungumzia Mtume wetu Muhammad (s.a.w.) ni kumzungumzia kiumbe mtukufu sana aliyeumbwa na Allah, binadamu mkamilifu zaidi aliyetembea juu ya mgongo wa ardhi hii na Mtume bora zaidi alietumwa na Allah kwa wanadamu. Kwa sababu hiyo, yeye ni bwana wa walimwengu, kiongozi wa wachamungu, Mtume wa mwisho na kipenzi cha Mola wa viumbe.

Katika mlango huu tutajaribu kumtambulisha msomaji mpenzi sehemu ndogo tu inayohusiana na wasifu binafsi wa Mtume, maisha yake na harakati zake. Kwa uwezo wa Allah tunasema kuwa:

❖ Yeye ni Muhammad Bin Abdallah Bin Abdulmuttalib Bin Hashim Bin Abdulmanaf. Nasaba yake inaishia kwa Nabii wa Allah Ismail Bin Ibrahim, Allah awape amani. Mama yake ni Amina Binti Wahab Bin Abdimanafi Bin Zuhra. Mama yake alimzaa akiwa na umbo lililo sawa sawa, mwenye sura nzuri afya nzuri. Alizaliwa mwaka wa tembo, sawa na mwaka mia tano na sabini na moja (571) Miladiya (Tangu kuzaliwa kwa Yesu Kristo).

❖ Alizaliwa Makka na kukulia humo akiwa yatima. Baba yake alikufa huku yeye akiwa tumboni mwa mama yake. Mama yake alikufa huku yeye akiwa na umri wa miaka sita, na malezi yake yakasimamiwa na babu yake Abdulmuttalib. Baadae babu akafa, na malezi yake yakasimamiwa na ami yake Abutalib na akawa chini ya ulezi wake.

❖ Wakati wa utoto wake alifanya kazi ya kuchunga kondoo kama ilivyo kanunui ya Allah kwa Mitume wake. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Allah Hakuleta Mtume yeyote isipokuwa kwamba alichunga kondoo. Swahaba wake wakasema: Na wewe pia (ulichunga kondoo)?. Mtume akasema: Ndiyo. Nilikuwa nachunga kondoo wa watu wa Makka kwa malipo ya kiasi kadhaa cha dinari".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

Baadae Mtume alfanya biashara na kumuoa mwanamke bora mwenye busara wa kabila la Quraish Khadija Binti Khuwaylid, Allah amuwiye radhi. Alizaa naye watoto wawili wanaume ambao ni Abdallah na Kassimu ambaye Mtume amekuwa akiitwa kwa umaarufu kwalo (Abalqasim = Baba Kasiimu). Kwa upande wa watoto wa kike amezaa naye Zainab, Ruqayyah, Ummukulthum na Fatma. Ibrahim alimzaa na mama Mariya wa kabila la Kibti (Copts) ambaye alipewa zawadi na Mfalme wa Misri Muqawqis katika wakati wa utawala wake. Watoto wake wa kiume walikufa wakiwa wadogo. Ama watoto wake wanawake walikufa pia wakati wa uhai wake lakini baada ya kuwa wamekuwa wakubwa, wameolewa na wamekuwa Waislamu, isipokuwa Fatma ambaye alikufa baada ya Mtume kufa kwa miezi sita.

❖ Mtume wetu (s.a.w.) amekulia katika tabia njema na mwenendo mzuri, mpaka akajulikana baina ya watu wake kwa sifa ya ***Mkweli Muaminifu.*** Pamoja na kuwepo kwa tabia mbovu wakati wake na katika jamii yake, lakini yeye hakuwahi kufanya chochote katika tabia hizo mbovu. Hakuwahi kulewa kabisa. Pamoja na kwamba watu wake walikuwa wakiabudu mizimu na masanamu ambayo waliyaunda kwa mikono yao, wakati ambapo kuabudu masanamu lilikuwa jambo lililonea mno; kila kabila lilikuwa na sanamu lake wanaloliabudu badala ya Allah, pamoja na yote hayo, Allah alimkinga. Kamwe hakulisujudia sanamu, hakuhudhuria mkusanyiko wowote katika mikusanyiko iliyokuwa ikifanywa kwa ajili ya matambiko ya kikafiri na hajawahi kufanya jambo lolote la uchafu na uovu lililokuwa likifanywa katika kaumu yake.

❖ Tabia na maadili ya Mtume yalikuwa yanatoa ushahidi kwamba

Allah ndiye aliyemchagua na kumteua kwa ajili ya kuwaongoza watu waelekee kwa Allah, kuwarejesha katika njia iliyonyooka, kuwarejesha katika maumbile safi ambayo ni kumuabudu Allah pekee asiyekuwa na mshirika.

❖ Mtume akiwa katika umri wa miaka arubaini, Allah Mtukufu alimtuma kwake Mtendaji Muaminifu wa Wahyi Jibrili, Allah ampe amani, ili amjuilishe kwamba yeye ni Mtume wa Allah aliyetumwa kwa watu wote, amepewa jukumu la kuwahubiria watu kumuabudu Allah pekee na kuwahubiria dini ya Kiislamu ambayo Allah ameiridhia na ambayo kwayo amehitimisha ujumbe wa mbinguni. Pia alimteremshia Qur'ani ili aisome kwa watu, awaonye kwayo na ili Qur'ani hiyo iwe katiba na mwongozo wa maisha yao.

❖ Kuanzia hapo, Mtume alianza harakati za kulingania watu iwamuabudu Allah pekee na kuacha kuabudu masanamu waliyokuwa wakiyaaabudu. Alikuwa anawasomea maneno ya Allah yaliyokuwa yakiteremshwa kwake. Watu wake walimpinga, walimfanyia inda na kumuudhi. Mara walimtuhumu  kwamba ni mwendawazimu na wakati mwengine wakamtuhumu kwamba ni mchawi. Walikuwa wanawazuia watu wasimkubali na wasimfuate. Pamoja na yote hayo, baadhi ya watu walimuamini wakiongozwa na mkewe Bi Khadija, rafiki yake Abubakar na mtoto wa ami yake Ali bin Abiitalib, Allah awawiye radhi wote.  Baadae watu wakafululiza kuingia katika dini ya Allah. Hapo maudhi ya makafiri yakaongezeka. Swahaba wake walikumbana na kila aina mbaya  za maudhi na mateso mpaka baadhi yao  wakauawa. Mtume aliwaamrisha Swahaba kuhamia Madina. Baadae  yeye pia akahamia Madina. Huko Allah akampa watetezi wenye kumuunga mkono na kumnusuru yeye na dini yake mpaka Allah akampa ushindi yeye na ushindi wa dini yake. Uislamu ulienea Bara Arabu. Mji wa makka ulikombolewa. Mji wa Makka ambao ni mji wa Mtume na Mji Mtukufu wa Allah ulikombolewa. Masanamu yalivunjwa na makaburi yaliyokuwa yamechomoz yalisawazishwa na kuwekwa sawa juu ya ardhi, ikiwa ni ishara ya kufuata itikadi sahihi, kutangaza na Tawhidi (kumpwekesha Allah) na kutangazia kumalizika kwa dola ya ukafiri na ushirikina katika Bara Arabu. Amesema Ali, Allah amuwiye radhi, kumwambia Abulhayyaaj Al-

asadiy kwamba: ***"Je, unaonaje nikutume kwa yale aliyonituma mie Mtume (s.a.w.) - Ali alikuwa ametumwa kabla ya ukombozi wa Makka - kwamba: Usiache sanamu ila ulivunje, wala kaburi lililosimama ila ulisawazishe".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. Allah alimpa faraja Mtume wake kwa Uislamu kushika hatamu na Waislamu kuwa na nguvu. Allah alimfisha Mtume wake akiwa na umri wa miaka sitini na tatu. Miaka arubaini kati ya hiyo aliishi kabla ya utume na miaka ishirini na tatu aliishi akiwa Nabii na Mtume.

❖ Kwa kuja Mtume Muhammad Allah amehitimisha Mitume na Manabii. Pia kwa sharia zake amehitimisha sharia zote. Hakuna Nabii mwengine baada yake wala hakuna sharia nyingine baada sharia zake. Sharia zake zimefuta sheria zote zilizopita. Mtu yeyote hawi na imani mpaka amuamini yeye, afuate dini yake na sheria zake. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Nina'apa kwa yule ambaye nafsi ya Muhammad iko mkononi mwake kwamba, hakuna yeyote atakayenisikia katika umma huu; awe Myahudi au Mkristo halafu akafa na akawa hakuyaamini yale niliyotumwa isipokuwa kwamba atakuwa mtu wa motoni"***. Hadithi hii imepokewa na Muslim.

❖ Baada ya Mtume kufariki, Swahaba wake waliendeleza sera zake, waliendelea kufikisha ujumbe na mahubiri yake, walizikomboa nchi kwa Uislamu, waliitangaza dini ya haki mpaka ikaenea mashariki na magharibi ya dunia. Dini yake itabaki hadi mwisho wa dunia.

## BAADHI YA TABIA ZA MTUME (s.a.w.)

Mtume (s.a.w.) alikuwa na tabia, maadili na desturi nzuri na maridhawa sana kuliko watu wote. Alikuwa hivyo kabla ya utume. Je, alikuwaje baada ya utume? Na ilhali Alla anamwambia kwamba:

﴿وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ﴾ القلم: ٤.

***"Na bila shaka una tabia njema kabisa”.*** Sura Al-qalam: 4.

Kwa hakika, Allah alimfunza Mtume tabia na mafunzo hayo aliyafanya mazuri sana. Pia alimlea na malezi yake akayafanya mazuri sana. Tabia zake zilikuwa Qur'ani; anafuata maadili ya Qur'ani na kuwafunza watu wafuate maadili ya Qur'ani. Baadhi ya

tabia nzuri za Mtume ni hizi zifuatazo:

❖ Mtume alikuwa mtu mpole sana, muadilifu sana, mwenye tabia safi sana, mkarimu sana na shujaa sana kuliko watu wote. Alikuwa mnyenyekevu sana; akitengeneza viatu vyake mwenyewe, akishona nguo zake mwenyewe, akiwasaidia wake zake nyumbani, anaitikia mwaliko anaopewa na yeyote, anapokea zawadi japo iwe ndogo na anailipizia. Alikuwa akikasirika kwa ajili ya Allah, wala hakasiriki kwa ajili ya nafsi yake. Alikuwa akishinda na njaa baadhi ya wakati na kufunga jiwe tumboni kwa njaa. Alikuwa akila chakula kilichopo na hakatai kilichopo madamu ni halali. Alikuwa hakikosoi chakula; akikipenda atakila na kama hakukipenda anakiacha. Alikuwa akivaa nguo halali alizoweza kuzipata. Alikuwa akitumia usafiri uliopo; wakati mwingine akipanda farasi, wakati mwingine nyumbu, wakati mwingine punda au akienda kwa miguu bila ya kuvaa viatu. Alikuwa akikaa na wanyonge na kula pamoja na masikini. Alikuwa akiunga ndugu bila ya kubagua yupi bora. Hakuwa katili wala mkali wala mpiga makelele sokoni. Alikuwa halipizi baya kwa baya, bali alikuwa akipenda kusamehe. Alikuwa anakubali udhuru wa mwenye kumomba radhi. Alikuwa akifanya utani na hasemi ila kweli tu. Alikuwa akicheka lakini haangui kicheko. Alikuwa mwenye haya sana kuliko watu wote. Alikuwa akitembelea wagonjwa na akienda mazikoni. Alikuwa akipita peke yake baina ya adui zake bila ya mlinzi. Hamdharau fukara kwa sababu ya ufukara wake, na hamuogopi mtawala kwa sababu ya utawala wake. Miongoni mwa tabia zake ni kuanza kumsalimia anayekutana naye. Akikutana na Swahaba wake yeyote alikuwa anaanza kumpa mkono. Haji mtu yeyote na shida yake ila atamtatulia. Alikuwa akiwaita Swahaba wake kwa majina yao ya mafumbo, mfano: Ewe Baba Fulani. Hii ilikuwa ni kuonesha heshima kwao na kuzikonga nyoyo zao. Alikuwa mtu mwenye huruma sana kwa watu kuliko watu wote, mpenda kheri sana kwa watu kuliko watu wote na mwenye manufaa sana kwa watu kuliko watu wote.

❖ Alikuwa anapenda wepesi na anachukia uzito. Alikuwa hamkabili mtu kwa jambo analolichukia. Anayemuona kwa mara ya kwanza anamuogopa. Anayechanganyika naye anampenda. Alikuwa

hatumii wakati wake ila kwa ajili ya Allah pekee, au kwa ajili ya lile la lazima kwa faida ya nafsi yake. Hizi ni baadhi ya tabia zake njema. Ametukuka yule aliyemfunza, kumlea na kumpamba kwa tabia njema.

## BISHARA ZA MANABII WALIOPITA KUMBASHIRI MTUME

❖ Qur'anI imetuelezea bishara za Mitume waliotangulia kubashiri utume wa Mtume (s.a.w.) na kwamba utajo wake umo katika vitabu vilivyotangulia. Miongoni mwa maelezo hayo ni kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿وَإِذۡ أَخَذَ ٱللَّهُ مِيثَٰقَ ٱلنَّبِيِّـۧنَ لَمَآ ءَاتَيۡتُكُم مِّن كِتَٰبٖ وَحِكۡمَةٖ ثُمَّ جَآءَكُمۡ رَسُولٞ مُّصَدِّقٞ لِّمَا مَعَكُمۡ لَتُؤۡمِنُنَّ بِهِۦ وَلَتَنصُرُنَّهُۥۚ قَالَ ءَأَقۡرَرۡتُمۡ وَأَخَذۡتُمۡ عَلَىٰ ذَٰلِكُمۡ إِصۡرِيۖ قَالُوٓاْ أَقۡرَرۡنَاۚ قَالَ فَٱشۡهَدُواْ وَأَنَا۠ مَعَكُم مِّنَ ٱلشَّٰهِدِينَ﴾ آل عمران: ٨١.

*"**Na (kumbukeni) Allah alipochukua ahadi kwa Manabii (akawaambia kuwa): Nikishakupeni kitabu na hekima, kisha akakujieni Mtume msadikishaji wa yale mliyo nayo (kwamba) ni juu yenu kumuamini na kumsaidia. Akasema (Allah): Je, mmekiri na kushika agizo langu juu ya hayo?. Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na mimi pamoja nanyi ni katika mashahidi".*** Sura Al-imraan: 81. Aya hii inatoa ushahidi, kama walivyosema baadhi ya wanazuoni, kwamba Allah amechukua ahadi kwa kila Nabii kwamba akiletwa Nabii Muhammad katika wakati wa uhai wake atamfuata na kuacha sheria zake ili afuate sheria za Muhammad. Hii ni dalili kwamba jina la Muhammad limetajwa na Manabii wote waliotangulia.

❖ Amesema Allah kuhusu Mtume Muhammad, na hapo ni katika mnasaba wa kuwazungumzia watu wa Mtume Mussa, kwamba:

﴿وَٱكۡتُبۡ لَنَا فِي هَٰذِهِ ٱلدُّنۡيَا حَسَنَةٗ وَفِي ٱلۡأٓخِرَةِ إِنَّا هُدۡنَآ إِلَيۡكَۚ قَالَ عَذَابِيٓ أُصِيبُ بِهِۦ مَنۡ أَشَآءُۖ وَرَحۡمَتِي وَسِعَتۡ كُلَّ شَيۡءٖۚ فَسَأَكۡتُبُهَا لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ وَيُؤۡتُونَ ٱلزَّكَوٰةَ وَٱلَّذِينَ هُم بِـَٔايَٰتِنَا يُؤۡمِنُونَ ١٥٦ ٱلَّذِينَ يَتَّبِعُونَ ٱلرَّسُولَ ٱلنَّبِيَّ ٱلۡأُمِّيَّ ٱلَّذِي يَجِدُونَهُۥ مَكۡتُوبًا عِندَهُمۡ فِي ٱلتَّوۡرَىٰةِ

وَٱلۡإِنجِيلِ يَأۡمُرُهُم بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَيَنۡهَىٰهُمۡ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيۡهِمُ ٱلۡخَبَٰٓئِثَ وَيَضَعُ عَنۡهُمۡ إِصۡرَهُمۡ وَٱلۡأَغۡلَٰلَ ٱلَّتِي كَانَتۡ عَلَيۡهِمۡۚ فَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِهِۦ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَٱتَّبَعُواْ ٱلنُّورَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ مَعَهُۥٓ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ ﴾ الأعراف: ١٥٦-١٥٧.

*"Na tuandikie mazuri katika dunia hii na katika akhera. Sisi tumerejea kwako. Akasema (Allah): Adhabu yangu nitamfikishia nimtakaye (katika wabaya hawa na wabaya wengineo. Hakuna wa kunizuia). Na rehema yangu imekienea kila kitu. Tutaandika wapate neema hiyo wale wenye uchamungu na wanaotoa zaka na wanaoziamini aya zetu. Ambao wanamfuata Mtume Nabii asiyejua kusoma na kuandika ambaye wanamkuta ameandikwa kwao katika Taurati na Injili, ambaye anawaamrisha kutenda mema na anawakataza kufanya yaliyo mabaya na anawahalalishia vitu vizuri na anawaharamishia vitu vibaya na anawaondolea ahadi zao (nzito) na minyororo iliyokuwa juu yao (yaani sheria ngumu za zamani na mila za kikafiri). Basi wale waliomuamini yeye (Mtume Muhammad) na wakamtukuza na wakamnusuru na wakaifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye (yaani Qur'ani) hao ndio wenye kufaulu".* sura al-aaraf: 156-157.

❖ Allah ametuambia kwamba Issa, Allah ampe amani, alimbashiri Mtume wetu Muhammad pale Allah aliposema kuwa:

﴿ وَإِذۡ قَالَ عِيسَى ٱبۡنُ مَرۡيَمَ يَٰبَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ إِنِّي رَسُولُ ٱللَّهِ إِلَيۡكُم مُّصَدِّقٗا لِّمَا بَيۡنَ يَدَيَّ مِنَ ٱلتَّوۡرَىٰةِ وَمُبَشِّرَۢا بِرَسُولٖ يَأۡتِي مِنۢ بَعۡدِي ٱسۡمُهُۥٓ أَحۡمَدُۖ فَلَمَّا جَآءَهُم بِٱلۡبَيِّنَٰتِ قَالُواْ هَٰذَا سِحۡرٞ مُّبِينٞ ﴾ الصف: ٦.

*"Na (wakumbushe) aliposema (Nabii) Issa Bin Mariyamu (kuwaambia Wayahudi kwamba): Enyi Wana wa Israili, mimi ni Mtume wa Allah kwenu, nisadikishaye Taurati iliyokuepo kabla yangu, na nikitoa habari njema ya Mtume atakayekuja baada yangu ambaye jina lake litakuwa Ahmad. (Lakini) Alipowajia kwa hoja zilizo wazi, walisema kuwa: Huu ni uchawi ulio dhahiri".* Sura Assaff: 6. **Ahmad** ni miongoni mwa majina ya Mtume wetu Mohammad kama ilivyothibiti kunukuliwa kwa Jubeir Bin Mut-am akisema kuwa, nilimsikia Mtume (s.a.w.) akisema kwamba: ***"Mimi ni mwenye majina mengi. Mimi ni Muhammad na mimi ni Ahmad***

***na mimi ni Almaahiy (Mfutaji) ambaye Allah anafuta kupitia kwangu kufuru na mimi ni Alhaashir (Mkusanyaji) ambaye watu watakusanywa kati ya miguu yangu na mimi ni Al-aaqib (Mhitimishaji) ambaye hakuna (Mtume) mwengine baada yake ".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

❖ Imethibiti kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Mimi kwa Allah niliandikwa kuwa ni Nabii wa Mwisho wakati (Nabii) Adamu bado akiwa katika umbile lake la udongo. Na nitakuhadithieni mwanzo wa hayo: Dua ya baba yangu Ibrahimu na bishara njema ya Issa (juu ya kuja kwangu) na ndoto ya mama yangu ambayo ameiota usingizini aliponizaa kwamba imetoka kwake nuru iliyo angaza majumba ya Sham".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad na Ibnihibban.

❖ Umekuja wasifu wa Mtume katika Torati. Imenukuliwa kwa Ataa Bin Yasaar akisema kuwa: ***"Nilikutana na Abdallah Bin Amri Bin Al-aas nikamwambia: Hebu nipe wasifu wa Mtume wetu (s.a.w.) katika Torati. Akasema: Sawa, nina'apa kwa Allah kuwa (Mtume Muhammad) ametajwa ndani ya Torati kwa baadhi ya sifa zake kama zilivyo ndani ya Qur'ani: Ewe Mtume, sisi tumekutuma ukawe mtoaji habari njema na mtoaji habari za onyo na kinga kwa (Waarabu) wasiojua kusoma na kuandika (dhidi ya kila mabaya). Wewe ni mja wangu na Mtume wangu. Nimekuita Mutawakkil (Mtegemaji Allah). Wewe si mbabe wala katili na wala hupigi makelele sokoni. Wala hurudishi baya kwa baya, lakini unasamehe. Wala Allah hamuondoshi (Mtume) duniani mpaka asahihishe kupitia kwake dini iliyopinda kwa (watu) kusema: Laa Ilaaha Illallaah = Hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah tu. Na kwa Tamko hilo atayafunua macho yaliopofoka na masikio yaliyoziba na nyoyo zilizofunikwa".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari. Kuna bishara nyingine nyingi mbali ya hizi zenye kubashiri kuja kwa Mtume (s.a.w.).

❖ Bishara hizi zilikuwa zimeenea kabla ya kuja kwa Mtume (s.a.w.). Waliokuwa wakizieneza bishara hizi ni Wayahudi na Wakristo ambao ni Ahlilkitaab wakidai kwamba watamfuata atakapokuja. Lakini

kwa masikitiko alipokuja na ujumbe wake, wakaumjua na kuuona wasifu wake kama ulivyokuja vitabuni mwao walimkufuru, walimkadhibisha na kumpiga vita. Allah amesema kuwa:

﴿ وَلَمَّا جَآءَهُمۡ كِتَٰبٞ مِّنۡ عِندِ ٱللَّهِ مُصَدِّقٞ لِّمَا مَعَهُمۡ وَكَانُواْ مِن قَبۡلُ يَسۡتَفۡتِحُونَ عَلَى ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ فَلَمَّا جَآءَهُم مَّا عَرَفُواْ كَفَرُواْ بِهِۦۚ فَلَعۡنَةُ ٱللَّهِ عَلَى ٱلۡكَٰفِرِينَ﴾ البقرة: ٨٩.

***"Na kilipowafikia (wakati wa nabii Muhammad hiki) kitabu kitokacho kwa Allah kisadikishacho yaliyo pamoja nao (walikadhibisha) na zamani walikuwa wakiwafungulia makafiri (habari ya Mtume huyu). lakini yalipowajia yale waliyokuwa wakiyajua waliyakataa. Basi laana ya Allah iwe kwa makafiri (hao)".*** Sura Albaqara: 89. Haya yametokea wakati ambapo watu wengi wa mji wa Madina walifaidika na bishara hizi baada ya kuzisikia kwa Ahlulkitaab. Walipozisikia tu walikimbilia kumuamini Mtume na kumfuata na wakatusimulia habari za Wayahudi kuhusu bishara hizi kabla ya kuja kwa Mtume.

## MIUJIZA YA MTUME:

❖ Allah aliwapa nguvu Mitume wake kwa alama na miujiza. Miujiza ni mambo yaliyo kinyume na kawaida anayapitisha Allah kwa Mitume ili kuwathibitisha ukweli wao na kuwapa nguvu na ili miujiza hiyo iwe ushahidi wa haki waliyokuja nayo. Hakuna Mtume yeyote katika Mitume wa Allah isipokuwa kwamba Allah amempa miujiza inayo onesha ukweli wao. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Hakuna Mtume yeyote katika Mitume isipokuwa tu katika miujiza amepewa miujiza ambayo mfano wake watu waliiamini. Na muujiza niliopewa mimi ni Wahyi (ufunuo) ulioshushwa na Allah kwangu. Na nataraji niwe na wafuasi wengi zaidi kuliko wao Siku ya Kiyama".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

❖ Mtume wetu ana fungu la kutosha la alama na miujiza hii. Allah alimpa Mtume miujiza mingi yenye kuonesha ukweli wake na kwamba yeye ametumwa na Allah. Miongoni mwa miujiza hiyo ni kama ifuatavyo:

**1) Qur-ani Tukufu**. Hiki ni kitabu cha Allah cha milele kisichoweza kupotoshwa wala kubadilishwa. Allah amesema kuwa:

﴿وَإِنَّهُۥ لَكِتَٰبٌ عَزِيزٌ ۝ لَّا يَأْتِيهِ ٱلْبَٰطِلُ مِنۢ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِۦ ۖ تَنزِيلٌ مِّنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ﴾ فصلت: ٤١-٤٢.

***"Na hicho ni kitabu kihishimiwacho. Batili haikifii mbele yake wala nyuma yake. Ni uteremsho utokao kwa mwenye hekima, ahimidiwaye".*** Sura Fussilat: 41- 42.

Mtume, kwa kutumia kitabu hiki, aliwapa changamoto Waarabu fasaha - amabo fasihi na uhodari wa kuzungumza yalikuwa mambo waliyoyabobea - kwamba walete mfano wa Qur'ani wakashindwa au walete baadhi ya aya wakashindwa. Halafu aliwaambia kuwa hata kama watajumuika Majini na wanadamu ili walete mfano wa Qur'ani wasingeweza. Allah amesema kuwa:

﴿قُل لَّئِنِ ٱجْتَمَعَتِ ٱلْإِنسُ وَٱلْجِنُّ عَلَىٰٓ أَن يَأْتُوا۟ بِمِثْلِ هَٰذَا ٱلْقُرْءَانِ لَا يَأْتُونَ بِمِثْلِهِۦ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا﴾ الإسراء: ٨٨.

***"Sema: Kwa yakini kabisa, kama watu (wote) na majini wangejumuika ili kuleta mfano wa hii Qur'ani basi hawataleta mfano wake hata kama watasaidiana".*** Sura Al-israa: 88.

**2)** Na miongoni mwa miujiza mikubwa ya Mtume (s.a.w.) ni msafara wa Israi na Miraji. Allah amesema kuwa:

﴿سُبْحَٰنَ ٱلَّذِىٓ أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِۦ لَيْلًا مِّنَ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ إِلَى ٱلْمَسْجِدِ ٱلْأَقْصَا﴾ الإسراء: ١.

***"Utukufu ni wa (Allah) ambaye alimpeleka mja wake usiku (mmoja tu) kutoka Msikiti Mtukufu (wa Makka) mpaka Msikiti wa Al-aqsaa (uliopo Palestina)".*** Sura Al-israa:1. Jibrili alimchukua Mtume na kuondoka naye usiku wakiwa wamepanda mnyama aliyeitwa Buraq kutoka Msikiti Mtukufu wa Makka hadi Msikiti Mtukufu wa Al-aqsaa. Huko Allah alimkusanyia Mtume Manabii na kuwasalisha huku yeye akiwa imamu. Halafu Jibrili alipanda na Mtume kwenda mbingu za juu. Walizivuka mbingu zote hadi kufikia mahali panapoitwa Sidrat Muntaha na kuona mambo makubwa. Miongoni mwa mbambo hayo ni: Kumuona Jibrili akiwa katika umbile lake halisi aliloumbiwa, kuzungumza na Mola wake, kusogezwa karibu ya allah na kufaradhishiwa sala tano. Amesema Allah kuwa:

﴿ أَفَتُمَٰرُونَهُۥ عَلَىٰ مَا يَرَىٰ ﴿١٢﴾ وَلَقَدْ رَءَاهُ نَزْلَةً أُخْرَىٰ ﴿١٣﴾ عِندَ سِدْرَةِ ٱلْمُنتَهَىٰ ﴿١٤﴾ عِندَهَا جَنَّةُ ٱلْمَأْوَىٰٓ ﴿١٥﴾ إِذْ يَغْشَى
ٱلسِّدْرَةَ مَا يَغْشَىٰ ﴿١٦﴾ مَا زَاغَ ٱلْبَصَرُ وَمَا طَغَىٰ ﴿١٧﴾ لَقَدْ رَأَىٰ مِنْ ءَايَٰتِ رَبِّهِ ٱلْكُبْرَىٰٓ ﴾ النجم: ١٢-١٨.

***"Je, Mnabishana naye juu ya yale anayoyaona?. Na kwa yakini (Mtume) alimuona (Jibrili) mara nyingine (kwa sura yake ya Kimalaika katika usiku wa Miraji). Kwenye Sidrat Muntaha (Mkunazi wa Kumalizia). Karibu yake kuna hiyo bustani (pepo) itayokaliwa (maisha na hao watu wema). Kilipoufunika Mkunazi huo kilichoufunika (katika mambo ya kiajabu ya kimbinguni). Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka (uliowekwa). Kwa yakini, (Nabii Muhammad) aliona baadhi ya alama kubwa (miujiza mikubwa) za Mola wake".*** Sura Annajm: 12-18. Halafu alirudi Makka. Safari yote hii ilichukua sehemu tu ya usiku. Hakika Allah ni muweza wa kila kitu.

**3)** Miongoni mwa miujiza ya Mtume ni kuponya wagonjwa. Haya yametokea kwa Swahaba kadhaa. Miongoni mwao ni Ali Bin Abitalib katika vita vya Khaibar. Mtume alimuulizia Ali ili ampe bendera na Swahaba wakamwambia Mtume kuwa Ali anaumwa na macho. Mtume alimuita Ali na kutabana katika macho yake na kwa idhini ya Allah alipona na kunyanyuka palepale kama vile hakuwa akiumwa. Kuna miujiza mingine mingi ya Mtume ambayo Allah amemtia nguvu Mtume wake kwa miujiza hiyo kwa ajili ya kumuunga mkono, kuthibitisha ukweli wake na kumnusuru.

## SIFA MAHUSUSI ZA MTUME

Allah amempa Mtume wetu Muhammad (s.a.w.) ubora na sifa nyingi mahususi ambazo, kwa sifa hizo, amemfanya bora zaidi kuliko Mitume wengine na kumfanya awe tofauti na watu wengine. Mtume (s.a.w.) ameielezea tunu na neema hii ya Allah kwa kusema kuwa: ***"Nimepewa mambo matano ambayo hajapewa Mtume yeyote kabla yangu".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Katika nukuu nyingine imepokewa kwamba Mtume amesema kuwa: ***"Nimefanywa bora zaidi kuliko Manabii (wengine) kwa mambo sita…".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. Na katika mapokezi mingine imenukuliwa kwamba Mtume amesema kuwa: ***"Nimepewa mambo ambayo***

***hakupewa Mtume yeyote".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad. Katika maelezo yafuatayo tutataja baadhi ya sifa hizi mahususi:

**1) Ujumbe wake unawahusu watu wote na majini wote.** Ni lazima watu na majini wamfuate Mtume na wauamini ujumbe wake. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَمَآ أَرْسَلْنَٰكَ إِلَّا كَآفَّةً لِّلنَّاسِ بَشِيرًا وَنَذِيرًا﴾ سبأ: ٢٨.

***"Na hatukukutuma wewe ila tu kwa watu wote, ukiwa mtoaji wa habari njema na muonyaji".*** Sura Sabai: 28. Pia Allah amesema kuwa:

﴿تَبَارَكَ ٱلَّذِى نَزَّلَ ٱلْفُرْقَانَ عَلَىٰ عَبْدِهِۦ لِيَكُونَ لِلْعَٰلَمِينَ نَذِيرًا﴾ الفرقان: ١.

***"Ametukuka aliyeteremsha Qur'ani kwa mja wake ili awe muonyaji kwa walimwengu (wote)".*** Sura Alfurqan: 1.

❖ Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Nimepewa mambo matano ambayo hajapewa Mtume yeyote kabla yangu. Nabii alikuwa anatumwa kwa watu wake tu, na (lakini mimi) nimetumwa kwa watu wote".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Pia Mtume amesema kuwa: ***"Nina'apa kwa yule ambaye nafsi ya Muhammad iko mkononi mwake kwamba, hakuna yeyote atakayenisikia katika umma huu; awe Myahudi au Mkristo halafu akafa na akawa hakuyaamini yale niliyotumwa isipokuwa kwamba atakuwa miongoni mwa watu wa motoni"***. Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**2) Yeye ni Nabii na Mtume wa Mwisho. Hakuna Mtume mwengine baada yake.** Allah amesema kuwa:

﴿مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَآ أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رَّسُولَ ٱللَّهِ وَخَاتَمَ ٱلنَّبِيِّۦنَ﴾ الأحزاب: ٤٠.

***"Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu na lakini yeye ni Mtume wa Allah na Mwisho wa Mitume".*** Sura Al-ahzaab: 40**.** Na Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Kwa yakini kabisa, mfano wangu na mfano wa Manabii waliokuwepo kabla yangu ni mfano wa mtu aliyejenga nyumba na kuitengeneza vizuri isipokuwa mahali pa tofali moja pembeni. Watu wakawa wanaizunguka nyumba ile, wanaishangaa na kusema: Si ingekuwa vyema lingejengwa tofali hili? Akasema (Mtume kuwa:) Mimi ndio tofali hilo na mimi ndiye***

***Nabii wa mwisho".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**3) Umma wake ni umma bora zaidi na watu wake ni wengi zaidi peponi.** Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ ﴾

آل عمران: ١١٠.

***"(Nyinyi) Mmekuwa umma bora zaidi kuliko umma zote zilizodhihirishwa kwa watu; mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu na mnamuamini Allah".*** Sura Al-imraan: 110. Imenukuliwa kwa Abdallah Bin Masoud, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***"Tulikuwa na Mtume (s.a.w.) katika hema, akasema: Je, mnaridhia muwe robo ya watu wa peponi? Tukasema: Naam. Akasema: Je, mnaridhia muwe theluthi ya watu wa peponi? Tukasema: Naam. Akasema: Je, mnaridhia muwe nusu ya watu wa peponi? Tukasema: Naam. Akasema: Nina'apa kwa (Allah) ambaye nafsi ya Muhammad iko mkononi mwake kwamba, hataingia peponi ila mtu Muislamu, na nyinyi kulinganisha na makafiri ni kama unywele mweupe kwenye ngozi ya ngo'mbe mweusi au unywele mweusi kwenye ngozi ya ngo'mbe mweupe".*** Ameipokea Hadithi hii Bukhariy na Muslim.

**4) Yeye ni bora zaidi katika watoto wa Adamu Siku ya Kiyama**. Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa, amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Mimi ni bwana wa watoto wa Adamu Siku ya Kiyama, na ni wa mwanzo ambaye kaburi lake litajipasua (ili nitoke) na ni muombezi wa mwanzo na ni wa mwanzo katika watakaokubaliwa uombezi wao"***. Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**5) Yeye ndiye mtu wa Maombezi Makubwa (Shafaa'a) Siku ya Kiyama** pale atakapowaombea watu wahukumiwe na Mola wao. Hilo litatokea baada ya kuwa Mitume bora wameomba wasipewe jukumu hilo. Hiyo ndio hadhi kubwa iliyotajwa katika kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿ وَمِنَ ٱلَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِۦ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰٓ أَن يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴾ الإسراء: ٧٩.

***"Na katika usiku jiondoshee usingizi (kidogo) kwa (kusoma)***

***hiyo (Qur'ani ndani ya sala) ikiwa ni ibada ya ziada kwako ili Mola wako akuinue cheo kinachosifika".*** Sura Al-israa: 79.

**6) Yeye ndiye mtu wa Wasila.** Hii ni daraja kubwa peponi. Hataipata ila mtu mmoja tu. Ni daraja kubwa sana katika daraja za peponi. Imenukuliwa kwa Abdallah Bin Amri Bin Al-aas akisema kuwa, alimsikia Mtume (s.a.w.) akisema kwamba: ***"Mkimsikia muadhini semeni kama anavyosema, halafu niombeeni rehema (nisalieni). Ilivyo ni kwamba, mwenye kunisalia (kuniombea rehema) mara moja Allah atampa rehema mara kumi. Halafu muombeni Allah anipe Wasila. Hiyo ni daraja kubwa peponi. Haipati ila mja mmoja tu miongoni mwa waja wa Allah, na nataraji mimi niwe mja huyo. Yeyote anayeniombea Wasila Uombezi (wangu) utakuwa halali yake (ataupata tu).*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Kuna sifa nyingine nyingi mahususi za Mtume zinazo onesha utukufu wa hadhi yake kwa Mola wake na heshima yake kubwa duniani na akhera.

## HAKI ZAKE KWA UMMA WAKE

Umma una wajibu wa mambo mengi ya kumfanyia Mtume wake ikiwa ni haki yake. Miongoni mwa mambo hayo ni haya yafuatayo:

**1) Wajibu wa kuamini kwamba Mtume (s.a.w.) amefikisha ujumbe, amefikisha amana na ameunasihi umma.** Hakuna kheri yoyote isipokuwa kwamba ameuelekeza umma kheri hiyo na kuushawishi waifanye, na hakuna jambo lolote baya isipokuwa kwamba, ameukataza umma wasilifanye na kuuhadharisha umma wake jambo hilo. Amesema Allah kuwa:

﴿ٱلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِى وَرَضِيتُ لَكُمُ ٱلْإِسْلَٰمَ دِينًا﴾ المائدة: ٣.

***"Leo nimekukamilishieni dini yenu na kukutimizieni neema yangu na nimeridhia kwenu Uislamu (iwe) dini (yenu)".*** Sura Almaaida: 3. Katika Hija ya Kuaga Mtume aliwahutubia Waislamu hotuba iliyojaa mafunzo mengi. Aliwabainishia yale ambayo Allah ameyawajibisha kwao na yale ambayo ameyaharamisha kwao. Aliwausia kushikamana na kitabu cha Allah mpaka akawaambia

kuwa: ***"Na nyinyi mtaulizwa kuhusu mimi. Je, mtasema nini? (Swahaba) Wakasema: Tunakiri kwamba umefikisha (ujumbe) na umefikisha (amana) na umetoa nasaha. Mtume akasema kwa kuashiria kwa kidole chake cha shahada akikinyanyua juu na kukielekeza kwa watu na kusema kwamba: Ewe Mola wangu, shuhudia. Ewe Mola wangu, shuhudia. Mtume alikariri kusema hayo mara tatu".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. Amesema Abudharr, Allah amuwiye radhi, kuwa: ***"(Mtume) Muhammad ametuacha na hakuna ndege anayepaa angani isipokuwa kwamba ametuelimisha".*** Ameipokea Imam Ahmad.

**2) Kumpenda Mtume na kutanguliza kumpenda kuliko nafsi, watoto na watu wote.** Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: "***Hawi muumini mmoja wenu mpaka mimi niwe kipenzi chake zaidi kuliko mzazi wake na mtoto wake na watu wote".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Omar, Allah amuwiye radhi, alipomwambia Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Kwa yakini kabisa, ewe Mtume wa Allah, mimi ninakupenda kuliko kitu chochote isipokuwa tu nafsi yangu***, ***Mtume alisema kuwa: Hapana. Nina'apa kwa Yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake kwamba (imani yako haiwi kamili) mpaka mimi niwe ni kipenzi chako zaidi kuliko hata nafsi yako. Akasema Omar: Nina'apa kwa Allah na kwa yakini kabisa, hivi sasa nakupenda zaidi kuliko nafsi yangu. Akasema Mtume: Sasa hivi sawa sawa ewe Omar".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

**3) Kumtukuza Mtume (s.a.w.) na kumheshimu**. Hii ni katika haki za Nabii ambazo Allah amezitaja katika kitabu chake kwamba ni wajibu. Amesema Allah kuwa:

﴿لِّتُؤْمِنُوا۟ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ وَتُعَزِّرُوهُ وَتُوَقِّرُوهُ ۚ وَتُسَبِّحُوهُ بُكْرَةً وَأَصِيلًا﴾ الفتح: ٩.

***"Ili mumuamini Allah na Mtume wake, na mumtukuze (Mtume) na mumheshimu na mumuadhimishe (Allah) asubuhi na jioni".*** Sura Alfat-hi: 9. Amesema Ibniabbas kuwa: *"Kumtukuza Mtume ni wajibu baada ya kufa kwake kama ilivyokuwa wajibu wakati wa uhai wake. Hayo ni pale Mtume anapotajwa, Sunna na Hadithi zake zinaposomwa na wakati wa kusikia jina na wasifu wake*

*ukitajwa".*

**4) Kumsalia (Kumuombea rehema na amani) Mtume (s.a.w.) na kukithirisha kufanya hivyo.** Amesema Allah kuwa:

﴿ إِنَّ ٱللَّهَ وَمَلَٰٓئِكَتَهُۥ يُصَلُّونَ عَلَى ٱلنَّبِيِّۚ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ صَلُّواْ عَلَيۡهِ وَسَلِّمُواْ تَسۡلِيمًا ﴾ الأحزاب: ٥٦.

***"Hakika, Allah anemteremshia rehema Mtume na Malaika wake (wanamuombea rehema). Enyi mlioamini, msalieni (Mtume kwa kumuombea rehema) na muombeeni amani".*** Sura Al-ahzaab: 56.

**5) Kutochupa mipaka katika kumuamini Mtume na kuwa na tahadhari juu ya hilo.** Kufanya hivyo ni kumuudhi sana Mtume (s.a.w.). Amesema Allah akimuamrisha Mtume wake auambie umma kwamba:

﴿ قُلۡ إِنَّمَآ أَنَا۠ بَشَرٞ مِّثۡلُكُمۡ يُوحَىٰٓ إِلَيَّ أَنَّمَآ إِلَٰهُكُمۡ إِلَٰهٞ وَٰحِدٞۖ فَمَن كَانَ يَرۡجُواْ لِقَآءَ رَبِّهِۦ فَلۡيَعۡمَلۡ عَمَلٗا صَٰلِحٗا وَلَا يُشۡرِكۡ بِعِبَادَةِ رَبِّهِۦٓ أَحَدَۢا ﴾ الكهف: ١١٠.

***"Sema: ilivyo ni kwamba, mimi ni binadamu kama nyinyi, ninaletewa Wahyi kwamba, Mungu (muabudiwa) wenu ni mungu mmoja. Kwa hiyo, anayetaraji kukutana na Mola wake afanye vitendo vizuri na asimshirikishe yeyote katika kumuabudu Mola wake".*** Sura Alkahf: 110.

Imenukuliwa kwa Omar Bin Alkhattab, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa, amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Msipitilize katika kunisifu kama Wakristo walivyopitiliza katika kumsifu (Issa) Mwana wa Maryamu. Ilivyo ni kwamba mimi ni mja wake. Kwa hiyo, semeni (katika kunisifu): Mja wa Allah na Mtume wake"***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

**6) Kuwapenda Swahaba wake, watu wa Familia yake na wake zake. Kuwapenda wote, kujihadhari kuwadharau au kuwatukana au kuwatia hila kwa jambo lolote.** Allah amefanya ni wajibu kwa umma huu kuwapenda Swahaba wa Mtume (s.a.w.) na akawataka wanaokuja baada yao wawaombee msamaha na kumuomba Allah ajaalie

nyoyo zao zisiwa na chuki nao. Baada ya kuwataja Muhajirina (Waislamu wa Makka waliohamia Madina) na Ansaar (Waislamu wa Madina waliowanusuru Waislamu wenzao wa Makka), Allah amesema kuwa:

﴿وَٱلَّذِينَ جَآءُو مِنۢ بَعۡدِهِمۡ يَقُولُونَ رَبَّنَا ٱغۡفِرۡ لَنَا وَلِإِخۡوَٰنِنَا ٱلَّذِينَ سَبَقُونَا بِٱلۡإِيمَٰنِ وَلَا تَجۡعَلۡ فِي قُلُوبِنَا غِلّٗا لِّلَّذِينَ ءَامَنُواْ رَبَّنَآ إِنَّكَ رَءُوفٞ رَّحِيمٌ﴾ الحشر: ١٠.

"Na wale waliokuja baada yao wanasema***: Mola wetu, tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia (kufa) katika Uislamu na usijaalie katika nyoyo zetu chuki (ya kuwachukia) Waislamu (wenzetu). Ewe Mola wetu, hakika wewe ni mpole sana, mwenye rehema mno".*** Sura Alhashri: 10.

Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa, amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Msiwatukane Swahaba wangu. Msiwatukane Swahaba wangu. Nina'apa kwa Yule ambaye nafsi yangu iko mkononi mwake kwamba, hata kama mmoja wenu angetoa (sadaka ya) dhahabu sawa na mlima wa Uhud asingefikia kibaba cha mmoja wao wala nusu yake".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Hizi ni baadhi ya haki za wajibu zinazoupasa umma kumfanyia Mtume (s.a.w.). Tunamuomba Allah atujaalie tuwe miongoni mwa wenye kuzitekeleza haki hizi na kuzienzi, atuimarishe katika dini yake na katika kufuata Sunna za Mtume wake na atufufue chini ya bendera yake. Yeye Allah ni muweza wa hayo.

# NGUZO YA NNE

# KUAMINI VITABU

Miongoni mwa rehema kubwa za Allah kwa waja wake ni kuwapelekea Mitume wake ili wawarejeshe kwenye njia sahihi, ya haki na uongofu. Hilo limefanyika baada ya kuwa waja wametumbukia katika dimbwi la Shirki na kuabudu masanamu na baada ya kuwa wako mbali na maumbile salama ambayo Allah amewaumbia. Aidha imekuwa ni ukamilifu wa neema ya Allah kwamba, amewateremshia Mitume hawa vitabu ambavyo Allah ameweka humo sheria zake, mafunzo yake na mwongozo wake ili vitabu hivyo viwe katiba na mfumo wa maisha yao. Waja wanatakiwa kufuata muongozo wa vitabu hivyo, nuru yake iwaangazie na hekima zilizomo humo ziwaongoze kheri, furaha na mafanikio ya duniani na akhera, na nafsi zao kuendelea kuwa hai na kutakasika.

Kwa sababu hii, kuamini vitabu vya Allah alivyoviteremsha kwa Mitume wake imekuwa miongoni mwa nguzo za imani ambazo ni lazima kuziamini na kuzikubali. Katika mlango huu tutajaribu kutoa mwangaza juu ya nguzo hii na kuelezea yale yanayohusiana nayo. Kwa msaada wa Allah tunasema yafuatayo:

## KWANZA: MAANA YA VITABU

Makusudio ya vitabu hapa ni mafunzo aliyoyateremsha Allah kwa Mitume wake, yakiwa ni rehema kwa viumbe na mwongozo wao ili kwa mafunzo hayo wafike kwenye mafanikio ya duniani na akhera. Vitabu alivyotufahamisha Allah katika Qur’ani kwamba ameviteremsha kwa Mitume ni hivi vifuatavyo:

**1) Torati.** Hiki ni kitabu cha Allah alichokiteremsha kwa (Nabii) Musa, Allah ampe amani. Allah amesema kuwa:

﴿وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَى ٱلْكِتَٰبَ مِنۢ بَعْدِ مَآ أَهْلَكْنَا ٱلْقُرُونَ ٱلْأُولَىٰ بَصَآئِرَ لِلنَّاسِ﴾ القصص: ٤٣.

***'Na kwa hakika kabisa, tulimpa Mussa kitabu baada ya kuwa tumeziangamiza umma za kwanza (zilizopita) kikiwa kifumbua macho kwa watu (kiwaangazie)'.*** Sura Alqasas: 43. Katika Hadithi ya Uombezi (Shafaa'a) Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***'Nendeni kwa Mussa, mja ambaye Allah amezungumza naye na amempa Torati'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**2) Injili.** Hiki ni kitabu cha Allah alichokiteremsha kwa (Nabii) Issa Mwana Maryamu, Allah awape amani. Amesema Allah kuwa:

﴿وَقَفَّيْنَا عَلَىٰٓ ءَاثَٰرِهِم بِعِيسَى ٱبْنِ مَرْيَمَ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ ٱلتَّوْرَىٰةِ ۖ وَءَاتَيْنَٰهُ ٱلْإِنجِيلَ فِيهِ هُدًى وَنُورٌ وَمُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ ٱلتَّوْرَىٰةِ وَهُدًى وَمَوْعِظَةً لِّلْمُتَّقِينَ﴾ المائدة: ٤٦.

***"Na tukawafuatishia baada yao (Mitume hao) Issa Mwana wa Maryamu akiithibitisha Taurati iliyokuwepo kabla yake na tumeampa Injili ndani yake ukiwemo mwongozo na nuru ikiithibitisha Taurati iliyokuwepo kabla yake na ni mwongozo na mawaidha kwa wenye uchamungu".*** Sura Almaida: 46.

**3) Zaburi.** Hiki ni kitabu cha Allah alichokiteremsha kwa (Nabii) Daudi, Allah ampe amani. Amesema Allah kuwa:

﴿وَءَاتَيْنَا دَاوُۥدَ زَبُورًا﴾ النساء: ١٦٣.

***'Na tumempa Daudi Zaburi'.*** Sura Annisaa: 163.

**4) Nyaraka za Ibrahimu na Musa.** Nyaraka hizi zimetajwa katika sehemu mbili katika kitabu ch Allah. Sehemu ya kwanza ni katika sura Annajmi pale Allah aliposema kuwa:

﴿أَمْ لَمْ يُنَبَّأْ بِمَا فِى صُحُفِ مُوسَىٰ ﴿٣٦﴾ وَإِبْرَٰهِيمَ ٱلَّذِى وَفَّىٰٓ ﴿٣٧﴾ أَلَّا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ﴾ النجم: ٣٦-٣٨.

"***Au hakuambiwa yaliyomo katika Nyaraka za Mussa? Na (za) Ibrahimu aliyetimiza (ahadi ya Allah)? kwamba nafsi haibebi dhambi***

***za nafsi nyingine?”.*** Sura Annajmi: 36-39. Sehemu ya pili ni katika sura Al-aalaa. Allah amesema kuwa:

﴿قَدۡ أَفۡلَحَ مَن تَزَكَّىٰ ١٤ وَذَكَرَ ٱسۡمَ رَبِّهِۦ فَصَلَّىٰ ١٥ بَلۡ تُؤۡثِرُونَ ٱلۡحَيَوٰةَ ٱلدُّنۡيَا ١٦ وَٱلۡأٓخِرَةُ خَيۡرٞ وَأَبۡقَىٰٓ ١٧ إِنَّ
هَٰذَا لَفِي ٱلصُّحُفِ ٱلۡأُولَىٰ ١٨ صُحُفِ إِبۡرَٰهِيمَ وَمُوسَىٰ﴾ الأعلى: ١٤-١٩.

***‘Hakika amekwisha faulu aliyejitakasa (na mabaya). Akakumbuka jina la Mola wake akasali. Lakini (nyinyi) mnapenda zaidi maisha ya kidunia. Na ilhali akhera ni bora zaidi na yenye kudumu. Hakika, haya (mnayoambiwa humu katika Qur’ani) yamo katika kurasa za mwanzo (vitabu vilivyotangulia). Nyaraka za Ibrahimu na Mussa”.*** Sura Al-aalaa: 14-19. Allah ametueleza baadhi ya Wahyi wake uliomo katika nyaraka hizi na ambao ameuteremsha kwa Mitume wake wawili Ibrahimu na Musa, Allah awape amani.

**5) Qur’ani Tukufu**. Hiki ni kitabu cha Allah alichokiteremsha kwa Mtume wetu Muhammad (s.a.w.). Ni kitabu cha mwisho kuteremshwa, kitukufu zaidi na kikamilfu zaidi kuliko vyote na kinafuta vitabu vilivyopita. Mahubiri yake yanawahusu wanadamu wote na majini wote. Allah amesema kuwa:

﴿وَأَنزَلۡنَآ إِلَيۡكَ ٱلۡكِتَٰبَ بِٱلۡحَقِّ مُصَدِّقٗا لِّمَا بَيۡنَ يَدَيۡهِ مِنَ ٱلۡكِتَٰبِ وَمُهَيۡمِنًا عَلَيۡهِۖ فَٱحۡكُم بَيۡنَهُم
بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُۖ وَلَا تَتَّبِعۡ أَهۡوَآءَهُمۡ عَمَّا جَآءَكَ مِنَ ٱلۡحَقِّۚ لِكُلّٖ جَعَلۡنَا مِنكُمۡ شِرۡعَةٗ وَمِنۡهَاجٗاۚ وَلَوۡ شَآءَ ٱللَّهُ
لَجَعَلَكُمۡ أُمَّةٗ وَٰحِدَةٗ وَلَٰكِن لِّيَبۡلُوَكُمۡ فِي مَآ ءَاتَىٰكُمۡۖ فَٱسۡتَبِقُواْ ٱلۡخَيۡرَٰتِۚ إِلَى ٱللَّهِ مَرۡجِعُكُمۡ جَمِيعٗا
فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمۡ فِيهِ تَخۡتَلِفُونَ﴾ المائدة: ٤٨.

***“Na tumekuteremshia kitabu kwa haki kikithibitisha kitabu kilichokuwepo kabla yake na kikitawala. Basi hukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Allah, na usifuate utashi wa nafsi zao ukaacha haki iliyokufikia. Kila umma katika nyinyi tumeuwekea sheria namfumo (wa maisha). Na kama Allah angetaka angekufanyeni kundi moja (la kufuata sheria moja), lakini anataka kukujaribuni katika hayo aliyokupeni. Basi shindaneni katika mambo ya kheri. Nyinyi nyote marudio yenu ni kwa Allah tu, na atakuambieni (yote) yale mliyokuwa mkitofautiana”.*** Sura Almaaida: 48. Maana ya Qur’ani kuvitaja vitabu vilivyopita ni kwamba, inatoa ushahidi wa

kuwepo kwa vitabu hivyo na kwamba sheria zake ziko juu ya sheria za vitabu hivyo. Allah amesema kuwa:

﴿قُلْ أَيُّ شَيْءٍ أَكْبَرُ شَهَادَةً ۖ قُلِ ٱللَّهُ ۖ شَهِيدٌۢ بَيْنِى وَبَيْنَكُمْ ۚ وَأُوحِىَ إِلَىَّ هَٰذَا ٱلْقُرْءَانُ لِأُنذِرَكُم بِهِۦ وَمَنۢ بَلَغَ﴾ الأنعام: ١٩.

***“Sema (uwaulize): Ni kitu gani ushahidi wake ndio mkubwa zaidi? Sema (ujibu): Allah ni shahidi baina yangu na baina yenu. Na Qur’ani hii imefunuliwa kwangu ili kwayo nikukanyeni nyinyi na kila imfikiayo”.*** Sura Al-an-aam: 19.

Qur’an ina majina mengi. Majina mashuhuri zaidi ni haya yafuatayo: Alfurqan (Kitenganishi), Alkitab (Kitabu), Attanziil (Uteremsho) na Adh- dhikri (Ukumbusho).

## PILI: HUKUMU YA KUAMINI VITABU

Kuamini vitabu vya Allah alivyoviteremsha kwa Mitume wake ni nguzo kubwa miongoni mwa nguzo za imani, ni msingi mkubwa katika misingi ya dini na imani haitimii bila ya kuwepo kwa nguzo hii. Allah amesemakuwa:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ ءَامِنُوا۟ بِٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦ وَٱلْكِتَٰبِ ٱلَّذِى نَزَّلَ عَلَىٰ رَسُولِهِۦ وَٱلْكِتَٰبِ ٱلَّذِىٓ أَنزَلَ مِن قَبْلُ ۚ وَمَن يَكْفُرْ بِٱللَّهِ وَمَلَٰٓئِكَتِهِۦ وَكُتُبِهِۦ وَرُسُلِهِۦ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًۢا بَعِيدًا﴾ النساء: ١٣٦.

***“Enyi mlioamini, mwaminini Allah na Mtume wake na kitabu alichokiteremsha kwa Mtume wake na vitabu alivyoviteremsha zamani. Na yeyote mwenye kumkataa Allah na Malaika wake na vitabu vyake na Mitume wake na siku ya mwisho, basi bila shaka amepotea upotevu ulio mbali (na haki)”.*** Sura Annisaa: 136.

Allah amewaamrisha waja wake waumini wamuamini Allah, Mtume wake Muhammad (s.a.w.), Qur’ani kitabu alichokiteremsha kwa Mtume wake na vitabu alivyoviteremsha zamani kama vile Torati, Injili, Zaburi na Nyaraka. Mwisho wa aya Allah amebainisha kwamba anayekataa kitu katika nguzo za imani, ikiwemo Qur’ani, atakuwa amepotea upotevu wa mbali kabisa.

## TATU: NAMNA YA KUAMINI VITABU

Kuamini vitabu vya Allah kunajumuisha mambo kadhaa ambayo

ni lazima kuwa na itikadi nayo na kuyakubali ili nguzo hii kubwa ikamilike. Mambo haya ni haya yafuatayo:

**1)** Kuwa na Imani thabiti kwamba vitabu vyote hivyo vimeteremshwa na Allah, ni maneno ya Allah na sio maneno ya mwengine, Allah ameyasema kwa hakika kama alivyotaka na katika hali aliyotaka.

**2)** Kuwa na imani kwamba vitabu vyote hivyo vimehubiri kumuabudu Allah pekee na kwamba vitabu hivyo vimeleta kheri, uongofu na nuru.

**3)** Kuyaamini na kuyakubali majina ya vitabu hivi ambayo Allah ameyataja kwa kuainisha. Vitabu vilivyotajwa kwa majina ni hivi: Qur'ani, Torati, Injili, Zaburi na Nyaraka za Ibrahimu na Musa. Ama vile vitabu ambavyo Allah hakututajia majina yake tunaviamini kwa jumla kama Allah alivyomuamrisha Mtume wake kwa kusema kuwa:

﴿وَقُلْ ءَامَنتُ بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ مِن كِتَٰبٍ﴾ الشورى: ١٥.

***"Na sema: Nimeamini vitabu alivyoteremsha Allah".*** Sura Ash-shuuraa: 15.

**4)** Kuamini habari sahihi za vitabu hivyo, kama habari za Qur'ani na habari za vitabu vitukufu vya zamani ambazo hazikubadilishwa au kupotoshwa.

**5)** Kuwa na itikadi thabiti kwamba Qur'an imefuta na kubadili sheria zilizomo katika nyaraka na vitabu vyote vya zamani alivyoviteremsha Allah kwa Mitume wake. Allah, kwa kuileta Qur'ani, amefuta sharia zote zilizokuwemo katika vitabu vya zamani, isipokuwa tu sheria ambazo Qur'ani imeziridhia. Kwa sababu hiyo, si halali kwa mtu yeyote au jini yeyote, si watu wa vitabu vilivyotangulia wala wengineo, kumuabudu Allah baada ya kuteremshwa kwa Qur'ani kwa kutumia mafunzo yasiyokuwa ya Qur'ani au kuhukumu kwa kutumia sheria za vitabu vingine vya nyuma badala ya Qur'ani. Allah amesema kuwa:

﴿تَبَارَكَ ٱلَّذِى نَزَّلَ ٱلْفُرْقَانَ عَلَىٰ عَبْدِهِۦ لِيَكُونَ لِلْعَٰلَمِينَ نَذِيرًا﴾ الفرقان: ١.

***"Ametukuka (Allah) ambaye ameteremsha Qur'ani kwa mja wake ili iwe muonyaji kwa walimwengu (wote)".*** Sura Alfurqan: 1.

Pia Allah amesema kuwa:

﴿يَٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ قَدۡ جَآءَكُمۡ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمۡ كَثِيرٗا مِّمَّا كُنتُمۡ تُخۡفُونَ
مِنَ ٱلۡكِتَٰبِ وَيَعۡفُواْ عَن كَثِيرٖۚ قَدۡ جَآءَكُم مِّنَ ٱللَّهِ نُورٞ وَكِتَٰبٞ مُّبِينٞ﴾ المائدة: ١٥.

***"Enyi watu wa kitabu, amekwisha kufikieni Mtume wetu, akikudhihirishieni mengi mliyokuwa mkiyaficha katika kitabu, na anasamehe mengi. Bila shaka imekwisha kufikieni nuru kutoka kwa Allah na kitabu kinachobainisha(kila jambo)".*** Sura Almaaida: 15. Pia Allah, akimuamrisha Mtume wake awahukumu Watu wa Kitabu kwa kutumia Qur'ani, amesema kuwa:

﴿فَٱحۡكُم بَيۡنَهُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُۖ وَلَا تَتَّبِعۡ أَهۡوَآءَهُمۡ عَمَّا جَآءَكَ مِنَ ٱلۡحَقِّۚ﴾ المائدة: ٤٨.

***"Basi wahukumu kwa kutumia yale aliyoyateremsha Allah, na usifuate utashi wa nafsi zao ukaacha haki iliyokufikia".*** Sura Almaaida: 48.

## NNE: WATU WA KITABU NA UPOTOSHAJI WA MANENO YA ALLAH

Allah ametufahamisha ndani ya Qur'ani kwamba, Wayahudi na Wakristo ambao ni Watu wa Kitabu, wamebadilisha, kugeuza na kupotosha vitabu vya Allah vilivyoteremshwa kwao. Allah amesema kuhusu Wayahudi kwamba:

﴿أَفَتَطۡمَعُونَ أَن يُؤۡمِنُواْ لَكُمۡ وَقَدۡ كَانَ فَرِيقٞ مِّنۡهُمۡ يَسۡمَعُونَ كَلَٰمَ ٱللَّهِ ثُمَّ يُحَرِّفُونَهُۥ مِنۢ بَعۡدِ مَا
عَقَلُوهُ وَهُمۡ يَعۡلَمُونَ﴾ البقرة: ٧٥.

***"Hivi Mnatumaini (nyinyi Waislamu) kwamba (hao Wayahudi) watakuaminini na ilhali baadhi yao walikuwa wanasikia maneno ya Allah kisha wanayabadili baada ya kuwa wameyafahamu na ilhali wanajua?"*** Sura Albaqara: 75**.** Na kuhusu Wakristo Allah amesema kuwa:

﴿يَٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ قَدۡ جَآءَكُمۡ رَسُولُنَا يُبَيِّنُ لَكُمۡ كَثِيرٗا مِّمَّا كُنتُمۡ تُخۡفُونَ
مِنَ ٱلۡكِتَٰبِ وَيَعۡفُواْ عَن كَثِيرٖۚ قَدۡ جَآءَكُم مِّنَ ٱللَّهِ نُورٞ وَكِتَٰبٞ مُّبِينٞ﴾ المائدة: ١٥.

***"Enyi watu wa kitabu, amekwisha kufikieni Mtume wetu,***

***akikudhihirishieni mengi mliyokuwa mkiyaficha katika kitabu, na anasamehe mengi. Bila shaka imekwisha kufikieni nuru kutoka kwa Allah na kitabu kinachobainisha (kila jambo)".*** Sura Almaaida: 15.

Kuna aya na Hadithi nyingine nyingi zenye kubainisha ubadilishaji wa maneno ya Allah uliofanywa na Watu wa Kitabu.

Ama Qur'ani imesalimika na ubadilishaji na upotoshaji uliovikumba vitabu vilivyopita. Qur'ani imehifadhiwa na ina kinga ya Allah. Amesema Allah kuwa:

﴿ إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا ٱلذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَـٰفِظُونَ ﴾ الحجر: ٩.

***"Hakika, sisi ndio tulioteremsha ukumbusho (Qura'ni) na hakika sisi tu ndio wenye kuulinda".*** Sura Alhijri: 9.

## TANO: SIFA MAHUSUSI ZA KUIAMINI QUR'ANI

Kwa kuwa Qur'ani ni kitabu chenye kufuta vitabu vilivyopita, kipo juu yake na kinatumiwa na majini na wanadamu kwa kuabudu baada ya kuja kwa Mtume wetu Muhammad (s.a.w.) na kushushiwa kitabu hicho, imepewa sifa maalumu ambazo ni lazima kuzitekeleza ili imani iwe sahihi. Sifa hizo ni kama ifuatavyo:

**1)** Kuwa na itikadi kwamba mahubiri ya Qur'ani na sheria zake zinawahusu binadamu wote na majini wote. Ni lazima kila mmoja aiamini, awe jini au binadamu. Allah amesema kuwa:

﴿ تَبَارَكَ ٱلَّذِى نَزَّلَ ٱلْفُرْقَانَ عَلَىٰ عَبْدِهِۦ لِيَكُونَ لِلْعَـٰلَمِينَ نَذِيرًا ﴾ الفرقان: ١.

***"Ametukuka (Allah) ambaye ameteremsha Qur'ani kwa mja wake ili iwe muonyaji kwa walimwengu (wote)".*** Sura Alfurqaan: 1.

**2)** Kuwa na itikadi kwamba Qur'ani imefuta vitabu vyote vilivyotangulia. Haifai kwa Watu wa Kitabu na kwa watu wengine kumuabudu Allah kwa kutumia mafundisho ya kitabu kingine baada ya kuteremka kwa Qur'ani. Hakuna dini ila tu ile iliyoletwa na Qur'ani. Hakuna ibada ila tu ile ambayo Allah ameiweka ndani ya Qur'ani. Hakuna cha halali ila tu kile ambacho Allah amekihalalisha ndani ya Qur'ani na hakuna cha haramu ila tu kile ambacho Allah

amekiharamisha ndani ya Qur’ani. Allah amesema kuwa:

﴿وَمَن يَبۡتَغِ غَيۡرَ ٱلۡإِسۡلَٰمِ دِينٗا فَلَن يُقۡبَلَ مِنۡهُ﴾ آل عمران: ٨٥.

***“Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake”.*** Sura Aal-imraan: 85.

**3)** Wepesi na uzuri wa sheria za Qur’ani. Sheri za Qur’ani ni tofauti na sheria zilizomo katika vitabu vilivyopita ambazo zilikuwa na ugumu na uzito mwingi uliowekwa kwa wafuasi wake. Allah amesema kuwa:

﴿ٱلَّذِينَ يَتَّبِعُونَ ٱلرَّسُولَ ٱلنَّبِيَّ ٱلۡأُمِّيَّ ٱلَّذِي يَجِدُونَهُۥ مَكۡتُوبًا عِندَهُمۡ فِي ٱلتَّوۡرَىٰةِ وَٱلۡإِنجِيلِ يَأۡمُرُهُم بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَيَنۡهَىٰهُمۡ عَنِ ٱلۡمُنكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيۡهِمُ ٱلۡخَبَٰٓئِثَ وَيَضَعُ عَنۡهُمۡ إِصۡرَهُمۡ وَٱلۡأَغۡلَٰلَ ٱلَّتِي كَانَتۡ عَلَيۡهِمۡ﴾ الأعراف: ١٥٧.

***"Ambao wanamfuata Mtume Nabii asiyejua kusoma na kuandika ambaye wanamkuta ameandikwa kwao katika Taurati na Injili, ambaye anawaamrisha kutenda mema na anawakataza kufanya yaliyo mabaya na anawahalalishia vitu vizuri na anawaharamishia vitu vibaya na anawaondolea ahadi zao (nzito) na minyororo iliyokuwa juu yao (yaani sheria ngumu za zamani na mila za kikafiri)”.*** Sura Al-aaraf: 157.

**4)** Qur’ani ni kitabu pekee baina ya vitabu vya Allah ambacho Allah amedhamini kuyalinda matamshi yake na madhumuni yake. Hakuna uwezekano wa kufanyika ubadilshaji au upotoshaji wa matamshi au maana. Allah anasema kuwa:

﴿إِنَّا نَحۡنُ نَزَّلۡنَا ٱلذِّكۡرَ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَٰفِظُونَ﴾ الحجر: ٩.

***“Hakika, sisi ndio tulioteremsha ukumbusho (Qura’ni) na hakika sisi tu ndio wenye kuulinda”.*** Sura Alhijri: 9. Pia Allah amesema kuwa:

﴿لَّا يَأۡتِيهِ ٱلۡبَٰطِلُ مِنۢ بَيۡنِ يَدَيۡهِ وَلَا مِنۡ خَلۡفِهِۦۖ تَنزِيلٞ مِّنۡ حَكِيمٍ حَمِيدٖ﴾ فصلت: ٤٢.

***"Batili haikifikii mbele yake wala nyuma yake. Ni uteremsho utokao kwa mwenye hekima, ahimidiwaye”.*** Sura Fussilat: 42.

**5)** Allah Mtukufu amebainisha katika Qur’ani kila kitu ambacho

wanadamu wanakihitaji katika mambo ya dini yao na mambo ya dunia yao; maisha yao ya duniani na maisha yao ya akhera. Amesema Allah kuwa:

﴿وَنَزَّلۡنَا عَلَيۡكَ ٱلۡكِتَٰبَ تِبۡيَٰنٗا لِّكُلِّ شَيۡءٖ وَهُدٗى وَرَحۡمَةٗ وَبُشۡرَىٰ لِلۡمُسۡلِمِينَ﴾ النحل: ٨٩.

***"Na tumekuteremshia kitabu kwa ajili ya kufafanua kila kitu, na ni mwongozo na ni rehema na ni habari njema kwa Waislamu".*** Sura Annahli: 89. Pia Allah amesema kuwa:

﴿مَّا فَرَّطۡنَا فِي ٱلۡكِتَٰبِ مِن شَيۡءٖ﴾ الأنعام: ٣٨.

***"Hatukupuuza kitabuni (mwetu) kitu chochote".*** Sura Al-an-aam: 38.

**6)** Allah ameifanya Qur'ani nyepesi kwa wenye kuzingatia na kutafakari. Hii ni katika sifa yake kubwa sana. Amesema Allah kuwa:

﴿وَلَقَدۡ يَسَّرۡنَا ٱلۡقُرۡءَانَ لِلذِّكۡرِ فَهَلۡ مِن مُّدَّكِرٖ﴾ القمر: ١٧.

***"Na kwa yakini kabisa, tumeifanya Qur'ani nyepesi kwa ajili ya kukumbuka. Je, yupo mwenye kukumbuka?"*** Sura Alqamar: 17**.** Maana ni kwamba, tumefanya usomaji wa Qur'ani mwepesi katika ndimi.

**7)** Qur'ani imekusanya muhtasari wa mafunzo yote yaliyomo ndani ya vitabu vilivyopita na misingi ya sheria za Mitume. Allah amesema kuwa:

﴿وَأَنزَلۡنَآ إِلَيۡكَ ٱلۡكِتَٰبَ بِٱلۡحَقِّ مُصَدِّقٗا لِّمَا بَيۡنَ يَدَيۡهِ مِنَ ٱلۡكِتَٰبِ وَمُهَيۡمِنًا عَلَيۡهِۖ﴾ المائدة: ٤٨.

***"Na tumekuteremshia kitabu kwa haki kikithibitisha kitabu kilichokuwepo kabla yake na kikitawala".*** Sura Almaaida: 48. Pia Allah amesema kuwa:

﴿شَرَعَ لَكُم مِّنَ ٱلدِّينِ مَا وَصَّىٰ بِهِۦ نُوحٗا وَٱلَّذِيٓ أَوۡحَيۡنَآ إِلَيۡكَ وَمَا وَصَّيۡنَا بِهِۦٓ إِبۡرَٰهِيمَ وَمُوسَىٰ
وَعِيسَىٰٓۖ أَنۡ أَقِيمُواْ ٱلدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُواْ فِيهِۚ﴾ الشورى: ١٣.

***"Amekupeni sharia ya dini ile ile aliyo muusia Nuhu na tuliyokufunulia wewe na tuliyowausia Ibrahimu na Mussa na Issa kwamba, simamisheni dini wala msifarakane humo".*** Sura

Ash-shuuraa: 13.

Hizi ni baadhi ya sifa za Qur’ani Tukufu ambazo ni tofauti na sifa za vitabu vyengine. Imani haiwi kamili bila ya kuziamini sifa hizi na kuzifanyia kazi kwa kujua na kwa kivitendo.

## NGUZO YA TANO

## KUAMINI SIKU YA MWISHO

Miongoni mwa nguzo za imani ambazo ni wajibu kwa Muislamu kuziitakidi, na imani yake haiwi sahihi ila kwa kuzikubali ni kuamini Siku ya Mwisho. Amesema Allah kuwa:

﴿لَّيۡسَ ٱلۡبِرَّ أَن تُوَلُّواْ وُجُوهَكُمۡ قِبَلَ ٱلۡمَشۡرِقِ وَٱلۡمَغۡرِبِ وَلَٰكِنَّ ٱلۡبِرَّ مَنۡ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِ وَٱلۡمَلَٰٓئِكَةِ وَٱلۡكِتَٰبِ وَٱلنَّبِيِّـۧنَ وَءَاتَى ٱلۡمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ ذَوِي ٱلۡقُرۡبَىٰ وَٱلۡيَتَٰمَىٰ وَٱلۡمَسَٰكِينَ وَٱبۡنَ ٱلسَّبِيلِ وَٱلسَّآئِلِينَ وَفِي ٱلرِّقَابِ وَأَقَامَ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَى ٱلزَّكَوٰةَ وَٱلۡمُوفُونَ بِعَهۡدِهِمۡ إِذَا عَٰهَدُواْۖ وَٱلصَّٰبِرِينَ فِي ٱلۡبَأۡسَآءِ وَٱلضَّرَّآءِ وَحِينَ ٱلۡبَأۡسِۗ أُوْلَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ صَدَقُواْۖ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُتَّقُونَ﴾ البقرة: ١٧٧.

***"Sio wema (tu) kuelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi (katika kusali. Yapo mema mengine). Bali wema (hasa) ni ( wa wale) waloamuamini Allah na Siku ya Mwisho na Malaika na vitabu na Manabii, na wanawapa mali, pamoja na kuipenda, ndugu na yatima na masikini na wasafiri (walioharibikiwa) na wanao omba na katika (kuwakomboa) watumwa, na wakawa wanasimamisha sala na kutoa zaka, na watekelezao ahadi zao walizoahidi na wavumilivu katika shida na dhara na (katika) wakati wa vita. Hao ndio waliosema kweli (katika Uislamu wao) na hao ndio wamchao mungu".*** Sura Albaqara: 177.

Katika mlango huu tutajaribu kuzungumzia maana ya Siku ya Mwisho, majina yake, wajibu wa kuiamini, alama za Kiyama, mtihani wa kaburini, adhabu za kaburini na neema zake, kupulizwa kwa parapanda, kufufuliwa na kukusanywa, matukio ya kutisha ya Siku ya Kiyama, hesabu, mizani, malipo, njia (Siraat), pepo na wasifu wake, moto na wasifu wake, na matunda ya kuiamini siku hiyo.

## KWANZA: MAANA YA SIKU YA MWISHO

**Siku ya Mwisho** ni siku ya Kiyama ambayo Allah katika siku hiyo atawafufua watu kutoka makaburini mwao kwa ajili ya hesabu na malipo. Imeitwa Siku ya Mwisho kwa sababu hakuna siku nyingine baada ya siku hiyo, ambapo watu wa peponi watakuwa katika makazi yao na watu wa motoni watakuwa katika makazi yao.

Kuamini Siku ya Mwisho kunajumuisha: kuamini kila habari sahihi iliyonukuliwa kuhusu siku hiyo na mambo yanayohusiana nayo. Inaingia katika habari sahihi za siku hiyo kuamini alama za Kiyama zenye kuashiria kwamba Kiyama kipo karibu, kuamini kufa na yanayofuatia kifo ikiwa ni pamoja na mitihani ya kaburini; adhabu na neema zake, kuamini kupulizwa kwa parapanda ambalo ni alama ya kuanza kwa Siku ya Mwisho, kuamini kufufuka kwa viumbe kutoka makaburini, kuamini hesabu na malipo, kuamini kuwepo kwa matukio ya kutisha ya Siku ya Kiyama, kuamini kugaiwa kwa madaftari yenye amali za waja, kuamini mizani za kupimia mema na mabaya, kuamini Sirati ambayo ni daraja litakalokuwepo motoni na watu watapita juu yake. Muumini ataokoka na kafiri ataanguka na kutumbukia motoni. Pia kuamini Hodhi la Mtume (s.a.w.) ambalo waumini watakunywa humo na kukata kiu yao siku hiyo, kuamini pepo na neema zake ambayo neema yake kubwa kabisa na ya juu ni kuuona uso wa Allah, kuamini moto (wa Jahanamu) na adhabu zake kubwa ambayo ni wasiokuwa Waislamu kuzuiwa kumuona Mola wao Mtukufu.

## PILI: MAJINA YA SIKU YA MWISHO

Allah ameipa Siku ya Mwisho ambayo itakuwa ndio mwisho wa ulimwengu majina mengi ndani ya Qur’ani. Imeitwa siku ya Kiyama (kusimama) kwa sababu, hiyo ni siku ambayo waja watasimama mbele ya Allah, siku ya kufufuliwa, kwa sababu watu katika siku hiyo watafufuliwa kutoka makaburini, siku ya utengano, kwa sababu siku hiyo watu watatenganishwa baina yao, siku ya hesabu, siku ya kufichuliwa siri na majina mengine mengi yenye kuonesha umuhimu wa siku hiyo na ukubwa wa matukio yake.

## TATU: WAJIBU WA KUAMINI SIKU YA MWISHO

Ni wajibu kwa Muislamu kuwa na itikadi thabiti kwamba kuna siku ambayo uhai wa maisha ya duniani utaishia hapo, na watu watakuwa katika ulimwengu mwingine. Allah amejipendelea yeye mwenyewe kuijua siku hiyo. Siku hiyo Allah atawakusanya watu wa mwanzo na wa mwisho na kuwalipa wote kwa mujibu wa amali zao. Watu watakuwa makundi mawili, kundi moja la peponi na kundi jingine la motoni. Allah amesema kuwa:

﴿ لَّيْسَ ٱلْبِرَّ أَن تُوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ قِبَلَ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ وَلَٰكِنَّ ٱلْبِرَّ مَنْ ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةِ وَٱلْكِتَٰبِ وَٱلنَّبِيِّۦنَ ﴾ البقرة: ١٧٧.

***"Sio wema (tu) kuelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi (katika kusali yapo na mema mengine). Bali wema (hasa) ni (wa wale) wanaomuamini Allah na Siku ya Mwisho na Malaika na kitabu na Manabii".*** Sura Albaqara: 177.

Kuamini Siku ya Mwisho ni nguzo ya tano kati ya nguzo sita za imani, kama ilivyokuja katika Hadithi ya Jibrili, Allah ampe amani, pale Jibrili alipomuuliza Mtume kuhusu imani na Mtume (s.a.w.) akajibu kuwa: "Ni kumuamini Allah na Malaika wake na vitabu vyake na Mitume wake na Siku ya Mwisho, na kuamini Qadari; kheri na shari yake". Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Imani ya mja haiwi sahihi bila ya kuamini Siku ya Mwisho. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿ وَمَن يَكْفُرْ بِٱللَّهِ وَمَلَٰٓئِكَتِهِۦ وَكُتُبِهِۦ وَرُسُلِهِۦ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَٰلًۢا بَعِيدًا ﴾ النساء: ١٣٦.

***"Na yeyote mwenye kumkanusha Allah na Malaika wake na vitabu vyake na Mitume wake na Siku ya Mwisho, basi bila shaka amepotea upotevu ulio mbali (na haki)".*** Sura Annisaa: 136**.**

## NNE: ALAMA ZA KIYAMA

Miongoni mwa mambo yaliyo wajibu kuamini ni mambo tangulizi ya Siku ya Mwisho ambayo Mtume (S.A.W.) ameyaeleza. Wanazuoni wamezigawanya alama hizi katika mafungu mawili:

**LA KWANZA**: **Alama ndogo**. Hizi ni alama zinazoashiria kukaribia kwa Siku ya Kiyama na kwisha kwa ulimwengu. Alama hizi ni nyingi, na nyingine yake tayari zimekwishatokea. Miongoni mwa hizo zilizokwishatokea ni: Kupotea kwa uaminifu, nyakati kukaribiana, kutokea kwa vurugu na hofu duniani, vifo vingi, kuongezeka kwa zinaa na uchafu, na kadhalika. Allah amesema kuwa:

﴿ٱقۡتَرَبَتِ ٱلسَّاعَةُ وَٱنشَقَّ ٱلۡقَمَرُ﴾ القمر: ١.

***"Saa (ya kufika kwa Kiyama) imekaribia na mwezi umepasuka".*** Sura Alqamar: 1.

**LA PILI**: **Alama kubwa**. Hizi ni alama ambazo zitatokea wakati wa kutokea kwa Kiyama na kutoa tahadhari ya kutokea kwake. Ni alama kumi, na bado haijatokea hata moja kati ya hizo. Imenukuliwa kwa Hudhayfa Bin Usaid Alghifariy, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***"Alitujia Mtume (s.a.w.) tukiwa tunakumbushana, akasema: Mnakumbushana nini? Tukasema: Tunakumbasha Kiyama. Mtume akasema: Hakika, Kiyama hakitokei mpaka muone kabla yake mambo kumi. Akataja kuwa ni: (kutokea kwa) Moshi na Dajali na Mnyama na jua kuchomoza kutokea magharibi yake na kuteremka kwa Issa Bin Mariyamu na Yaajuju na Maajuju na kupatwa kwa jua mara tatu; mara mashariki na mara magharibi na mara Bara Arabu. Mwisho wa hayo ni moto utakaotokea Yemen na ambao utawafukuza watu kuelekea mahali pao watakapokusanywa"***. Hadithi hii imepokewa na Muslim.

## TANO: MTIHANI WA KABURINI

Maiti anapotiwa kaburini wanamjia Malaika wawili wanaoitwa Munkar na Nakiir. Wanamuuliza kuhusu Mola wake, dini yake na Mtume wake. Allah anamfanya imara Muislamu (katika kujibu) na kusema: ***"Mola wangu ni Allah na dini yangu ni Uislamu na Nabii wangu ni Muhammad (s.a.w.)".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. Ama kafiri na mnafiki watasema: ***"Aah! Aah! Sijui"***. Hadithi hii imepokewa na Abudaudi. Katika nukuu nyingine imenukuliwa kwamba, kafiri na mnafiki watajibu kuwa: ***"Nimewasikia watu wakisema maneno nami nikayasema. Sijui".***

Ni wajibu kuamini mafundisho ya Hadithi (zilizotajwa) ambayo ni kuwepo kwa maswali ya Malaika wawili na hali itakavyokuwa, atakavyojibu muumini na atakavyojibu kafiri na mnafiki.

Mtihani huu wa kaburini unawahusu walengwa wote wa sharia (mukallafiin) isipokuwa tu Manabii, Mashahidi (waliokufa katika vita vya Jihadi), walinzi wa mipaka ya dola ya Kiislam, Muislamu anayekufa siku ya Ijumaa, na Muislamu anayekufa kwa maradhi ya tumbo. Haya ni kwa mujibu wa Hadithi sahihi.

## SITA: ADHABU ZA KABURINI NA NEEMA ZAKE

Ni wajibu kuamini adhabu za kaburi na neema zake. Kaburi kwa maiti linakuwa ama bustani miongoni mwa bustani za peponi au mashimo miongoni mwa mashimo ya motoni.

Neema na adhabu za kaburini zinahusu mwili na roho kwa pamoja. Wakati mwingine neema na adhabu hizo zinahusu roho peke yake. Neema za kaburi ni za waumini wa kweli, na adhabu zake ni kwa makafiri, wanafiki na baadhi ya Waislamu waliofanya dhambi.

Kuna hoja za maandiko na za kiakili zinazo onesha wajibu wa kuamini adhabu na neema za kaburini. Hoja za maandishi ni kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿وَحَاقَ بِـَٔالِ فِرۡعَوۡنَ سُوٓءُ ٱلۡعَذَابِ ٤٥ ٱلنَّارُ يُعۡرَضُونَ عَلَيۡهَا غُدُوّٗا وَعَشِيّٗاۚ وَيَوۡمَ تَقُومُ ٱلسَّاعَةُ
أَدۡخِلُوٓاْ ءَالَ فِرۡعَوۡنَ أَشَدَّ ٱلۡعَذَابِ﴾ غافر: ٤٥-٤٦.

***“Na adhabu mbaya imewaangukia watu wa Firauni; moto unaowachoma asubuhi na jioni. Na siku Kiyama kitakapotokea (kutasemwa): Waingizeni watu wa Firauni katika adhabu kali zaidi (kuliko hii waliyoipata kaburini)”.*** Sura Ghafir: 45-46.

Allah Mtukufu amebainisha kwamba, Firauni na watu wake wanaadhibiwa adhabu mbili. Moja ni kabla ya Siku ya Kiyama wakiwa makaburini asubuhi na jioni. Ya pili ni siku Kiyama kitakaposimama watakuwa na adhabu kali mno ndani ya Jahanamu.

Imekuja katika Hadithi ya Albaraa Bin Azib, Allah amuwiye

radhi, kuhusu Muislamu katika kuulizwa na Malaika wawili awapo kaburini kwamba, Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Atatangaza mtangazaji kutokea mbinguni kwamba, amesema kweli mja wangu. Mtandikieni (thamani za) peponi na mvalisheni (nguo za peponi) na mfungulieni mlango wa kuelekea peponi. Atapata upepo wa peponi na harufu yake, na kaburi lake litapanuliwa hadi mwisho wa upeo wa macho yake. Ama kuhusu kafiri, Mtume amesema kuwa: Atatangaza mtangazaji kutokea mbinguni kwamba, mja wangu amesema uongo. Mtandikieni (thamani za) motoni na mfungulieni mlango wa kuelekea motoni. Litamjia joto la motoni na upepo wake mkali, na kaburi lake litafanywa finyu na kumbana mpaka mbavu zake ziachane humo kaburini".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad na Abudaudi.

Ama hoja ya kuamini Siku ya Mwisho kiakili ni kwamba, mtu mwenye kulala anaweza kuota ndoto yenye kumpendeza, akasikia raha na kupata faraja kwa ndoto hiyo kuleta athari katika nafsi yake. Kama ambavyo pia anaweza kuota ndoto mbaya ikamuumiza na kumtia majonzi. Neema au adhabu hii ya usingizini inatokea katika roho kwa hakika na roho inapata athari yake na haitambuliki kwa vitambuzi vya hisia, wala hatuioni na hakuna yeyote anaye ikanusha. Sasa vipi ipingwe neema au adhabu ya kaburini ambayo ni mfano wake?

## SABA: KUPULIZWA KWA PARAPANDA

Parapanda ni kitu mfano wa pembe ambayo Malaika Israfil ataipuliza. Atapuliza mpulizo wa mwanzo na viumbe vyote vitakufa, ila amtakae Allah. Halafu atapuliza mpulizo wa pili na vitafufuka viumbe vyote tangu Allah alipoumba dunia mpaka kusimama kwa Kiyama. Allah amesema kuwa:

﴿وَنُفِخَ فِي ٱلصُّورِ فَصَعِقَ مَن فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَن فِي ٱلۡأَرۡضِ إِلَّا مَن شَآءَ ٱللَّهُۖ ثُمَّ نُفِخَ فِيهِ أُخۡرَىٰ فَإِذَا هُمۡ قِيَامٞ يَنظُرُونَ﴾ الزمر: ٦٨.

***"Na litapulizwa baragumu watoke roho waliomo mbinguni na waliomo ardhini ila yule amtakaye Allah. Halafu litapulizwa mara***

***nyingine, mara tu wote watafufuka na kusimama (wawe) wanatazama (nini kitatokea)”*** Sura Azzumar: 68.

## NANE: KUFUFULIWA NA KUKUSANYWA

Maana ya kufufuliwa na kukusanywa ni Allah kuwapa uhai waliokufa pale itakapopulizwa Parapanda kwa mara ya pili na watu kusimama mbele ya Allah. Allah atakapoamrisha kupulizwa kwa Parapanda na roho kurejeshwa kwenye miili yake, hapo watu watasimama kutoka makaburini mwao na watatoka kwa haraka. Watakusanywa na kuongozwa kuelekea kwenye ardhi ya kuhesabiwa, kulipwa na kuhukumiwa baina yao. Allah amesema kuwa:

﴿وَنُفِخَ فِي ٱلصُّورِ فَإِذَا هُم مِّنَ ٱلۡأَجۡدَاثِ إِلَىٰ رَبِّهِمۡ يَنسِلُونَ﴾ يس: ٥١.

***“Na kisha litapulizwa Parapanda (la kufufuliwa), tahamaki wao wanatoka makaburini kwenda mbio mbio kwa Mola wao”.*** Sura Yasin: 51. Pia Allah amesema kuwa:

﴿وَحَشَرۡنَٰهُمۡ فَلَمۡ نُغَادِرۡ مِنۡهُمۡ أَحَدٗا﴾ الكهف: ٤٧.

***“Na tutawafufua (wote) na hatutamuacha yeyote katika wao”.*** Sura Alkahf: 47.

Ni wajibu kwa Muislamu kuamini kufufuliwa kwa sababu jambo hilo limethibiti kisheria kama ambavyo limethibiti kwa utambuzi.

Ama kisheria, amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِن كُنتُمۡ فِي رَيۡبٖ مِّنَ ٱلۡبَعۡثِ فَإِنَّا خَلَقۡنَٰكُم مِّن تُرَابٖ ثُمَّ مِن نُّطۡفَةٖ ثُمَّ مِنۡ
عَلَقَةٖ ثُمَّ مِن مُّضۡغَةٖ مُّخَلَّقَةٖ وَغَيۡرِ مُخَلَّقَةٖ لِّنُبَيِّنَ لَكُمۡۚ وَنُقِرُّ فِي ٱلۡأَرۡحَامِ مَا نَشَآءُ إِلَىٰٓ أَجَلٖ
مُّسَمّٗى ثُمَّ نُخۡرِجُكُمۡ طِفۡلٗا ثُمَّ لِتَبۡلُغُوٓاْ أَشُدَّكُمۡۖ وَمِنكُم مَّن يُتَوَفَّىٰ وَمِنكُم مَّن يُرَدُّ إِلَىٰٓ أَرۡذَلِ
ٱلۡعُمُرِ لِكَيۡلَا يَعۡلَمَ مِنۢ بَعۡدِ عِلۡمٖ شَيۡـٔٗاۚ وَتَرَى ٱلۡأَرۡضَ هَامِدَةٗ فَإِذَآ أَنزَلۡنَا عَلَيۡهَا ٱلۡمَآءَ ٱهۡتَزَّتۡ
وَرَبَتۡ وَأَنۢبَتَتۡ مِن كُلِّ زَوۡجِۭ بَهِيجٖ ٥ ذَٰلِكَ بِأَنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلۡحَقُّ وَأَنَّهُۥ يُحۡيِ ٱلۡمَوۡتَىٰ وَأَنَّهُۥ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ
قَدِيرٞ ٦ وَأَنَّ ٱلسَّاعَةَ ءَاتِيَةٞ لَّا رَيۡبَ فِيهَا وَأَنَّ ٱللَّهَ يَبۡعَثُ مَن فِي ٱلۡقُبُورِ﴾ الحج: ٥-٧.

***“Enyi watu, ikiwa nyinyi mna shaka juu ya kufufuliwa (mnaona***

***haimkiniki kufufuliwa) basi (tazameni namna tulivyokuumbeni). Kwa hakika, tulikuumbeni kwa udongo (mzee wenu nabii Adamu, kisha (tukawa tunakuumbeni nyinyi) kwa manii (mbegu ya uzazi) kisha (hayo manii yanageuka kuwa) kipande cha damu kisha (huwa) kipande cha nyama kinachoumbika (kinachofanyika sura) na kisicho umbika, ili tukubainishieni (uwezo wetu). Nasi tunakituliza matumboni tunachokitaka mpaka muda maalumu. Kisha tunakutoeni kwa hali ya utoto, kisha (tunakuleeni) ili mfikie balehe yenu. Na kuna wanaokufa (kabla ya kufikia hali hii) na katika nyinyi wako wanaorudishwa katika umri dhalili, asijue chochote baada ya kule kujua kwake. Na unaiona ardhi imetulia kimya lakini tunapoyateremsha maji (mvua) juu yake inatingishika na kutuna na kuotesha kila namna ya mimea mizuri. Hayo ni kwa sababu Allah ni haki (yupo) na kwamba yeye huwahuisha wafu na kwamba yeye ni mwenye uwezo wa (kufanya) kila kitu na kwamba Kiyama kitakuja hapana shaka ndani yake, na kwa hakika Allah atawafufua waliomo makaburini".*** Sura Alhaj: 5-7.

Na amesema Mtume (s.a.w.) ***"Halafu litapulizwa Parapanda. Hakuna yeyote atakayelisikia Parapanda hilo ila atainamisha shingo ili kusikiliza kwa makini na watu watakufa. Halafu Allah atashusha - au kupeleka - mvua kama za rasharasha au kivuli. Miili ya watu itamea kutokana na mvua hiyo. Halafu litapulizwa tena Parapanda na hapo watu watasimama wanatazama"***. Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Ama kuthibiti kuhuisha watu kwa utambuzi ni kwamba, Allah amewaonyesha waja wake kuhuisha wafu katika dunia hii. Katika sura Albaqara kuna mifano mitano ya jambo hili. Mfano wa watu Nabii Musa ambao Allah aliwahuisha baada ya kuwafisha, mtu aliyeuawa katika Wana wa Israeli, wale watu waliotoka majumbani mwao wakikimbia mauti, yule aliyepita kijijini akisema: Vipi Allah atawahuisha wafu baada ya kufa kwao? Na ndege wa Nabii Ibrahim.

## TISA: MATUKIO YA KUTISHA YA SIKU YA KIYAMA

Siku ya Kiyama ina matukio ya kutisha na mambo mazito yatakayowafanya wanawake wanaonyonyesha wawasahau watoto wao wanaowanyonyesha, na yatakayowafanya watoto kuwa wazee.

Allah ameyataja matukio ya siku hiyo katika aya nyingi. Miongoni mwa aya hizo ni kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱتَّقُوا۟ رَبَّكُمْ ۚ إِنَّ زَلْزَلَةَ ٱلسَّاعَةِ شَىْءٌ عَظِيمٌ ﴿١﴾ يَوْمَ تَرَوْنَهَا تَذْهَلُ كُلُّ مُرْضِعَةٍ عَمَّآ
أَرْضَعَتْ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمْلٍ حَمْلَهَا وَتَرَى ٱلنَّاسَ سُكَـٰرَىٰ وَمَا هُم بِسُكَـٰرَىٰ وَلَـٰكِنَّ عَذَابَ
ٱللَّهِ شَدِيدٌ﴾ الحج: ١-٢.

***"Enyi watu, mcheni Mola wenu. Hakika, mtetemeko wa Kiyama ni jambo kubwa (kabisa). Siku mtakapo kiona (hicho Kiyama) kila mwanamke anyonyeshae atamsahau (mtoto) amnyonyeshaye, na kila mwenye mimba ataizaa mimba yake (kabla ya wakati kufika), na utawaona watu wamelewa kumbe hawakulewa na lakini adhabu ya Allah ni kali".*** Sura Alhajj 1-2.

Miongoni mwa matukio hayo makubwa ni uteketeaji mkubwa wa ulimwengu na wa kutisha utakaokikumba dunia, milima yake, mbingu zake, nyota zake, jua na mwezi wake. Allah ametufahamisha kwamba ardhi itatikiswa na kupasukapasuka, milima itavunjwavunjwa na kupeperushwa, bahari itawashwa moto na kulipuliwa, mbingu zitachanikachanika na kupeperuka, jua litakunjwa na kutoweka, mwezi utapatwa na nyota zitapukutika na mwanga wake kuzimika.

Kwa sababu ya uzito wa siku hiyo, kafiri atatamani kutoa kila kitu ili aweze kujikomboa aepukane na adhabu. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَلَوْ أَنَّ لِكُلِّ نَفْسٍ ظَلَمَتْ مَا فِى ٱلْأَرْضِ لَٱفْتَدَتْ بِهِۦ﴾ يونس: ٥٤.

***"Na kama kila mtu aliyedhulumu angekuwa na (yote) yaliyomo ardhini, bila shaka angeyatoa fidia (yote kwa) kujikombolea".*** Sura Yunus: 54**.**

Hali itamfikisha kafiri kwenye kutamani kuwatoa kafara watu wake anaowapenda sana ili wao ndio waingie motoni na yeye aokoke asiingie kwenye moto huo. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿يُبَصَّرُونَهُمْ ۚ يَوَدُّ ٱلْمُجْرِمُ لَوْ يَفْتَدِى مِنْ عَذَابِ يَوْمِئِذٍۭ بِبَنِيهِ ﴿١١﴾ وَصَـٰحِبَتِهِۦ وَأَخِيهِ ﴿١٢﴾ وَفَصِيلَتِهِ ٱلَّتِى تُـْٔوِيهِ ﴿١٣﴾
وَمَن فِى ٱلْأَرْضِ جَمِيعًا ثُمَّ يُنجِيهِ ﴿١٤﴾ كَلَّآ ۖ إِنَّهَا لَظَىٰ﴾ المعارج: ١١-١٥.

***"(Ndugu watawezeshwa kutambuana na) Wataonana. Mwenye kosa atatamani ajikomboe katika adhabu ya siku hiyo kwa kuwatoa kafara watoto wake. Na mke wake na ndugu yake. Na jamaa zake wanaomhami. Na (kuwatoa kafara) vyote vilivyomo katika ardhi kisha aokoke, lakini wapi! Kwa hakika, huo ni moto uwakao (barabara)".*** Sura Almaarij: 11-15.

Imepokewa katika Hadithi kwamba, watu watafufuliwa Siku ya Kiyama wakiwa miguu mitupu; hawana viatu, watupu; hawana nguo, wana magovi; hawajatahiriwa, watupu; hawana kitu chochote.

Kisimamo kitakuwa kirefu siku hiyo na jua litashushwa na kuwa karibu na vichwa kiasi cha maili moja. Watu watakuwa katika dimbwi la jasho. Miongoni mwao kuna ambaye jasho litafika kwenye vifundo vya miguu yake, kuna ambaye jasho litafika kwenye magoti yake, kuna ambaye jasho litafika kwenye kiuno chake, kuna ambaye jasho litafika kwenye matiti yake, kuna ambaye jasho litafika kwenye mabega yake na kuna ambaye atazama kabisa ndani ya jasho. Yote hayo ni kwa mujibu wa kiasi cha amali zao.

## KUMI: HESABU NA MALIPO

Maana ya hesabu na malipo ni Allah kuwasimamisha waja wake mbele yake na kuwajulisha amali zao walizozitenda.

Hesabu inajumuisha mambo ambayo Allah atawaambia waja wake, Majibu watakayojibu, hoja na dalili atakazowasimamishia, utoaji ushahidi wa mashahidi, kulipa kisasi baina ya waja, kupimwa kwa amali na mengineyo. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿إِنَّ إِلَيْنَا إِيَابَهُمْ ﴿٢٥﴾ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُم﴾ الغاشية: ٢٥-٢٦.

***"Hakika, marejeo yao ni kwetu. Kisha bila shaka, hisabu yao ni juu yetu".*** Sura Alghashia: 25-26. Pia amesema Allah kuwa:

﴿يَوْمَ يَبْعَثُهُمُ ٱللَّهُ جَمِيعًا فَيُنَبِّئُهُم بِمَا عَمِلُوٓا۟ ۚ أَحْصَىٰهُ ٱللَّهُ وَنَسُوهُ ۚ وَٱللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ شَهِيدٌ﴾ المجادلة: ٦.

***"Siku Allah atakapowafufua wote, awaambiye yale waliyoyatenda. Allah ameyadhibiti, na (wao) wameyasahau. Na Allah ni shahidi wa kila kitu".*** Sura Almujaadala: 6.

Hesabu itakuwa tofauti. Kuna hesabu nzito na nyepesi. Kuna hesabu ya heshima na ukarimu. Kuna hesabu ya karipio na tahayuri. Kuna hesabu ya fadhila na msamaha. Yote hayo atayatawalia (Allah) Mkarimu zaidi wa wakarimu na hakimu muadilifi zaidi wa mahakimu.

Kuhesabiwa kwa waumini wachamungu kutafanyika kwa kuoneshwa amali zao ili wapate kutambua neema ya Allah kwao kwa kuwasitiria amali hizo duniani na kuwapa msamaha wake akhera. Ama makafiri wapinzani, watahesabiwa hesabu nzito na ya kina kwa kuhojiwa kila dogo na kubwa (walilolifanya duniani).

Wakati wa hesabu Malaika wataleta vitabu vya amali ambavyo yamesajiliwa humo matendo na harakati za waja. Ni vitabu ambavyo havikuacha jambo kubwa na dogo ila vimelihifadhi. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَكُلَّ إِنسَٰنٍ أَلْزَمْنَٰهُ طَٰٓئِرَهُۥ فِى عُنُقِهِۦ ۖ وَنُخْرِجُ لَهُۥ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ كِتَٰبًا يَلْقَىٰهُ مَنشُورًا ۝١٣ ٱقْرَأْ كِتَٰبَكَ كَفَىٰ بِنَفْسِكَ ٱلْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيبًا﴾ الإسراء: ١٣-١٤.

***"Na kila mwanadamu tumemfungia (jaza ya) vitendo vyake shingoni mwake, na Siku ya Kiyama tutamtolea daftari (iliyoandikwa ndani yake kila alilolifanya) atakayoikuta imefunuliwa (na aambiwe): Soma daftari yako. Nafsi yako inakutosha leo kukuhesabu".*** Sura Al-israa: 13-14.

Miongoni mwa waja, kuna atakayepewa kitabu chake kwa mkono wa kulia, na kuna atakayepewa kwa mkono wa kushoto nyuma ya mgongo, kama Allah alivyobainisha jambo hilo katika aya zaidi ya moja katika kitabu chake, kama hii isemayo kuwa:

﴿فَأَمَّا مَنْ أُوتِىَ كِتَٰبَهُۥ بِيَمِينِهِۦ ۝٧ فَسَوْفَ يُحَاسَبُ حِسَابًا يَسِيرًا ۝٨ وَيَنقَلِبُ إِلَىٰٓ أَهْلِهِۦ مَسْرُورًا ۝٩ وَأَمَّا مَنْ أُوتِىَ كِتَٰبَهُۥ وَرَآءَ ظَهْرِهِۦ ۝١٠ فَسَوْفَ يَدْعُوا۟ ثُبُورًا ۝١١ وَيَصْلَىٰ سَعِيرًا﴾ الانشقاق: ٧-١٢.

***"Basi ama atakayepewa daftari lake katika mkono wake wa kulia. Basi yeye atahesabiwa hesabu nyepesi. Na atarudi kwa watu wake (peponi) akiwa ni mwenye furaha. Na ama atakayepewa daftari lake nyuma ya mgongo wake. Basi yeye atayaita mauti (yamjie ili afe apumzike na wala hayatomjia). Na ataingia motoni".*** Sura Al-inshiqaaq: 7-12.

Imethibiti katika Suna Sahihi kwamba, umma wa mwanzo kabisa kuhesabiwa katika umma zote ni umma wa Muhammad (s.a.w.). Pia imethibiti kwamba, haki ya mwanzo kabisa atakayohojiwa mja katika haki za Allah ni sala, na haki ya mwanzo kabisa kuhukumiwa baina ya watu ni damu (mauaji). Vilevile kisasi kitapitishwa baina ya watu, ambapo aliedhulumiwa atalipiza kisasi dhidi ya dhalimu.

## KUMI NA MOJA: MIZANI

Maana ya mizani ni ile zana atakayoiweka Allah Siku ya Kiyama kwa ajili ya kupima amali za waja. Ni mizani ya hakika yenye sahani mbili na mhimili kati kati. Zitapimwa kwayo amali. Amali njema zitawekwa kwenye kisahani kimoja na amali mbaya zitawekwa kwenye kisahani kingine. Allah amesema kuwa:

﴿وَنَضَعُ ٱلۡمَوَٰزِينَ ٱلۡقِسۡطَ لِيَوۡمِ ٱلۡقِيَٰمَةِ فَلَا تُظۡلَمُ نَفۡسٞ شَيۡـٔٗاۖ وَإِن كَانَ مِثۡقَالَ حَبَّةٖ مِّنۡ خَرۡدَلٍ أَتَيۡنَا بِهَاۗ وَكَفَىٰ بِنَا حَٰسِبِينَ﴾ الأنبياء: ٤٧.

***"Na tutaweka mizani za uadilifu kwa ajili ya Siku ya Kiyama. Nafsi haitadhulumiwa chochote. Na hata kama jambo lina uzito wa punje ya haradali tutalileta. Na sisi tunatosha kuwa wenye kuhesabu".*** Sura Al-anbiyaa: 47.

Pia amesema Allah kuwa:

﴿وَٱلۡوَزۡنُ يَوۡمَئِذٍ ٱلۡحَقُّۚ فَمَن ثَقُلَتۡ مَوَٰزِينُهُۥ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ ٨ وَمَنۡ خَفَّتۡ مَوَٰزِينُهُۥ فَأُوْلَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ خَسِرُوٓاْ أَنفُسَهُم بِمَا كَانُواْ بِـَٔايَٰتِنَا يَظۡلِمُونَ﴾ الأعراف: ٨-٩.

***"Na kipimo siku hiyo kitakuwa sawa (kabisa cha kulipiwa kila mtu amali zake). Basi watakao kuwa na uzani mzito hao ndio watakao faulu. Na watakaokuwa na uzani hafifu, basi hao ndio waliozitia hasara nafsi zao kwa sababu ya kuzifanyia ujeuri aya zetu".*** Sura Al-aaraaf: 8-9.

Na amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Twahara ni nusu ya imani na 'Alhamdulillahi' inajaza mizani".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

## KUMI NA MBILI: HODHI

Hili ni hodhi la maji yanayoingia kutoka katika mto wa Mtume (s.a.w.) uitwao Kauthar utakaokuwepo katika sehemu ya watu kuhesabiwa Siku ya Kiyama, kabla ya watu hawajapita juu ya Sirati. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿إِنَّآ أَعۡطَيۡنَٰكَ ٱلۡكَوۡثَرَ﴾ الكوثر: ١.

***“Hakika, tumekupa wewe Kauthar (kheri nyingi)”.*** Sura Alkauthar: 1.

Na amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***“Hodhi langu ni (lenye urefu wa) mwendo wa mwezi. Maji yake ni meupe sana kuliko maziwa, na harufu yake ni nzuri sana kuliko ya miski. Bilauri zake ni mfano wa nyota zilioko juu. Atakayekunywa humo hatahisi kiu tena”.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Hodhi ni miongoni mwa vitu ambavyo Allah amemkirimu mja wake Muhammad (s.a.w.) katika siku hiyo kubwa. Waumini watakwenda kuchota hapo, na Hodhi hilo linalindwa. Walioritadi dini ya Allah na waliozusha mambo yasiyomridhisha Allah watafukuzwa wasinywe humo. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***“Mimi nitakutangulieni kwenye Hodhi. Watu miongoni mwenu wataletwa kwangu mpaka nikitaka kuwanywesha watazuiwa wasinifikie. Nami nitasema: Ewe Mola, watu wangu hawa. (Allah) Atasema: Hapana. Wewe hujui yale waliyoyazusha baada yako”.***

## KUMI NA TATU: SIRATI

Hili ni daraja litakalowekwa juu ya Jahanamu watu wapite juu yake kuelekea peponi. Allah amesema kuwa:

﴿وَإِن مِّنكُمۡ إِلَّا وَارِدُهَاۚ كَانَ عَلَىٰ رَبِّكَ حَتۡمٗا مَّقۡضِيّٗا ٧١ ثُمَّ نُنَجِّي ٱلَّذِينَ ٱتَّقَواْ وَّنَذَرُ ٱلظَّٰلِمِينَ فِيهَا جِثِيّٗا﴾ مريم: ٧١-٧٢.

***“Na hakuna yeyote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia (hiyo Jahanamu). Ni wajibu wa Mola wako uliokwisha hukumiwa. Kisha tutawaokoa wale wamchao (Mungu), na tutawaacha madhaalimu humo wamepiga magoti”.*** Sura Maryam: 71-72.

Maulamaa wa Tafsiri wamefasiri kwamba, kufika kwa waumini kwenye Jahanamu ni kupita juu yake. Ama makafiri kufika kwao kwenye Jahanamu ni kwa kutumbukia motoni moja kwa moja. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Na itawekwa Sirati juu ya Jahanamu. Katika Mitume mimi nitakuwa Mtume wa mwanzo kuvuka na umma wangu. Na hakuna yeyote atakayezungumza siku hiyo ila Mitume tu. Na maneno ya Mitume siku hiyo ni: Ewe Mola, Tunaomba Salama! Tunaomba Salama! Katika Jahanamu yapo makulabu mfano wa miba ya mmea wa Saadan. Hakuna anayetambua wingi wake isipokuwa Allah tu. Yatawanyakua watu kwa mujibu wa amali zao. Miongoni mwao kuna atakayezamishwa na amali zake, na kuna ambaye kulabu zitamjeruhi kisha atasalimika".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**Na katika wasifu wa kulabu hizo ni kwamba** ni kali sana kuliko upanga, mwembamba kuliko unywele na ni wenye kuteleza. Haitatulia miguu ya mtu katika Sirati hiyo ila tu yule ambaye Allah atakayemjaalia miguu yake itulie. Waumini watapita kwenye Sirati kwa mujibu wa amali zao. Miongoni mwao kuna atakayepita kama vile kufumba macho na kufumbua, kuna atakayepita kama umeme, kuna atakayepita kama upepo, kuna atakayepita kama ndege, kuna atakayepita kama farasi, kuna atakayepita akienda mbio na wa mwisho atapita kama mtu anayevutwa kwa nguvu.

## KUMI NA NNE: DARAJA

Daraja hili ni mahali palipo baina ya pepo na moto. Waumini watasimamishwa mahali hapo baada ya kuvuka Sirati na kuokoka na moto ili walipiziane visasi viliopo baina yao kabla ya kuingia peponi. Wakimalizana visasi na kutakasika ndio watapewa ruhusa na kuanza kuingia peponi. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Waumini wataepushwa na moto na watawekwa kwenye Daraja lililopo baina ya pepo na moto. Watamaliziana hapo kulipana baadhi ya vitu walivyodhulumiana duniani. Wakishakuwa safi, watapewa ruhusa ya kuingia peponi. Nina apa kwa (jina la) Yule ambaye nafsi ya Muhammad iko mkononi mwake kwamba, hakika kila mmoja wao ataijua vizuri nyumba yake ya peponi kuliko alivyokuwa akiijua***

***nyumba yake ya duniani”.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

## KUMI NA TANO: PEPO NA WASIFU WAKE

Pepo ni nyumba ya neema ambayo Allah ameiandaa huko Akhera kwa ajili ya waumini. Allah amesema kuwa:

﴿وَأُدْخِلَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ جَنَّٰتٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِمْ تَحِيَّتُهُمْ فِيهَا سَلَٰمٌ﴾ إبراهيم: ٢٣.

***“Na wale walioamini na kufanya vitendo vizuri wataingizwa katika mabustani yapitayo mito mbele yake, wakae milele humo kwa idhini ya Mola wao. Kuamkiana kwao humo ni amani”.*** Sura Ibrahim: 23.

Miongoni mwa sifa za pepo zilizotajwa katika Qur’ani na Hadithi ni kwamba, peponi kuna mito yenye kupita, majumba ya ghorofa, wake wazuri. Pia kuna kila nafsi inachotamani na kupendeza machoni na ambavyo havijawahi kusikika masikioni, wala kuonekana machoni, wala kuhisiwa moyoni. Harufu ya pepo inahisika kutokea umbali wa mwenendo wa miaka arubaini. Neema kubwa kabisa humo ni waumini kumuona Mola wao wazi wazi.

Pepo ina daraja mia moja. Baina ya kila daraja na jingine ni kama baina ya mbingu na ardhi. Pepo ya juu kabisa ni pepo ya Firdaus. Paa lake ni Arshi ya Rahman (Allah mwingi wa rehema). Ina milango minane. Upana wa kila mlango ni sawa na masafa baina ya Makka na Al-ahsaa’ (kilomita elfu moja). Daraja ya mtu wa chini kabisa peponi ni mithili ya dunia mara kumi. Pepo imeumbwa na ipo hivi sasa. Allah ameiandaa kwa ajili ya waja wake wachamungu. Allah amesema kuwa:

***“Na uendeeni upesi upesi msamaha wa Mola wenu na pepo (yake) ambayo upana wake (tu) ni (sawa na) mbingu na ardhi. (Pepo) iliyowekewa wamchao Mungu”.*** Sura Aal-imraan: 133.

Neema za peponi hazimaliziki na haziondoki. Ni za kudumu; hazikatiki. Watu wa peponi watadumu milele humo. Amesema Allah kuwa:

﴿ جَزَآؤُهُمۡ عِندَ رَبِّهِمۡ جَنَّٰتُ عَدۡنٖ تَجۡرِي مِن تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدٗاۖ رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنۡهُمۡ وَرَضُواْ عَنۡهُۚ ذَٰلِكَ لِمَنۡ خَشِيَ رَبَّهُۥ ﴾ البينة: ٨.

***“Malipo yao kwa Mola wao ni mabustani ya kudumu ambayo mito inapita mbele yake, wakae humo milele. Allah Amewaridhia, nao wamemridhia. (Malipo) Hayo ni kwa yule anayemuogopa Mola wake”.*** Sura Albayyina: 8.

## KUMI NA SITA: MOTO NA WASIFU WAKE

Moto ni nyumba ya adhabu ambayo Allah ameiandaa huko akhera kwa ajili ya makafiri na waovu wenye kufanya maasi. Allah amesema kuwa:

﴿ وَكَذَٰلِكَ حَقَّتۡ كَلِمَتُ رَبِّكَ عَلَى ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ أَنَّهُمۡ أَصۡحَٰبُ ٱلنَّارِ ﴾ غافر: ٦.

***“Namna hivi limewathibitikia makafiri neno la Mola wako ya kwamba wao ni watu wa motoni”.*** Sura Ghaafir: 6.

Miongoni mwa sifa za moto kama zilivyotajwa katika Qur’ani na Sunna ni kwamba, ndani ya moto kuna aina nyingi na tofauti za adhabu kali na mateso makali. Kuni za moto huo ni watu na mawe. Chakula cha huko ni mti wa Zakum, na kinywaji chake ni usaha na maji ya moto. Moto wa duniani ni sehemu moja ya sehemu sabini za moto wa Jahanamu, na umeuzidi kwa mara sitini na tisa. Zote zimefanana kwa joto.

Moto una ngazi tofauti zinazopishana kwa adhabu. Moto una milango saba na kila mlango una gawio maalumu (la watu watakaoingia kupitia hapo). Walinzi wake ni Malaika wakali, wenye hasira na wasiokuwa na huruma. Malaika hao hawatosheki na wanotiwa humo na kutumbukizwa chini kabisa, bali watauliza kwamba: Je, kuna ziada?

Moto umeshaumbwa na upo hivi sasa. Allah ameuandaa moto huo kwa ajili ya makafiri. Adhabu ya moto ni ya kudumu, haikatiki wala haiondoki. Watu wa motoni ni makafiri watakao kaa humo milele. Amesema Allah kuwa:

﴿إِنَّ ٱللَّهَ لَعَنَ ٱلۡكَٰفِرِينَ وَأَعَدَّ لَهُمۡ سَعِيرًا ٦٤ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدٗاۖ لَّا يَجِدُونَ وَلِيّٗا وَلَا نَصِيرٗا﴾ الأحزاب: ٦٤-٦٥.

***"Kwa hakika Allah amewalaani makafiri na amewaandalia moto (unaowaka kweli kweli). Watakaa humo daima. Hawatapata kipenzi wala msaidizi".*** Sura Al-ahzaab: 64-65.

Ama waumini waliotenda maovu na maasi wataadhibishwa, na baadae watatolewa, kimsingi, kwa rehema za Allah Rahimu zaidi wa wenye huruma na pia kwa maombezi ya wenye kuombea. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Allah atawaingiza watu wa peponi peponi. Atamuingiza amtakaye kwa rehema zake, na atawaingiza watu wa motoni motoni, halafu atasema kuwa: Tazameni. Mkimkuta mtu ambaye katika nafsi yake kuna imani yenye uzito wa punje ya haradali mtoeni. Watatolewa humo maungo yakiwa yameshaungua na kubaki mifupa. Watatiwa kwenye mto wa uhai, na wataota kama yaotavyo majani pembeni mwa mto"***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

## KUMI NA SABA: FAIDA ZA KUAMINI SIKU YA MWISHO

Kuamini Siku ya Mwisho kuna faida kubwa. Miongoni mwa faida hizo ni hizi zifuatazo:

**a)** Kuamini Siku ya Mwisho kunaleta utulivu ndani ya nafsi ya Muislamu, kwa sababu anakuwa na yakini kwamba, dunia hii itatoweka, ni nyumba ya mpito na kwamba akhera ndio nyumba ya kudumu na ndio kwenye furaha ya kudumu au huzuni ya milele.

**b)** Kuamini Siku ya Mwisho kunamfanya mja ashindane na kufanya haraka katika kutenda kheri na kujiepusha na mambo ya haramu, kwa sababu anakuwa na yakini kwamba, ataulizwa juu ya yote hayo mbele ya Allah.

**c)** Katika kuamini Siku ya Mwisho kuna maliwazo kwa Muislamu juu ya raha na mapambo ya dunia anayoyakosa. Analiwazika kwa kuamini kuwa kuna neema za akhera na thawabu zake anazozitarajia.

**d)** Kuamini Siku ya Mwisho ni msingi wa kutengemaa kwa maadili

ya mtu binafsi na jamii. Mwanadamu anapoamini kwamba, Allah atawafufua viumbe baada ya kufa kwao, atawahesabu, atawalipa kwa mujibu wa amali zao na atamlipizia aliyedhulumiwa dhuluma yake kutoka kwa aliyedhulumu, atasimama imara katika kumtii Allah, na mzizi wa maovu utakatika na, kwa sababu hiyo, kheri na amani vitaenea katika jamii.

**e)** Kujua uadilifu wa Allah, fadhila na hekima zake kwakuwa Allah anamlipa mweye kustahiki thawabu kwa fadhila zake, na anamlipa mwenye kustahiki adhabu kwa uadilifu wake.

# NGUZO YA SITA

# KUAMINI QADARI

Kuamini Qadari ni nguzo ya sita katika nguzo za imani ambazo ni wajibu kwa Muislamu kuziitakidi, na bila ya nguzo hizi imani yake haiwi sahihi. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi sahihi ya malaika Jibrili, Allah ampe amani, pale alipomuuliza Mtume (s.a.w.) kuhusu imani, na Mtume akajibu kuwa imani ni: ***"Wewe kumuamini Allah na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume wake na Siku ya Mwisho na uamini Qadari; kheri yake na shari yake".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**Kuamini Imani Qadari** ni kuwa na itikadi thabiti kwamba, Allah ni Muumbaji wa kila kitu, Mlezi wake na mmiliki wake. Amepanga mambo ya viumbe kabla hajawaumba. Amepanga mauti yao, riziki zao, amali zao na hatima ya kheri au ya shari. Yote hayo yapo kwake ameyaandika katika Ubao Uliohifadhiwa (Allauhul Mahfuudh). Kila kheri na kila shari inatokea kwa uamuzi wa Allah na mipango yake. Halitokei jambo ulimwenguni isipokuwa tu analijua na ametaka litokee. Hakuna jambo linaloweza kutokea bila ya utashi wake na bila ya mipango yake. Amesema Allah kuwa:

﴿ إِنَّا كُلَّ شَيْءٍ خَلَقْنَٰهُ بِقَدَرٍ ﴾ القمر: ٤٩.

***"Kwa hakika, sisi tumekiumba kila kitu kwa Qadari (mpango mahususi)".*** Sura Alqamar: 49. Pia amesema Allah kuwa:

﴿أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ ٱللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِى ٱلسَّمَآءِ وَٱلْأَرْضِ ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ فِى كِتَٰبٍ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى ٱللَّهِ يَسِيرٌ﴾

الحج: ٧٠.

***"Je, hujui kwamba Allah anajua yaliyomo mbinguni na ardhini? Bila ya shaka, (yote) hayo yamo kitabuni (mwake). Hakika (kudhibiti)***

***hayo kwa Allah ni jambo dogo (sana)”.*** Sura Alhajj: 70**.**

Allah anajua yaliyotokea, yanayotokea na yasiyotokea na kama yangetokea yangetokeaje. Analolitaka linakuwa na asilolitaka haliwi. Allah ndiye Muumba wa waja na Muumba wa matendo yao. Allah anasema kuwa:

﴿وَٱللَّهُ خَلَقَكُمۡ وَمَا تَعۡمَلُونَ﴾ الصافات: ٩٦.

***“Na Allah amekuumbeni nyinyi na mnayoyafanya”.*** Sura Assaaffat: 96.

Waja ni watendaji wa matendo yao kiuhakika, kwa sababu Allah amewapa waja utashi na uwezo wa kutenda. Utashi na uwezo wa wanadamu unatokea kwa matakwa ya Allah. Amesema Allah kuwa:

﴿لِمَن شَآءَ مِنكُمۡ أَن يَسۡتَقِيمَ ۝٢٨ وَمَا تَشَآءُونَ إِلَّآ أَن يَشَآءَ ٱللَّهُ رَبُّ ٱلۡعَٰلَمِينَ﴾ التكوير: ٢٨-٢٩.

***“Kwa yule miongoni mwenu anayetaka kushika njia iliyo nyooka. Na nyinyi hamtataka isipokuwa tu atake Allah Mola wa walimwengu wote”.*** Sura Attakwiir: 28-29.

Lililo wajibu kwa Muislamu ni kuamini Qadari yote; kheri yake na shari yake, tamu yake na chungu yake, na kwamba hayo yanatoka kwake. Mja akipata kheri ni wajibu wake kumsifu Allah na kmshukuru kwa mpango wake mzuri na kwa fadhila na hisani aliyomfanyia. Allah anasema kuwa:

﴿وَمَا بِكُم مِّن نِّعۡمَةٖ فَمِنَ ٱللَّهِ﴾ النحل: ٥٣.

***“Na neema yoyote mliyonayo, basi imetoka kwa Allah”.*** Sura Annahl :53.

Kuzitendea haki neema na fadhila za Allah ni mja kumshukuru Allah kwa ulimi wake na azitumie pia ziwe msaada kwake katika kumtii Allah. Allah amesema kuwa: “Walikuwa wakimfanyia alipendalo, kama ngome na masanamu na mabunguu makubwa kama mahodhi, na masufuria makubwa sana yasiyoondolewa mahali pake. (Tukawaambia**):**

﴿ٱعۡمَلُوٓاْ ءَالَ دَاوُۥدَ شُكۡرٗا﴾ سبأ: ١٣.

***"Fanyeni (amali nzuri) enyi watu wa Daudi kwa kushukuru (neema mlizopewa)".*** Sura Sabai: 13.

Inatakiwa athari ya neema ionekane kwa mja, kwa sababu kuionesha neema na kuihadithia ni namna mojawapo ya namna za kushukuru neema. Amesema Allah kuwa:

﴿وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ﴾ الضحى: ١١.

***"Na neema ya Mola wako isimulie".*** Sura Adh- dhuhaa: 11.

Likimsibu mja jambo asilolipenda miongoni mwa mambo yaliyopangwa na Allah, anapaswa kufanya mambo kadhaa yafuatayo:

**KWANZA:** Awe na subira juu ya alichokadiriwa; asife moyo, asipaparike na ajue kwamba lililomfika halikupangwa kumkosa, na lililomkosa halikupangwa kumfika. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Kwa hakika, wewe hutapata ladha ya kweli ya imani mpaka utambue kwamba, lililokufika halikupangwa likukose na lililokukosa halikupangwa likufike"***. Hadithi hii imepokewa na Abudaudi.

**PILI**: Aridhike na aikubali Qadari, kwa sababu hiyo ndio imani kamilifu juu ya ulezi wa Allah kwamba, yote anayoyatenda Allah na anayo yaamua ni ya kheri, ni ya uadilifu na ya busara.

Muislamu akiwa na imani hii atapata utulivu na raha ya nafsi kwa yaliyopangwa na Allah yamtokee. Kwa sababu hiyo, hawi na haraka au wasiwasi kwa kupoteza anachokipenda au kufikwa na jambo la maudhi. Atamshukuru Allah kwa kila hali, kwa sababu anajua kwamba yote yanayomtokea ni kwa Qadari ya Allah Mmiliki wa mbingu na ardhi na yatatokea tu; hakuna jinsi. Amesema Allah kuwa:

﴿مَآ أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ فِي ٱلْأَرْضِ وَلَا فِيٓ أَنفُسِكُمْ إِلَّا فِي كِتَٰبٍ مِّن قَبْلِ أَن نَّبْرَأَهَآ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى ٱللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾ لِّكَيْلَا تَأْسَوْاْ عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرَحُواْ بِمَآ ءَاتَىٰكُمْ ۗ وَٱللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ﴾ الحديد: ٢٢-٢٣.

***"Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwishaandikwa katika kitabu (cha Allah) kabla hatujauumba.***

***Kwa yakini, hilo ni jambo dogo kwa Allah. Ili msihuzunike sana juu ya kitu kilichokupoteeni (na kinachokupoteeni), wala msifurahi sana kwa alichokupeni (na kwa anachokupeni). Na Allah hampendi kila mwenye majivuno, ajifaharishaye sana".*** Sura Alhadid: 22-23.

Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Yanastaajabisha mambo ya Muislamu. Mambo yake yote ni kheri, na haya hayapatikani isipokuwa kwa Muislamu tu. Akipata ya kufurahisha anashukuru na hiyo inakuwa kheri kwake, na akifikwa na ya kuhuzunisha anakuwa na subira na hiyo inakuwa kheri kwake".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**TATU:** Kuchukua hatua ya kufanya baadhi ya sababu zinazoweza kuondosha anayoyachukia katika mambo yaliyopangwa na Allah, kwa sababu Allah ameyawekea mambo yaliyopangwa sababu za kuyaondoa na kuyazuia, ikiwa na pamoja na dua, sadaka, dawa na mengineyo.

Kutumia sababu hakupingani na kuamini Qadari au kumtegemea Allah katika kuleta kheri na kuondoa shari. Kufanya hivyo ndio utegemezi kamili wa kumtegemea Allah. Kwenye hili, Mtume (s.a.w.) Allah ametupa maelekezo kwa kauli yake isemayo kuwa: ***"Fanya bidii kwenye jambo lenye manufaa na wewe, na muombe msaada Allah, na usishindwe (usifanye uzembe). Na likikukifika jambo usiseme: 'Kama ningefanya (hivi) ingekuwa hivi na hivi'. Lakini sema: '(Hii ni) Qadari ya Allah na analolitaka linakuwa', kwa sababu neno 'kama' linafungua amali za shetani".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

# DHAMBI ZILIZOHADHARISHWA NA UISLAMU

## YA KWANZA: UCHAWI

**1) Maana ya uchawi**:

Uchawi ni vifundo vinavyopuliziwa (vinavyotabanwa) au maandishi ya kishirikina yasiyofahamika maana, yanayotamkwa au kuandikwa na mchawi, au mchawi kutengeneza kitu kinacholeta athari katika mwili au moyo au akili ya anayerogwa kwa njia ya siri na kificho. Mazingaombwe ni miongoni mwa uchawi. Mazingaombwe ni harakati fulani za haraka haraka zinazofanywa kwa kutumia mkono na zinazomdhanisha mtu aone kitu fulani ni kweli kumbe sio kweli.

**2) Aina za uchawi:** Uchawi uko wa aina mbili:

**a.** Kiinimacho na mazingaombwe. Hivi ni vitu visivyokuwa na ukweli au vinaweza kuwa ukweli lakini mtu hawezi kuujua ukweli huo ila baada ya kufumbuliwa.

**b.** Uchawi wa hakika na wenye athari katika mwili. Uchawi huu husababisha maradhi na madhara kwa aliyerogwa.

**3) Hukumu ya uchawi na kujifunza uchawi:**

Uchawi ni miongoni mwa matendo ambayo Uislamu umeyaharamisha, bali umeharamishwa na sheria zote za mbinguni, ni mojawapo ya mambo yanaymtoa mtu katika Uislamu na ni mojawapo ya Madhambi Makubwa. Qur'ani, Hadithi sahihi za Mtume na makubaliano ya wanazuoni yametamka wazi uharamu wa uchawi. Allah amesema kuwa:

﴿ إِنَّمَا صَنَعُوا۟ كَيْدُ سَٰحِرٍ ۖ وَلَا يُفْلِحُ ٱلسَّاحِرُ حَيْثُ أَتَىٰ ﴾ طه: ٦٩.

***"Kwa hakika, walichofanya ni vitimbi vya mchawi, na mchawi hafaulu popote afikapo".*** Sura Taahaa: 69. Pia Allah amesema kuwa:

﴿وَلَٰكِنَّ ٱلشَّيَٰطِينَ كَفَرُواْ يُعَلِّمُونَ ٱلنَّاسَ ٱلسِّحۡرَ﴾ البقرة: ١٠٢.

"***Na lakini mashetani ndio waliokufuru; wanawafundisha watu uchawi".*** Sura Albaqara: 102.

Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa, amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Yaepukeni mambo saba yaangamizayo. Swahaba wakasema: Ewe Mjumbe wa Allah, ni yapi mambo hayo? Mtume akasema: Ni kumfanyia ushirika Allah na uchawi…".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Mtume amebainisha (katika Hadithi hii) kwamba, uchawi ni katika Madhambi Makubwa ambayo inapasa kujiepusha nayo na ni haramu kuyatenda.

Kutokana na hayo, tunajifunza kwamba uchawi ni haramu na ni moja ya milango ya kuingia katika ukafiri na kumfanyia ushirika Allah. Mchawi hawi mchawi ila kwa kufanya mambo ambayo kwayo anakuwa kafiri, kama vile kujiweka karibu na majini na mashetani na kuwaomba msaada.

Aghlabu mchawi hafanyi uchawi wake ila tu kwa kuwadhuru wengine na kuwasababishia maumivu. Allah ameyaelezea hayo aliposema kuwa:

﴿فَيَتَعَلَّمُونَ مِنۡهُمَا مَا يُفَرِّقُونَ بِهِۦ بَيۡنَ ٱلۡمَرۡءِ وَزَوۡجِهِۦۚ وَمَا هُم بِضَآرِّينَ بِهِۦ مِنۡ أَحَدٍ إِلَّا بِإِذۡنِ ٱللَّهِۚ وَيَتَعَلَّمُونَ مَا يَضُرُّهُمۡ وَلَا يَنفَعُهُمۡ﴾ البقرة: ١٠٢.

***"Kwa hiyo, wanajifunza kwao yale mambo ambayo kwayo wanafarakanisha kati ya mtu na mkewe, na wao si wenye kumdhuru yeyote kwa uchawi huo isipokuwa tu kwa idhini ya Allah, na wanajifunza mambo ambayo yanawadhuru na hayawanufaishi'.*** Sura Albaqara:102.

Mazingaombwe na viinimacho vya kichawi vinaingia katika hukumu ya uharamu, kwa sababu ni sehemu ya uchawi. Mtume Mussa, Allah ampe amani, aliwashutumu vikali wachawi wa Firauni na kuwaelezea

kuwa ni waharibifu. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿فَلَمَّآ أَلْقَوْا۟ قَالَ مُوسَىٰ مَا جِئْتُم بِهِ ٱلسِّحْرُ ۖ إِنَّ ٱللَّهَ سَيُبْطِلُهُۥٓ ۖ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُصْلِحُ عَمَلَ ٱلْمُفْسِدِينَ﴾ يونس: ٨١.

***“(Wachawi) Walipotupa (kamba zao) Mussa alisema: Mlichokuja nacho ni uchawi. Kwa yakini, Allah ataubatilisha. Kwa yakini, Allah hastawishi vitendo vya waharibifu (mafisadi)”.*** Sura Yunus: 81. Allah amewapa sifa ya uchawi pamoja na kwamba walichokifanya kilikuwa ni mazingaombwe na taswira danganyifu. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿فَإِذَا حِبَالُهُمْ وَعِصِيُّهُمْ يُخَيَّلُ إِلَيْهِ مِن سِحْرِهِمْ أَنَّهَا تَسْعَىٰ﴾ طه: ٦٦.

“***Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana kwake, kutokana na uchawi wao, kwamba zinakweda mbio”.*** Sura Twaha: 66.

Vitendo hivyo, pamoja na kuwa havikuwa uchawi, lakini vinafanana na vitendo vya kichawi na vinaleta athari za kimazingaombwe na taswira danganyifu ndani ya nyoyo za wanaoufuatilia.

**4) Hukumu ya kwenda kwa wachawi:**

Mtu anakwenda kwa mchawi kwa sababu ya mojawapo ya mambo mawili:

**a.** Kutafuta tiba ya mgonjwa kwa wachawi.

**b.** Kumfuata mchawi afanye uchawi ili kumdhuru mtu mwengine au kumvuta mpenzi au kutafuta kitu kilichopotea. Kwa sababu yoyote ile, kwenda kwa wachawi ni jambo lililoharamishwa katika dini ya Kiislamu. Abdallah Bin Masoud, Allah amuwiye radhi, amemnukuu Mtume (s.w.a.) akisema kuwa: ***“Mtu yeyote atakayemuendea mpigaramli au mchawi au mtabiri akayakubali anayoyasema, basi ameyakufuru yaliyoteremshwa kwa Muhammad (s.a.w.)”.*** Ameipokea Hadithi hii Abuuyaalaa.

Na imepokewa kwa Imraan Bin Huswein akimnukuu Mtume (s.a.w.) kwamba, amesema kuwa: ***“Si miongoni mwetu apigae ramli au apigiwae ramli, au anayeamini mkosi au anayeaminishwa mkosi”. Imran amesema: Nadhani Mtume (s.a.w) alisema pia “au alifanya uchawi au aliyefanyiwa uchawi”***. Hadithi hii imepokewa na Tabaraaniy.

Pia imenukuliwa kwa Jabir, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***“Mtume (s.a.w.) aliulizwa kuhusu Nushra, akasema: (Nushra) ni katika matendo ya shetani”.*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad na Abudaudi. Hassan Albaswriy amesema kuwa: “ Nushra ni uchawi”. Maana ya Nushra hapa ni kuondoa (kutibu ) uchawi kwa kutumia uchawi.

Ukiongezea kwenye katazo hilo la wazi (kama tulivyoona ) ni kwamba, mtu akienda kwa mchawi kwa malengo tuliyoyataja hapo awali, basi ndani ya mtu huyo kuna mafungamano na mahusiano na kitu kingine badala ya Allah ambaye yeye ndiye mwenye uwezo wa kudhuru na kunufaisha. Kufanya hivyo ni kumuunga mkono na kumkubali mchawi juu ya vitendo vyake na ukafiri anaoufanya. Jambo hili halitakiwi kwa Muislamu anayemuamini Allah Mtukufu.

## PILI: UTABIRI, RAMLI NA UNAJIMU

### 1) Utambulisho wake:

**Utabiri** ni kueleza habari za mambo yasiyo onekana kwa macho (Ghaibu) kwa msaada wa majini; sawa mambo hayo yawe yamepita au yanayokuja. Yule anayejihusisha na hayo huitwa Mtabiri.

**Ramli** ni kudai kujua mambo yasiyo onekana kwa macho (Ghaibu) kwa njia ya kuchora ardhini, au kusoma kiganja au kwa njia nyingine yoyote. Anayeyafanya hayo huitwa Mpigaramli.

**Unajimu** ni kudai kujua mwenendo wa nyota angani, na kwamba nyota hizo zina athari kwa maisha ya hapa duniani. Mnajimu ni mtu anayezitazama nyota akidai kuwa ndio zenye kuleta taathira katika matukio ya duniani, ikiwemo mvua, upepo, joto, baridi, kheri, shari,

furaha na majonzi.

### 2) Hukumu ya Utbiri, Ramli na Unajimu

Utabiri, upigaji ramli na unajimu ni haramu katika dini ya Allah, ni katika Madhambi Makubwa na ni miongoni mwa milango ya kumkufuru Allah Mtukufu. Haifai kwa Muislamu kujifunza mambo hayo wala kuyafanya wala kwenda kwa wataalamu wake. Mtume (s.a.w.) ameweka wazi hatari ya mambo haya katika imani ya mtu na amali zake njema. Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa, amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Yeyote mwenye kwenda kwa Mtabiri au Mpigaramli akakubali anayosema, basi ameyakufuru yale yaliyoteremshwa kwa Muhammad".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Hakim na Baihaqiy. Pia imepokewa kwa Sofia akiwanukuu baadhi ya wake wa Mtume (s.a.w) kwamba, Mtume (s.a.w) amesema kuwa: ***"Yeyote atakayemuendea mpigaramli akamuuliza kuhusu jambo lolote, sala zake hazitakubaliwa kwa siku arubaini".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Imenukuliwa pia kwa Ibniabbas, Allah awawiye radhi, akisema kuwa, amesema Mtume wa Allah (s.a.w) kwamba: ***"Mtu atakayejifunza kidogo tu elimu ya nyota, basi huwa amechuma sehemu ya uchawi, huzidi kadiri anavyozidi".*** Onyo hili kali kwa wanaokwenda kwa watabiri, wapigaramli na wanajimu linaonesha wazi jinsi dhambi hii ilivyokuwa kubwa. Hii ni kwa kuzingatia yafuatayo:

**a.** Utabiri, unajimu na upigaji ramli ni aina ya uchawi.

**b.** Kujihusisha na mambo hayo ni kudai kujua Ghaibu (mambo yasiyo onekana kwa macho) ambayo hakuna aijuwae ila Allah Mtukufu tu.

**c.** Utabiri, unajimu na upigaji ramli ni kufungua mlango wa uzushi na uongo, pamoja na kujenga mahusiano na mafungamano na vitu vingine badala ya Allah.

### 3) Vitendo ambavyo vinaingia katika Utabiri, Unajimu na Ramli

Yanaingia katika utabiri na ramli mambo mengi. Miongoni mwa

hayo ni haya:

**a.** Kuita mizungu. Kuita mizungu ni mtu kudai kuziita na kuzileta roho za watu waliokufa, kuzungumza nao, kuwaomba ushauri katika kutatua matatizo, kuwaomba msaada wa kutibu wagonjwa, kufichua vilivyojificha na kutabiri yatakayotokea.

**b.** Kusoma kiganja, kikombe na karata. Hii ni mtu kudai kujua wasifu na hali ya baadae ya mtu kwa kuangalia michoro ya kiganja chake au mipindomipindo ya kahawa katika kikombe au kwa kuangalia karatasi ya karata.

**c.** Kutabiri kwa kutumia kuchezea nyumba za chaza kwa namna ya kuzichanganyachanganya ili kujua hali ya baadae ya mtu.

**d.** Kuchora kwenye mchanga. Hii ni mchawi kudai kujua hali ya baadae ya mtu mwengine kwa kusoma mistari aliyoichora kwenye mchanga.

**e.** Kusoma nyota. Hii ni kudai kujua wasifu wa watu na kuwatabiria maisha yao ya baadae kwa kujengea juu ya sayari au nyota ambayo mtu anahusishwa nayo.

Bila shaka aina na matendo yote haya yanaingia katika utabiri, ramli na unajimu, na ni kudai kujua Ghaibu ambayo hakuna aijuwaye ila Allah tu.

Yeyote atakayetumia moja tu kati ya haya anakuwa ameingia katika mambo yaliyoharamishwa na sheria, na pia anaingia katika onyo la Mtume (s.a.w). Kwa hiyo, haifai kujifunza mambo haya wala kwenda kwa wanaoyatumia, wala kuwakubalia wayasemayo, hata kama ikitokezea kama walivyotabiri. Mambo hutokea kwa mujibu wa mpango wa Allah. Watabiri, wapigaramli na wanajimu wao ni kama alivyotubainishia Mtume (s.a.w) kwamba, wanatoa habari fulani baada ya kupewa na watumishi wao majini na wanaongeza ya kwao ya uongo mara mia moja. Kwa sababu hiyo, asiyejua upotofu wao hudhania kuwa wanayoyasema yanatokea kama walivyoyatabiri bila kuzingatia uongo walioujaza katika maneno yao. Abuhuraira,

Allah amuwiye radhi, amemnukuu Mtume (s.a.w) akisema kuwa: ***“Allah akihukumu jambo mbinguni Malaika hupiga mbawa zao wakiinyenyekea kauli yake, kama mnyororo upitao juu ya jiwe laini (la kinoo) (wakiwa wamezimia). “Inapoondolewa hofu nyoyoni mwao wanasema: Mola wenu anasema nini? Watasema”*** kumwambia amesema ***“haki, naye ndiye aliye juu, Mkubwa”. Sura Sabai: 23. Basi shetani mviziaji atalisikia neno hilo, na kila mmoja humpa mwengine na huwa wamepandiana mmoja juu ya mwengine. Sufiani ametoa wasifu kwa viganja vyake na kuvipandanisha kimoja juu ya kingine. Na mviziaji hulisikia neno na kulipeleka kwa aliye chini yake mpaka linashuka katika ulimi wa mchawi au mtabiri. Huenda akapigwa na kimondo kabla hajalishusha au hufanikiwa kulishusha kabla hajapigwa na kimondo. Na yeye hudanganya mara mia moja, na husemwa, kwani siku fulani si aliwahi kutuambia hivi na hivi, na hapo husadikiwa kwa lile neno moja ambalo limesikika kutoka mbinguni”.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

## HIRIZI NA AZIMA

Miongoni mwa mambo ambayo Uislamu umeyahadharisha na kuwakataza wafuasi wake, kutokana hatari yake katika itikadi yao na Tawhidi yao, ni kuvaa hirizi na azima, na kuzitegemea katika kuondoa mambo wanayohofu kuwadhuru au kuleta mambo wanayo ona yana manufaa kwao.

### 1) Maana ya hirizi:

Hirizi ni kitu avaacho mtu au kuvishwa mnyama au kutundikwa kwenye kipando (chombo cha usafiri), kama vile kitambaa, uzi, mfupa au vinavyofanana na hivyo kwa lengo la kukinga kijicho au shari au kuvuta kheri na manufaa.

### 2) Hukumu ya kuvaa hirizi:

Kufunga au kuvaa hirizi ni katika mambo yaliyoharamishwa na Uislamu, kwa sababu ni katika matendo maovu ya makafiri katika zama za ujinga (Jaahiliyya). Mtume (s.a.w.) amehadharisha sana na

kubainisha kwamba matendo hayo ni katika njia za kujitumbukiza katika Shirki. Imenukuliwa kwa Ibnimasoud, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: Nilimsikia Mtume wa Allah akisema kwamba: ***"Hakika, zinguo na hirizi na dawa za uganga wa mapenzi ni Shirki"***. Ameipokea Hadithi hii imam Ahmad na Abudaudi na Ibnimajah.

Pia imenukuliwa kwa Ukba Bin Amir, Allah amuwiye radhi, akisema kwamba: ***"Mtume (s.a.w.) alifikiwa na kundi la watu fulani, akawapa mkono wa kukubali kiapo cha utiifu (Bay-ah) watu tisa na mmoja wao akamkatalia. Swahaba wakasema: Ewe Mtume wa Allah, kwa nini umewapa mkono watu tisa na kumkatalia mmoja? Mtume akasema: Huyu amevaa hirizi. Aliuingiza mkono wake akaikata ile hirizi na akampa mkono na akasema: Atakayevaa hirizi amefanya Shirki".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Abuyaalaa na Hakim.

Mtu akiwa na itikadi kwamba hirizi, zenyewe zinanufaisha au zinadhuru na sio Allah (s.w), hii ni Shirki ya wazi inayomtoa mtu katika Uislamu. Tunamuomba atukinge na hilo.

Ama mtu akiwa na itikadi kwamba hirizi hizo ni sababu alizoziweka Allah za kujikinga na shari, kijicho na majini, hii ni Shirki ndogo, kwa sababu Allah hakuzifanya hirizi ni sababu ya masuala hayo.

### 3) Baadhi ya aina za hirizi:

Kuna aina nyingi za hirizi zilizoharamishwa katika Uislamu. Baadhi yake ni za zamani zilizorithiwa na nyingine mpya za kisasa, lakini lengo lake ni moja. Lengo ni kuondoa mabalaa au kuvuta manufaa. Zote hizo hazina tofauti kwamba hukumu yake ni haramu tu.

Miongoni mwa aina za hirizi ni **Tiwala** (Uganga wa Mapenzi). Tiwala ni kitu anachokifanya mke kumfanyia mumewe kwa madai ya kuzidisha mapenzi kwa kila mmoja wao kumpenda mwenzie.

Miongoni mwa aina za hirizi ni kwato za farasi, kiatu kidogo, shanga za rangi ya bluu, picha za jicho na kiganja, kufunga (kuvaa) nyuzi au kipande cha kitambaa mkononi au shingoni au kiunoni,

kutundika aina maalumu za chaza au karatasi zenye michoro na talasimu.

## NNE: KUAMINI NUKSI NA UCHURO

Miongoni mwa mambo ambayo Uislamu umeyaharamisha na kuamrisha kujiepusha nayo ni kuamini nuksi, kwa sababu mambo hayo yana athari mbaya kwa usafi wa Tawhidi na imani ya Muislamu.

### 1) Maana ya Nuksi:

Nuksi ni mtu kuamini kukumbwa na jambo baya kwa sababu ya kitu alichokiona au kukisikia, kama mtu kuamini kupata mkosi kwa kusikia sauti ya kunguru au kumuona bundi.

### 2) Aina za kuamini Nuksi:

Aina za kuamini nuhusi ni nyingi sana kwa watu. Miongoni mwa hizo ni hizi: kuamini kupata mkosi kwa kumuona mtu mwenye chongo au kunguru au bundi au paka mweusi au kutokea kwa ajali, au kuamini mwezi fulani una mkosi au siku fulani au namba fulani, au jicho kutikisika na mengineyo.

### 3) Hukumu ya kuamini Nuksi:

Kuamini nuksi ni miongoni mwa mambo yaliyoharamishwa na Uislamu, kwa sababu yana athari katika kuidhoofisha itikadi na imani ya kuamini maamuzi ya Allah na Qadari yake. Mtume (s.a.w) amelihesabu jambo hilo kuwa ni aina ya Shirki. Imepokewa kwa Ibnimasoud, Allah amuwiye radhi, akimnukuu Mtume (s.a.w) kwamba amesema kuwa: ***"Kuamini Nuhusi ni Shiriki, Kuamini Nuhusi ni Shiriki, Kuamini Nuhusi ni Shiriki".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi na Tirmidhiy. Pia imenukuliwa kwa Abdallah Bin Amri (r.a.) akisema kuwa, amesema Mtume wa Allah kwamba: ***"Mtu yeyote ambaye kuamini nuksi kumemzuia asifanye jambo (alilopanga kulifanya) basi amefanya Shirki".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad.

Kuamini nuhusi kumefanywa ni Shirki kwa sababu watu wanaamini

kwamba mambo hayo wanayo ona yana mkosi ndiyo yanayoleta manufaa au madhara. Kwa kufanya hivyo, ni kama vile wameyafanya mambo hayo ni mshirika wa Allah katika kudhuru na kunufaisha, jambo ambalo linapingana na itikadi anayotakiwa kuwa nayo Muislamu ya kuamini kwamba suala hilo la kudhuru na kunufaisha liko mkononi mwa Allah peke yake. Allah amesema kuwa:

﴿وَإِن يَمْسَسْكَ ٱللَّهُ بِضُرٍّ فَلَا كَاشِفَ لَهُۥٓ إِلَّا هُوَ ۖ وَإِن يُرِدْكَ بِخَيْرٍ فَلَا رَآدَّ لِفَضْلِهِۦ﴾ يونس: ١٠٧.

***“Na kama Allah akikugusisha madhara, basi hakuna yoyote wa kuyaondoa isipokuwa yeye tu. Na kama atakutakia kheri basi hakuna yeyote wa kuzuia fadhila zake”.*** SuratYunus: 107.

Pia kuamini nuksi au mkosi kunapingana na ibada ya kumtegemea Allah, na kunamfungulia mwanadamu mlango wa hofu na kujenga mahusiano na mafungamano na vitu vingine badala ya Allah.

**4) Tiba ya tatizo la kuamini mikosi:**

Inaweza ikaingia katika moyo wa mtu hali ya kuamini nuksi na, kwa sababu hiyo, akakumbwa na wasiwasi na mfadhaiko kwa sababu ya watu kumueleza kuwa wao pia walikumbwa na mikosi au nuhusi. Haya yanaingia moyoni kwa sababu tu ya wasiwasi wa shetani na udhaifu wa kumtegemea Allah. Hapa ndio tunamkuta Mtume (s.a.w) anato tiba ya suala hili. Imenukuliwa kwa Abdallah Bin Amri (r.a.) akisema kuwa, amesema Mtume wa Allah kwamba: ***“Mtu yeyote ambaye kuamini nuksi kumemzuia asifanye jambo (alilopanga kulifanya) basi amefanya Shirki. Swahaba waliuliza: Ewe Mjumbe wa Allah, ni nin kafara ya hilo? Mtume alijibu: Mmoja wao aseme hivi: Ewe Mola wetu, hakuna kheri ila kheri yako tu, na hakuna shari ila shari yako tu, na hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila wewe tu”.*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad.

Wahaka wa moyo unaotokana na kuhisi nuksi ni vigumu sana kwa mtu kuepukana nao, lakini inawezekana kuuondoa kwa kumtegemea Allah. Amesema Ibnimasoud, Allah amuwiye radhi, kuwa: ***“Na hakuna yeyote miongoni mwetu ila inamkuta hali hiyo, lakini Allah anaiondoa kwa kumtegemea yeye”.*** Hadithi hii imepokewa na

Ahmad, Abudaudi, Tirmidhy na Ibnimajah.

## TANO: KUMUOMBA MWENGINE BADALA YA ALLAH

Maombi (Dua) ni ibada yenye na nafasi adhimu sana katika dini ya Allah, kwa sababu maombi ni mawasiliano baina ya mja na Mola wake. Allah amesema kuwa:

﴿وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ﴾ البقرة: ١٨٦.

***"Na waja wangu watakapokuuliza kuhusu mimi (waambie) mimi niko karibu (nao), nayajibu maombi ya muombaji anaponiomba. Basi waniitikie na waniamini ili wapate kuongoka".*** Sura Albaqara: 186.

Kwa kuzingatia nafasi hii kubwa ya dua, Mtume ameifanya ni katika aina kuu za ibada. Mtume amesema kuwa: ***"Dua ndio ibada"***. Ameipokea Hadithi hii Abudaudi, Tirmidhiy na Ibnimajah.

### 1) Dua ni anuani ya Tawhidi:

Anaye itafakari ibada ya dua atagundua kwamba dua imekusanya aina tatu za Tawhidi.

Mja, kwa kuomba, anakuwa amethibitisha Tawhidi ya utendaji (Tawhidi Rubuubiyya), kwa sababu mja anakuwa amemkusudia Allah ili amkidhie haja zake na kutatua matatizo yake, kwa kukiri kwake kwamba Allah ni Muweza wa kila jambo, na mambo yote yako mkononi mwake.

Vile vile mja, kwa dua, anakuwa amethibitisha Tawhidi ya ibada (Tawhiid Uluuhiyya), kwa sababu kwa nia yake safi ya kumuomba Allah anakuwa ametangaza uhitaji na udhaifu wake kwa Mola wake, na pia kutangaza utegemezi kwa Mola wake kwa hofu na matumaini; hofu ya kuogopa adhabu zake na matumaini ya kupata thawabu zake.

Pia, kwa kuomba dua, mja anakuwa ametekeleza Tawhidi ya

Majina na Sifa. Hii ni kwa sababu mja anapomuomba Allah huwa kwanza anatanguliza kumsifia kwa sifa na majina yake mazuri yanayostahiki.

**2) Kumuomba mwengine badala ya Allah Mtukufu:**

Allah Mtukufu amewaamrisha waja wake wawe na nia safi ya kumkusudia yeye tu katika maombi yao, na katika hilo wasimshirikishe naye kiumbe yeyote, vyovyote awavyo; awe Malaika aliye karibu na Allah au Mtume au mja mwema. Allah amesema kuwa:

﴿فَٱدۡعُوهُ مُخۡلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ﴾ غافر: ٦٥.

"***Kwa hiyo, muombeni yeye mkimtakasia yeye tu dini (utiifu)".*** Sura Ghafir: 65.

Pia allah amebainisha kwamba, yeyote atakayemuomba mwengine ya yeye atakuwa amejiingiza katika upotevu mkubwa, na pia atakuwa amewaiga makafiri wa zama za ujinga. Allah amesema kuwa:

﴿وَمَنۡ أَضَلُّ مِمَّن يَدۡعُواْ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَن لَّا يَسۡتَجِيبُ لَهُۥٓ إِلَىٰ يَوۡمِ ٱلۡقِيَٰمَةِ وَهُمۡ عَن دُعَآئِهِمۡ غَٰفِلُونَ﴾ الأحقاف: ٥.

***"Na ni nani mpotevu zaidi kuliko yule anayewaomba badala ya Allah wasioweza kumjibu mpaka Siku ya Kiyama na wao hawatambui dua zao?".*** Sura Al-ahqaaf: 5.

Na Allah amesema pia kuwa:

﴿وَمَن يَدۡعُ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ لَا بُرۡهَٰنَ لَهُۥ بِهِۦ فَإِنَّمَا حِسَابُهُۥ عِندَ رَبِّهِۦٓۚ إِنَّهُۥ لَا يُفۡلِحُ ٱلۡكَٰفِرُونَ﴾ المؤمنون: ١١٧.

***"Na yeyote anayemuomba mungu mwengine, pamoja na Allah, asiyekuwa na ushahidi naye basi bila shaka hesabu yake iko kwa Mola wake. Kwa hakika, makafiri hawafanikiwi".*** Sura Almuuminun: 117.

-Imenukuliwa kwa Ibnimasoud, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Yeyote atakayekufa huku***

***akimuomba mwenza badala ya Allah ataingia motoni”.*** Hadithi hii ameipokea Bukhari.

Kutokea hapa, tunajifunza kwamba kuwaomba msaada viumbe wa jambo ambalo hakuna aliwezae ila Allah tu, kunamuingiza mtu katika Shirki kubwa inayomtoa katika dini ya Kiislamu, inayobatilisha matendo yake na kumfanya aishi milele katika moto wa Jahanamu. Tumuombe Allah atukinge na moto.

Ama kumuomba msaada kiumbe wa jambo ambalo ana uwezo nalo, na aombwaye akawa yuko hai (sio maiti) na hayupo mbali, basi sio vibaya kumuomba msaada.

Ikikosekana sharti moja tu kati ya shuruti hizi, basi mja huwa ameipeleka ibada kwa mwengine badala ya Allah.

Hebu tafakari ndugu yangu Muislamu jinsi Allah alivyofanya ni batili kuwaomba viumbe kwa kubainisha udhaifu wao wa kushindwa kuyajibu maombi ya wawaombao. Allah amesema kuwa:

﴿قُلِ ٱدۡعُواْ ٱلَّذِينَ زَعَمۡتُم مِّن دُونِهِۦ فَلَا يَمۡلِكُونَ كَشۡفَ ٱلضُّرِّ عَنكُمۡ وَلَا تَحۡوِيلًا﴾ الإسراء: ٥٦.

***“Sema: waombeni wale mnaodai (kuwa ni waungu) badala yake. Hawataweza kukuondoleeni madhara wala kubadilisha”.*** Sura Israa:56.

Pia Allah akasema jywa:

﴿قُلۡ أَرَءَيۡتُم مَّا تَدۡعُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ أَرُونِي مَاذَا خَلَقُواْ مِنَ ٱلۡأَرۡضِ أَمۡ لَهُمۡ شِرۡكٞ فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِۖ ٱئۡتُونِي بِكِتَٰبٖ مِّن قَبۡلِ هَٰذَآ أَوۡ أَثَٰرَةٖ مِّنۡ عِلۡمٍ إِن كُنتُمۡ صَٰدِقِينَ ٤ وَمَنۡ أَضَلُّ مِمَّن يَدۡعُواْ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَن لَّا يَسۡتَجِيبُ لَهُۥٓ إِلَىٰ يَوۡمِ ٱلۡقِيَٰمَةِ وَهُمۡ عَن دُعَآئِهِمۡ غَٰفِلُونَ ٥ وَإِذَا حُشِرَ ٱلنَّاسُ كَانُواْ لَهُمۡ أَعۡدَآءٗ وَكَانُواْ بِعِبَادَتِهِمۡ كَٰفِرِينَ﴾ الأحقاف: ٤-٦.

***“Sema: Hivi mnawaonaje wale mnaowaomba badala ya Allah? Nionesheni: ni kipi walichokiumba katika ardhi? Au wao wana***

***ushirika mbinguni? Nileteeni kitabu kilichokuwa kabla ya hiki au alama yoyote ya elimu ikiwa mnasema kweli. Na wapotofu wakubwa ni nani kama sio wale wanaowaomba viumbe, badala ya Allah, ambao hawatajibu (maombi yao) mpaka Siku ya Kiyama na wala hawatambui maombi yao. Na watu watakapokusanywa watakuwa maadui zao, na watakana kuabudiwa kwao".*** Sura Ahqaf:4-6.

Hayo ni maelezo ya wazi na ya kutosha kwamba, haifai kuwaomba viumbe badala ya Allah, kwa sababu viumbe hawana uwezo wa kumnufaisha au kumdhuru yeyote. Viumbe hawakushirikiana na Allah katika kuumba wala wao wenyewe hawawezi kuumba kitu. Sasa ni kwa msingi gani viumbe wawaombe viumbe wenzao?

## SITA: KUTAFUTA BARAKA KWENYE MAKUMBUSHO

### 1) Maana ya kutafuta baraka:

Maana ya baraka ni wingi wa kheri na kudumu kwake, na kutafuta baraka ni kuomba kheri zaidi na kuendelea kudumu kwake.

### 2) Aina za kutafuta baraka:

Kheri na baraka ni mambo mawili yaliyomo katika mikono ya Allah ambaye baadhi ya mambo ameyahusisha na kheri na baraka na kuweka ndani yake fadhila na baraka. Mambo yenyewe yamegawanyika katika vigawanyo vingi. Miongoni mwa vigawanyo hivyo ni hivi vifuatavyo:

**Kwanza:** Kutafuta baraka kwenye kauli, kama vile kutafuta baraka kwa kusoma Qur'ani au kwa kuyatamka majina ya Allah na sifa zake, kwa kosoma nyiradi na dua zilizonukuliwa kwa Mtume (s.a.w). Kutafuta baraka kwenye kauli sio kwa kuzifanya mapambo ya nyumba na kuzipachika katika kuta za nyumba, kwenye magari au kwenye mabaraza au maskani. Inavyotakiwa ni mja kudumu juu ya kumkumbuka Allah na kumtakasa kwa majina yake na sifa zake, na kufanya hima ya kusoma Qur'ani itakiwavyo na kuyafanyia kazi mafunzo yake kwa ajili ya kutaka baraka, thawabu, utulivu wa moyo, kusamehewa dhambi na uombezi Siku ya Kiyama.

**Pili:** Kutafuta baraka kwenye sehemu takatifu kama vile mji wa Makka na Msikiti wake Mtukufu, mji wa Madina na Msikiti wake Mtukufu, Masjid Aqswa, Masjid Qubaa na misikiti yote mengine. Hii ni kwa sababu Allah amezipa sifa maalumu za wingi wa fadhila na malipo makubwa.

**Tatu:** Kutafuta baraka kwenye nyakati takatifu, kama vile mwezi wa Ramadhani, usiku wa Lailatulqadri, siku kumi za mwanzo katika mwezi wa Mfunguo Tatu, siku ya Ijumaa, na sehemu ya mwisho ya kila usiku. Mja anatakiwa kujitahidi kufanya ibada nyingi ndani ya sehemu na nyakati kama hizi zenye fadhila na baraka ili apate ujira mwingi, malipo makubwa, mema zaidi pamoja na kupandishwa daraja.

**Nne:** Kutafuta baraka kwenye vitu vitukufu, kwa mfano: maji ya Zamzam na mti wa Mzaituni. Allah amejaalia ndani ya maji ya Zamzam na Mzaituni tiba. Pia kutafuta baraka kwenye maji ya mvua, kwa sababu Allah ameweka ndani yake kheri na manufaa makubwa kwa sababu mvua ni sababu ya kuotesha mimea na kuifufua ardhi iliyokufa.

**Tano:** Kutafuta baraka kwenye matendo mema.

**Sita:** Kutafuta baraka kwa watu wema. Kwa mfano: kutafuta Baraka kwa Mitume, Allah awape amani, na kumbukumbu zao, kutafuta baraka kwa waja wa Allah walio wema ambao wako hai. Hilo linatakiwa kufanyika kwa kufuata muongozo wao, kuiga mwenendo wao, kunufaika na elimu zao na dua zao. Kwa kufanya hivyo, Muislamu atapata manufaa ya dunia na akhera.

### 3) Hukumu ya kutafuta baraka kuliko katazwa:

Kutafuta baraka ni miongoni mwa mambo yasio kubali maoni na ambayo Muislamu katika kuyatenda ni lazime awe na hoja ya kisheria ya Qur'ani na Sunna (Hadithi sahihi za Mtume). Haifai kwa Muislamu kuzusha jambo katika kutafuta baraka bila ya kuwa na hoja sahihi, vinginevyo kutafuta baraka huko kutakuwa haramu na kusikokubalika kisheria.

Kutafua baraka kuliko haramishwa ni miongoni mwa mambo yanayohatarisha imani ya mja, na ni katika njia kuu za kuitia kasoro Tawhidi. Hii ni kwa sababu, mwenye kuamini kupata baraka katika aina fulani ya miti au mawe au baadhi ya makaburi au baadhi ya sehemu au aina fulani ya mchanga au baadhi ya milima na mapango bila ya kuwa na hoja ya kisheria na akaona kwamba, ni halali kujigusisha na kujipangusapangusa kwenye vitu hivyo na kuchukua baadhi ya makumbusho yake, basi atakuwa ameingia katika dhambi kubwa na kwenda kinyume na sheria takatifu.

Imenukuliwa kwa Abuwaqid Allaithiy, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***"Tulitoka pamoja na Mtume (s.a.w) nasi tukiwa tumetoka katika ukafiri hivi karibuni - walikuwa wamesilimu siku ulipokombolewa mji wa Makka -. Tukafika kwenye mti ambao makafiri walikuwa wakitundika silaha zao kwenye mti huo wakikaa hapo kila mwaka. Mti huo unaitwa Dhaat An-waat. Tukasema: Tutengenezee na sisi Dhaat An-waat. Mtume akasema: Allahu Akbar. Mmesema kama walivyosema watu wa Mussa kwamba: Tufanyie sisi mungu kama wao walivyo na miungu*** (Sura Aaraf: 138). ***Kisha Mtume akasema kuwa: Kwa yakini, nyinyi mtafuata nyendo za waliopita kabla yenu".*** Ameipokea Hadithi hii Ahmad, Tirmidhiy na Tabarani.

Mtume (s.a.w.) amefananisha ombi la Waislamu hao la kutaka kuwekewa mti kwa ajili ya kutafuta baraka kwenye mti huo na kupachika silaha zao na kukaa hapo, amefananisha ombi hilo na lile ombi la Wana wa Islrail la kutaka na wao wawekewe mungu pamoja na Allah, ingawa wao hawakuuabudu mti huo wala hawakuuomba.

Pia imenukuliwa kwa Naafii kwamba ***"Zilimfikia Omar, Allah amuwiye radhi, habari kwamba kuna watu wanakwenda kwenye mti - Ni mti Ridhwaan - na kusali hapo. Aliwakemea vikali na kuamrisha mti huo ukatwe na ukakatwa".*** Ameipokea Hadithi hii Ibnuabiishaiba na Ibnisaad.

Imepokewa kwa Maaruur Bin Suweid akisema kuwa: ***"Tulitoka pamoja na Omar, Allah amuwiye radhi, katika safari ya Hija aliyohiji. Alitusomea sura Alfiil na sura Quraish katika sala ya***

***Alfajiri. Alipomaliza Hija yake na kurudi aliwaona watu wakiwa na haraka na kusukumana. Aliuliza: Kuna nini? Wakasema: Huu ni msikiti ambao Mtume alisali. Omar akasema: Hivi ndivyo walivyoangamia Watu wa kitabu (Wayahudi na Wakristo). Waliyafanya makumbusho ya Mitume wao mahekalu (sehemu za ibada). Yeyote atakayefikiwa na sala miongoni mwenu katika msikiti huu, asali. Na ambaye sala haijamfikia humu asisali".*** Ameipokea Hadithi hii Ibnuabiishaiba.

Atakayeamini kuwa mambo hayo yenyewe yananufaisha na kudhuru, au kutoa na kunyima baraka mambo ambayo yanayomuhusu Allah peke yake, hiyo inazingatiwa kuwa ni Shirki inayomtoa mtu katika Uislamu. Ama atakayefanya hayo kwa kutaraji baraka kwa Allah Mtukufu, huyo atakuwa amezusha jambo ambalo Allah hajaliruhusu na kulifanya sheria.

## SABA: KUHAMA KWA ROHO

**1) Maana ya kuhama kwa roho**:

Kuhama kwa roho ni mtu kuwa na itikadi kwamba, roho ikiondoka katika mwili uliokufa inakwenda kuishi kwenye mwili mwingine. Kama mtu alikuwa muovu, roho yake inakwenda kwenye mwili wa mnyama, ikiwa ni adhabu yake. Na kama mtu alikuwa mwema, roho inakwenda katika mwili wa binadamu mwengine. Roho hii inaendelea kuhama kutoka katika mwili hadi mwili mwingine, na hali hii inakuwa haina mwisho.

**2) Hukumu ya kuamini kuhama kwa roho:**

Mtu mwenye kuitafakari itikadi ya kuhama kwa roho atagundua kwamba, itikadi hii inapingana na sharia na dini za mbinguni kwa njia nyingi:

**a)** Roho ni umbile la Ghaibu na ni siri miongoni mwa siri za Allah Mtukufu ambazo amejipendelea yeye tu kuzijua. Hakuna ajuae hakika yake ila yeye tu. Allah amesema kuwa***:***

﴿وَيَسۡـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلرُّوحِۖ قُلِ ٱلرُّوحُ مِنۡ أَمۡرِ رَبِّي وَمَآ أُوتِيتُم مِّنَ ٱلۡعِلۡمِ إِلَّا قَلِيلٗا﴾ الإسراء: ٨٥.

***"Na wanakuuliza kuhusu roho. Sema: Roho ni miongoni mwa jambo la Mola wangu, na nnyinyi hamkupewa katika elimu ila kidogo tu".*** Sura Israa: 85.

**b)** Njia ya kujua mambo ya Ghaibu, ikiwemo roho, ni Wahyi wa Allah ambao ameuteremsha kwa Mitume na Manabii wake. Je, iko wapi hoja sahihi juu ya uzushi huu?

**c)** Hali halisi ya maisha ya duniani na misingi ya taaluma za kisayansi zinasisitiza kwamba, uzushi huu ni batili. Hakuna uvumbuzi wowote wa kisayansi unao onesha kuwepo utaratibu wa roho kuhama au kujivua na kujivika katika viwiliwili vingine. Siri ya kifo na maisha ya kaburini haiwezekani kuyagundua au kuyavumbua kwa vifaa. Ukweli huu unatilia mkazo kwamba, roho ni jambo la Ghaibu ambalo binadamu hana uwezo wa kujua siri yake na hakika yake kwa kuangalia na kwa majaribio.

## NANE: KUOGOPA MAJINI NA MASHETANI

Hofu kwa binadamu inagawika katika vigawanyo vitatu:

**Kigawanyo cha kwanza**: **Ni hofu ya asili**, kama kuogopa adui, nyoka, simba n.k. Hofu ya aina hii inakubalika na ipo kwa viumbe wote, hata kwa Mitume. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿فَخَرَجَ مِنۡهَا خَآئِفٗا يَتَرَقَّبُۖ قَالَ رَبِّ نَجِّنِي مِنَ ٱلۡقَوۡمِ ٱلظَّٰلِمِينَ﴾ القصص: ٢١.

***"Basi (Mussa) akatoka katika mji huo akiwa na hofu huku anangoja (lipi litamfika). Akasema: Ewe Mola wangu, niokoe dhidi ya watu madhalimu".*** Sura Al-qasas: 21.

**Kigawanyo cha pili: Ni hofu ya kuwaogopa viumbe** inayosababisha kuacha mambo ya wajibu au kufanya mambo ya haramu, kama mtu kutoa ushahidi wa uongo kwa kumuogopa mtu mwenye nguvu au mamlaka. Mtume, Allah ampe rehema na amani, ameielezea hofu hii

kwa kusema kuwa: ***"Kamwe, kuwaogopa watu kusimzuie mmoja wenu kusema ukweli".*** Ameipokea Hadithi hii Ahmad na Ibnihibban. Aina hii ya hofu ni haramu, kwa sababu ina mahusiano na haki za watu.

**Kigawanyo cha tatu: Ni hofu ya siri**. Hii ni hofu ya kumuogopa kiumbe kwa jambo ambalo hakuna aliwezaye ila Allah tu, kama kuwaogopa majini, mashetani, wachawi au watu wa mazingaombwe, kwa kuamini kuwa wana uwezo binafsi wa kumnufaisha au kumdhuru binadamu.

Aina hii ya hofu ni miongoni mwa ibada za moyoni ambazo haifai kuzielekeza kwa yoyote ila kwa Allah tu. Haitakiwi iwepo katika moyo wa mwanadamu hofu isipokuwa tu ya kumuogopa Allah, kwa sababu yeye ndiye mwenye kudhuru, mwenye kunufaisha, ndiye muumbaji wa kheri na shari na mpangaji wa haya mambo ya viumbe na kuyawekea sababu zitoazo taathira.

Viumbe, wawe majini au mashetani, wao si chochote isipokuwa tu ni sababu alizoziweka Allah ili kupitisha alilolipanga na kulihukumu. Kwa sababu hiyo, Muislamu hatakiwi kuviogopa viumbe hivyo kwa dhati yake, kwa sababu Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ﴾ آل عمران: ١٧٥.

***"Msiwaogope na niogopeni mimi ikiwa nyinyi ni waumini (wa kweli)***". Sura Aal-imraan: 175.

Mtu akiwa na hofu hii, anakuwa ameingia katika Shirki kubwa. Tunamuomba Allah atukinge nayo.

Na miongoni mwa mambo yasiyokuwa na shaka ni kwamba, majini na mashetani ni viumbe dhaifu sana kuliko mwanadamu muumini ambaye moyo wake ameujaza imani na kuustawisha kwa ibada. Hii ni kwa mujibu wa ushahidi wa kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿فَقَٰتِلُوٓاْ أَوۡلِيَآءَ ٱلشَّيۡطَٰنِۖ إِنَّ كَيۡدَ ٱلشَّيۡطَٰنِ كَانَ ضَعِيفًا﴾ النساء: ٧٦.

***“Basi piganeni na marafiki wa shetani. Hakika, hila za shetani ni dhaifu”.*** Sura Annisaa: 76.

Pia majini na mashetani ni viumbe dhaifu sana kuliko muumini, kwa sababu Allah Mtukufu hakuwapa nguvu yoyote juu ya waja wake waumini. Allah amesema kuwa:

﴿ إِنَّ عِبَادِى لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَٰنٌ ۚ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ وَكِيلًا ﴾ الإسراء: ٦٥.

***“Hakika, waja wangu huna mamlaka juu yao, na Mola wako anatosha kuwa mlinzi”.*** Sura Al-israa: 65.

Mtume, Allah ampe rehema na amani, ametueleza kwamba shetani anawaogopa waumini pale alipomwambia Omar kuwa***: “Kwa yakini kabisa, shetani anakuogopa ewe Omar”.*** Ameipokea Hadithi hii Tirmidhiy.

Na sio kwamba jambo hili linamhusu Omar tu, bali kila ambaye imani yake imekuwa na nguvu, na moyo wake ukajenga mahusiano na Allah pekee, anakuwa kama alivyo Omar. Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kwamba Mtume (SAW) amesema kuwa: ***“Hakika Muislamu huwataabisha mashetani wake kama mmoja wenu anavyomtaabisha ngamia wake katika safari”.*** Ameipokea Hadithi hii Ahmad.

Miongoni mwa yanayo onesha udhaifu wa mashetani ni kwamba, hawawezi kuhimili kusikiliza jina la Allah likitajwa au Adhana au nyiradi au Takbira. Mashetani huikimbia sehemu litwajapo jina la Allah. Pia hawawezi kufungua mlango uliofungwa au chombo kilichofunikwa iwapo vitasomewa jina la Allah.

**LAKINI NINI CHANZO CHA MWANADAMU KUWAOGOPA MAJINI NA MASHETANI?**

Jibu la swali hilo lipo katika kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿ إِنَّمَا سُلْطَٰنُهُۥ عَلَى ٱلَّذِينَ يَتَوَلَّوْنَهُۥ وَٱلَّذِينَ هُم بِهِۦ مُشْرِكُونَ ﴾ النحل: ١٠٠.

***“Ilivyo ni kwamba, nguvu yake ni juu ya wale wanaomfanya***

***rafiki (wakamfuata), na wale wanaofanya naye Shrki”.*** Sura Annahl: 100.

Pia Allah amesema kuwa:

﴿وَأَنَّهُۥ كَانَ رِجَالٌ مِّنَ ٱلْإِنسِ يَعُوذُونَ بِرِجَالٍ مِّنَ ٱلْجِنِّ فَزَادُوهُمْ رَهَقًا﴾ الجن: ٦.

***“Na ilivyo ni kwamba, kulikuwa na wanadamu wanaume wakitafuta kinga kwa majini wanaume, kwa hiyo wakawazidishia uzito, (Uzito wenyewe ni kama hivi: Wenye pepo wakataka hao mapepo kuchezewa ngoma na kuchinjiwa wanyama”.*** Sura Aljinn: 6.

Na akasema tena Allah kuwa:

﴿أَلَمْ تَرَ أَنَّآ أَرْسَلْنَا ٱلشَّيَٰطِينَ عَلَى ٱلْكَٰفِرِينَ تَؤُزُّهُمْ أَزًّا﴾ مريم: ٨٣.

***“Je, huoni kwamba sisi tumewatuma mashetani kwa makafiri, wakiwachochea (kufanya mabaya)?”.*** Sura Maryam :83.

Yule ambaye moyo wake hauna imani, akaacha kumtaja Allah na pia akaacha kuomba hifadhi kwake, basi huyo huvamiwa na mashetani, humkera na moyo wake hujazwa hofu ya kuwaogopa, kwa sababu ya kule kukosa kumtegemea Allah Mtukufu, nusra yake, hifadhi na ulinzi wake. Kwa sababu hiyo, anakuwa hana kinga itakayomzuia na shari zao.

Hofu ya kuwaogopa majini ikifimfikisha mja kwenye itikadi kwamba, majini wana uwezo wa kumletea madhara bila ya kuwepo sababu, hii ni hofu ya siri ambayo ni Shirki Kubwa. Tunamuomba Allah atukinge nayo.

Ama hofu ya kuwaogopa majini na mashetani itakapokuwa imetokana na udhaifu wa kibinadamu, na kwa sababu hiyo mwanadamu akawa anaogopa madhara na uovu wao kwa sababu maalumu, kama vile kuingia sehemu zilizohamwa au zenye kiza, hii inaingia katika hofu ya asili, kwa sababu majini na mashetani kwa asili yao ni kero kwa wanadamu. Hofu hii haingii katika hofu iliyo haramu ya Shirki.

## TISA: KUSHEREHEKEA NA KUSHIRIKI SIKUKUU ZISIZOKUWA ZA WAISLAMU

Sikukuu za mataifa na za kidini huzingatiwa kuwa ni utambulisho na anuani ya itikadi zao za kidini. Kila taifa lina sikukuu yake linayoisherehekea, na kujiwekea utaratibu maalumu kulingana na itikadi zake. Hayo ameyaashiria Mtume (s.a.w.) pale aliposema kuwa: ***"Kila watu wana sikukuu yao, na hii ni sikukuu yetu".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**1) Muislamu kusherehekea na kushiriki sikukuu zisizokuwa za Waislamu:**

Kwa vile sikukuu inawakilisha itikadi ya mwenye kusherekea, na ni utambilisho wake ambao anajivunia, Uislamu umejitambulisha kwa sikukuu zake ili ziwe kielelezo cha utambulisho wa itikadi yake thabiti na ya kudumu. Kwa sababu hiyo, Uislamu umekataza kusherehekea sikukuu zote ambazo Allah hakuziidhinisha katika sheria ya dini hii. Imenukuliwa kwa Anas Bin Maalik, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***"Mtume alifika Madina na kukuta wenyeji wake wana siku mbili wakicheza katika siku hizo. Akauliza: Siku mbili hizi zina nini? Wakasema: Tulikuwa tukicheza katika siku hizi zama za ujinga (kabla ya Uislamu). Mtume wa Allah (s.a.w.) akasema: Kwa yakini, Allah amekubadilishieni siku bora zaidi kuliko hizo. Ni siku ya kuchinja (Idd El-adh-haa) na siku ya kufungua (Idd Elfitri)".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad na Abudaudi. Kwa hiyo, utaona kwamba Mtume (s.a.w.) hakuwakubalia Swahaba wake kufurahia sikukuu za wakati wa kabla ya Uislamu kulingana na mazoea yao. Aliwabainishia kuwa Allah amewawekea sikukuu bora kuliko za kwao. Kwa sababu hiyo si sahihi kukusanya pamoja kilichobadilishwa na kilichobadilishiwa.

Hivi ndivyo walivyofahamu Wema Waliotangulia wa umma huu, ikiwa ni pamoja na Swahaba na Taabiina (kizazi kinachowafuatia Swahaba). Wema Waliotangulia walitahadharisha sana suala la kushirikiana na wasiokuwa Waislamu katika sikukuu zao. Imenukuliwa kwa Omar, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***"Jitengeni na maadui wa Allah katika sikukuu zao".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

Na imenukuliwa kwa Abdallah Bin Amri Bin Al-aas, Allah amuwiye radhi yeye na baba yake, akisema kuwa: ***"Yeyote aliyejenga (na kuishi) kwenye miji ya Waajemi akafanya sherehe za sikukuu zao na maadhimisho yao na akajifananisha nao mpaka akafikia kufa akiwa bado yumo katika hali hiyo, atafufuliwa pamoja nao Siku ya Kiyama".*** Ameipokea Hadithi hii Al-bayhaiy.

Na imenukuliwa kwa Ibniabbas, Allah amuwiye radhi yeye na baba yake, katika kuitafsiri kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿وَٱلَّذِينَ لَا يَشۡهَدُونَ ٱلزُّورَ﴾ الفرقان: ٧٢.

***"Na ambao hawashuhudii uzushi".*** Sura Alfurqan:72**.** Amesema Ibniabbas kuwa uzushi uliotajwa katika ayah hii ni ***"Sikukuu za makafiri".*** Kauli hii imepokewa na Alkhatib katika kitabu chake cha Taariikh Baghdad. Na Ibnisiirin ametafsiri uzushi uliotajwa katika aya hiyo kuwa ni ***"Sikukuu ya Matawi".*** Sikukuu ya Matawi ni miongoni mwa sikukuu za Wakristo. Pia imenukuliwa kwa Rabii Bin Aas akisema kuwa uzushi uliotajwa katika aya hiyo ni ***"Sikukuu za makafiri".***

Kwa hiyo Muislamu ameamrishwa kuwa tofauti na wasiokuwa Waislamu katika itikadi zao na desturi zao, kwa sababu kujifananisha na sura ya nje kunapelekea kujifananisha na yaliyoko moyoni. Mtume ameyatahadharisha hayo kwa kusema kuwa: ***"Ajifananishaye na watu (fulani) basi yeye ni miongoni mwao".*** Ameipokea Hadithi hii Ahmad na Abudaudi.

**2) Hukumu ya kuwapongeza wasiokuwa Waislamu katika sikukuu zao:**

Kupongeza maana yake ni kuomba dua baada ya furaha kwa sababu ya kuja upya kwa neema au kuondoka kwa balaa. Watu hupongezana kwa kadiri ya kiasi cha mapenzi yaliopo baina yao yaliyotokana na kuchanganyikana na kujuana.

Viongozi wa Kiislamu wamebainisha kwamba kuwapongeza wasiokuwa Waislamu kwa kutumia nembo za dini zao na sikukuu

zao zinazowahusu ni miongoni mwa mambo yaliyoharamishwa, kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni. Kwa sababu hiyo, haifai kuwaombea baraka katika sherehe zao na pia haifai kuwapa pongezi katika sikukuu zao, hata kama wao watawapongeza Waislamu katika sikukuu zao. Hii ni kwa sababu Muislamu anaamini kwamba dini yake ndio ya haki na mafunzo yake ni ya haki, na kwamba dini nyingine zilizopotoshwa na wafuasi wake au walizo zibuni kwa mikono yao ni batili.

Kwa sababu sikukuu ni sehemu isiyokubali kujitenga ya itikadi, ndio maana sikukuu za wasiokuwa Waislamu ni miongoni mwa upotevu wao ambao haifai kwa Muislamu kuwaunga mkono wala kuwapa pongezi, kwa sababu kutoa pongezi za sikukuu hizo ni kuziunga mkono na pia ni kuunga mkono upotevu uliomo katika sikukuu hizo. Haifai kwa Muislamu kuwaunga mkono wapotevu katika upotevu wao.

Kwa kumalizia, masuala haya ambayo tumeelezea sehemu yake yana umuhimu mkubwa sana. Kwa hiyo, inampasa Muislamu kufanya hima ya kujua hukumu zake ili kulinda imani yake isije ikachanganyika na yanayoweza kuichafua au kuiondoa kabisa, ili akaonane na Mola wake akiwa radhi, mwenye kuridhiwa, mwenye kulipwa na kupewa thawabu.

# MLANGO WA TATU

# IBADA ZA MUISLAMU

## SHERIA ZA TOHARA

Tohara ni nusu ya Imani, ni ufunguo wa sala, ni sharti kuu la sala na ni tendo la kwanza alifanyalo anayetaka kusali, kwa sababu sharti hukitangulia kilichowekewa sharti hilo. Tohara ni ibada ambayo mwenye kusali anaifanya kwa ajili ya kujiweka karibu na Allah. Kwa sababu hiyo, Allah amewasifu watu wa Qubaa kwa kusema kuwa:

﴿ فِيهِ رِجَالٌ يُحِبُّونَ أَن يَتَطَهَّرُوا۟ ۚ وَٱللَّهُ يُحِبُّ ٱلْمُطَّهِّرِينَ ﴾ التوبة: ١٠٨.

"***Humo wamo watu wanaopenda kujitoharisha, na hakika Allah anawapenda wenye kujitoharisha".*** Suratu Attauba: 108 .

Na Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Usafi ni nusu ya imani".*** Ameipokea Hadithi hii Muslim.

Katika mlango huu, tutazungumzia: Maana ya Tohara katika lugha ya Kiarabu na katika sheria, vigawanyo vya maji yanayotumika katika kujitoharisha, sheria za vyombo ambavyo maji huhifadhiwa humo, taratibu za kwenda chooni na kunawa; mambo ambayo kwa kawaida yanafanyika kabla ya kutawadha. Halafu tutaeleza sheria za Udhu na masuala yanayuhusiana na Udhu ikiwa ni pamoja na kupaka maji viatu (khofu), sheria za kuoga na kutayamamu ambako kunafanyika wakati wa kukosa maji au wakati wa kushindwa kuyatumia.

### KWANZA: MAANA YA TOHARA

**Tohara katika lugha ya Kiarabu** ni kusafisha uchafu wa maada, kama vile mkojo na kinyesi, au uchafu wa maanani kama vile Shirki na dhambi. Allah amesema kuwa:

﴿ إِنَّمَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنكُمُ ٱلرِّجْسَ أَهْلَ ٱلْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا ﴾ الأحزاب: ٣٣.

***"Ilivyo ni kwamba, Allah anataka kukuondoleeni uchafu enyi watu wa nyumba (ya Mtume) na kukutoharisheni (kukusafisheni) kabisa kabisa".*** Sura Al-ahzaab: 33.

**Tohara katika sheria ya Kiislamu** ni kuondoa Hadathi na Najisi.

**Maana ya Hadathi** ni hali iliyokuwepo katika mwili inayomzuia Muislamu kutekeleza ibada ya sala na ibada nyingine.

**Hadathi zipo za aina mbili**: Hadithi Ndogo. Hii inamfanya Muislamu alazimike kutawadha, kama vile kutokwa na upepo. Nyingine ni Hadathi Kubwa. Hii ni ile inayomfanya Muislamu alazimike kuoga, kama kutokwa na Manii kwa matamanio. Mtu mwenye Hadathi anaitwa Muhdith (asiye tohara).

Maana ya kuondoa Najisi ni kuondoa na kusafisha Najisi mwilini, nguoni au sehemu ya kusalia.

## PILI: VIGAWANYO VYA MAJI

Maji yana vigawanyo vitatu:

**1) Maji tohara.**

Haya ni maji halisi yaliyo katika umbile lake la asili; sawa yawe yametoka ardhini au yametoka mawinguni, kama vile maji ya chemchemi, bahari, mito, visima na mvua.

**Hukumu ya maji haya** ni tohara na yenye kufaa kukitoharisha kitu kingine. Yanaondoa Hadathi Ndogo na, kwa maana hiyo, yanafaa kutawadhia, na pia yanaondoa Hadathi Kubwa na, kwa maana hiyo, yanafaa kuogea ili kuondoa Janaba. Pia yanasafisha Najisi. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَيُنَزِّلُ عَلَيْكُم مِّنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً لِّيُطَهِّرَكُم بِهِۦ﴾ الأنفال: ١١.

***"Na anakuteremshieni maji kutoka mawinguni ili akutoharisheni kwayo".*** Sura Al-nfaal :11.

Mtume (s.a.w.) katika kuyaelezea maji ya bahari amesema kuwa: ***"Ni tohara maji yake, ni halali mfu (maiti) wake"***. Ameipokea Hadithi hii Abudaudi, Tirmidhiy, Nasaai na Ibnimaajah.

Maji yakichanganyika na kitu ambacho ni tohara. kama vile

majani ya miti au mkunazi au kitu kingine tohara na kitu kisiwe na asilimia kubwa kwenye maji hayo, maji hayo ni tohara yanayofaa kutoharisha kwayo.

**2) Maji tohara yasiyofaa kutoharishia kitu kingine**. Haya ni maji ambayo imebadilika sana rangi yake au ladha yake au harufu yake kwa sababu ya kukutana na kitu tohara kilichobadilisha jina lake mpaka, kwa mfano, yakawa kama vile siki, na kuondoa sifa ya utohara. Hukumu ya maji haya ni kwamba inafaa kuyatumia kwa matumizi mengine, lakini sio kwa kuondoa Hadathi au kusafisha Najisi.

**3) Maji yaliyonajisika.**

Haya ni maji ambayo imeingia humo Najisi na kubadilisha mojawapo ya sifa zake tatu: ladha yake, rangi yake au harufu yake.

**Najisi** ni uchafu ambao Mwislamu inampasa kujiepusha nao na kusafisha kitu au mahali ulipoingia. Najisi ni kama vile mkojo wa binadamu, kinyesi cha binadamu, damu yenye kutiririka na nyinginezo.

Muislamu pindi akiyatilia shaka maji juu ya kuingia Najisi au kukosa utohara wake, atajengea hakika (ambayo ni hii isemayo kwamba, **Msingi katika vitu ni utohara**). Na hali ikimchanganya mtu baina ya maji yapi yanayofaa kujitoharishia na yapi yasiyofaa kujitoharishia, basi atapaswa kuacha kuyatumia yote na atatayamamu.

## TATU: SHERIA ZA VYOMBO

**1) Maana ya vyombo:**

Chombo ni kifaa ambacho hutumiwa kuhifadhia maji na vitu vingine. visivyokuwa maji. Jambo la msingi katika vyombo ni kwamba ni halali kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿هُوَ ٱلَّذِى خَلَقَ لَكُم مَّا فِى ٱلْأَرْضِ جَمِيعًا﴾ البقرة: ٢٩

“***Ni yeye aliyekuumbieni vyote vilivyomo ardhini*”.** Sura Albaqara :29.

**2) Masharti ya vyombo:**

Katika kuvitumia vyombo kuna masharti matatu:

**Sharti la kwanza ni**: Vyombo viwe tohara. Haifai kutumia vyombo vilivyotengezwa kutokana na ngozi ya mbwa au nguruwe katika kujitoaharishia, kwa sababu ngozi za wanyama hao hazitohariki, si kwa kuwachinja wanyama hao wala kwa ngozi zao kufanyiwa usafi wa kutumia kemikali. Vile vile haifai kutumia vyombo vilivyotengenezwa kutokana na ngozi ya mfu, isipokuwa tu kama ngozi hiyo ni ya mnyama ambaye ni halali kula nyama yake, iwapo ngozi hiyo itasafishwa. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Ngozi ikisafishwa basi imeshatoharika".*** Ameipokea Hadithi hii Muslim.

**Sharti la Pili ni:** Vyombo viwe vinamilikiwa na mtumiaji au amepewa idhini ya kuvitumia. Kwa sababu hiyo, si halali kujitoharisha kwa kutumia vyombo vilivyoibwa wala vile ambavyo mwenyewe hakuruhusu kutumiwa.

**Sharti la tatu ni:** Vyombo visiwe vimekatazwa na sheria kuvitumia. Kwa maana hiyo haifai, katika kujitoharisha, kutumia vyombo vya dhahabu na fedha na vilivyo chovywa kwenye madini hayo. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Msinywe katika vyombo vya dhahabu na fedha wala msile kwenye sahani zake, kwa sababu vyombo hivyo ni vyao (makafiri) duniani na ni vyetu sisi (Waislamu) huko akhera".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Katazo la kuvitumia vyombo vya dhahabu na fedha katika kujitoharisha au kunywa, linawahusu wanaume na wanawake. Muislamu akitumia vyombo vya dhahabu na fedha au chombo kilichoibwa na mfano wake katika kujitoharisha: atapata dhambi na Tohara yake ni sahihi.

Inafaa kutumia chombo kilichozibwa kwa fedha kidogo ikitokezea haja. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Anas, Allah amuwiye radhi, ambaye ameeleza kwamba ***"Glasi ya Mtume (s.a.w.) ilivunjika na Mtume akaweka sehemu ya ufa fedha kidogo".*** Ameipokea Hadithi

hii Bukhari.

**3) Hukumu ya kutumia vyombo vya wasiokuwa Waislamu na nguo zao:**

**a.** Kimsingi vyombo vya wasiokuwa Waislamu ni Tohara, kwa sababu Mtume (s.a.w.) ***"Alimimina maji kutoka katika chombo cha mwanamke kafiri na akawapa watu wanywe na pia akampa mwanaume mmoja ambaye alipatwa na Janaba ili aoge kwayo".*** Ameiokea Hadithi hii Bukhari.

**b.** Pindi ikafahamika kwa wasiokuwa Waislamu kwamba wanatumia vyombo katika Najisi, basi itapasa kuviosha vyombo hivyo kabla ya kuvitumia. Hii ni kwa mujibu wa nukuu ya Abuthaalaba Alkhushaniy, Allah amuwiye radhi, aliyesema kuwa: ***"Nilimuuliza Mtume kwamba: Ewe Mtume wa Allah, sisi tunaishi katika nchi ya Watu wa Kitabu (Wakristo na Wayahudi). Je, tule kwenye vyombo vyao? Mtume akasema: Ikiwa mtapata vyombo vingine badala ya vya kwao basi msile kwenye vyombo hivyo, na iwapo hamtapata vyombo vingine basi viosheni kisha kuleni kwenye vyombo vyao hivyo".*** Ameipokea Hadithi hii Bukhari na Muslim.

**c.** Nguo zilizotengenezwa na wasiokuwa Waislamu ni Tohara. Pia inafaa kuvaa nguo walizokwishazivaa (mtumba). Lakini ikiwa nguo hizi ni za ndani ni wajibu kuzifua kabla ya kuzitumia, kwa sababu wao hawajichungi na Najisi.

**d.** Shaka ya kunajisika kitu haidhuru madamu Muislamu hajakuwa na uhakika wa kunajisika kwa kitu hicho, kwa sababu ***msingi wa vitu ni Tohara.***

## NNE: TARATIBU ZA KWENDA CHOONI NA KUJISAFISHA

**1) Kujisafisha ni aina mbili:**

Aina ya kwanza ni **Kustanji** ambako maana yake ni kusafisha uchafu utokao kwenye njia mbili za mwanadamu (ya mbele au ya nyuma) kwa kutumia maji.

Aina ya pili ni **Istijmari** ambayo maana yake ni kusafisha uchafu utokao kwenye njia mbili za mwanadamu (ya mbele au ya nyuma) kwa kutumia jiwe au karatasi na mfano wake.

Kutumia maji ni bora zaidi kuliko kutumia jiwe au mfano wake, kwa sababu maji ni yenye kukata Najisi kabisa na yana nguvu zaidi katika usafi. Kama Muislamu akitumia mawe na maji kwa pamoja basi ni bora zaidi.

**2) Hukumu ya kujisafisha:**

Kujisafisha ni wajibu kwa kila kitokacho nyuma au mbele, kwa mujibu wa kauli ya Mtume, Allah ampe rehema na amani, isemayo kuwa: ***"Mmoja wenu akienda chooni na aende na mawe matatu ajisafishie, kwa sababu yanamtosha".*** Ameipokea Hadithi hii Abudaudi. Pia Mtume, Allah ampe rehema na amani, katika kuyaelezea Madhii (Huu ni ute kama Manii umtokao mwanaumu katika uume wake wakati ashikwapo na ashiki) amesema kuwa: ***"Aoshe Dhakari yake na atawadhe".*** Ameipokea Hadithi hii Bukhari na Muslim.

Endapo kilichotoka ni tohara, kama vile hewa basi sio wajibu kujisafisha.

**3) Taratibu za kwenda chooni na kujisafisha:**

**a.** Inakatazwa Muislamu kujisafisha kwa kutumia mkono wake wa kulia, kutumia mawe chini ya idadi ya mawe matatu, kutumia mfupa au kinyesi cha mnyama au chakula.

**b.** Anatakiwa asielekee Kibla wala asikipe mgongo Kibla wakati wa kufanya haja.

**c.** Awe faragha ili watu wasimuone, hasa wakati wa haja kubwa.

**d.** Atangulize mguu wake wa kushoto wakati wa kuingia chooni, na kusoma dua hii: "Kwa jina la Allah. Ewe Mola wangu, hakika mimi naomba hifadhi kwako unikinge dhidi ya ***mashetani wa kuime na mashetani wa kike".*** Wakati wa kutoka chooni atangulize mguu wake wa kulia na kuomba dua hii: ***"Naomba msamaha wako ewe***

***Mola wangu".***

**e.** Wakati wa kwenda haja ndogo atafute sehemu nzuri ambayo cheche za mkojo hazitamrukia au mkojo kumtiririkia, ili asije akanajisika. Ni jambo bora zaidi Muislamu afanye haja ndogo akiwa amechuchumaa. Sio vibaya mwanaume kukojoa akiwa amesimama, ikiwa atasalimika na kujichafua.

**f.** Asiwe amechukua kitu chochote ambacho ndani yake mna jina la Allah wakati wa kwenda haja ila tu kama kuna haja ya kufanya hivyo.

**g.** Asizungumze na mtu mwengine ila kwa dharura, kama kumuongoza kipofu ambaye anaweza kuanguka.

**h.** Asifanye haja ndogo au kubwa kwenye njia wapitayo watu au kivulini au sehemu ya kutekwa maji au chini ya mti wenye matunda au penginepo ambapo watu hupatumia.

**i.** Aoshe sehemu iliyopatwa na Najisi katika mwili au katika nguo. Ikiwa atashindwa kujua sehemu gani imepata Najisi atalazimika kuoga mwili mzima au kuosha nguo yote.

## TANO: SHERIA ZA UDHU

### 1) Maana ya Udhu:

Udhu katika sheria ya Kiisalamu ni kutumia maji safi katika kuosha viungo vinne vifuatavyo: Uso, mikono, kichwa na miguu, kwa utaratibu maalumu wa kisheria; kwa maana ya kuyafanya hayo, pamoja na faradhi nyingine za Udhu, yakiwa yamepangiliwa, yamefuatana.

### 2) Hukumu ya kutawadha:

Kutawadha ni wajibu kwa Muhdith (mtu asiyekuwa na Tohara) anapotaka kusali au kufanya ibada nyingine zinazohitaji mtu kuwa na Udhu, kama vile kutufuAlkaaba au kushika Msahafu. Allah amesema kuwa:

﴿ يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا قُمۡتُمۡ إِلَى ٱلصَّلَوٰةِ فَٱغۡسِلُواْ وُجُوهَكُمۡ وَأَيۡدِيَكُمۡ إِلَى ٱلۡمَرَافِقِ وَٱمۡسَحُواْ بِرُءُوسِكُمۡ وَأَرۡجُلَكُمۡ إِلَى ٱلۡكَعۡبَيۡنِۚ ﴾ المائدة: ٦.

***"Enyi mlioamini, mkitaka kusimama kwa ajili ya sala, basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka kwenye kongo na panguseni vichwa vyenu na (osheni) miguu yenu mpaka kwenye nguyu".*** Sura Almaaida: 6.

Sala haikubaliki bila ya Udhu, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Allah haikubali sala ya mmoja wenu anapokuwa na Hadathi mpaka atawadhe".*** Ameipokea Hadithi hii Bukhari na Muslim.

**3) Fadhila za Udhu**:

Zipo Hadithi nyingi zilizonukuliwa kwa Mtume (s.a.w.) zinazo onesha fadhila na faida za Udhu. Miongoni mwa Hadithi hizo ni kauli ya Mtume isemayo kuwa: ***"Mja Muislamu au Muumini anapotawadha. Anapo osha uso wake, inatoka pamoja na maji, au pamoja na tone la mwisho la maji, kupitia usoni mwake kila dhambi aliyoiangalia kwa kutumia macho yake. Na anapo osha mikono yake inatoka, pamoja na maji- au pamoja na tone la mwisho la maji, kila dhambi iliyotendwa na mikono yake. Na anapo osha miguu yake inatoka, pamoja na maji- au pamoja na tone la mwisho la maji, kila dhambi iliyotendwa na miguu yake mpaka atoke akiwa msafi, hana dhambi".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**4) Faradhi za Udhu:**

Faradhi za Udhu ni sita:

**Ya kwanza:**Kuosha uso.

**Ya pili:** Kupaka paji kichwa pamoja na masikio mawili.

**Ya tatu:** Kuosha mikono miwili pamoja na kongo mbili.

**Yan ne:** Kuosha miguu miwili pamoja na nguyu mbili.

**Ya tano:** Kufuata mpangilio baina ya viungo vya udhu kwa kuanza kuosha uso, kupangusa kichwa na kuosha miguu miwili.

**Ya sita:** Kufuatanisha baina ya viungo; kwa maana ya kutopitisha muda mrefu baina ya kuosha kiungo kimoja na kingine.

**5) Suna za Udhu:**

Suna za Udhu ni:

**a.** Kupiga mswaki.

**b.** Kusoma Bismillahi mwanzo wa kutia Udhu.

**c.** Kuosha viganja vya mikono kabla ya kutawadha. Iwapo Muislamu ameamka kutoka usingizini, ni wajibu kuviosha viganja mara tatu kabla ya kuviingiza ndani ya chombo.

**d.** Kusukutua na kupandisha maji puani, na kuanza kufanya mambo mawili hayo kabla ya kuosha uso, kwa gao moja la maji na kuyafikisha mbali maji kwa asiyekuwa mwenye funga.

**e.** Kupekenyua ndevu zilizo nyingi, pia vidole vya mikono na vya miguu.

**f.** Kuanza mikono na miguu ya kulia kabla ya kushoto.

**g.** Kusugua viungo pamoja na au baada ya kumwagia maji.

**h.** Kuosha viungo mara mbili au tatu.

**i.** Kukamilisha vizuri utiaji Udhu, na kufikisha juu ukoshaji wa viungo.

**j.** Kumshukuru Allah na kuomba dua baada ya kutia Udhu.

**6) Namna ya kutawadha:**

Udhu kamili wenye faradhi na suna zake ni kama ifuatavyo:

**a.** Kutia nia moyoni ya kutawadha bila ya kutamka.

**b.** Kisha aseme ***Bismillahi***.

**c.** Kisha aoshe viganja viwili mara tatu. Kabla ya kuosha ni lazima aondoshe kitu kilichoganda kwenye mikono na ambacho

kinazuia maji kufika kwenye ngozi, kama vile gundi n.k.

**d.** Kisha atasukutua na kutia maji puani kwa gao moja la maji kwa mkono wake wa kulia, na kutoa maji hayo puani kwa mkono wake wa kushoto. Atafanya hivyo mara tatu, pamoja na kuyafikisha maji mbali puani ila atakapokuwa mwenye kufunga.

**e.** Kisha ataosha uso mara tatu kuanzia kwenye sikio mpaka sikio kwa upana, na kuanzia kwenye maoteo ya nywele mpaka chini ya ndevu na kidevu kwa urefu, na kupekenyua ndevu zake.

**f.** Kisha ataosha mkono wake wa kulia mara tatu kuanzia kwenye ncha ya vidole vyake mpaka kwenye dhiraa zake. Atasugua mkono wake, ataosha kongo yake na kupekenyua baina ya vidole vyake. Kisha ataosha mkono wake wa kushoto kama hivyo.

**g.** Kisha atapaka maji kichwa chake mara moja; atarowesha kiganja chake kwa maji kisha atakipitisha kuanzia mbele ya kichwa chake mpaka kwenye kisogo chake. Kisha atakirejesha kiganja chake pale alipoanzia. Kisha ataweka vidole vyake vya shahada kwenye masikio yake na kuvipangusia ndani ya masikio yake, na kupangusa nje ya masikio yake kwa vidole vyake gumba.

**h.** Kisha ataosha mguu wake wa kulia mara tatu kuanzia kwenye ncha za vidole vyake mpaka kwenye nguyu. Ataosha nguyu zake, na kupekenyua baina ya vidole vyake. Kisha ataosha mkono wake wa kushoto kama hivyo.

**i.** Kisha atasomma uradi huu:

**(أشهدُ أنْ لا إله إلاّ اللّهُ وحده لا شريك له، وأشهد أنَّ محمَّداً عبده ورسوله، اللَّهمَّ اجعلني من التوَّابين، واجعلني من المتطهِّرين).**

Ash-hadu Allaa ilaaha illallaah, Wa-ash-hadu Anna Muhammadan Abduhuu Warasuuluh. Allaahummaj-alnii Minat-tawwaabiin Waj-alnii Minalmutatwahhiriin = Ninakiri kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa isipokuwa Allah tu, na ninakiri kuwa Muhammad ni Mja wake na Mtume. Ewe Mola wangu, nifanye niwe miongoni mwa wenye kutubu, na nifanye niwe miongoni mwa wenye kujitoharisha).

**7) Mambo yanayotengua Udhu:**

Mambo yanayotengua udhu ni matano :

**La kwanza:** Kutoka kwa kitu kwenye njia mbili; utokapo mkojo na kinyesi.

**La pili:** Kutoka kwa Najisi kwenye sehemu nyingine ya mwili.

**La tatu:** Kutokwa na akili, kwa sababu ya kupatwa na wendawazimu, ulevi, kuzirai au usingizi.

**La nne:** Kugusa utupu kwa matamanio.

**La tano:** Kutoka kwenye Uislamu (kuritadi), Allah atulinde na hilo.

## SITA: SHERIA ZA KUPAKA MAJI KHOFU (VIATU) NA MFANO WAKE:

**1) Maana ya kupaka maji viatu wakati wa kutia Udhu:**

**Khofu** ni kile kinachovaliwa kwenye mguu, kilichotengenezwa kwa ngozi na mfano wake. Kinaunganishwa na khofu kila kinachovaliwa mguuni kilichotengenzwa kwa sufi au mfano wake. Makusudio ya kupaka maji khofu ni kupitisha mkono uliroweshwa kwa maji juu ya miguu miwili iliyovaa khofu kwa nia ya kujitoharisha, na kwa kufanya hivyo sio lazima tena kuosha miguu.

**2) Hukumu ya kupaka maji khofu:**

Hii ni ruhusa iliyotoka kwa Allah ili kuwafanyia wepesi waja wake, na kuwaondolea uzito na usumbufu. Iwapo mtu amevaa khofu ni bora kwake kupaka maji khofu hizo kuliko kuzivua na kuosha miguu, kwa sababu Mtume, Allah ampe rehema na amani, alikuwa hajisumbui kufanya tofauti na hali ya miguu yake ilivyo. Alipokuwa amevaa khofu (viatu) alikuwa akipaka maji khofu hizo, na alipokuwa hakuvaa khofu alikuwa akiosha miguu.

**3) Muda wa kupaka maji khofu:**

Inajuzu kwa mkazi kupaka maji khofu kwa muda wa siku moja;

mchana na usiku wake. Kwa msafiri ni siku tatu. Muda wa kupaka unaanza kutoka pale atakapopata Hadathi baada ya kuvaa khofu hizo akiwa na Tohara. Kwa mkazi muda wa kupaka maji unamalizika baada ya siku moja (saa ishirini na nne), na siku tatu (saa sabini na mbili) kwa msafiri.

**4) Masharti ya kupaka maji khofu:**

Masharti ya kupaka maji khofu ni matano:

**a.** Khofu ziwe zimevaliwa kwenye tohara kamili.

**b.** Khofu ziwe halali. Zisiwe za kunyang’anya, kuiba wala za hariri kwa wanaume.

**c.** Khofu ziwe Tohara; zisiwe zimetengenezwa kwa ngozi ya nguruwe, mbwa au mfu (mzoga).

**d.** Khofu ziwe zinafunika sehemu ya miguu iliyo faradhi kuoshwa.

**e.** Khofu ziwe nzito zisizo onesha ngozi iliyo chini yake.

**f.** Kupaka maji kuwe ndani ya muda ulioainishwa kisheria.

**5) Namna ya kupaka maji khofu:**

Mahali pa kisheria kupakwa maji ni nje ya khofu na sio chini yake au kisiginoni mwake. Namna ya kupaka maji ni kuweka mikono yake iliyoroweshwa kwa maji juu ya viodole vya mguu wake, kisha aipitishe mikono hiyo mpaka mwanzo wa mguu wake. Mkono wake wa kulia utapaka maji mguu wake wa kulia, na mkono wake wa kushoto utapaka maji mguu wake wa kushoto, mara moja tu na hatakiwi kurudia kupaka.

**6) Yanayobatilisha kupaka maji Khofu:**

Yanayobatilisha kupaka maji khofu ni moja kati ya mambo matatu:

**a.** Pakitokea jambo linalowajibisha kuoga, kama vile kuota kujamiiana na mengineyo.

**b.** Kumalizika kwa muda wa kupaka maji.

**c.** Kuvua khofu.

Sheria inamruhusu Muislamu kupaka maji soksi zake kwa kuchunga masharti yaliyotangulia kutajwa katika kupaka maji khofu. Kwa maana hiyo, haruhusiwi kupaka maji soksi zikiwa nyepesi au zimetoboka au hazifuniki kikamilifu mahali palipo faradhi kuoshwa.

**7) Kupaka maji kichacha:**

Inafaa kupaka maji juu ya kichacha wakati wa kutawadha. Kichacha ni vijiti au vitambaa na mfano wake vinavyofungwa kwenye kiungo cha mwili kilichovunjika. Pia inafaa kupaka maji juu ya bendeji iliyofungwa kwenye jeraha au plasta inayowekwa kwenye kidonda, katika Hadathi Ndogo na Hadathi Kubwa, kwa sharti kwamba kichacha hicho kiwe kwa kadiri ya haja –kiwe kimewekwa pahala palipovunjika, au kwenye jeraha na saehemu za karibu yake tu. Kichacha kinatakiwa kupakwa maji chote, na kupakwa kwake maji hakuna muda maalumu. Mtu anaruhusiwa kupaka maji mpaka atakapokitoa au kupona jeraha lililopo chini yake. Pia hakuna sharti la kuwepo kwa Tohara kwanza kabla ya kukifunga.

## SABA: SHERIA ZA KUOGA:

**1) Maana ya kuoga:**

Katika sheria ya Kiislamu kuoga ni kueneza maji kwenye mwili wote kwa namna maalumu ambayo maelezo yake yatakuja.

**2) Hukumu ya kuoga:**

Kuoga ni wajibu kwa Muislamu pale linapopatikana jambo la kuwajibisha kuoga. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَقۡرَبُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَنتُمۡ سُكَٰرَىٰ حَتَّىٰ تَعۡلَمُواْ مَا تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا إِلَّا عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّىٰ تَغۡتَسِلُواْ﴾ النساء: ٤٣.

***"Enyi mloamini, msiikaribie sala (msisali) na ilhali nyinyi***

***mmelewa mpaka muelewe mnachokisema. Na (msiikaribie sala (msisali) na ilhali nyinyi ni) wenye Janaba, isipokuwa labda muwe wapita njia, mpaka muoge”.*** Sura Annisaa: 43.

Na Mtume (s.a.w) amesema kuwa: ***“(Mwanaume) Anapokaa kwenye pande zake nne (za mwanamke) na tupu kukutana na tupu, basi kuoga kumekuwa wajibu”.*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**3) Mambo yanayowajibisha kuoga:**

Mambo yanayowajibisha kuoga ni sita, nayo ni haya yafuatayo:

**a.** Ni mwanaume au mwanamke kutokwa na manii kwa kuchupa kwa kuhisi raha. Mwenye kulala atalazimika kuoga kwa kule tu kuona manii hata kama hakumbuki kuota tendo la kujamiiana.

**b.** Kuingia kwa kichwa cha dhakari ya mwanaume kwenye tupu ya mwanamke.

**c.** Kifo cha Muislamu, isipokuwa tu Shahidi aliyekufa katika vita. Yeye haoshwi.

**d.** Kukatika kwa damu ya Hedhi. Damu hii hutoka katika tumbo la uzazi la mwanamke baada ya kubalehe.

**e.** Kukatika kwa damu ya Nifasi. Damu hii hutoka katika tumbo la uzazi la mwanamke baada ya kujifungua.

**4) Majosho ya Suna:**

Yapo majosho ambayo sio wajibu kwa Muislamu kuoga lakini inapendeza kwake kudumu kuyatekeleza. Miongoni mwa majosho hayo ni haya yafuatayo:

**a.** Kuoga kwa ajili ya sala ya Ijumaa.

**b.** Kuoga kwa ajili ya sala ya Idi.

**c.** Kuoga kwa ajili kuhirimia Hija au Umra.

**d.** Kuoga kwa ajili ya kuingia Makkah.

**e.** Kuoga kwa ajili ya kusimama Arafa.

**f.** Kuoga kwa sababu ya kuosha maiti.

**g.** Kuoga kwa sababu ya kupoteza fahamu.

**h.** Kuoga kwa sababu ya kuingia kwenye Uislamu.

**5) Faradhi za kukoga**:

Faradhi za kuoga ni:

**a.** Ni kunuwia. Kunuwia ni kukusudia kuondosha Hadathi; iwe ni Janaba, Hedhi, Nifasi au kutia nia ya kuoga josho la Suna analotaka kuoga.

**b.** Kujieneza maji mwili mzima. Kueneza huku ni pamoja na kufikisha maji kwenye sehemu za mwili za wazi na zilizojificha. Sehemu zilizojificha ni kama vile mdomo, pua, kitovu, chini ya kidevu, kwapa, sehemu iliopo baina ya mapaja mawili na sehemu ya ndani ya goti n.k.

**c.** Kupekenyua nywele ili kufikisha maji kwenye maoteo yake hadi kwenye ngozi.

**d.** Mwanamke atafumua nywele zake kwa ajili ya kuoga Hedhi na Nifasi na sio kuoga Janaba.

**6) Suna za kuoga:**

Suna za kuoga ni:

**a.** Kupiga ***Bismillah.***

**b.** Kuosha viganja viwili mara tatu.

**c.** Kuanza kwa kuondosha uchafu pamoja na kusugua mkono na kuuosha.

**d.** Kujimiminia maji kichwani mara tatu.

**e.** Kutia Udhu kabla ya kuoga.

**f.** Kuanza upande wa kulia katika kuosha kichwa chake na viungo vingine.

**g.** Kujisugua kwa kupitisha mkono kwenye sehemu zote za mwili.

**h.** Kuosha miguu na sehemu nyingine mbali ya alipoanzia kutia Udhu.

**i.** Kutumia maji vizuri na kutofanya ubadhirifu katika kutumia maji.

**j.** Kuleta Uradi na kuomba dua mwisho wa kuoga kama ilivyo kwenye Udhu.

**7) Namna ya kuoga:**

Kuna namna mbili za kuoga: **Namna ya ukamilifu** na **Namna ya kutosheleza**.

**Kwanza: Namna ya kuoga kuliko kamili**. Hii ni namna iliyokusanya faradhi na suna kama ifuatavyo:

- Kunuwia kuoga kwenye moyo wake.

- Kisha atasema ***Bismillahi*** na kuosha mikono yake mara tatu.

- Kisha ataosha tupu yake kwa mkono wake wa kushoto, na ataosha kwa maji na sabuni ili kuondosha uchafu uliopo.

- Kisha atatawadha Udhu kamili, pamoja na kuosha miguu yake. Mara nyingine ataahirisha kuosha miguu yake mpaka mwisho wa kuoga.

- Kisha atakimwagia maji kichwa chake magao matatu kwa mkono wake, akianzia upande wa kulia wa kichwa chake, kisha kushoto, kisha kati na kuzipekua nywele zake mpaka ayaroweshe maji maoteo ya nywele zake.

- Kisha ataueneza maji mwili wake wote, na kuusugua kwa

mikono yake ili maji yaweze kufika.

- Kisha ataleta nyiradi zilizothibiti kunukuliwa katika Udhu.

**Pili: Namna ya kuoga kunakotosheleza** ni mtu kutia nia na kuueneza maji mwili wake wote pamoja na kusukutuwa na kupandisha maji puani.

**8) Mambo yaliyo haramu kwa mwenye Hadathi Kubwa:**

Ni haramu kwa mweneye Hadathi Kubwa mambo yafuatayo:

**a.** Kusali.

**b.** Kutufu Alkaaba.

**c.** Kukaa msikitini.

**d.** Kushika Msahafu Mtukufu.

**e.** Kusoma Qur’ani.

## NANE: SHERIA ZA KUTAYAMAMU:

**1) Maana ya Kutayamamu:**

Kutayamamu ni kupaka uso na mikono miwili mchanga ulio Tohara kwa utaratibu maalumu ambao ufafanuzi wake utakuja.

**2) Hukumu ya kutayamamu**:

Mwenye kutaka kusali au kufanya ibada nyingine na akakosa maji au kushindwa kuyatumia, amewekewa sheria ya kutayamamu. Hii ni ruhusa kutoka kwa Allah. Amesema Allah kuwa:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا قُمۡتُمۡ إِلَى ٱلصَّلَوٰةِ فَٱغۡسِلُواْ وُجُوهَكُمۡ وَأَيۡدِيَكُمۡ إِلَى ٱلۡمَرَافِقِ
وَٱمۡسَحُواْ بِرُءُوسِكُمۡ وَأَرۡجُلَكُمۡ إِلَى ٱلۡكَعۡبَيۡنِۚ وَإِن كُنتُمۡ جُنُبٗا فَٱطَّهَّرُواْۚ وَإِن كُنتُم مَّرۡضَىٰٓ أَوۡ
عَلَىٰ سَفَرٍ أَوۡ جَآءَ أَحَدٞ مِّنكُم مِّنَ ٱلۡغَآئِطِ أَوۡ لَٰمَسۡتُمُ ٱلنِّسَآءَ فَلَمۡ تَجِدُواْ مَآءٗ فَتَيَمَّمُواْ صَعِيدٗا طَيِّبٗا
فَٱمۡسَحُواْ بِوُجُوهِكُمۡ وَأَيۡدِيكُم مِّنۡهُۚ مَا يُرِيدُ ٱللَّهُ لِيَجۡعَلَ عَلَيۡكُم مِّنۡ حَرَجٖ وَلَٰكِن يُرِيدُ
لِيُطَهِّرَكُمۡ وَلِيُتِمَّ نِعۡمَتَهُۥ عَلَيۡكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَشۡكُرُونَ ﴾ المائدة: ٦.

*“**Enyi mlio amini, Mnapo simama kwa ajili ya sala basi osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka kwenye kongo, na mpake (maji) vichwa vyenu, na (osheni) miguu yenu mpaka kwenye nguyu. Na mkiwa na Janaba basi jitoharisheni (ogeni). Na mkiwa wagonjwa au mmo safarini au mmoja wenu ametoka chooni au mmewagusa wanawake (mmejamiiana) na hamkupata maji, basi tayamamuni mchanga ulio safi. Kwa hiyo, mpake nyuso zenu na mikono yenu. Allah hapendi kukutieni katika tabu bali anataka kukutakaseni na kutimiza neema yake juu yenu ili mpate kushukuru”.*** Sura Almaidah: 6.

Amesema Mtume (s.aw.) kuwa: ***“Hakika, mchanga ulio safi ni tohara kwa Muislamu hata kama hakupata maji kwa muda wa miaka kumi. Akiyapata maji basi ayagusishe mwili wake, kwani hiyo ni kheri”.*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi na Tirmidhiy.

Kutayamamu kwa kutumia mchanga na mfano wake kunaondosha Hadathi Kubwa na Hadathi Ndogo mpaka dharura ya kutayamamu iondoke au apate maji. Dharura itakapoondoka au maji yakipatikana basi Tayamamu yake itabatilika.

**3) Ni nani aliyewekewa sheria ya kutayamamu?**

**a.** Mwenye kuyakosa maji, ima kwa kukosekana kwake au kwa umbali wake na hawezi kuyafikia.

**b.** Mwenye kuogopa kuyatumia maji kwa sababu ya ugonjwa au baridi kali.

**c.** Mwenye maji kidogo anayoyahitaji kwa kunywa yeye mwenyewe au kunywa mtu mwengine, na akawa na hofu ya kudhurika kwa kiu. Iwapo mtu hakupata maji yanayomtosha kwa kutawadhia na kuoga, basi atatawadha kwa maji aliyoyapata au kuogea ikiwa ni mwenye Janaba, kisha atatayamamu kwa ajili ya viungo visivyopata maji.

**4) Faradhi za kutayamamu:**

Faradhi za kutayamamu ni:

**a.** Kutia nia. Anatakiwa, kwa kutayamamu kwake, awe na nia ya kuondosha Hadathi.

**b.** Kupaka mchanga uso.

**c.** Kupaka mchanga kiganja mpaka kwenye kiungio kilichopo baina ya kiganja na mkono.

**d.** Kufuatanisha baina ya kupaka mchanga uso na mikono.

**5) Suna za kutayamamu:**

Suna za kutayamamu ni hizi zifuatazo:

**a.** Kupiga ***Bismillahi***.

**b.** Kufuata mpangilio baina ya kupaka mchanga uso na mikono.

**c.** Kupekenyua vidole.

**d.** Kukung'uta au kupulizia mikono kama kuna kitu kilichoganda kutoka kwenye ardhi.

**6) Namna ya kutayamamu:**

Ni kunuwia. Kisha kupiga Bismillahi na kupiga viganja vyake kwenye ardhi mara moja tu. Kisha, kwa kutumia viganja hivyo, apake uso wake na viganja vyake. Atapaka kiganja kwa kiganja akiaanzia ncha za vidole mpaka kwenye kiungio kilichopo baina ya kiganja na mkono.

**7) Mambo yanayobatilisha kutayamamu:**

Tayamamu inabatilika kwa kupatikana kwa moja kati ya mambo mawili:

**La kwanza:** Kupata maji au kuondoka kwa udhuru ambao umefanya sheria iruhusu kutayamamu.

**La pili:** Kupatikana kwa mojawapo kati ya mambo yanayotengua Udhu

au yanayotengua kuoga, yaliyotangulia kutajwa. Hii ni kwa sababu, kutayamamu ni badala ya Udhu na kuoga, na chenye kutengua asili kinatengua badala yake pia.

Kama Muislamu atakosa maji au kushindwa kuyatumia na akatayamamu na kusali, kisha baada ya kumaliza kusali, akapata maji au akaweza kuyatumia hatarudia kusali hata kama muda wa sala bado upo. Lakini kama akipata maji au akaweza kuyatumia maji hayo wakati akiwa kwenye sala, basi sala yake itabatilika na atalazimika kujitoharisha kwa maji.

**8) Hukumu ya aliyekosa vitoharisho vya maji na mchanga:**

Kama Muislamu hana maji wala mchanga, na hakuweza kuvitafuta viwili hivyo au amepata maji lakini akashindwa kuyatumia, basi atasali kulingana na hali yake ilivyo, kama vile mtu aliyefungwa kamba asiyeweza kutawadha wala kutayamamu.

# SHERIA ZA SALA

## KWANZA: Maana ya Sala:

Sala ni ibada yenye maneno na vitendo maalumu vinavyo anza kwa Takbira na kumalizika kwa Salamu. Ufafanuzi wake umo katika maelezo yafuatayo:

## PILI: Hukumu ya sala:

Sala ni nguzo kubwa katika nguzo za Kiislamu baada ya Shahada mbili na ni kielelezo chake kikubwa. Sala ni mhimili wa Uislamu kama alivyoeleza Mtume wa Uislamu (s.a.w.). Allah ameifaradhisha sala kwa Nabii wake Muhammad (s.a.w.) siku ya Miraji juu ya mbingu saba, jambo ambalo linaonesha utukufu wa hadhi yake na nafasi yake mbele ya Allah Mtukufu, kama ambavyo pia inaonesha umuhimu wake katika maisha ya Muislamu. Kwa sababu hiyo, imekuja amri ya kuienzi sala na kudumu kuitekeleza. Amesema Allah kuwa:

﴿حَـٰفِظُواْ عَلَى ٱلصَّلَوَٰتِ وَٱلصَّلَوٰةِ ٱلْوُسْطَىٰ وَقُومُواْ لِلَّهِ قَـٰنِتِينَ﴾ البقرة: ٢٣٨.

***“Dumuni kusali, na (hasa) sala ya katikati, na simameni kwa ajili ya Allah mkiwa ni wenye kunyenyekea”.*** Sura Albaqara: 238.

## TATU: Faida za sala:

Mtume (s.a.w.) amebainisha faida za sala katika Hadithi zake nyingi. Miongoni mwa Hadithi hizo ni hizi zifuatazo:

- Kauli ya Mtume isemayo kuwa:

***“Sala tano, Ijumaa mpaka Ijumaa, na Ramadhani mpaka Ramadhani***

***ni zenye kufuta madhambi baina yao iwapo Madhambi Makubwa yataepukwa".*** Ameipokea Hadithi hii Muslim.

- Kauli ya Mtume isemayo kuwa:

***"Mnaonaje kama mto uko kwenye mlango wa mmoja wenu naye akawa anaoga kwenye mto huo mara tano kila siku. Je, taka zitabaki kwenye mwili wake? Swahaba wakasema: Kwenye mwili wake hapatabaki taka zozote. Mtume akasema: Basi huo ni mafano wa sala tano. Allah anafuta madhambi kwa sala hizo".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**NNE: Idadi ya sala za faradhi na nyakati zake:**

Idadi ya sala za faradhi ni tano, mchana na usiku (kwa siku moja). Sala hizo ni hizi zifuatazo: Alfajiri (rakaa mbili), Adhuhuri (rakaa nne), Alasiri (rakaa nne), Magharibi (rakaa tatu) na Isha (rakaa nne). Kila moja katika sala hizi ina wakati wake maalumu ambao inatakiwa itekelezwe ndani ya wakati huo. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتۡ عَلَى ٱلۡمُؤۡمِنِينَ كِتَٰبٗا مَّوۡقُوتٗا﴾ النساء: ١٠٣.

"***Hakika, sala kwa waumini ni faradhi iliyowekewa wakati maalumu***''. Sura Annisaa: 103. Nyakati hizo ni kama ifuatavyo:

**1) Sala ya Adhuhuri**. Wakati wake unaanza kwa jua linapotenguka, yaani linapohama kutoka katikati ya mbingu kuelekea upande wa magharibi. Wakati wake unendelea mpaka kivuli cha kitu kinapokuwa na urefu sawa na kitu chenyewe, na wakati wa sala hii humalizika hapo.

**2) Sala ya Alasiri.** Wakati wake unaanza kutokea ulipokwisha wakati wa sala ya Adhuhuri, kwa maana kwamba ni wakati wa kivuli cha kitu kinapokuwa na urefu sawa na kitu chenyewe. Wakati wa sala hii unendelea mpaka kuzama kwa jua.

**3) Sala ya Magharibi.** Wakati wake unaanza kwa kuzama kwa jua na kuendelea mpaka utakapotoweka ukungu mwekundu.

**4) Sala ya Isha.** Wakati wake unaanza kutoka unapotoweka ukungu mwekundu na kuendelea mpaka katikati ya usiku.

**5) Sala ya Alfajiri**. Wakati wake unaanza kutoka alfajiri ya hakika inapoingia na kuendelea mpaka kuchomoza kwa jua.

Hizi ndio nyakati za sala tano ambazo Allah amefaradhisha zisaliwe ndani ya nyakati hizo. Kwa maana hiyo, ni wajibu kwa Muislamu kufuata utaratibu huo kiasi kwamba asisali sala yoyote kabla ya wakati wake, na asiicheleweshe na kuisali nje ya wakati wake.

Allah amewakemea vikali wanaochelewa kusali na kusali nje ya wakati kwa kusema kuwa:

﴿فَوَيۡلٞ لِّلۡمُصَلِّينَ﴾ الماعون: ٤.

"***Basi adhabu kali imewathibitikia wenye kusali. Ambao husahau sala zao".*** Sura Almaauun:4. Maana ya wanaosahau sala zao ni wale ambao wanaahirisha sala mpaka muda wake wake unakwisha.

Muislamu ambaye amesahau kusali au amelala na sala ikampita, inampasa kufanya haraka kuilipa sala hiyo. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Aliyesahau kusali au aliyelala na sala ikampita, kafara yake ni kuisali sala hiyo anapoikumbuka".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Muislamu aelewe kuwa kusali sala ndani ya nyakati zake ni katika amali bora na zinazopendwa sana na Allah, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) aliyoisema pale alipoulizwa kuwa: ***"Ni amali gani bora zaidi? Akajibu: Ni kusali sala katika wakati wake".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

## TANO: Je, ni watu gani walio na wajibu wa kusali?

Kusali ni wajibu kwa kila Muislamu wa kiume, aliye balehe na mwenye akili timamu. Pia kusali ni wajibu kwa Muislamu wa kike, balehe, mwenye akili timamu na ambaye hayumo ndani ya Hedhi

wala Nifasi. Kwa maana hiyo, kusali sio wajibu kwa kafiri, mtoto mdogo, mwendawazimu, mwanamke Muislamu mwenye Hedhi au mwenye Nifasi. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Kalamu imenyanyuliwa (isiandike dhambi) kwa watu watatu: Kwa mwenye kulala mpaka atakapoamka, kwa mtoto mdogo mpaka atakapo balehe na kwa mwendawazimu mpaka ataporejea kwenye akili yake timamu".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi. Pia hii ni kwa mujibu wa Hadithi iliyonukuliwa na Muadha Adawiyyah pale aliposema kuwa: ***"Nilimuuliza Aisha, Allah amuwiye radhi, kwamba: Kwa nini mwanamke mwenye Hedhi analipa funga na halipi sala? Akajibu kuwa: Tulikuwa tunapata hali hiyo (wakati wa Mtume) na (tulikuwa) tukiamrishwa (na Mtume) kulipa saumu na hatuamrishwi kulipa sala".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Lakini mtoto anapofikia umri wa miaka saba anatakiwa kuamrishwa kusali, ili azoweshwe, na anatakiwa kupigwa akiwa kwenye umri wa miaka kumi kama hataki kusali. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Waamrisheni watoto wenu kusali wakiwa kwenye umri wa miaka saba na wapigeni (kama hawataki kusali) wakiwa kwenye umri wa miaka kumi, na watenganisheni baina yao kwenye vitanda".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi.

### SITA: Masharti ya kusihi kwa sala:

Ili sala iwe sahihi, kuna masharti kadhaa yaliyowekwa na ambayo ni haya yafuatayo:

**1) Uislamu**. Kafiri akisali, sala yake sio sahihi.

**2) Akili timamu**. Sala ya mwendawazimu na mlevi si sahihi.

**3) Mtu kuwa tohara kwa kutokuwa na Hadathi Kubwa na Hadathi Ndogo**. Sala haiwi sahihi kwa mtu asiyekuwa na Tohara, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Hakuna sala bila ya Tohara".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. **Hadathi Ndogo** ni ile hali ambayo kwa sababu yake ni wajibu kutia Udhu, kama kukojoa au kwenda haja kubwa. **Hadathi Kubwa** ni ile hali

ambayo kwa sababu yake ni wajibu kuoga, kama vile kutokwa na Manii.

**4) Kuingia kwa wakati wa sala**. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتۡ عَلَى ٱلۡمُؤۡمِنِينَ كِتَٰبٗا مَّوۡقُوتٗا﴾ النساء: ١٠٣.

***"Hakika, sala kwa waumini ni faradhi iliyowekewa wakati maalumu".*** Sura Annisaa: 103. Sala haiwi sahihi kama wakati wake haujaingia.

**5) Kuwa na uwezo wa kusitiri uchi kwa kitu ambacho hakioneshi ngozi**. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿يَٰبَنِيٓ ءَادَمَ خُذُواْ زِينَتَكُمۡ عِندَ كُلِّ مَسۡجِدٖ﴾ الأعراف: ٣١.

***"Enyi wanadamu, chukueni mapambo yenu (nguo zenu) kila muendapo msikitini".*** Sura Al-aaraaf: 31. Maana ni kwamba, kila wakati wa kusali. Uchi wa mwanaume balehe ni baina ya kitovu na magoti. Mwili wote wa mwanamke ni uchi isipokuwa tu uso wake na viganja vyake.

**6) Kuwa na uwezo wa kujiepusha na Najisi**. Anayesali anatakiwa aepukane kabisa na Najisi, kuanzia mwilini mwake, nguoni mwake na mahali anaposimama ili asali.

**7) Kuelekea Kibla, ambayo ni Alkaaba**, **iwapo itawezekana**. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿فَوَلِّ وَجۡهَكَ شَطۡرَ ٱلۡمَسۡجِدِ ٱلۡحَرَامِ﴾ البقرة: ١٤٤.

***"Hivyo, elekeza uso wako upande wa Amasjid Alharaam (Msikiti Mtukufu wa Makka)".*** Sura Albaqara:144.

**8) Kutia nia.** Hilo linapatikana kwa mtu, kwa mfano, kuwa na nia moyni mwake kuwa anasali sala Adhuhuri au Alasiri au Magharibi n.k. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Ilivyo ni kwamba amali ni kwa nia".*** Hadithi hii imepokewa na

Bukhari na Muslim. Sio sheria kutamka nia, kwa sababu Mtume (s.a.w.) hakuwa akitamka nia.

**9) Mtoto awe mpambanuzi**. Sala ya mtoto ambaye bado hajabalehe ni sihihi iwapo atakuwa mpambanuzi. Mtoto mpambanuzi ni yule aliyefikia umri wa miaka saba, au anayeweza kupambanua baina ya mambo ya kawaida na yale ya ibada.

## SABA: Nguzo za sala:

Makusudio ya nguzo za sala ni yale maneno na vitendo ambavyo vinaitengeneza sala. Nguzo hizo ni kumi na nne, na ni lazima mwenye kusali azilete zote, vinginevyo sala yake haitakuwa sahihi hata kama ameziacha kwa kusahau au kwa kutojua. Nguzo hizo ni hizi zifuatazo:

**1) Mtu kusali akiwa amesimama** – kwa sala ya faradhi- ikiwa anaweza kusimama. Katika sala ya suna sio lazima kusimama.

**2) Takbira ya kuanzia sala** (Takbiiratul Ihram). Takbira hii ni kusema اللَّه أكبر = ***Allahu Akbar*** mwanzo wa Sala. Haijuzu kutamka matamshi mengine badala ya Takbira hiyo.

**3) Kusoma Suratul Faatiha**.

**4) Kurukuu.**

**5) Kunyanyuka kutoka kwenye kurukuu na kusimama vizuri wima (Itidali).**

**6) Kusujudu.** Kusujudu kunafanyika kwa kutumia viungo saba ambavyo ni: paji la uso pamoja na pua, mikono miwili, magoti mawili na miguu miwili.

**7) Kunyanyuka kutoka kwenye kusujudu**.

**8) Kukaa kitako baina ya sijida mbili**.

**9) Utulivu katika kutekeleza nguzo hizi**.

**10) Kukaa kwa ajili ya Tashahudi.**

**11) Tashahudi.** Tashahudi ni kusoma maneno yafuatayo kabla ya kutoa Salamu na akiwa amekaa:

(التحيات للَّهِ والصَّلوات والطّيِّبات، السَّلامُ عَلَى النَّبيِّ ورحمةُ اللَّهِ وبركاتُه، السَّلامُ عَلينا وعلى عبادِ اللَّهِ الصَّالحينَ، أشهدُ أنْ لا إله إلاّ اللَّهُ وأشهدُ أنَّ محمَّداً عبدُه ورسولُه).

**Attahiyyaatu Lillaah. Wasswalawaat Wattwayyibaat. Assalaamu alannabiyyi Warahmatullaahi Wabarakaatuh. Assalaamu alaynaa wa-alaa ibaadillaahisw-swaalihiin. Ash-hadu Allaa ilaaha illallaah Wa-ash-hadu Anna Muhammadan Abduhuu Warasuuluh.**

**12) Kumsalia Mtume (s.a.w.).** Kumsalia Mtume ni kusoma dua hii ifuatayo baada ya Tashahudi ya Mwisho:

(اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحمَّد)

**(Allaahumma Swalli Alaa Muhammad)**

Namna bora zaidi ni kusoma dua hii ifuatayo:

(اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحمَّد وعَلَى آلِ مُحمَّد، كما صَلَّيتَ على إبراهيمَ و عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّد، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيد)

**(Allaahumma Swalli Alaa Muhammad Wa-alaa Aali Muhammad Kamaa Swallaita Alaa Ibraahiim Wa-alaa Aali Ibraahiim Innaka Hamiidun Majiid. Allaahumma Baarik Alaa Muhammad Wa-alaa Aali Muhammad Kamaa Baarakta Alaa Ibraahiim Wa-alaa Aali Ibraahiim Innaka Hamiidun Majiid)**

**Kutoa Salamu.** Kutoa salamu ni kusoma dua hii ifuatayo mara mbili baada ya kumaliza kusoma Tashahudi na kumsalia Mtume:

(السَّلامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ)

**(Assalaamu Alaykum Warahmatullaah)**

**13)** Ni kuzitekeleza nguzo hizi kwa mpangilio huu uliotajwa. Ufafanuzi wake utaelezwa wakati wa kufafanua namna ya kusali inshaa-allah.

## NANE: Suna za sala:

Suna za sala ni matamshi na vitendo kadhaa ambavyo inapendekezwa kwa mwenye kusali kuvifanya. Akivifanya atapata thawabu na kwa maana hiyo zinakuwa thawabu za nyongeza, na iwapo hakuvifanya basi hana makosa na sala yake ni sahihi.

Suna hizi ziko za aina mbili: Suna za vitendo na suna za matamshi.

**Suna za vitendo ni hizi zifuatazo:**

**1) Kunyanyua mikono mpaka kwenye mabega au masikio** wakati wa Takbira ya kuanzia sala, wakati wa kurukuu, wakati wa kunyanyuka kutoka kwenye kurukuu na wakati wa kusimama kutoka kwenye Tashahudi ya Kwanza kwenda kwenye rakaa ya tatu.

**2) Kuweka kiganja cha mkono wa kulia juu ya kiganja cha mkono wa kushoto au juu ya mkono wa kushoto** na kuviweka viganja hivyo juu ya kifua chake wakati wa kusimama.

**3) Kuangalia mahali pake anaposujudu**.

**4) Kuweka mikono kwenye magoti wakati wa kurukuu**.

**5) Kunyoosha mgongo wake vizuri wakati wa kurukuu, na kuweka kichwa chake sawa sawa na mgongo wake** bila ya kukiinamisha au kukiinua.

**6) Kugusisha vyema viungo vya kusujudia kwenye ardhi.**

**7) Kuepusha muungabega wake usigusane na mbavu zake katika kusujudu**. Hilo linatakiwa kufanyika kwa kuepusha muungabega wake usigusane na mbavu zake, tumbo lake lisigusane na mapaja yake, mapaja yake yasigusane na miundi (miguu) yake.

**8) Kukaa Iftirashi wakati wa kukaa baina ya sijida mbili na wakati wa kusoma Tashahudi ya Kwanza**. Kukaa Iftirashi kuutandaza mguu wake wa kushoto na kukalia, kuusimamisha mguu wake wa kulia na kuweka mikono yake juu ya mapaja yake.

**9) Kukaa Tawaruki katika Tashahudi ya Mwisho**. Kukaa Tawaruki ni kuyaweka makalio yake ardhini, kuuweka mguu wake wa kushoto chini ya paja lake na chini ya muundi (mguu) wake wa kulia na kuusimamisha mguu wake wa kulia.

**Suna za matamshi ni hizi zifuatazo:**

**1) Dua ya kufungulia sala.** Dua hii inatakiwa kufanyika kwa kuomba kimya kimya baada ya Takbira ya kuanzia sala na kabla ya kusoma sura Alfaatiha, kwa kutumia moja wapo ya dua ambazo Mtume (s.a.w.) alikuwa akiomba kwa kutumia hizo. Dua hizo ni pamoja na hii:

(سُبْحانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ، وَتَبَارَكَ اسْمُكَ، وَتَعَالَى جَدُّكَ، وَلا إِلَهَ غَيْرُكَ)

**Sub-haanakallaahumma Wabihamdik, Watabaarakasmuk, Wataalaa Jadduk, Walaa Ilaaha Ghairuk**

**2) Kusema:**

(أَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ)

***Auudhu Billahi Minash-shaytwaanir-rajiim***

kabla ya kusoma sura Alfatihah.

**3) Kupiga *Bismillahi* kabla ya kusoma Sura Alfatihah.**

**4) Kusema *Aamiin* baada kumaliza kusoma sura Alfatihah.**

**5) Kusoma sura nyingine kamili au sehemu yoyote ya Qur’ani baada ya kusoma sura Alfatiha katika (rakaa zote mbili za) sala ya Alfajiri na katika rakaa ya kwanza na ya pili ya sala nyingine zilizobaki`katika sala tano za faradhi.**

**6) Kuleta Takbira wakati wa kuhama kutoka kwenye tukio kwenda kwenye tukio jingine ndani ya sala.** Ataleta Takbira wakati wa kurukuu, wakati wa kusujudu, wakati wa kunyanyuka kutoka kwenye kusujudu na wakati wa kusimama kwenda kwenye rakaa inayofuata. Ama Takbira ya kuanzia sala inayopigwa mwanzo wa sala, Takbira hiyo ni nguzo kama ilivyotangulia kuelezwa.

**7) Kusoma Qur’ani kwa sauti inayosikika** katika rakaa za sala ya Alfajiri, rakaa ya mwanzo na ya pili katika sala ya Magharibi na Isha, na kusoma Qur’ani kwa sauti ndogo kwenye rakaa nyinginezo.

**8) Kusema:**

(سُبْحَانَ رَبِّيَ العَظِيم)

**(Subhaana Rabbiyal Adhiim)** mara tatu au zaidi katika kurukuu.

**9) Kusema:**

(سَمِعَ اللَّهُ لِمَنْ حَمِدَه)

**(Samiallaahu Liman-hamidah)** wakati wa kunyanyuka kutoka kwenye kurukuu. Atasema hivi Imamu au mtu anayesali peke yake.

**10) Kusema:**

(رَبَّنَا وَلَكَ الحَمْد)

**(Rabbanaa Walakal-hamdu)** baada ya kusema **Samiallaahu Liman-hamidah**. Atasema hivi Imamu au Maamuma au mtu anayesali peke yake. Inapendekezwa aongeze kusema:

(مِلْءَ السَّمَوَاتِ وَالأَرْضِ وَمِلْءَ مَا بَيْنَهُمَا وَمِلْءَ مَا شِئْتَ مِنْ شَيْءٍ بَعْدُ)

**Mil-assamaawaati Wal-ardhi Wamil-a Maabainahumaa Wamil-a Maas hi-ita Min-shai-in Baadu.** Au aongeze kusoma uradi wowote uliothibiti kunukuliwa kwa Mtume.

**11) Kusema:**

(سُبْحَانَ رَبِّيَ الأَعْلَى)

**(Subhaana Rabbiyal-Aalaa)** mara tatu au zaidi wakati wa kusujudu.

**12)** Kusema:

(رَبِّ اغْفِرْ لِي)

**Rabbighfir lii** baina ya Sijida mbili.

**13)** Kuleta Dua baada ya Tashahudi ya Mwisho na kabla ya kutoa

Salamu, kuomba kinga ya Jahanamu, kuomba kinga ya adhabu ya kaburini, kinga ya mtihani wa maisha na wa mauti na kinga ya mtihani wa Masihi Dajali.

## TISA: Namna Ya kusali:

Baada ya kuwa tumebainisha nguzo za sala na suna zake za matamshi na za vitendo, ni vyema kwetu tutaje namna ya kusali sala kamili yenye kujumuisha nguzo na suna kwa mujibu wa namna ilivyo katika nukuu za matamshi ya kisheria yaliyonukuliwa kuhusu namna Mtume alivyosali, ili namna hiyo iwe kigezo kwa Muislamu katika sala yake, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Salini kama mlivyoniona mimi nikisali".*** Hadithi hii imesimuliwa na Bukhari na Muslim.

Huu hapa mtiririko wa namna hiyo ya kusali:

❖ Mtume (s.a.w.) alipokuwa akisimama kwa ajili ya kusali alikuwa anaelekea Kibla, ananyanyua mikono yake miwili mpaka kwenye mabega au masikio yake, matumbo ya vidole vyake anayaelekeza Kibla na kusema: **Allahu Akbar**.

❖ Halafu anaweka kiganja chake cha mkono wa kulia juu ya kiganja chake cha mkono wa kushoto au juu ya mkono wake wa kushoto na kuviweka juu ya kifua chake.

❖ Kisha alikuwa anaomba dua ya kufungulia sala, kama ilivyotangulia kuelezwa katika Suna za sala za matamshi.

❖ Halafu alikuwa anasema: ***Auudhu Billaahi Minash-shaytwaanir-rajiim***. ***Bismillaahi-rahmaani-rahiim.***

❖ Kisha alikuwa anasoma sura Alfaatiha. Akimaliza kuisoma anasema: ***Aamin***.

❖ Kisha baada hapo alikuwa akisoma sura nyingine. Mara nyingine alikuwa akisoma sura ndefu, mara nyingine sura za wastani na mara nyingine sura fupi.

Pia alikuwa akirefusha zaidi kusoma katika sala ya Alfajiri kuliko

sala nyingine. Alikuwa akisoma kwa sauti ya kusikika katika sala ya Alfajiri na rakaa mbili za mwanzo za sala ya Magharibi na Isha, na kusoma kwa sauti ya chini katika sala na rakaa zisizokuwa hizo. Alikuwa akiifanya ndefu zaidi rakaa ya mwanzo ya kila sala kuliko rakaa ya pili.

❖ Kisha alikuwa ananyanyua mikono yake kama alivyoinyanyua wakati wa Takbira ya kuanzia sala na kusema: ***Allahu Akbar***. Halafu anainama kwa kurukuu akiiweka mikono yake juu ya magoti yake akiyashika vizuri huku vidole vyake vikiwa vimeachanishwa. Alikuwa ananyoosha mgongo wake na kichwa chake kukiweka sawa sawa; hakinyanyui wala hakiinamishi. Alikuwa akisema: ***Sub-haana Rabbiyal-adhiim*** (mara tatu au zaidi).

❖ Halafu alikuwa ananyanyua kichwa chake huku akisema: ***Samiallaahu limanhamidah*** na kunyanyua mikono yake kama alivyoinyanyua wakati wa kurukuu.

❖ Akishasimama sawa sawa, alikuwa akisema: ***Rabbanaa walakalhamdu, Mil-assamaawaati wal-ardhi, Wa mil-amaa Baynahumaa, Wamil-amaa Shi-ta min shay-in Baadu.*** Mtume alikuwa akikifanya kirefu kisimamo hiki ambacho kinaitwa *Itidali*.

❖ Kisha alikuwa akitoa Takbira, bila ya kunyanyua mikono yake, akiinama kuelekea kwenye kusujudu. Alikuwa anasujudu kwa kutumia paji lake la uso pamoja na pua yake, mikono yake, magoti yake na ncha za miguu yake. Alikuwa akivielekeza Kibla vidole vya miguu na vya mikono yake. Alikuwa anatulizana katika kusujudu kwake. Alikuwa akiligusisha vizuri paji lake la uso na pua yake kwenye ardhi, na kuegemea viganja vyake huku akinyanyua kongo zake zake isiguse ardhi. Pia alitenganisha miungabega yake isiguse mbavu zake, tumbo lake lisiguse mapaja yake na mapaja yake yasiguse miundi ya miguu yake. Katika kusujudu kwake alikuwa akisema: ***Subhaana Rabbiyal–aalaa*** mara tatu.

❖ Kisha alinyanyua kichwa chake huku akisema: ***Allahu Akbaru***. Kisha akitandaza mguu wake wa kushoto na kuukalia, na kuusimamisha mguu wake wa kulia na kuweka mikono yake juu ya

mapaja yake akisema: ***Rabbighfirlii, Rabbighfirlii*** au akisema:

(اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي وَارْحَمْنِي وَاجْبُرْنِي وَاهْدِنِي وَعَافِنِي وَارْزُقْنِي)

❖ Kisha alitoa Takbira na kusujudu. Katika kusujudu alikuwa akifanya kama alivyofanya kwenye sijda ya kwanza.

❖ Kisha alinyanyua kichwa chake huku akitoa Takbira, na kukaa kwenye mguu wake wa kushoto katika hali ya kutulizana, mpaka kila kiungo kirejee kwenye mahali pake. Kisha alinyanyuka akiegemea mikono yake kwenda kwenye rakaa ya pil.

❖ Akishasimama vyema, anaingia kwenye kisomo na kusali rakaa ya pili kama alivyosali ile ya mwanzo.

❖ Kisha alikaa kwa ajili ya Tashahudi ya Mwanzo akiwa amekaa kama alivyokaa baina ya sijida mbili. Aliweka mkono wake wa kulia juu ya paja lake la kulia, na mkono wake wa kushoto juu ya paja lake la kushoto na kuweka dole gumba lake la mkono wake wa kulia juu ya kidole chake cha kulia, na kufanya mfano wa duara kwa vidole hivyo. Aliashiria kwa kidole chake cha Shahada huku akikiangalia na kusema:

(التَّحِيَّاتُ لِلَّهِ وَالصَّلَوَاتُ وَالطَّيِّبَاتُ...) إلى آخر التشهّد.

Mpaka mwisho wake.

❖ Kisha alinyanyuka huku akitoa Takbira na kusali rakaa ya tatu na ya nne. Rakaa ya tatu na ya nne alikuwa akizifanya nyepesi kuliko rakaa ya kwanza na ya pili. Alikuwa anasoma sura Alfatiha kwenye rakaa hizo (ya tatu na ya nne).

❖ Kisha alikaa kwa ajili ya Tashahudi ya Mwisho na kutandaza makalio yake juu ya ardhi, na mguu wake wa kushoto kuupitisha chini ya paja la mguu wake wa kulia na kuusimamisha mguu wake wa kulia.

❖ Kisha alitoa Tashahudi ya Mwisho. Tashahudi hii ni ile ile Tashahudi ya Mwanzo, ila alikuwa akiongeza:

(اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحمَّد وعَلَى آلِ مُحمَّد، كما صلَّيتَ على إبراهيمَ و عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ

حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدٍ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ)

❖ Kisha alikuwa anaomba kinga kwa Allah amlinde na adhabu ya Jahanamu, adhabu ya kaburini, mtihani wa maisha na mtihani wa mauti, mtihani Masihi Dajali. Pia aliomba kheri za duniani na akhera alizotaka.

❖ Kisha alitoa Salamu upande wake wa kulia na kushoto akisema:

السَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ

❖ Akishatoa Salamu alikuwa akisema أستغفر الله mara tatu.

(اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلَامُ، وَمِنْكَ السَّلَامُ، تَبَارَكْتَ يَا ذَا الجَلَالِ وَالإِكْرَامِ)

Halafu alikuwa akisema:

(لا إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ، وَلَهُ الحَمْدُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، لا إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَلا نَعْبُدُ إِلاَّ إِيَّاهُ، لَهُ النِّعْمَةُ، وَلَهُ الفَضْلُ، وَلَهُ الثَّنَاءُ الحَسَنُ، لا إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ وَلَوْ كَرِهَ الكَافِرُونَ).

❖ Halafu alikuwa akimtukuza Allah akisema ***Sub-haanallaah*** mara thalathini na tatu. Halafu akimshukuru Allah akisema ***Alhamdu Lillaah*** mara thalathini na tatu. Halafu anamtukuza Allah akisema ***Allahu Akbar*** mara thalathini na tatu. Hizi ni mara tisini na tisa. Ili kukamilisha mia moja, alikuwa akisema:

(لا إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ، وَلَهُ الحَمْدُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ)

## KUMI: Mambo yanayobatilisha sala:

Mwenye kusali iwapo atafanya moja kati ya mambo yafuatayo, sala yake itabatilika na itamlazimu kurudia kuisali:

**1) Kuacha sharti katika masharti ya sala yaliyotangulia kutajwa bila ya udhuru.**

**2) Kuacha nguzo kati ya nguzo za sala**. Sawa awe ameiacha nguzo hiyo kwa makusudi au kwa kusahau, kama maelezo yake yatakavyokuja wakati wa kuielezea Sijida ya Kusahau.

**3) Kula au kunywa kwa makusudi.**

**4) Kuzungumza kwa kukusudia.**

**5) Kucheka.**

**6) Kufanya vitendo vingi ambavyo sio vitendo vya sala.**

**7) Kuongeza nguzo ya vitendo kwenye sala kwa makusudi, kama vile kuzidisha kurukuu au sijida n.k.**

## KUMI NA MOJA: Sijida ya Kusahau:

Inampasa mwenye kusali kuwa na unyeyekevu, kuelekeza fikra zake kwa Allah na kuitafakari Qur'ani anayosoma. Unyenyekevu ndio roho na ladha ya sala. Sala bila ya unyeyekevu ni mfano wa mwili bila ya roho. Allah Mtukufu amewasifia wenye unyeyekevu katika sala zao kwa kusema kuwa:

﴿قَدۡ أَفۡلَحَ ٱلۡمُؤۡمِنُونَ ۝١ ٱلَّذِينَ هُمۡ فِي صَلَاتِهِمۡ خَٰشِعُونَ﴾ المؤمنون: ١-٢.

*“**Hakika, wamefaulu waumini. Ambao ni wanyenyekevu katika sala zao”.*** Sura Almuuminuun:1-2.

Pamoja na hayo, mtu katika sala yake anaweza kusahau au kupitiwa, hasa ikitiwa maanani kuwa shetani anafanya bidii ya kumshawishi kwa kumtia wasiwasi na kumkumbusha mambo ya kidunia. Matokeo yake ni mtu mara nyingine huongeza au kupunguza, au kuwa na shaka kwamba Je, amezidisha au amepunguza?

Kwa mwenye kusali likimtokea moja kati ya hayo, basi Allah amemuwekea sheria ya kusujudu sijida mbili mwisho wa sala yake kwa sababu ya kusahau. Hii ni kumtia adabu shetani, kuziba upungufu na kumridhisha Allah mwingi wa rehema Atasujudu kama anavyosujudu katika sala. Kusujudu huku wanachuoni wanakuita kusujudu kwa ajili ya kusahau. Ufuatao ni uafafanuzi wa sheria zake:

Kusujudu kwa sababu ya kusahau kunatakiwa wakati wa kutokea kwa mambo matatu: Kuzidisha, kupunguza au kuwa na shaka katika kuzidisha au kupunguza.

❖ Iwapo mwenye kusali atazidisha kitendo katika vitendo vya sala kwenye sala yake, kama vile kuzidisha kurukuu, sijida, kisimamo au kukaa ni wajibu kwake kusujudu kwa sababu ya kusahau. Iwapo atajua ziada wakati akiwa kwenye sala atalazimika kuiacha ziada hiyo, atakamilisha sala yake na kusujudu kwa ajili ya kusahau.

❖ Ama atakapopunguza kwenye sala yake kwa kusahau na kuacha kitu, iwapo kilichowachwa ni nguzo na nguzo hiyo ikawa ni Takbira ya kuanzia sala, sala yake itakuwa haipo na kusujudu kwa ajili ya kusahau hakutasaidia. Atalazimika kuleta Takbira ya kuanzia sala na kurudia upya kusali.

❖ Iwapo kilichowachwa ni nguzo lakini sio Takbira ya kuanzia sala, kama vile kurukuu au kusujudu, basi iwapo atakumbuka kabla hajaanza kusoma kisomo cha rakaa nyingine, hapo atalazimika kurejea, kuleta hiki alichokiacha na pia kuleta nguzo zinazofuatia, kukamilisha sala yake na kuleta Sijida ya Kusahau.

Iwapo ataikumbuka nguzo iliyoachwa baada ya kuwa ameshaanza kusoma kisomo cha rakaa nyingine, rakaa yake ambayo amesahau nguzo yake itabatilika. Wakati huo, ataiweka rakaa inayofuatia mahali pa hii rakaa iliyobatilika, atakamilisha sala yake na kusujudu kwa ajili ya kusahau.

❖ Kama hakuijua nguzo iliyoachwa ila baada ya kutoa Salamu, basi ataihesabu kama imewachwa rakaa kamili. Kwa maana hiyo, iwapo ataikumbuka nguzo hiyo mara tu baada ya kusali au baada ya kusali kwa muda mfupi, naye bado yumo kwenye Tohara yake, basi ataleta rakaa kamili, atasujudu kwa ajili ya kusahau kutoa Salamu. Na iwapo ataikumbuka nguzo hiyo baada ya muda mrefu, au udhu wake umetenguka, atarejea kusali upya.

❖ Iwapo iliychowachwa ni Tashahudi ya Mwanzo, atalazimika kusujudu kwa ajili ya kusahau. Katika hali hii, atakapokumbuka kuwa amesahau kabla ya kukamilisha kusimama kwake kwenda kwenye rakaa ya tatu, hapo atalazimika kurejea ili kuileta Tashahudi hiyo. Na iwapo ameshakamilisha kusimama kwake, itakuwa makuruhu

kurejea. Iwapo atarejea, sala yake haitobatilika. Ama kama amesha anza kisomo cha rakaa ya tatu, hapo itakuwa haramu kwake kurejea.

❖ Iwapo atatia shaka katika sala yake kwamba, Je amesali rakaa mbili au tatu? Au amesali rakaa tatu au nne? Iwapo shaka mojawapo kati ya hizo mbili haikuwezekana kuwa na nguvu, hapo atachukua ile idadi ya chini zaidi na kukamilisha sala yake kwa kujenga juu ya idadi hiyo na atasujudu sijida mbili kwa ajili ya kusahau. Ama mojawapo ya shaka mbili itakapokuwa na nguvu zaidi, hapo atafanyia kazi uwezekano huo wenye nguvu zaidi na kukamilisha sala yake kwa kujengea uwezekano huo na atasujudu sijida mbili kwa ajili ya kusahau.

❖ **Angalizo:** Inamtosha mtu kusujudu kwa ajili ya kusahau baada ya kutoa Salamu au kabla yake.

# SHERIA ZA MAZISHI

Hekima ya Allah imeamua kuwa, vyovyote mwanadamu atakavyo ishi na umri wake ukawa mrefu, hatima yake ni kuondoka na kutoweka. Allah ataichukua roho yake na kiwiliwili chake kufunikwa kwenye udongo ili, katika siku ambayo hakuna ajuae wakati wake ila Allah, aje ajione amesimama mbele ya Mola wa viumbe kwa ajili ya kuhesabiwa. Hataona chochote mbele yake isipokuwa tu kauli na vitendo alivyovifanya duniani.

Hakika, hayo ni mauti ambayo mtu ayasikiapo tu moyo wake huenda mbio na ngozi yake kusisimka kwa sababu ya kuogopa kujiwa na mauti ghafla wakati bado hajajitayarisha nayo, na hajayafanyia hesabu.

Kwa sababu hii, imekuwa ni miongoni mwa balaa kubwa sana kwa mwanadamu kusahau kukumbuka mauti, na kutojishughulisha nayo kwa kufanya ulafi wa kukimbilia anasa na matamanio ya dunia. Siku moja Jibril alikwenda kwa Nabii (s.a.w.) na kumwambia: ***"Ewe Muhammad, ishi utakavyo, kwa hakika wewe utakufa. Na mpende umtakaye, kwa hakika wewe utatengana naye. Na fanya utakayo, kwa hakika wewe utalipwa kwa mujibu wake".*** Hadithi hii imepokewa na Tabaraniy na Hakim.

Ewe ndugu yangu Muislamu, ukumbuke muda huu adhimu, na kwamba kila mtu muda wake utamjia bila ya pingamizi. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ ٱلْمَوْتِ﴾ آل عمران: ١٨٥.

***"Kila nafsi ni yenye kuonja Mauti".*** Sura Aal-imraan:185.

Je, umejiandaa na nini kwa kukutana na Mola wako pale

atakapokuuliza kuhusu umri wako umeutumia kwa kitu gani? Ujana wako umeutumia kwenye nini? Elimu yako umeitumia vipi? Mali yako umeichuma vipi na umeitumia kwenye nini? Je, umeandaa jibu lolote kwa ajili ya siku kama hii?

Usidhani kwamba mali yako itakuokoa au kwamba cheo chako na mamlaka yako yatakulinda usife. Katika muda huo, anakuwa sawa yule aliyekufa na kuacha mali na cheo kikubwa na yule aliyekufa ilhali hakuacha hata shilingi. Katika muda huo anakuwa sawa yule aliyefariki akiwa peke yake na yule aliyefariki akiwa amezungukwa na madakatari, ndugu na marafiki.

Hivyo, inatakiwa kwa Muislamu kujiandaa siku zote kwa ajili ya kukutana na saa hii kubwa kwa kuzidisha kufanya amali njema, kujiepusha kutenda yaliyoharamishwa na kuifanya dunia hii kuwa ni kivuko cha usafiri kuelekea Akhera. Anatakiwa ajiandalie kwenye dunia hii yale mambo ambayo yatakayomfikisha kwenye radhi za Allah, rehema zake, msamaha wake na pepo yake.

## KWANZA: Hali ya Muislamu wakati wa kuugua na wakati wa kifo

**1)** Mwanadamu kuugua ni jambo lililopangwa na kufaradhiwa na Allah kwake, kwa lengo la kumfanyia mtihani na kumjaribu. Ni wajibu wa Muislamu kuridhia maamuzi ya Allah, kuivumilia mipango yake na kuwa na dhana nzuri kwa Mola wake. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Nabii (s.a.w.) isemayo kuwa: ***“Yanastaajabisha mambo ya Muislamu! Hakika, mambo yake yote ni kheri tupu, na hali hiyo haiwi kwa yeyote yule ila kwa Muumini tu. Iwapo mambo ya furaha yamemfika anashukuru, na hivyo inakuwa kheri kwake. Na iwapo yatamfika matatizo basi anakuwa na subira, na hivyo inakuwa kheri kwake”.*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. Pia hii ni kwa mujibu wa kauli ya Nabii (s.a.w.) isemayo kuwa: ***“Kamwe, asife mmoja wenu ila awe na dhana nzuri kwa Allah”***. Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**2)** Haijuzu kwa Muislamu kutamani mauti kutokana na maradhi kuwa mazito kwake au kutokana na tatizo zito lililomkuta, kwa

mujibu wa kauli ya Mtume isemayo kuwa: ***“Kamwe, mmoja wenu asitamani mauti kutokana na tatizo lililomkuta. Ikiwa hana budi kufanya, basi aseme hivi: Ewe Mola wangu, niweke hai maadamu uhai ni bora kwangu, na nipe mauti ikiwa mauti ni bora kwangu”.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**3)** Anayehisi kuwa muda wake kufa umekaribia, na anacho kitu anataka kuusia au anayo haki ya mtu mwengine juu yake, basi ni wajibu kwake kuandika Wasia wake. Hii ni kutokana na kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***“Sio haki kwa mtu Muislamu kulala siku mbili naye anacho kitu anachotaka kuusia isipokuwa tu Wasia wake uwe umeshaandikwa na upo chini ya kichwa chake”.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**4)** Iwapo mgonjwa amekaribia kufa na kufikia wakati wa kukata roho (Sakratul Mauti), basi ni wajibu kwa waliopo karibu naye kumkumbusha Shahada na kumtamkisha (لا إله إلا الله) ili anapoondoka duniani neno hilo liwe ndio neno lake la mwisho. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***“Watamkisheni maiti wenu neno la*** (لا إله إلا الله) ***Laa ilaha illa allah kwa sababu, yule ambaye neno lake la mwisho wakati wa mauti yake ni*** (لا إله إلا الله) ***Laa ilaha illa allah ataingia peponi siku moja, hata kama lilimpata la kumpata kabla”.*** Hadithi hii imepokewa na Ibnihibbaan.

**5)** Roho ikishatoka na jamaa wa marehemu wakawa na yakini kwamba kweli amekwishakufa, yafumbwe macho yake. Hii ni kwa sababu, Mtume (s.a.w.) alipoingia kwa Abusalamah na kukuta macho yake yamekodoka, aliyafumba kisha akasema kuwa: ***“Hakika, roho inapotolewa, macho yanaifuatilia”.*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**6)** Ni wajibu kwa aliyepo kwa maiti baada ya kutoka roho yake kumuombea dua. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***“Msijiombee isipokuwa kheri tu, kwa sababu Malaika wanaitikia Aamin kwa munayoyasema”, kisha akasema:***

(اللَّهُمَّ اغْفِرْ لأَبِي سَلَمَةَ، وَارْفَعْ دَرَجَتَهُ فِي الْمَهْدِيِّينَ، وَاخْلُفْهُ فِي عَقِبِهِ فِي الْغَابِرِينَ، وَاغْفِرْ لَنَا وَلَهُ يَا رَبَّ الْعَالَمِينَ، وَافْسَحْ لَهُ فِي قَبْرِهِ، وَنَوِّرْ لَهُ فِيهِ)

***Ewe Mola wangu, msamehe Abusalama na inyanyue daraja yake awe pamoja na walio ongoka, na muwekee mbadala baada yake pamoja na waliotangulia, na tusamehe sisi na yeye ewe Mola wa walimwengu, na mfanyie wasaa katika kaburi lake na muwekee nuru humo".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**7)** Ni wajibu kwa ndugu wa maiti kufumba mdomo wake na kuufunika mwili wake kwa kitu kinachousitiri, ili asije akawa maonesho kwa watazamaji. Iwapo maiti ni mwenye kuhirimia Hija au Umrah, hakifunikwi kichwa chake wala uso wake. Hii ni kutokana na kauli ya Mtume (s.a.w.) katika kumuelezea Swahaba aliyekufa kwa kukanyagwa na ngamia wake kwamba: ***"Muosheni kwa maji ya Mkunazi na mtieni sanda kwenye nguo mbili. Msimtie manukato wala musimfunike kichwa chake, kwa sababu Siku ya Kiyama atafufuliwa akiwa anatoa Talbiya".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**8)** Ni wajibu kwa ndugu wa maiti kufanya haraka kulipa deni la maiti iwapo analo, kutoka kwenye mali yake aliyoiacha na kabla ya kugaiwa kwa warithi. Iwapo maiti hana mali, inafaa kwa yeyote kujitolea kumlipia deni hilo.

## PILI: Kuosha maiti:

Kuosha maiti ni faradhi miongoni mwa faradhi za kutoshelezana, kwa maana kwamba iwapo baadhi watafanya, basi wajibu utawaondokea wengine. Hivyo, ni wajibu kwa wenye maiti kufanya haraka kumuosha, kumvisha sanda na kumuandaa kwa ajili ya kuzika. Katika uoshaji wa maiti ni wajibu kuzingatia mambo yafuatayo:

**1)** Aongoze kuosha maiti mwanaume Muislamu, ajuae sheria za uoshaji, mwenye kukubalika na muaminifu, ili asitiri mambo yasiyopendeza atakayoyaona kwenye mwili wa maiti, kama vile kiza cha uso wake na athari za aibu kwenye mwili wake n.k. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Mwenye kuosha maiti akamfichia aibu zake, Allah atamsamehe kutokana na kuficha huko mara arubaini".*** Hadithi hii imepokewa na Tabarany, Hakim na Bayhaqiy.

❖ Mtu bora zaidi kumuosha maiti mwanaume ni yule mtu ambaye marehemu ameusia aoshwe na yeye. Kisha anayefuatia ni baba wa marehemu, kisha mwanawe, kisha ndugu wa karibu zaidi na kuendelea.

❖ Iwapo maiti ni mwanamke mtu bora zaidi wa kumuosha ni mwanamke ambaye marehemu ameusia aoshwe na yeye. Kisha anayefuatia ni mama wa marehemu, kisha binti yake, kisha ndugu zake wa kike wa karibu zaidi kuendelea.

❖ Inajuzu kwa kila mmoja kati ya mke na mume kumuosha mwenzake. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) aliyomwambia bibi Aisha, Allah amuwiye radhi, kwamba: ***"Hakuna ubaya kwako iwapo utafariki kabla yangu nikakuosha".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Ibnimajah na Nasaaiy kwenye Sunan Kubraa. Naye Asmaa Binti Umais alimuosha mumewe Abubakar Assiddiq, Allah amuwiye radhi. Athar hii imepokewa na Malik.

❖ Inajuzu kwa mwanamke au mwanaume kumuosha maiti wa kike au wa kiume aliye chini ya umri wa miaka saba.

❖ Ikiwa maiti ni wa kiume aliyepo kwa wanawake kando, au maiti ni mwanamke aliyepo kwa wanaume kando, na akakosekana mtu wa kumuosha wa jinsia yake au maharimu wake, basi atafanyiwa Tayamamu. Anayemfanyia Tayamamu atampigisha mchanga kwa mikono yake kisha atampaka kwa mikono yake hiyo uso na mikono yake.

**2)** Maiti anavuliwa nguo zake wakati wa kuoshwa, kuwekewa kitu kinachositiri tupu yake, kuwekwa kwenye sehemu itakayomsitiri asionwe na watu.

**3)** Inapendekezwa kwa muoshaji kulainisha viungo vya maiti ikiwa jambo hilo litakuwa jepesi kwake, vinginevyo ataacha kufanya hivyo ikiwa atahofia viungo vya maiti kuvunjika.

**4)** Muoshaji atanyanyua kichwa cha maiti mpaka afikie kwenye hali ya karibu na kukaa kitako, na kukamua tumbo lake kwa upole sana ili kutoa uchafu uliomo.

**5)** Muoshaji anatakiwa aoshe tupu ya maiti na afunge kitambaa mkononi au avae glovu ili kusugulia tupu bila ya kuigusa kwa mkono wake usiokuwa na kitambaa au glovu na pia anatakiwa kutoiangalia.

**6)** Baada ya kuosha tupu ya maiti, muoshaji atapiga Bismillahi na kumtia Udhu maiti kama ule Udhu wa sala. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) alipomwambia aliyemuosha binti yake Zainabu kwamba: ***"Anzeni kwenye pande zake za kulia na sehemu zake za Udhu".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Muoshaji anatakiwa ajiepushe kuingiza maji kwenye pua au kinywa cha maiti. Anatakiwa afunge kitambaa kilicho loweshwa maji kwenye kidole chake ili kwa kutumia kidole hicho asafishe meno yake na tundu za pua yake.

**7)** Muoshaji anatakiwa aweke kwenye maji mkunazi kidogo au kitu chochote cha usafi kwa ajili ya kumuoshea maiti. Anatakiwa aanze kuosha kichwa chake na ndevu zake mara tatu.

**8)** Kisha ataosha mwili wa maiti akianzia upande wa kulia. Atamlaza upande wake wa kulia na kuosha upande wake wa kushoto mbele na nyuma. Kisha atamlaza upande wake wa kushoto na kuosha upande wake wa kulia mbele na nyuma.

**9)** Inapendekezwa kwa muoshaji kurudia kuosha mwili wa maiti mara tatu. Anaweza kuzidisha zaidi ya mara tatu ikihitajika kufanya hivyo, hata kama ikifikia mara saba au zaidi. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) kwa kinamama waliomuosha binti yake kwamba: ***"Muosheni mara tatu au saba au zaidi ya mara hizo mkiona inahitajika kufanya hivyo".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**10)** Iwapo utatoka uchafu kwa maiti baada ya kuoshwa, itasafishwa sehemu ulipotekea uchafu, kisha pazibwe kwa pamba. Kisha atatiwa Udhu kama Udhu wa sala. Ama kikitoka chochote kwa maiti baada ya kuvalishwa sanda haitarudiwa kumuosha.

**11)** Ni suna kwa muoshaji kutia Kafuri (Karafuu Maiti) kwenye josho la mwisho au manukato yoyote yale. Hii ni kutokana na kauli

ya Mtume (s.a.w.) aliyowaambiwa wanawake waliomuosha binti yake kuwa: ***“Wekeni kwenye josho la mwisho Kafuri au kitu chochote katika Kafuri”.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Kafuri ni manukato baridi ambayo harufu yake inafukuza wadudu.

Ama maiti kama ni mwenye kuhirimia Hijah au Umrah, asitiwe manukato mwilini mwake wala kwenye sanda yake.

**12)** Kama maiti ni mwanaume haipendekezwi kuchana nywele zake au kukata kucha zake au kunyoa nywele zake za siri au kunyoa nywele zake za kwapa. Ama maiti mwanamke, nywele zake zitafanywa mashungi matatu na kuwekwa nyuma ya mgongo wake.

**13)** Mimba iliyoharibika (Kipomoko) ambacho ni kichanga kilichotoka kwenye tumbo la mama yake kabla ya kutimia, ikiwa bado hakijatimiza miezi minne na umbile lake bado halijajulikana, kitakuwa hakioshwi wala kusaliwa, kama itakavyokuja kuelezwa. Kinatakiwa kufungwa kwenye kitambaa na kuzikwa. Kitakapotimiza miezi minne au zaidi kitaoshwa na kusaliwa, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) inayosema kuwa: ***“Na kipomoko husaliwa na wazazi wake kuombewa masamaha na rehema”***. Hadithi hii imepokewa na Ahmad na Abudaudi.

**14)** Inapendekezwa kwa mwenye kuosha maiti kuoga, na sio wajibu. Hii ni kutokana na kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***“Aliyeosha maiti aoge”.*** Hadithi hii imepokewa na Daarqutniy.

### TATU: Kumvisha sanda maiti:

Baada ya kumuosha maiti na kukausha mwili wake ni wajibu kuvishwa sanda kwa kutumia nguo inayositiri mwili wake wote. Kuvisha sanda kunafanyika kwa namna ifuatavyo:

**1)** Mwanaume atatiwa sanda kwa kutumia majamvi (shuka) matatu meupe, yaliyotiwa manukato na yaliyowekwa moja juu ya jingine. Baina ya kila moja yanawekwa manukato maalumu yaitwayo Hanuti (Karafuu Maiti).

Ama maiti mwanamke, sanda yake anayovishwa ni nguo tano: Shuka inayofunika sehemu ya chini ya mwili, mtandio unaofunika kichwa, gauni na majamvi mawili kwa ajili ya kufunika mwili wote.

**2)** Maiti anawekwa juu ya majamvi (shuka) matatu akiwa amelazwa chali.

**3)** Inatakiwa kuweka pamba iliyotiwa manukato kwenye makalio ya maiti ili kuzuia harufu mbaya isitoke. Pia yawekwe manukato kwenye mwili mzima na sehemu za kusujudia.

**4)** Ncha ya jamvi la mwanzo huwekwa juu ya upande wake wa kulia, na ncha yake nyingine juu ya upande wa kushoto. Kitaondolewa kitambara kilichokuwa kinafunika tupu yake. Kisha jamvi lake la pili na la tatu litafanywa hivyo hivyo.

Ama maiti mwanamke, mwanzo atawekewa shuka, kisha gauni juu yake, kisha mtandio juu ya kichwa chake na shingo yake, kisha kufunikwa kwenye majamvi wawili kama vile mwanaume.

**5)** Ncha za majamvi (shuka) zitafungwa upande wa kichwa na upande wa miguu ili yasifumuke. Sanda iliyobakia na ambayo inafunika mwili wa maiti itafungwa kwa uzi unaokazia ncha zake.

### NNE: Kumsalia maiti:

Baada ya kumaliza kumtia sanda maiti ni wajibu kwa Waislamu waliohudhuria kumsalia. Namna ya kumsalia maiti ni hii:

**1)** Maiti anawekwa chini akielekezwa upande wa Kibla.

**2)** Ni Suna kwa imamu kusimama kwenye kichwa ikiwa maiti ni mwanaume, na kusimama katikati ikiwa maiti ni mwanamke, na kichwa cha maiti kinakuwa kuliani mwa imamu.

**3)** Wanaosalia hupanga safu nyuma ya imamu. Inajuzu panapokuwa na nafasi finyu kusimama kuliani na kushotoni mwa imamu. Inapendekezwa kwa wanaosalia kusimama safu tatu nyuma ya imamu.

**4)** Imamu atatoa Takbira nne akiwa amesimama. Atanyanyua mikono yake pamoja na kila Takbira. Wanaosalia nyuma yake nao watatoa Takbira pamoja naye.

❖ Imamu na Maamuma baada ya Takbira ya kwanza watasoma sura Alfaatiha baada ya kusoma بسم الله الرحمن الرحيم , أعوذ بالله من الشيطان الرجيم

❖ Baada Takbira ya pili watamsalia Mtume (s.a.w):

(اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحمَّدَ وعَلَى آلِ مُحمَّدَ، كما صَلَّيتَ على إبراهيمَ و عَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيدٌ، اللَّهُمَّ بَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَعَلَى آلِ مُحَمَّدَ، كَمَا بَارَكْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَعَلَى آلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَمِيدٌ مَجِيد).

❖ Baada ya Takbira ya tatu atamuombea maiti dua hii ifuatayo:

(اللَّهُمَّ اغْفِرِ لِحَيِّنا ومَيِّتِنا، وصَغِيرنا وكَبِيرنا، وذَكَرِنا وأُنْثانا، وَشاهِدِنا وَغائِبِنا، اللَّهُمَّ مَنْ أَحْيَيْتَهُ مِنَّا فَأَحْيِهِ عَلَى الإيمانِ، وَمَنْ توَفَّيْتَهُ مِنَّا فتَوَفَّهُ على الإسلامِ، اللَّهُمَّ لا تَحرِمْنا أَجْرَه وَلا تُضِلَّنَا بَعْدَه) -رواه ابو داود-.

(اللَّهُمَّ اغْفِرِ لَهُ وَارْحَمْهُ، وَعافِهِ واعفُو عَنْه، وأَكْرِم نُزُلَه، وَوَسِّعْ مُدْخَلَه، وَاغْسِلْه بالماء والثلج والبَرَد، ونَقِّهِ من الخطايا كما نَقَّيْتَ الثوب الأبْيَضَ منَ الدَّنَس، وَأَبْدِلْهُ داراً خيراً من داره، وأَهْلاً خيراً من أهله، وزَوجاً خيراً من زوجه، وأَدْخِله الجنَّة، وَأَعِذْهُ مِنْ عَذابِ القَبْر، أو مِنْ عَذابِ النَّار)

Hadithi hii imepokewa na Muslim.

❖ Halafu ataleta Takbira ya nne na hataleta dua yoyote ile baada ya Takbira hiyo. Kisha atatoa Salamu kuliani na kushotoni mwake. Inajuzu kutoa Salamu moja tu. Maamuma watoa Salamu nyuma yake.

**5)** Iwapo maamuma atapitwa na baadhi ya Takbira za sala ya kumsalia maiti pamoja na imamu, basi ni juu yake kumfuata imamu katika zile Takbira alizoziwahi. Kisha baada ya Takbira ya nne atakamilisha Takbira zilizompita, na pia ataleta nyiradi zilizompita baada yake. Kisha atatoa Salamu akiweza kufanya hivyo kabla ya kunyanyuliwa kwa Jeneza. Vinginevyo ataleta Takbira mfululizo bila ya kuleta uradi wowote baina yake, na atatoa Salamu pamoja na imamu, na wala hana kosa juu ya hilo.

**6)** Aliyepitwa na sala ya Jeneza pamoja na imamu inajuzu kwake kumsalia maiti kaburini, na kuliweka kaburi baina yake na baina ya Kibla.

## TANO: Ubebaji wa Jeneza na uzikaji wa maiti:

Kumbeba maiti na kumzika ni katika faradhi za kutoshelezana; kwa maana kwamba baadhi ya Waislamu wakilifanya hilo, Waislamu wengine waliobaki watakuwa hawana dhambi. Hiyo ni kwa sababu kwamba, kumzika maiti ni kumhifadhi ili asije akawa kinyang'anyiro cha wanyama wakali au ndege. Pia ni kuwahifadhi walio hai wasipate kero kwa sababu ya uvundo na harufu mbaya za wafu inayotokana na kuvunda na kuoza kwa maiti.

Ni wajibu kwa Muislamu wakati wa kubeba maiti kuchunga mambo yafuatayo:

**1)** Maiti awekwe kwenye Jeneza au machela baada ya kutayarishwa na kutiwa kwenye sanda ili ubebwaji wake uwe mwepesi. Jeneza libebwe juu ya mabega katika pande zake nne. Inajuzu kulipakia Jeneza kwenye gari endapo makaburi yako mbali au kama kuna mvua inayonyesha au kama kuna sababu yoyote ile itakayofanya ubebaji wa Jeneza mabegani kuwa mgumu.

**2)** Ni suna Jeneza kwenda nalo haraka, kutokana na kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Lipelekeni haraka Jeneza. Kama ni jema basi mnalipeleka kwenye kheri, na kama ni kinyume na hivyo basi ni shari mnayoiondosha kwenye mabega yenu".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**3)** Sio sheria wakati wa kubeba maiti kupaza sauti kwa kusoma Qur'ani au uradi. Pia haijuzu kulisindikiza Jeneza kwa jambo lililokatazwa na sheria kama vile kulia kwa kupaza sauti, kulisindikiza kwa ubani au moto, kwa sababu Mtume wa Allah (s.a.w.) ***"Amekataza kusindikizwa Jeneza kwa mayowe".*** Hadithi hii imepokewa na Ibnimaajah. Abumusa Al-ash'ary alipofikwa na mauti alitoa Usia na kusema kuwa: ***"Msinisindikize kwa chetezo. Wakamuuliza: Je, umesikia chochote kuhusiana na jambo hilo? Akasema: Ndio. Nimesikia kwa***

***Mtume wa Allah (s.a.w.)”.*** Hadithi hii imepokewa na Ibnimaajah.

Ikiwa wakati wa kuzika ni usiku, itajuzu kuchuka kitu cha kuangazia njia wakati wa kubeba Jeneza na wakati wa kuzika.

**4)** Ni makuruhu kwa wanawake kusindikiza Jeneza, kwa mujibu wa kauli ya Ummu-atwiyyah, Allah amuwiye radhi, isemayo kuwa: ***“Tumekatazwa kusindikiza Jeneza, na katazo hilo halikukaziwa kwetu”.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**Ama wakati wa kuzika, inapasa kuzingatia mambo yafuatayo**:

**1)** Kutomzika maiti katika nyakati tatu zilizokatazwa, ila kwa dharura tu, kwa sababu ya kuwepo kwa katazo la Mtume (s.a.w.) juu ya jambo hilo. Nyakati hizo tatu ni hizi zifuatazo:

**a-** Toka kuchomoza kwa jua mpaka litakaponyanyuka kidogo kama robo saa.

**b-** Jua linapokuwa kati kati ya mbingu, mpaka litakapo ingia upande wa machweo. Muda huu uliokatazwa ni kabla ya Adhana ya Adhuhuri kwa dakika kumi.

**c-** Jua linapoinamia kutua mpaka litakapotua.

Maelezo haya ni kwa maujibu wa Hadithi ya Uqba bin Aamir, Allah amuwiye radhi, aliponukuliwa akisema kuwa: ***“Nyakati tatu Mtume wa Allah (s.a.w.) alikuwa akitukataza kusali na kuzika maiti wetu. Wakati Jua linapochomoza mpaka litakaponyanyuka, na wakati linaposimama mpaka litakapotenguka na wakati linapoinama kwa ajili ya kuzama”.*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**2)** Muislamu azikwe kwenye makaburi ya Waislam. Haifai Muislamu kuzikwa kwenye makaburi yasiyokuwa ya Waislamu.

**3)** Kaburi liwe na kina kirefu na pana ili kuhakikisha usalama wa maiti kutofikiwa na wanyama wakali au kutoka harufu yake. Mtume wa Allah (s.a.w) ameamrisha kufanya hivyo kwa kusema kuwa: ***“Chimbeni, fanyeni pana na mwende kina kirefu”.*** Hadithi hii imepokewa na Abudaud, Tirmidhiy, Annasai na Ibnimaaja.

**4)** Kwenye kaburi pawekwe mwanandani wa pembeni (mji) maiti awekwe humo. Mwanandani wa pembeni ni bora zaidi kuliko mwanandani wa katikati iwapo udongo wa kaburi ni mgumu na haujiachii. Ikiwa udongo wa kaburi ni laini na wenye kujiachia mwanandani wa katikati ya kaburi ni bora zaidi.

Mwanandani wa pembeni ni shimo chini ya ukuta wa kaburi upande wa kibla, ambalo linatosha kuingiza maiti. Ama mwanandani wa katikati ni shimo katikati ya kaburi kwa marefu, kiasi kwamba kaburi linakuwa kama vile hodhi na pembeni mwake hujengewa matofali na mfano wake, na maiti kuwekwa na kusakafiwa juu yake kwa mawe kwamba tu yasimguse maiti.

**5)** Mtu mwenye haki zaidi ya kumuingiza maiti kwenye kaburi lake ni yule ambaye marehemu ameusia, kisha ni ndugu zake wa karibu zaidi.

**6)** Ni Suna kumuingiza maiti kupitia upande itakapokuwa miguu ya maiti kaburini. Ikishindikana ataingizwa kupitia upande wa Kibla.

**7)** Anayemuingiza maiti kaburini aseme : (بسم اللَّه، وعلى مِلَّة رسول الله **Bismillah Wa-alaa Millati Rasuulillah** = Kwa jina la Allah tunazika na kwa mujibu wa mila ya Mtume wa Allah).

**8)** Maiti awekwe kwenye kaburi akiwa amelalia upande wake wa kulia huku uso wake ukiwa umeelekea Kibla. Kichwa chake kiwe kuliani mwa Kibla, miguu yake kushotoni mwa Kibla, nyuma ya mgongo wake uwekwe udongo wa kumzuia asibinuke akalala chali. Chini ya kichwa chake asiwekewe chochote kile.

**9)** Baada ya maiti kuwekwa kwenye kaburi, mafundo ya sanda kwenye kichwa na miguu yake yafunguliwe. Uso wake usiwekwe wazi, isipokuwa akiwa ni mwenye kuhirimia (Hija au Umra) kama ilivyotangulia kuelezwa.

**10)** Baada ya maiti kuwekwa kwenye mwanandani, yapangwe matofali kwenye uwazi wa mwanandani na kuziba matobo na mianya iliopo baina ya matofali kwa udongo ili mchanga usimfikie maiti.

**11)** Mchanga umiminwe kwenye kaburi. Ni suna kaburi kujazwa mchanga na kunyanyuliwa kiwango cha shubiri moja ili ijulikane kuwa ni kaburi na kwa sababu hiyo liweze kuwa katika hifadhi na kutopuuzwa. Liwe na muinuko wa nundu kama vile nundu ya ngamia. Liwekewe kokoto, na kokoto hizo zinyunyuziwe maji.

**12)** Kwenye kichwa cha kaburi pawekwe jiwe ili kaburi lijulikane na kulitofautisha na kaburi jingine.

**13)** Ni haramu kuweka jasi (chokaa) au kulijengeka kaburi au kulikanyaga kwa miguu, kwa sababu Mtume (s.a.w.) ***"Amekataza kulipaka jasi kaburi na kulikalia na kulijengea".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**14)** Inapendekezwa kwa mwenye kuhudhuria kuzika maiti baada ya kumaliza kuzika, asimame kwa muda amuombee maiti kusamehewa dhambi na amuombee kuwa imara katika kujibu maswali atakayoulizwa kaburini. Mtume (s.a.w.) baada ya kuzika maiti alikuwa akisimama kwenye kaburi na kusema kuwa: ***"Muombeeni ndugu yenu msamaha, kwakuwa yeye hivi sasa anaulizwa".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaud, Hakim na Bayhaqiy.

## SITA: Rambirambi (mkono wa pole):

Kinachokusudiwa kwa rambirambi ni kuwafanya wafiwa wapate moyo wa subira, kuwaliwaza na kuwapunguzia majonzi kutokana na huzuni, machungu na matatizo waliyoyapata kwa kuondokewa na mtu wao.

Inapasa kuchunga mambo yafuatayo wakati wa rambirambi:

**1)** Kutumia maneno ya kumfanya mfiwa awe na subira, kumliwaza na kumfanya aridhike na kuwa na imani kwa Allah (s.w.) kama vile kumwambia kuwa:

(أَعْظَمَ اللَّهُ أَجْرَكَ، وَأَحْسَنَ عَزَاءَكَ، وَغَفَرَ لِمَيِّتِكَ)

***"Allah ayafanye makubwa malipo yako, aufanye mzuri msiba wako na ampe msamaha maiti wako".***

Miongoni mwa maneno ya rambirambi ni kauli iliyothibiti kunukuliwa kwa Mtume (s.a.w.) kwamba, alisema katika kumfariji binti yake aliyefiwa na mwanawe kuwa:

(إِنَّ لِلَّهِ مَا أَخَذَ، وَلِلَّهِ مَا أَعْطَى، وَكُلُّ شَيْءٍ عِنْدَهُ إِلَى أَجَلٍ مُسَمًّى، فَلْتَصْبِرْ وَلْتَحْتَسِبْ)

***"Hakika, ni cha Allah tu alichokichukua, na ni cha Allah tu alichokitoa, na kila kitu kwake ni kwa muda maalumu. Basi awe na subira na atarajie malipo kwa Allah".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**2)** Rambirambi hazina idadi maalumu ya siku. Inajuzu kwa Muislamu kumfariji ndugu yake Muislamu hata baada ya siku tatu, kwa sababu lengo la rambirambi ni kupunguza machungu ya msiba, kumliwaza aliyepatwa na msiba ili aondokewe na huzuni. Mtume (s.a.w.) aliifariji familia ya Jafari baada ya siku tatu. Hadithi hii imepokewa na Ahmad.

**3)** Ni suna kwa ndugu wa familia ya wafiwa na majirani kuwatayarishia wafiwa chakula cha kuwashibisha, kwa sababu msiba ambao umewafika unawashughulisha washindwe kutayarisha chakula. Mtume (s.a.w.) alinukuliwa akisema kuwa: ***"Itayarishieni chakula familia ya Jafari, kwa sababu wamejiwa na jambo linalowashughulisha****"*. Hadithi hii imepokewa na Abudaudi, Tirmidhiy na Ibnimaja.

# SHERIA ZA ZAKA

## KWANZA: Maana ya Zaka

Zaka ni kima maalumu cha mali iliyofikia kiwango, kima ambacho ni wajibu kukitoa na kuwapa wanaostahiki kupewa kwa masharti maalumu. Ufafanuzi wake utafuata.

## PILI: Hukumu ya Zaka

Zaka ni faradhi katika faradhi za Kiislamu na ni nguzo kati ya nguzo tano za Uislamu. Ni nguzo muhimu sana baada ya Sala. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَأَقِيمُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُواْ ٱلزَّكَوٰةَ﴾ البقرة: ٤٣.

***"Na simamisheni Sala na toeni Zaka".*** Sura Albaqara: 43.

Pia Allah amesema kuwa:

﴿خُذۡ مِنۡ أَمۡوَٰلِهِمۡ صَدَقَةٗ تُطَهِّرُهُمۡ وَتُزَكِّيهِم بِهَا﴾ التوبة: ١٠٣.

***"Chukua kutoka kwenya mali zao zaka uwasafishe na uwatakase kwayo".*** Sura Attauba: 103.

Na imenukuliwa kwa Ibniumar, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano: Kukiri kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila Allah tu na kwamba Muhammad ni mjumbe wa Allah, na kusimamisha sala na kutoa zaka, na kuhiji na kufunga mwezi wa Ramadhani".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Zaka ni wajibu kwa kila Muislamu; awe mwanaume au mwanamke, mdogo au mkubwa, kwa masharti maalumu. Muislamu yeyote anayekana wajibu wa Zaka, Uislamu wake sio sahihi.

## TATU: Hekima ya kuwekwa kwa Zaka katika sheria

Allah ameiweka Zaka katika sheria na kuifanya ni wajibu kwa kuzingatia hekima nyingi kubwa. Miongoni mwa hekima hizo ni hizi zifuatazo:

**1)** Kuisafisha nafsi ya mwanadamu isiwe na tabia ya ubahili, tamaa na kuijengea mazoea ya kutoa kwenye njia ya Allah.

**2)** Kuikuza mali, kuisafisha na kuitia baraka.

**3)** Kuwafariji fukara, kukidhi mahitaji ya wenye shida na wasiokuwa na uwezo.

**4)** Kufanikisha miradi ya maslahi ya jamii ambayo maisha ya umma na ustawi wake unaitegemea miradi hiyo.

**5)** Kuzuia mrundikano wa mali kwa matajiri na wafanyabiashara, ili mali zisibaki tu kwenye mikono ya kundi maalumu kwenye jamii.

## NNE: Masharti ya kuwajibika kwa zaka.

Zaka inakuwa wajibu iwapo masharti yafuatayo yatapatikana:

**1) Uislamu.** Zaka sio wajibu kwa mtu ambaye sio Muislamu, kwa sababu hii ni ibada ambayo Muislamu kwa ibada hiyo anajisogeza karibu na Allah. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَمَا مَنَعَهُمْ أَن تُقْبَلَ مِنْهُمْ نَفَقَاتُهُمْ إِلَّآ أَنَّهُمْ كَفَرُوا۟ بِٱللَّهِ وَبِرَسُولِهِۦ﴾ التوبة: ٥٤.

***"Na hakuna kilichowazuia kutokubaliwa wanavyovitoa isipokuwa tu kwamba, wao walimkufuru Allah na Mtume wake".*** Sura Attauba: 54.

**2)** Kuwa huru. Zaka sio wajibu kwa mtumwa, kwa sababu anachomiliki mtumwa ni miliki ya bwana wake.

**3)** Umiliki kamili wa mali, ulio endelevu na uliozidi mahitaji ya lazima ya maisha ya mwanadamu, kama vile chakula, mavazi na makazi.

**4)** Mali kuzungukiwa na mwaka kamili wa kalenda ya Kiislamu (Hijriyah). Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa:

***"Hakuna Zaka kwenye mali mpaka izungukiwe na mwaka".*** Hadithi hii imepokewa na Ibnimaja. Sharti hili ni maalumu kwa zaka ya mifugo, vito vya thamani na bidhaa za biashara. Ama mazao ya kilimo, matunda, madini na Rikazi (mali iliyofukiwa ardhini na watu wa kale), mali hizi si sharti kuzungukiwa na mwaka. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَءَاتُواْ حَقَّهُۥ يَوۡمَ حَصَادِهِۦ﴾ الأنعام: ١٤١.

***"Na ipeni haki yake siku ya kuvunwa kwake".*** Sura Aal-imran: 141.

**5)** Mali kufikia kiwango. Kiwango ni kiasi maalumu cha mali ambacho lau kama kitapungua basi hakuna wajibu wa mali hiyo kuitolea zaka. Ufafanuzi wa viwango hivi utafuata.

## TANO : Mali ambazo ni wajibu kutolewa zaka na viwango vyake

Mali ambazo ni wajibu kutolewa zaka na viwango vyake ni hizi zifuatazo:

Thamani (dhahabu na fedha), mifugo, mazao yanayotoka kwenye ardhi na bidhaa za biashara.

**1) Thamani.** Thamani ni dhahabu, fedha na noti. Zaka inakuwa wajibu katika thamani hizi zikifikia kiwango, kama ifuatavyo:

❖ Kiwango cha dhahabu ni ile dhahabu yenye uzito wa (gramu 85 ) za dhahabu safi (Tola 24). Dhahabu ikifikia kiwango hiki cha uzito au zaidi, zaka yake ni robo ya moja ya kumi **(2.5%)**.

❖ Kiwango cha fedha ni fedha yenye uzito wa (gramu 595 ). Fedha ikifikia kiwango hiki cha uzito au zaidi, zaka yake pia ni robo ya moja ya kumi **(2.5%)**.

❖ Ama noti (fedha za karatasi) zinapimwa na kuthaminiwa kwa msingi wa kiwango cha dhahabu na fedha, pamoja na kuzingatia yenye manufaa zaidi kati ya dhahabu na fedha kwa masikini. Zaka yake pia ni robo ya moja ya kumi (**2.5%**).

***Zaka ya Mapambo:**

Mapambo ni dhahabu na fedha ambayo mwanadamu anaitumia kihalali katika kujipamba.

❖ Mapambo yaliyotayarishwa kwa ajili ya matumizi ya mapambo yaliyoruhusiwa – kama vile dhahabu inayotumiwa na mwanamke – sio wajibu kuyatolea zaka, iwapo yapo kwenye kiwango cha kujipambia tu. Ikiwa yatazidi kiwango hicho basi itakuwa wajibu kukitolea zaka kile kiasi kilichozidi endapo nacho kitafikia kiwango cha zaka.

❖ Vile vile zaka itakuwa wajibu kwenye mapambo ikiwa mmiliki wake atakusudia kuyahifadhi na kuyapatia faida.

**2) Mifugo:**

Mifugo inayokusudiwa ni ngamia, ng'ombe, mbuzi na kondoo. Zaka inakuwa wajibu kwenye mifugo hii kwa masharti yafuatayo:

**a.** Wanyama wawe wanafugwa kwa ajili ya maziwa na kuzalisha (biashara), na sio kwa ajili ya kufanyia kazi za kilimo au kubebea mizigo.

**b.** Wanyama, katika kipindi cha mwaka mzima au sehemu kubwa ya mwaka, wawe wanalishwa kwenye machunga ya asili ya Allah na ambayo hayakuoteshwa na mtu yeyote.

**c.** Wanyama wawe wamefikia kiwango cha kutolewa zaka. Kiwango cha ngamia ni watano (5), ng'ombe ni thalathini (30), mbuzi/kondoo ni arubaini (40). Hakuna zaka chini ya kiwango hiki cha wanyama wa kufuga.

**d.** Wanyama katika kumilikiwa kwake wawe wamezungukiwa na mwaka mmoja kamili wa Kiislamu (Hijiriya).

***Kiwango cha wajibu kutolewa katika zaka ya ngamia:**

Zaka haiwi wajibu katika ngamia isipokuwa tu wanapofika watano. Wakifika watano na zaidi zaka yake ni kama ifuatavyo:

| IDADI | | KIASI CHA WAJIBU |
|---|---|---|
| Kuanzia | Mpaka | |
| 5 | 9 | Kondoo mwenye mwaka mmoja au mbuzi mwenye miaka miwili |
| 10 | 14 | Kondoo wawili |
| 15 | 19 | Kondoo watatu |
| 20 | 24 | Kondoo wanne |
| 25 | 35 | Bintimakhaadh (Ngamia aliyetimiza mwaka mmoja kamili |
| 36 | 45 | Bintilabuni (Ngamia aliyetimiza miaka miwili kamili) |
| 46 | 60 | Hika (Ngamia aliyetimiza miaka mitatu kamili) |
| 61 | 75 | Jadhaa (Ngamia aliyetimiza miaka mine kamili) |
| 76 | 90 | Bintilabuni wawili |
| 91 | 120 | Hika wawili |
| 121 | 129 | Bintilabuni watatu |
| 130 | 139 | Hika mmoja na Bintilabuni wawili |
| 140 | 149 | Hika wawili na Bintilabuni mmoja |
| 150 | 159 | Hika watatu |
| 160 | 169 | Bintilabuni wanne |

❖ Ngamia wakiwa zaidi ya mia na ishirini, katika kila arubaini ni Bintilabuni mmoja na katika kila hamsini ni Hika mmoja.

***Kiwango cha wajibu kutolewa katika zaka ya n'gombe:**

Zaka haiwi wajibu katika n'gombe isipokuwa tu wanapofika thalathini. Wakifika thalathini na zaidi, zaka yake ni kama ifuatavyo:

| IDADI | | KIASI CHA WAJIBU |
|---|---|---|
| Kuanzia | Mpaka | |
| 30 | 39 | Tabii (N'gombe aliyetimiza mwaka mmoja) |
| 40 | 59 | Musina (N'gombe aliyetimiza miaka miwili) |
| 60 | 69 | Tabii wawili |
| 70 | 79 | Tabii mmoja na Musina mmoja |
| 80 | 89 | Musina wawili |
| 90 | 99 | Tabii watatu |
| 100 | 109 | Tabii wawili na Musina mmoja |
| 110 | 119 | Tabii mmoja na Musina wawili |
| 120 | 129 | Tabii wane au Musina watatu |

❖ N'gombe wakiwa zaidi ya sabini na tisa, katika kila thalathini ni Tabii mmoja na katika kila arubaini ni Musina mmoja.

***Kiwango cha wajibu kutolewa katika zaka ya mbuzi/ kondoo:**

Zaka haiwi wajibu katika mbuzi/kondoo isipokuwa tu wanapofika arubaini. Wakifika arubaini na zaidi, zaka yake ni kama ifuatavyo:

| IDADI | | KIASI CHA WAJIBU |
|---|---|---|
| Kuanzia | Mpaka | |
| 40 | 120 | Mbuzi mwenye mwaka mmoja au kondoo mwenye miezi sita |
| 121 | 200 | Kondoo wawili |
| 201 | 399 | Kondoo watatu |
| 400 | 499 | Kondoo wanne |
| 500 | 599 | Kondoo watano |
| 600 | 699 | Kondoo sita |
| 700 | 799 | Kondoo saba |

❖ Mbuzi/kondoo wakifika mia nne, katika kila mia ni kondooi mmoja.

❖ Wanyama kama wamefugwa kwa ajili ya biashara, itatolewa zaka ya bidhaa za biashara. Itatolewa robo ya moja ya kumi ( 2.5%) ya thamani yake.

**3) Kilichotoka kwenye ardhi:**

Zaka inakuwa wajibu katika nafaka zote na matunda yanayopimwa kwa uzito na yanayohifadhika, kama vile tende na zabibu. Zaka haitakuwa wajibu ila tu nafaka na matunda yatakapofikia kiwango, ambacho ni pishi mia tatu za Mtume (s.a.w.) ambazo takriban ni sawa na kilogramu (624). Nafaka na matunda yanapofikia kiwango na zaidi itakuwa wajibu kutolea zaka kama ifuatavyo:

**a-** Iwapo nafaka au matunda yamenyeshewa na maji ya mvua na hakukuwa na gharama kwenye kunyeshezewa kwake, kuna zaka ya

moja juu ya kumi (10%).

**b-** Iwapo nafaka au matunda yamemwagiliwa maji kwa gharama, kama vile maji ya visima, kuna zaka ya nusu ya moja ya kumi (5%).

**c-** Iwapo nafaka au matunda yamenyweshezewa maji kwa gharama na mara nyingine bila ya gharama, kuna zaka ya robo tatu ya moja ya kumi (7.5%).

❖ Zaka haiwi wajibu katika nafaka na matunda isipokuwa tu yanapokomaa na kufaa kwake kutumika kuwa dhahiri.

❖ Hakuna zaka kwenye matunda na mboga mboga, ila yatakapotayarishwa kwa ajili ya biashara. Hapo itatolewa zaka ya robo ya moja ya kumi (2.5%).

❖ Zaka ni wajibu katika Rikazi ambayo ni dhahabu, fedha au mali nyingine iliyofukuliwa ardhini na ambayo ilifukiwa zama za kabla ya Uislamu na ina alama ya kwamba ni ya makafiri. Ni wajibu kutoa zaka ya moja ya tano (5%) ya kiasi chochote kilichopatikana. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Na katika Rikazi kuna (zaka ya) moja ya tano".*** Hadithi hii imepokewa na Bukharin a Muslim.

Ama mali ya Rikazi iliyobaki ambayo ni nne ya tano (4/5) itakuwa ni ya yule aliye ivumbua.

**4) Bidhaa za Biashara:**

Bidhaa za biashara ni zile zilizondaliwa kwa ajili ya biashara kwa lengo la kupata faida, iwe ni kiwanja, mnyama, shamba, chakula, zana, hisa, nyaraka n.k.

❖ Zaka ni wajibu katika bidhaa za biashara endapo thamani yake, baada ya kutoa madeni na gharama za uendeshaji, zitafikia kiwango na kuzungukiwa na mwaka. Bidhaa hizi zitafanyanyiwa tathmini kwa thamani yenye faida zaidi kwa masikini kati ya dhahabu na fedha. Mtu atatoa zaka ya robo ya moja ya kumi (2.5%).

❖ Zaka ni wajibu katika bidhaa za biashara iwe imepatikana faida

au hasara, madamu mali iliyobaki imefikia kiwango.

❖ Kinachozingatiwa katika thamani ya bidhaa za biashara ni ile thamani ya soko wakati wa kukamilika kwa mwaka na sio thamani ya gharama iliyotumika kununulia.

❖ Inafaa kuitoa zaka bidhaa ya biashara iliyoko kwa mfanyabiashara ikiwa masikini anaihitaji bidhaa hiyo.

## SITA:Utoaji wa Zaka:

Masharti yaliyotangulia yakipatikana, ni wajibu kwa Muislamu kutoa zaka yake na kuwapa wanaostahiki kwa kuzingatia shuruti zifuatazo:

### 1) Wakati wa kutoa zaka:

❖ Ni wajibu kutoa zaka haraka mara tu wakati wake unapofika, na ambao ni kukamilika kwa mwaka. Na haijuzu kuichelewesha zaka isipokuwa tu kwa sababu maalumu, kama vile kungojea ndugu au jirani.

❖ Inajuzu kuharakisha mapema kutoa zaka ikiwa mali inayotolewa zaka imeshafikia kiwango kwa muda usiozidi miaka miwili. Hii ni kutokana na Hadithi ya Ali, Allah amuwiye radhi, ***“Kwamba, Mtume (s.a.w.) alitanguliza mapema kutoa zaka ya miaka miwili ya Abbas”***. Hadithi hii imepokewa na Abudaudi na Tirmidhiy.

### 2) Wapewao zaka:

Makundi ya ambao wanafaa kupewa zaka ni manane. Allah ameainisha makundi hayo katika kauli yake isemayo kuwa:

﴿إِنَّمَا ٱلصَّدَقَٰتُ لِلۡفُقَرَآءِ وَٱلۡمَسَٰكِينِ وَٱلۡعَٰمِلِينَ عَلَيۡهَا وَٱلۡمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمۡ وَفِي ٱلرِّقَابِ وَٱلۡغَٰرِمِينَ وَفِي سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱبۡنِ ٱلسَّبِيلِۖ فَرِيضَةٗ مِّنَ ٱللَّهِۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٞ﴾ التوبة: ٦٠.

***“Hakika zaka ni kwa ajili ya fukara, masikini, waifanyiao kazi zaka, wanaolainishwa nyoyo zao, katika kuachia (huru) watumwa, wenye madeni, kwenye njia ya Allah, msafiri, ikiwa ni faradhi toka***

***kwa Allah, na Allah ni mwingi wa ujuzi na mwingi wa Hekima".*** Sura Attauba: 60.

Ufuatao ni ufafanuzi wa hayo:

**1. Fukara:** Hawa ni wale watu ambao hawamiliki kitu cha kukidhi haja zao na haja za familia zao, kwa kutokuwa na kitu au kwakuwa na kitu lakini hakikdhi nusu ya mahitaji yanayomtosheleza. Watapewa kutoka kwenye zaka kiasi kitakacho watosheleza mwaka mzima**.**

**2. Masikini:** Hawa ni wale watu walio na nusu ya mahitajio yao au zaidi ya nusu, kama vile mtu mwenye mia moja na anahitajia mia mbili. Huyu atapewa kutoka kwenye zaka kiasi kitakachomtosheleza mwaka mzima.

**3. Wafanyakazi wa zaka**: Hawa ni wale watu walioajiriwa na kiongozi wa nchi kwa kazi ya kukusanya zaka, kuihifadhi na kuigawa kwa wanaostahiki. Hawa watapewa kutoka kwenye zaka kitakachowatosheleza muda wao wote wa kufanya kazi, hata kama ni matajiri.

**4. Wanaolainishwa nyoyo zao**. Hawa ni wale watu ambao wanatarajiwa kuingia kwao katika Uislamu au kuondosha shari zao au kuwafanya wawe imara katika imani yao.

**5. Kuacha huru watumwa.** Hawa ni watumwa wanaonunuliwa kwa kutumia mali ya zaka na kuachiwa huru, au watumwa ambao wameandikiana mkataba wa uhuru na wamiliki wao. Wanapewa zaka ili wajikomboe kutoka kwa wamiliki wao.

**6. Wenye madeni.** Hawa ni watu walio na madeni yasiyo ya kumuasi Allah na wakawa hawana cha kulipia. Ni sawa madeni hayo yawe kwa ajili yao wenyewe au kwa ajili ya watu wengine, kama vile kusuluhisha ugonvi.

**7. Kwenye njia ya Allah**. Hawa ni wapiganiaji dini wa kujitolea ambao wanapigana kwa ajili ya dini ya Allah na kumhubiri Allah.

**8. Msafiri**: Huyu ni msafiri aliyepata matatizo akiwa nje ya mjia

wake, na akawa hakupata mtu wa kumkopa.

❖ Si sharti kwa mwenye kutoa zaka kuyapa zaka makundi yote manane wakati wa kugawa zaka. Inajuzu kuligawia kundi lolote kati ya manane haya**.**

**3) Wasiofaa kupewa Zaka:**

Yeyote aliyepo katika kundi lolote lile kati ya makundi yafuatayo hafai kupewa zaka:

**a. Matajiri na wenye nguvu, wenye kuchuma.** Hii ni kutokana na kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***'Hakuna fungu kwenye hiyo zaka kwa tajiri wala mwenye nguvu anayechuma".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Abudaudi na Nasai. Wanatolewa katika hukumu hii wafanyakazi wanaoitumikia zaka, wenye madeni ambao ni matajiri na mwenye uwezo wa kuchuma ikiwa amejifunga katika kutafuta elimu ya sheria (ya Kiislamu) na akawa hana mali kwa ajili ya kujikimu.

**b. Yule ambaye mtoaji wa zaka ana wajibu wa kumhudumia**, kama vile baba, babu, mama, bibi, watoto na wajukuu. Hawa hawapewi zaka, kwa sababu huduma zao ni wajibu wa mwenye kutoa zaka.

**c. Makafiri wasiokuwa wenye kulainishwa nyoyo zao**. Hawa haijuzu kupewa zaka kwa sababu ya kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***'(Zaka) Huchukuliwa kutoka kwa matajiri wao na kurejeshwa kwa fukara wao'***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Maana ni kwamba, zaka inachukuliwa kutoka kwa matajiri wa Kiislamu na kugaiwa kwa fukara wao, na sio wengine.

**d. Watu wa familia ya Mtume (s.a.w.).** Hawa sio halali kupewa zaka, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***'Hakika, zaka si halali kwa familia ya Muhammad. Ilivyo ni kwamba, hiyo zaka ni takataka za watu'***. Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Watu wa familia ya Mtume (s.a.w) ni kila mwenye udugu wa

nasaba na Banihashim na Banimuttalib.

**4) Kuhamisha zaka kutoka nchi moja kuipeleka nchi nyingine**:

Inajuzu kuhamisha zaka kutoka nchi ambayo zaka imekuwa wajibu hapo kwenda nchi nyingine ya karibu au ya mbali, iwapo kuna haja ya kufanya hivyo, kama vile iwapo nchi ya mbali ni fukara zaidi, au ikiwa mwenye zaka anao ndugu fukara kwenye nchi ya mbali.

## SABA : Zaka ya Deni

Iwapo Muislamu analo deni kwa mtu, na deni hilo likafikia kiwango na kuzungukiwa na mwaka, basi hali yake hiyo haikosi kuwa kati ya mojawapo ya mambo haya mawili yafuatayo:

**LA KWANZA:** Kuwa na matario ya kulipwa deni, kwakuwa deni lake liko kwa mtu tajiri mwenye kukiri deni hilo. Mdai wa deni hilo atakuwa na wajibu wa kutoa zaka ya deni, ila tu hatatoa zaka mpaka pale atakapolipwa. Akishalipwa, atalitolea zaka ya kila mwaka katika miaka iliyopita.

**LA PILI:** Kutokuwa na matarajio ya kulipwa deni lake hilo, kwakuwa deni hilo liko kwa mtu msumbufu wa kulipa au liko kwa fukara au liko kwa mkata. Katika hali hii, mtu hatakuwa na wajibu wa zaka ya deni hilo ila tu baada ya kulipwa. Hapo atalijumuisha deni hilo kwenye jumla ya mali zake, na kuitolea zaka wakati wa kuzungukiwa na mwaka baada ya kulipwa. Ikiwa hana mali nyingine zaidi ya deni hilo, ataihesabia mwaka mpya.

## SHERIA ZA SAUMU

### KWANZA: Maana ya saumu

**Saumu** ni kujizuia kula, kunywa, kukutana kimwili (baina ya mke na mume) na mambo mengine yanayofunguza, kuanzia kuchomoza kwa alfajiri mpaka kutua kwa jua, kwa madhumuni ya kumuabudu Allah (s.w.).

### PILI: Uzuri wa Saumu

Saumu ina mazuri makubwa na faida adhimu zinazomletea mfungaji kheri za duniani na za akhera. Miongoni mwa mazuri hayo ni haya yafuatayo:

**1) Funga ni kinga ya mfungaji dhidi ya madhambi na moto.** Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa Mtume (s.a.w.) amesema kwamba: ***'Saumu ni ngao. Kwa hiyo, mfungaji asiseme maneno machafu, wala asifanye mambo ya kijinga. Iwapo mtu atampiga au kumtukana, basi aseme mara mbili kuwa : Mimi nimefunga'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari. Pia imenukuliwa kwa Jabir, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa Mtume (s.a.w.) amesema kwamba: ***'Funga ni ngao ambayo Muislamu anajikinga kwayo dhidi ya moto'.*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad.

**2) Kwenye Pepo upo mlango unaoitwa "Rayani". Hawaingii kupitia mlango huo isipokuwa wenye kufunga tu**. Imenukuliwa kwa Sahal, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa Mtume (s.a.w.) amesema kwamba: ***'Hakika, peponi upo mlango unaoitwa Rayani. Wafungaji wataingia kupitia mlango huo Siku ya Kiyama. Kamwe hataingia kupitia mlango huo yeyote isipokuwa wao tu. Patasemwa kuwa : Wako wapi wafungaji? Watasimama. Hataingia kupitia mlango huo yeyote yule isipokuwa wao tu. Wakishaingia, utafungwa na***

***hataingia yeyote yule kupitia hapo asiyekuwa wao'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**3) Mfungaji atakuwa na furaha siku atakayokutana na Mola wake.** Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***'Mfungaji ana furaha mbili anazozifurahi. Anapafuturu anafurahi na anapokutana na Mola wake anafurahi kwa saumu yake'.***Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**4) Funga ni ibada ambayo Muislamu atalipwa kwayo bila hisabu.** Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***'Kila amali ya mwanadamu inarudufishwa. Jema moja mara kumi mfano wake mpaka kufikia mara mia saba. Allah amesema kuwa: Isipokuwa saumu. Saumu ni yangu na mimi ndiye nitakaye ilipa'.*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**5) Funga ni sababu ya kufutiwa madhambi.** Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***'Sala tano na Ijumaa mpaka Ijumaa na Ramadhani mpaka Ramadhani ni vyenye kufuta (dhambi) baina yao iwapo mtu atajiepusha madhambi makubwa'.*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**6) Funga ni yenye kumuombea msamaha mwenye kufunga Siku ya Kiyama.** Imenukuliwa kwa Ibniumar, Allah amuwiye radhi, kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa**:** ***'Saumu na Qur'ani zitamuombea mja Siku ya Kiyama. Funga itasema : Ewe Mola wangu, nimemzuia mja wako kula chakula na matamanio yake wakati wa mchana, basi yakubali maombezi yangu kwake. Na Qur'ani itasema: Nimemzuwia mja wako kulala wakati wa usiku, basi yakubali maombezi yangu kwake. Mtume akasema : Utakubaliwa uombezi wao'.*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad.

## TATU: Hukumu ya kufunga mwezi wa Ramadhani.

Allah Mtukufu amefaradhisha funga ya mwezi wa Ramadahni na kuifanya nguzo katika nguzo za Uislamu ambazo Uislamu haukubaliwi bila ya nguzo hizo. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُتِبَ عَلَيۡكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ ﴾ البقرة: ١٨٣.

***'Enyi mlioamini, imefaradhishwa Saumu kwenu kama ilivyofaradhishwa kwa waliokuwepo kabla yenu ili mumche Allah'.*** Sura Albaqara: 183. Imenukuliwa kwa Ibniumar, Allah amuwiye radhi, kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa**: *'Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano. Kukiri kuwa hakuna mwenye haki ya kuabudiwa ila Allah tu na kwamba Muhammad ni Mjumbe wa Allah na kusimamisha sala na kutoa zaka na kuhiji na kufunga mwezi wa Ramadhani'***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

## NNE: Kuingia kwa mwezi wa Ramadhani.

**Kuingia kwa mwezi wa ramadhani kunapatikana kwa mojawapo ya mambo mawili:**

**1) Kuonekana kwa mwezi mwandamo wa Ramadhani**. Huku ni kuonekana kwa mwezi mwandamo usiku wa kuamkia tarehe thalathi ya mwezi wa Shabani. Mwezi ukionekana tu Ramadhani itakuwa imeshaingia na ni wajibu kufunga. Allah amesema kuwa:

﴿ فَمَن شَهِدَ مِنكُمُ ٱلشَّهۡرَ فَلۡيَصُمۡهُ ﴾ البقرة: ١٨٥

***'Kwa hiyo, yeyote miongoni mwenu atakayekuwa mjini (mwake) katika mwezi huo, aufunge'.*** Sura Albaqara:185.

**2) Kukamilika kwa hisabu ya siku thalathini za mwezi wa Shabani.** Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa Mtume (s.a.w.) amesema kwamba: ***'Fungeni kwa kuonekana kwake na fungueni kwa kuonekana kwake. Iwapo mwezi utaingia mawinguni msiuone, hisabuni (siku) thalathini (za mwezi wa Shabani)'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

❖ Katika kuthibiti kuonekana kwa mwezi wa Ramadhani unatosha ushahidi wa Muislamu mmoja muadilifu.

## TANO: Nani ana wajibu wa kufunga saumu ya Ramadhani?

Saumu ni wajibu kwa kila Muislamu, balehe, mwenye akili timamu, mkazi (sio msafiri), mwenye kuweza kufunga, asiyekuwa na vizuizi vya kisheria.

❖ Saumu sio wajibu kwa: Mtu ambaye sio Muislamu, mtoto mdogo ambaye sio mpambanuzi, mwendawazimu, mwanamke mwenye Hedhi na mwanamke mwenye Nifasi (damu ya uzazi). Kama watafunga, saumu yao haitakuwa sahihi na haitakubaliwa.

❖ Saumu pia sio wajibu kwa mtoto mwenye upambanuzi ambaye amefikia umri wa miaka minane, msafiri, mgonjwa ambaye funga inampa tabu au kumdhuru. Iwapo watafunga, funga yao itakuwa sahihi na itawatosheleza.

## SITA: Nguzo za saumu

Saumu ina nguzo mbili ambazo ni:

**1) Nia.** Nia ni mfungaji kukusudia kumuabudu Allah Mtukufu kwa funga yake hiyo. Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***'Ilivyo ni kwamba, kila amali (inazingatiwa) kwa nia'.*** Hadithi hii imepokewa na na Bukhari na Muslim.

Nia katika saumu ya Ramadhani inakuwa katika sura mbili:

**a. Nia ya jumla.** Nia hii ni mtu kunuwia kufunga mwezi mzima wakati wa kuthibitika kwake, kwa lengo la kumtii Allah na kujiweka karibu naye.

**b. Nia Maalumu.** Nia hii ni mtu, kila ifikapo usiku, kunuwia kufunga siku ambayo ni baada ya usiku huo. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kwamba: ***'Yeyote yule ambaye hakutia nia ya saumu usiku kabla ya alfajiri, basi huyo hana saumu'.*** Hadithi hii imepokewa na imepokewa na Tirmidhy, Nasai na Ibnimaja.

**2) Kujizuwia na yote yanayofunguza kuanzia kuchomoza kwa alfajiri mpaka kuzama kwa jua.** Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَكُلُوا۟ وَٱشْرَبُوا۟ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَكُمُ ٱلْخَيْطُ ٱلْأَبْيَضُ مِنَ ٱلْخَيْطِ ٱلْأَسْوَدِ مِنَ ٱلْفَجْرِ ۖ ثُمَّ أَتِمُّوا۟ ٱلصِّيَامَ إِلَى ٱلَّيْلِ﴾ البقرة: ١٨٧.

***'Na kuleni na kunyweni mpaka uwabainikie utepe mweupe upishane na utepe mweusi (hali) ambayo ni alfajiri. Kisha kamilisheni saumu mpaka usiku'.*** Sura Albaqara:187.

❖ Wakati wa kujizuwia unaanzia wakati wa kuchomoza kwa alfajiri ya kweli - ambayo inakuwa wakati wa adhana ya pili ya alfajiri -, na kumalizika kuzama kwa jua kunapothibitika.

## SABA : Nyudhuru zinazoruhusu kutofunga katika Ramadhani

Inaruhusiwa kutofunga katika mwezi wa Ramadhani kwa moja ya nyudhuru zifuatazo:

❖ **Ugonjwa na uzee.** Inajuzu kutofunga kwenye mwezi wa Ramadhani kwa mgonjwa ambaye ugonjwa wake unatarajiwa kupona. Atakapopona, itamlazimu kulipa siku ambazo hakufunga. Allah Mtukufu amesema kuwa :

﴿فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ فَعِدَّةٌ مِّنْ أَيَّامٍ أُخَرَ﴾ البقرة: ١٨٤.

'***Na yule ambaye miongoni mwenu atakuwa mgonjwa au yuko kwenye safari basi ni (alipe) idadi (ya siku asizofunga) katika siku nyingine'.*** Sura Albaqara : 184.

❖ Maradhi ambayo kutofunga kunaruhusiwa kwa sababu yake ni yale ambayo saumu inakuwa ngumu kwa mgonjwa kwa sababu yake, kama vile funga kumletea madhara au kumcheleweshea kupona.

❖ Mgonjwa asiyetarajiwa kupona au asiyeweza kufunga maishani mwake, kama vile kikongwe, yeye hatafunga na kila siku atakayoacha kufunga ataitolea fidia kwa kumpa chakula masikini mmoja. Na sio wajibu kwake kulipa siku ambazo hakuzifunga. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya AllahMtukufu isemayo kuwa:

﴿وَعَلَى ٱلَّذِينَ يُطِيقُونَهُۥ فِدۡيَةٞ طَعَامُ مِسۡكِينٖ﴾ البقرة: ١٨٤.

***'Na ni juu ya wale ambao hawawezi (kutoa) fidia ya chakula cha masikini'.*** Sura Albaqara : 184. Ibniabbas, Allah amuwiye radhi yeye na baba yake, amesema kuwa : ***'Hao (wanaokusudiwa katika aya hii) ni mzee kikongwe na mwanamke kikongwe wasioweza kufunga. Mahali pa kila siku moja watatoa chakula kumpa masikini'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

❖ Kiasi cha kumlisha masikini mmoja ni nusu pishi ya ngano, tende, mchele au mfano wake miongoni mwa chakula kikuu cha nchi husika. Kiwango cha pishi moja ni kujaa kwa viganja viwili vya mtu wa wastani mara nne, kitu ambacho ni sawa na kilogramu 2.5 za mchele. Kwa hiyo, chakula cha kulisha kila siku ni kilogramu moja na robo (1.25 Kg.) za mchele.

❖ **Safari.** Inaruhusiwa kwa msafiri wa masafa ya kupunguza sala kutofunga katika mwezi wa Ramadhani, na itakuwa wajibu kwake kulipa**,** kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu inayosema kuwa:

﴿فَمَن كَانَ مِنكُم مَّرِيضًا أَوۡ عَلَىٰ سَفَرٖ فَعِدَّةٞ مِّنۡ أَيَّامٍ أُخَرَ﴾ البقرة: ١٨٤.

**'*Na yule ambaye miongoni mwenu atakuwa mgonjwa au yuko kwenye safari basi ni (alipe) idadi (ya siku asizofunga) katika siku nyingine'.*** Sura Albaqara : 184.

❖ Masafa ya kupunguza sala ambayo ruhusa ya kutofunga na kupunguza sala imetolewa ni kilomita thamanini (80km).

❖ Hairuhusiwi kuacha kufunga ikiwa safari ni ya maasi au kwa kutaka kufanya hila ya kukwepa kufunga.

❖ Ni vyema kwa msafiri kufanya lililo jepesi zaidi kama ni kufunga au kutofunga pamoja na kutoa fidia. Imenukuliwa kwa Anas, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***'Tulikuwa tukisafiri pamoja na Mtume (s.a.w.) na mwenye kufunga hakuwa akimtia kasoro asiyefunga wala asiyefunga kumtia kasoro mwenye kufunga'***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Iwapo funga itampa shida msafiri au kumsababishia madhara, basi

kutofunga itakuwa bora zaidi kwake. Imenukuliwa kwa Jabir, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***'Sio katika wema kufunga katika safari'***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**3) Hedhi na Nifasi**. Ni wajibu kuacha kufunga kwa mwanamke aliyepatwa na damu ya Hedhi au Nifasi, na ni haramu kwake kufunga. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Abusaid Alkhudriy, Allah amuwiye radhi, kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***'Hivi, si anapopata Hedhi (mmoja wenu mwanamke) hasali na hafungi?'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari. Atalazimika kuzilipa siku ambazo hakufunga, kwa muijbu wa Hadithi iliyothibiti kunukuliwa kwa Bibi Aisha, Allah amuwiye radhi, kwamba amesema kuwa : ***'Tulikuwa tukifikwa na hilo – la kupata Hedhi – na tulikuwa tukiamrishwa kulipa Saumu, na hatukuamrishwa kulipa Sala'.*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**4) Mimba na Kunyonyesha.** Mwanamke anaruhusiwa kuacha kufunga akiwa mwenye mimba au mwenye kunyonyesha na akawa anajihofia yeye mwenyewe au mwanawe kupata madhara kwa sababu ya saumu. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Anas, Allah amuwiye radhi, kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***'Hakika Allah amemuondolea msafiri nusu ya sala, na (pia amemuondolea) saumu msafiri na mjamzito na mwenye kunyonyesha'.*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi, Nasai, Tirmidhiy na Ibnimaajah.

❖ Mjamzito au mnyonyeshaji atailipa kila siku asiyoifunga, ikiwa kutofunga kwake ni kwa sababu ya kujihofia yeye mwenyewe kupata madhara.

❖ Ikiwa mjamzito au mnyonyeshaji atamhofia mwanawe kupata madhara, basi yeye pamoja na kulipa atampa chakula masikini mmoja kwa kila siku moja. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Ibniabbas, Allah amuwiye radhi yeye na baba yake, aliyenukuliwa kusema kuwa : ***'Na mjamzito na mnyonyeshaji wakihofia -watoto wao- wataacha kufunga na watatoa chakula'.*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi.

❖ Wenye kazi ngumu na nzito wanaruhusiwa kutofunga iwapo wameanza kufunga na saumu ikawa nzito kwao, ikiwa wana mahitaji

makubwa ya kazi yao hiyo na ikiwa wana ulazima wa kuifanya kazi hiyo wakati wa mchana.

## NANE: Suna za funga na maadili yake.

Yanapendekezwa kwa mwenye kufunga mambo yafuatayo:

**1) Daku.** Hiki ni chakula kinacholiwa usiku wa manane ambao ni wakati wa mwisho wa usiku, kwa nia ya kufunga.

❖ Daku hupatikana kwa chakula kingi na kidogo, hata kama ni funda la maji. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) inayosema kuwa: ***'Kula Daku ni baraka, hivyo msiliache, japo mmoja wenu kunywa funda la maji, kwa sababu Allah na Malaika wake wanawaombea na kuwashushia rehema wenye kula daku'.*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad.

❖ Inapendekezwa kuchelewesha kula daku mpaka mwisho wa usiku kabla ya kuchomoza kwa alfajiri, kwa mujibu wa Hadithi ya Zaid bin Thabit, Allah amuwiye radhi, aliyesema kuwa: ***'Tulikula daku pamoja na Mtume (s.a.w.), kisha tukasimama kwenda kusali. Nikamwambia: Ilikuwa ni kipindi gani baina yao (baina ya kumaliza kula na kusali?). Akasema: Aya hamsini'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim**.**

**2) Kufanya haraka kufungua kinywa (kufuturu).** Kufungua kinywa kunatakiwa kuwe mara tu baada ya kuhakikisha kutua kwa jua, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) inayosema kuwa: ***'Watu wataendelea kuwa katika kheri madamu wanafanya haraka kufungua kinywa'***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**3) Kufungua kinywa kwa tende tosa**. **Asipopata tende tosa afungue kwa tende mbivu. Azifanye kwa idadi ya witri:** tatu au tano au saba. Asipopata tende, basi afungue kwa maji. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Anas, Allah amuwiye radhi, aliyesema kwamba Mtume (s.a.w.) ***"Alikuwa akifungua kinywa kwa tende tosa kabla ya kusali. Asipopata tende tosa alifungua kinywa kwa tende mbivu. Asipopata basi alifungua kinywa kwa funda la maji".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi na Tirmidhy.

**4) Dua wakati wa kufungua kinywa na ndani ya saumu.** Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) inayosema kwamba: ***'Watu wa aina tatu dua zao hazirejeshwi: Mwenye kufunga mpaka anapofungua kinywa na kiongozi muadilifu na dua ya mtu aliyedhulumiwa"***. Hadithi hii imepokewa na Tirmidhy. Ifuatayo ilikuwa Dua ya Mtume (s.a.w.) baada ya kufungua kinwa:

(ذهب الظمأ، وابتلَّت العروق، وثبت الأجر إن شاء الله).

***'Kiu kimeondoka na mishipa imerowa jasho na yamethibiti malipo Allah akipenda'.*** Hadithi hii ameipokea Abudaudi na Nasai kwenye kitabu chake cha SunanKubra.

**5) Kufanya ibada kwa wingi, kama vile kutoa sadaka, kusoma Qur'ani na kufuturisha wenye kufunga.** Imenukuliwa kwa Ibniabbas, Allah amuwiye radhi yeye na baba yake, kwamba amesema kuwa: ***'Mtume (s.a.w.) alikuwa mkarimu sana wa kheri, na alikuwa mkarimu sana anapokuwa katika Ramadhani pale anapokutana na Jibrili. Na Jibrili alikuwa akikutana naye katika kila usiku wa Ramadhani akidurusu naye Qur'ani. Kwa yakini kabisa, Mtume wa Allah anapokutana na Jibrili alikuwa mwepesi sana wa ukarimu kuliko upepo uliotumwa'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**6) Kujitahidi kusimama usiku na kusali Tarawehe,** kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***'Mwenye kusimama Ramadhani (kwa kusali) katika hali ya kuamini na kutaraji malipo kwa Allah husamehewa madhambi yake yaliyopita'***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**7) Kufanya Umra.** Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) inayosema kuwa: ***'Umra katika Ramadhani inalingana na Hija'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**8) Kuwa na tabia nzuri na kuvumila maudhi.** Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***'Itakapokuwa siku ya saumu ya mmoja wenu, basi asifanye maovu wala kupayuka. Iwapo atatokea yeyote akamtukana, basi aseme: Hakika, mimi ni mtu niliye na saumu'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

## TISA: Mambo yanayoruhusiwa katika saumu

Mwenye saumu ameruhusiwa kufanya lolote kati ya haya yafuatayo katika mchana wa mwezi wa Ramadhani:

**1)** Kuoga mchana wa Ramadhani. ***'Mtume (s.a.w.) alikuwa akijimwagia maji kichwani na ilhali yumo katika saumu, kwa sababu ya kiu au kwa sababu ya joto'.*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad na Abudaudi.

**2) Kuonja chakula, iwapo kuna haja ya kufanya hivyo**, kwa sharti kwamba chakula kisifike kwenye koo la mfungaji.

**3) Kujitia manukato na kujifukiza**, kwa sharti kwamba chembechembe za kitu kilichotengenezewa manukato hayo zisisifike kwenye koo, kama ilivyo katika moshi wa udi.

**4) Kuchoma sindano za dawa za kwenye nyama na mishipa**.

**5) Kutia wanja na dawa ya macho ya matone.**

**6) Kupiga mswaki.**

**7) Alfajiri kumpambazukia mwenye kufunga akiwa na Janaba.** ***'Mtume (s.a.w.) alikuwa akiamka alfajiri akiwa mwenye Janaba linalotokana na kukutana kimwili, halafu anaoga na anafunga'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Mfano wa mwenye Janaba ni mwanamke mwenye Hedhi au mwenye Nifasi. Akitoharika kabla ya sala alfajiri, saumu yake itakuwa sahihi, hata ikiwa bado hajaoga.

**8) Kubusu. Hii ni kwa yule mwenye kuweza kuidhibiti nafsi yake na matamamnio yake hayahemkwi**, kwa sababu Omar, Allah amuwiye radhi, aliihofia saumu yake alipombusu mkewe huku akiwa ni mwenye saumu. Mtume (s.a.w.) akamuuliza kuwa: "Unaonaje lau kama ungesukutuwa kwa maji nawe ukiwa umefunga? Nikamjibu kuwa: Hakuna ubaya katika hilo. Mtume (s.a.w.) akasema kuwa: Sasa kwa nini hilo liwe na ubaya?". Hadithi hii imepokewa na Ahmad na Abudaud.

**9) Kusukutua na kutia maji puani bila ya kuyafikisha mbali.**

## KUMI: Mambo yanayobatilisha saumu.

Mojawapo ya mambo yafuatayo linabatilisha saumu:

**1) Kutoka kwenye Uislamu**, kwa sababu ibada ikikutana na ukafiri haiwi sahihi, na ukafiri unaiporomosha amali. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿لَئِنۡ أَشۡرَكۡتَ لَيَحۡبَطَنَّ عَمَلُكَ﴾ الزمر: ٦٥.

***'Ukishirikisha (ukifanya Shirki) amali zako zitaporomoka'.*** Sura Azzumar :65.

**2) Kula na kunywa kwa makusudi.** Ama mtu atakapokula au kunywa akiwa amesahau, funga yake itakuwa sahihi na atalazimika kujizuia pale akumbukapo. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) aliposema kuwa: ***'Mwenye kusahau akiwa amefunga; akala au akanywa akamilishe funga yake, kwa sababu atakuwa amelishwa na kunyweshwa na Allah'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**3) Kuingiza kitu kwenye koo lake kwa makusudi**, kama vile mafukizo, sigara na ugoro. Ni sawa kuingiza huko kuwe kumefanyika kwa njia ya mdomo au pua.

❖ Dawa ya kupuliza inayotumiwa na wagonjwa wa pumu inahesabiwa kuwa ni miongoni mwa mambo yanayofunguza iwapo mgonjwa ataitumia mchana wa mwezi wa Ramadhani. Itakuwa wajibu kwake kulipa siku alizotumia dawa hiyo ikiwa matumizi yalikuwa kwenye vipindi mbali mbali. Kama matumizi yalikuwa ya kuendelea na hawezi kuyaepuka, itakuwa wajibu kwake kutoa fidia tu.

**4) Kubatilisha nia ya funga kwa kutia azma kuwa atafungua**. Aliyenuwia kufungua kabla ya wakati wa kufungua kinywa huku akiwa amefunga, funga yake itabatilika, hata kama hakufanya chochote kile kinachofunguza, kwa sababu atakuwa amebatilisha

nguzo katika nguzo za saumu.

**5) Kuingiza nia na kutoa (kusitasita) kwenye nia ya kufungua,** kwa sababu kusitasita kunaondoa uthabiti wa nia katika saumu.

**6) Kujitapisha kwa makusudi.** Kujitapisha ni kutoa chakula au kinywaji kilichomo tumboni kupitia mdomoni, kwa kutumia njia yoyote ile. Ni sawa matapishi hayo yawe mengi au kidogo.

❖ Iwapo mtu atashindwa nguvu na matapishi na kutapika bila ya hiyari yake, funga yake itakuwa sahihi, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) inayosema kuwa: ***'Aliyeshindwa nguvu na matapishi, hana wajibu wa kulipa, na aliyejitapisha kwa makusudi alipe'.*** Hadithi hii imepokewa Abudaudi, Tirmidhiy na Ibnimajah.

**7) Kutoka kwa damu ya Hedhi au Nifasi.** Iwapo mwanamke ataona damu ya Hedhi au Nifasi, funga yake itakuwa imetenguka, hata kama kutoka kwa damu kumetokea kabla ya kutua kwa jua kwa muda mchache sana.

**8) Kujitoa Manii kwa mfululizo wa kuangalia, kuchezeachezea, au kujitoa manii kwa mkono**, kwa sababu ladha hupatikana kwa njia hizo. Kwa sababu hiyo, kitendo hicho kinakuwa katika maana ya kujamiiana.

❖ Ama mwenye saumu akitokwa na Manii bila ya matamanio, kwa sababu ya maradhi, baridi au kuota basi funga yake haitoharibika kwa mujibu wa makubaliano ya wanazuoni wote.

**9) Kujamiiana.** Mwenye saumu ikiwa atafanya tendo la kujamiiana kwa makusudi, akiwa ni mwenye kukumbuka na kwa hiari yake katika mchana wa mwezi wa Ramadhani, saumu yake itakuwa imebatilika. Ni sawa Manii yametoka au hayakutoka. Ni wajibu kwake kutoa kafara ambayo ni kuacha huru mtumwa. Asipompata mtumwa, afunge miezi miwili yenye kufuatana. Kama hakuweza basi awape chakula masikini sitini.

## KUMI NA MOJA: Mambo yaliyo makuruhu katika saumu

Ni makuruhu kwa mwenye kufunga kila jambo ambalo kwa jinsi lilivyo linaweza kusababisha kuharibika kwa funga. Mambo hayo ni haya yafuatayo:

**1) Kuyafikisha ndani sana maji katika kusukutua na kutia maji puani**, kwa kuhofia maji yasije yakaingia tumboni mwake. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) aliposema kuwa: ***'Na fikisha ndani sana maji puani isipokuwa tu kama una saumu'.*** Hadithi hii imepokewa na Tirmidhy, Nasai na Ibnimaja.

**2) Kumbusu mke au kumuangalia sana au kukumbatiana naye kwa sehemu zisizokuwa za siri,** kwa sababu kufanya hivyo kunamsababishia mtu kuamsha matamanio yake au kutokwa na manii na hivyo kupelekea kuiharibu saumu.

**3) Kufikiria mambo yanao amsha matamanio**, kwa sababu kufanya ni kujipa raha inayoweza kusababisha kutoa Manii.

**4) Kuonja chakula bila ya haja**, kwa sababu jambo hilo linaifanya saumu kuwa katika hatari ya kuharibika kwa kuingia kitu kwenye koo lake.

**5) Kuchelewesha kufungua kinywa baada ya kuzama kwa jua bila ya haja**, kwa sababu katika kufanya hivyo kuna kujifananisha na Wayahudi.

**6) Kuacha kula daku,** kwa sababu kunasababisha udhaifu mchana na hivyo kupelekea kufungua.

**7) Kuunganisha saumu.** Kuunganisha saumu ni mtu kufunga siku mbili au zaidi bila ya kula au kunywa chochote baina ya siku hizo. Jambo hili matokeo yake ni mtu kudhoofu.

**8)** Kukusanya mate na kuyameza na kumeza kohozi ikiwa halijafikilia kwenye mdomo wake, kwa sababu jambo hilo linapingana na hekima ya funga.

**9)** Kupiga chuku. Kupiga chuku ni kupasua ngozi na kufyonza

damu nje kwa kutumia chombo cha kupigia chuku (pembe ya mnyama au chupa n.k.). Jambo hili ni makuruhu kwa yule ambaye linaweza kumsababibishia kudhoofika .

## KUMI NA MBILI : Zakatulfitri

Allah Mtukufu ameweka sheria ya Zakatulfitri mwisho wa mwezi wa Ramadhani ili kusafisha mambo ya upuuzi na machafu yaliyotokea katika ibada ya saumu na, wakati huo huo, Allah ameifanya zaka hiyo msaada kwa masikini wenye shida. Imenukuliwa kwa Ibniabbas, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa : ***'Mtume wa Allah amefaradhisha Zakatulfitri ili iwe kisafishaji cha mambo ya upuuzi na machafu na chakula kwa masikini'.*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi, Tirmidhiy na Ibnimaja.

Ndugu yangu Muislam ufuatao ni ufafanuzi wa sheria za Zakatulfitri.

### 1) Hukumu ya Zakatulfitri:

Zakatulitri ni wajibu kwa kila Muislamu, awe mwanaume au mwanamke, mdogo au mkubwa, aliye huru au mtumwa. Imenukuliwa kwa Ibniumar, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa : ***'Mtume (s.a.w.) amefaradhisha Zakatulfitri ; pishi moja ya tende au pishi ya ngano, kwa mtumwa na huru, na mwanaume na mwanamke, na mdogo na mkubwa, ambao ni Waislamu'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

❖ Ni wajibu kwa Muislamu kujitolea yeye mwenyewe Zakatulfitr na pia kuwatolea ambao huduma zao zinamlazimu yeye, kama vile mke na ndugu.

❖ Ni suna kumtolea Zakatulfitri mtoto aliyeko kwenye tumbo la mama yake (mimba) ikiwa tayari ameshatiwa roho.

### 2) Masharti ya kuwajibika kwa Zakatulfitri.

Zakatulfitri ni wajibu kwa masharti mawili yafuatayo:

**a-** Uislamu. Zakatulfitri sio wajibu kwa mtu ambaye sio Muislamu.

**b-** Muislamu awe na ziada ya chakula chake na familia yake na mahitaji yake mengine ya msingi katika siku ya Idi.

**3) Kiwango cha Zakatulfitri na chakula kinachotakiwa kutolewa:**

Kiwango cha wajibu kutolewa Zakatulfitri kwa kila Mislamu mmoja ni pishi moja ya Mtume (s.a.w.) ya chakula kinachotumika zaidi kwenye nchi husika, kama vile ngano, shairi, zabibu, jibini (maziwa makavu = chizi), mchele, mtama, mahindi n.k.

❖ Kiwango cha pishi ni vibaba vinne. Kibaba kimoja ni sawa na ujazo wa viganja viwili vya (umbile la mtu wa) wastani, ambapo kwa vipimo vya sasa ni karibu kilogramu (2.5) za mchele. Pazingatiwe tofauti katika ujazo wa pishi baina ya wepesi na uzito wa mchele (nafaka).

**4) Wakati wa kutoa Zakatulfitri.**

Zakatulfitr ni wajibu kwa kila Muislamu aliyewahi kutua kwa jua la siku ya mwisho ya mwezi wa Ramadhani. Wakati bora zaidi wa kutoa ni kuanzia kuchomoza kwa alfajri mpaka muda mchache sana kabla ya kutekeleza sala ya Idi. Pia inajuzu Zakatulfitri kutolewa kabla ya Idi kwa siku moja au mbili.

❖ Mwenye kuahirisha kutoa Zakatulfitri mpaka baada ya sala ya Idi, ni wajibu kwake kuitoa Zaka hiyo haraka kabla ya jua la siku hiyo ya Idi halijamchwea. Hii ni kwa maujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***'Mwenye kuitoa zaka hiyo kabla ya sala, hiyo ndiyo zaka inayokubalika. Na mwenye kuitoa baada ya sala, hiyo ni sadaka miongoni mwa sadaka'.*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi na Ibnimaja.

❖ Mwenye kuahirisha Zakatulfitri kwa makusudi atapata dhambi kwa kuahirisha kwake, na zaka hiyo itabaki kuwa deni lililopo katika dhima ambapo atapaswa kulilipa kwa kuitoa zaka hiyo.

**Wapewao Zakatulfitri:**

Yanapewa Zakatulfitri yale makundi manane ambayo yanapewa

zaka ya mali. Pamoja na hayo, jambo bora zaidi ni kupewa zaka hiyo masikini na fukara, kwa mujibu wa Hadithi ya Ibniabbas, Allah amuwiye radhi yeye na baba yake, inayosema kwamba ***'Mtume wa Allah amefaradhisha Zakatulfitri ili iwe kisafishaji cha mambo ya upuuzi na machafu na iwe chakula kwa masikini'.*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi, Tirmidhiy na Ibnimaja. Mtume amebainisha kuwa Zaka hii wapewe masikini, na kwa maana hiyo kupewa fukara ni jambo bora zaidi.

## KUMI NA TATU: Funga za hiari

Uislamu umeweka sharia ya funga za hiari. Funga hizi zinapendekezwa tu na sio wajibu. Mtume (s.a.w.) amehamasisha na kuuhimiza umma juu ya funga hizo kwa sababu ya mema ya ziada na makubwa yaliopo kwenye funga hizo. Siku ambazo Uislamu umehimiza kufungwa ni hizi zifuatazo:

**1) Siku ya Jumatatu na Alhamisi.** Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kwamba, amesema Mtume wa Allah kuwa: ***'Amali za waja huoneshwa (kwa Allah) siku ya Jumatatu na Alhamisi. Kwa hiyo, mimi napenda zioneshwe amali zangu*** **nikiwa nimefunga'**. Hadithi hii imepokewa na Abudaudi, Tirmidhiy, Nasai na Ibnimajah.

**2) Siku tatu katika kila mwezi.** Hizi ni *Siku Nyeupe* zilizopo katikati ya kila mwezi muandamo; mwezi kumi na tatu, kumi na nne na kumi na tano. Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***'Nimeusiwa na kipenzi changu (s.a.w.) mambo matatu: Kufunga siku tatu kila mwezi…'***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**3) Siku ya Ashura.** Hii ni siku ya kumi ya mwezi wa Muharram. Imenukuliwa kwa Abuqatada, Allah amuwiye radhi, kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***'Na funga ya siku ya Ashura nataraji kwa Allah afute (dhambi za) mwaka uliopo kabla yake'***. Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Ni suna kwa Muislamu kujumuisha baina ya kufunga siku ya tisa

na ya kumi za mwezi wa Muharram, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Kama nitabaki hai mpaka mwaka ujao, kwa yakini kabisa, nitafunga siku ya tisa".*** Amepokea Hadithi hii Muslim.

**4) Siku ya Arafa.** Hii ni siku ya tisa katika mwezi ya Dhulhija (Mfungotatu). Imenukuliwa kwa Abuqatada, Allah amuwiye radhi, kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Kufunga ya Siku ya Arafa nataraji kwa Allah kufute (dhambi za) mwaka kabla yake na mwaka baada yake".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**5) Siku tisa za mwezi wa Dhulhija**. Hizi ni siku tisa za mwanzo za mwezi wa Dhulhija. Imenukuliwa kwa baadhi ya wake wa Mtume (s.a.w.) wakisesema kuwa: ***"Mtume (s.a.w.) alikuwa akifunga siku tisa za mwezi wa Dhulhija".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Abudaudi na Nasai.

**6) Siku sita za mwezi wa Shawali (Mfungomosi).** Imenukuliwa kwa Abuayoub Al-ansariy, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Mwenye kufunga Ramadhani halafu akaifuatanisha (kufunga) siku sita za (mwezi wa) Shawali itakuwa kama kufunga mwaka mzima".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**7) Kufunga siku moja na kutofunga siku moja.** Imenukuliwa kwa Abdallah Bin Amri Bin Al-aas, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Funga inayopendwa sana na Allah ni funga ya (Mtume) Daudi. Alikuwa anafunga siku moja na kuacha kufunga siku moja".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**8) Kufunga siku nyingi za mwezi wa Shabani.**

Imenukuliwa kwa Aisha, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***"Mtume (s.a.w.) hakuwa akifunga siku nyingi sana za mwezi zaidi ya mwezi wa Shabani. Alikuwa akifunga mwezi wote mzima wa Shabani. Pia alikuwa akisema kwamba: Chukueni amali mnazoziweza, kwani Allah hachoki (kukulipeni) mpaka nyie mchoke (kutenda)".***

Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Katika mapokezi mengine imenukuliwa kwamba, Mtume (s.a.w.) ***"Alikuwa akifunga (mwezi wa) Shabani isipokuwa kidogo tu".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

**9) Mwezi wa Muharram.** Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Saumu bora zaidi baada ya Ramadhani ni mwezi wa Allah wa Muharram"***. Hadithi hii imepokewa na Muslim.

## KUMI NA NNE: Siku ambazo ni makuruhu kufunga.

Ni makuruhu kufunga siku zifuatazo:

**1) Kuikusudia siku ya Ijumaa peke yake kwa kufunga.** Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Asifunge mmoja wenu siku ya Ijumaa isipokuwa tu awe amefunga (siku) kabla yake, au atafunga (siku) baada yake".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**2) Kuikusudia siku ya Jumamosi peke yake kwa kufunga.** Imenukuliwa kwa Swammaa Binti Busri, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Msifunge siku ya Jumamosi isipokuwa tu zile funga zilizofaradhishwa kwenu. Na iwapo mmoja wenu hakupata isipokuwa ganda la zabibu au kijiti cha mti basi akitafune".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Abudaudi, Tirmidhiy, Nasai na Ibnimaja.

**3) Kufunga siku ya shaka**. Hii ni siku inayofuatia siku ys mwezi ishirini na tisa ya mwezi wa Shabani, ikiwa haikubainika kuonekana kwa mwezi wa Ramadhani, isipokuwa tu itakapowafikiana na siku ambayo Muislamu amejizowesha kuifunga kwa nia ya suna. Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Kamwe mmoja wenu asiitangulie Ramadhani kwa siku moja au siku mbili, ila tu kama mtu alikuwa anafunga funga yake basi afunge siku hiyo".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**4) Kufunga mwaka mzima**. Hii ni kufunga siku zote za mwaka

bila ya kufungua. Imenukuliwa kwa Abdillahi Bin Amri, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Hakufunga mwenye kufunga mwaka mzima".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**5) Kuunganisha funga.** Kuunganisha funga ni mfungaji kuunganisha siku kadhaa bila ya kufuturu baina yake, ila tu anaruhusiwa kuunganisha funga mpaka wakati wa kula daku. Imenukuliwa kwa Abusaid Al-khudriy, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa alimsikia Mtume (s.a.w.) akisema kwamba: ***"Msiunganishe (saumu). Na mmoja wenu yeyote anayetaka kuunganisha (saumu) aunganishe mpaka wakati wa kula daku. (Swahaba) Wakamwambia: Ewe Mtume wa Allah, wewe unaunganisha (saumu). Akawaambia: Mimi sio kama mlivyo nyiye. Hakika, mimi nalala nikiwa na mlishaji anayenilisha na mnyweshaji anayeninywesha"***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

## KUMI NA TANO: Siku ambazo ni haramu kufungwa:

Ni haramu kufunga siku zifuatazo:

**1) Siku ya Idd Elfitri na siku ya Idd El-haj.** Amesema Omar Bin Alkhattaab, Allah amuwiye radhi, kuwa: ***"Siku mbili hizi amekataza Mtume wa Allah kuzifunga; siku yenu mnayofungua saumu yenu, na siku mnayokula nyama zenu za kuchinja".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**2) Siku Tatu Za Tashriiq**. Hizi ni siku za mwezi kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu za mwezi wa Dhulhija ambazo zinakuwa baada ya Idd El-haj. Imepokewa kwa Nubaisha Alhudhaliy, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Siku za Tashriiq ni siku za kula, kunywa na kumtaja Allah"***. Hadithi hii imepokewa na Muslim.

# SHERIA ZA HIJA NA UMRA

Hija ni nguzo katika nguzo tano za Uislamu, na ni faradhi katika faradhi zake kubwa. Kamwe hauwi sahihi Uislamu wa anayekana wajibu wa Hija. Imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: alituhutbia Mtume (s.a.w.) na kusema kwamba: ***"Enyi watu, hakika Allah amefaradhisha Hija kwenu. Kwa hiyo, hijini".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Allah amekutanisha Hija na Umra na kuamrisha zitetekelezwe. Amesema kuwa:

﴿وَأَتِمُّوا۟ ٱلْحَجَّ وَٱلْعُمْرَةَ لِلَّهِ﴾ البقرة: ١٩٦.

***"Na kamilisheni Hija na Umra kwa ajili ya Allah".*** Sura Albaqarah: 197.

Aidha Mtume (s.a.w.) amehimiza kufuatanisha baina ya Hija na Umra na kusema kuwa: ***"Fuatanisheni baina ya Hija na Umra kwa sababu, (ibada hizo) zinaondosha ufukara na dhambi kama vile moto unavyo ondosha taka za chuma, dhahabu na fedha"***. Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Abudaudi, Tirmidhiy na Nasai. Pia imenukuliwa kwa Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w) kwamba: ***"Umra mpaka Umra ni kifutio cha dhambi baina yake na Hija kamilifu haina malipo isipokuwa pepo tu".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

## KWANZA: Maana ya Hija na Umra.

Hija ni kuikusudia Nyumba Tukufu ya Allah katika miezi maalumu, kwa ajili ya ibada ya kutufu, kutembea baina ya Swafa na Marwa, kusimama Arafa na ibada nyingine ambazo maelezo yake yatakuja. Umra ni kuizuru Nyumba Tukufu ya Allah kwa ajili ya kutufu na kusaayi.

## PILI: Masharti ya kuwajibika kwa Hija na Umra.

**1) Uislamu**. Hija sio wajibu kwa mshirikina, kafiri na aliyeuacha Uislamu. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿إِنَّمَا ٱلۡمُشۡرِكُونَ نَجَسٞ فَلَا يَقۡرَبُواْ ٱلۡمَسۡجِدَ ٱلۡحَرَامَ بَعۡدَ عَامِهِمۡ هَٰذَاۚ﴾ التوبة: ٢٨.

***"Ilivyo ni kwamba makafiri ni Najisi. Kwa hiyo, wasiusogelee Msikiti Mtukufu baada ya mwaka wao huu".*** Sura Attauba: 28.

**2) Akili timamu.** Hija sio wajibu kwa mwendawazimu, kwa mujibu wa kauli ya Mtume isemayo kuwa:

(رُفِعَ القَلَمُ عَنْ ثَلاثٍ: عَنِ النَّائِمِ حَتَّى يَسْتَيْقِظَ، وَعَنِ الصَّبِيِّ حَتَّى يَحْتَلِمَ، وَعَنِ المَجْنُونِ حَتَّى يَعْقِلَ).

***'Kalamu (ya kuandika dhambi) imeondolewa isiandike (dhambi) kwa watu watatu; kwa mwendawazimu mpaka arejee kwenye akili zake timamu, kwa aliyelala mpaka atakapoamka na kwa mtoto mdogo mpaka atakapobalehe".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Abudaudi, Tirmidhiy, Nasai na Ibnimaja.

**3) Kufikia umri wa balehe**. Hija sio wajibu kwa mtoto mdogo ambaye hajafikia umri wa balehe. Akihiji, Hija yake itakuwa sahihi, na Walii (mlezi) wake atatia Nia kwa niaba yake. Imenukuliwa kwa Ibniabbas, Allah amuwiye radhi yeye na baba yake, kwamba ***"Mtume (s.a.w.) alikutana na msafara katika eneo la Rawhaa akawauliza: Ni kina nani nyinyi? Wakamjibu: Ni Waislamu. Wakamuuliza: Na wewe ni nani? Akawajibu: Ni Mtume wa Allah. Mwanamke mmoja akamnyanyua mtoto wake na kumuuliza Mtume: Je, huyu anaweza kuhiji? Mtume akamjibu: Ndio, na wewe utapata malipo".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. Hata hivyo, Hija hii haimtoshelezi kuwa ndio Hija ya Uislamu (Hija ya faradhi). Imenukuliwa kwa Ibniabbas, Allah amuwiye radhi yeye na baba yake, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Mtoto yeyote aliyehiji (akiwa mdogo) na akafikia balehe, ni wajibu kwake kuhiji Hija nyingine".*** Hadithi hii imepokewa na Tabaraniy, Ibnikhuzaima, Hakim na Bayhaqiy.

**4) Kuwa na uwezo.** Amesema Allah kuwa:

﴿وَلِلَّهِ عَلَى ٱلنَّاسِ حِجُّ ٱلْبَيْتِ مَنِ ٱسْتَطَاعَ إِلَيْهِ سَبِيلًا﴾ آل عمران: ٩٧.

***"Na ni wajibu kwa watu kuhiji Nyumba (Tukufu) kwa ajili ya Allah (kwa) yule mwenye kuweza kuiendea".*** Sura Aal-imran: 97. Kinachokusudiwa kwa uwezo ni uwezo wa chakula, uwezo wa usafari, matumizi ya wakati wa kwenda na kurudi. Pia matumizi yake yawe ni ziada juu ya matumizi ya familia yake na watu wanaomlazimu kuwahudumia muda wake wa kwenda na kurudi.

❖ Ni katika uwezo pia uwezo wa mwili kwa anayekwenda kuhiji; kwa maana kwamba mwili wake uwe salama usiokuwa na maradhi au udhaifu unaomkwaza kuhiji, kama vile mzee kikongwe au mtu aliyepata tatizo ambalo linamzuwia kuhimili kukaa kwenye chombo chake cha usafiri na kuhimili usumbufu wa safari.

❖ Vile vile ni katika uwezo njia iwe salama, kwa namna ambayo mwenye kuhiji yeye mwenyewe na mali yake viwe salama.

**5) Kuwepo kwa Mahram.** Hili ni sharti maalumu kwa mwanamke. Iwapo mwanamke atataka kwenda kufanya Hija au Umra ni lazima afuatane na mumewe au mmoja wa Mahramu zake. Mahramu ni mwanaume balehe, mwenye akili timamu, aliye haramu kumuoa mwanamke huyo – uharamu wa milele. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Ibniumar, Allah amuwiye radhi yeye na baba yake, isemayo kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Mwanamke asisafiri – safari ya – siku tatu ila pamoja naye awepo mahramu".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

❖ Baadhi ya wanazuoni wameruhusu kwa mwanamke aliyekosa mahramu kusafiri kwa ajili ya Hija, akiwa kwenye msafara salama wa wanawake au wanaume wema. Ruhusa hii ni maalumu kwa Hija ya faradhi tu na sio Hija ya suna.

**6) Kutokuwepo kwa Eda.** Vile vile ni sharti kwa mwanamke asiwe kwenye Eda ya kuachwa au Eda ya kufiwa katika kipindi cha kuwepo kwake safarini kwenda Hija, kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿لَا تُخْرِجُوهُنَّ مِنۢ بُيُوتِهِنَّ وَلَا يَخْرُجْنَ إِلَّآ أَن يَأْتِينَ بِفَٰحِشَةٍ مُّبَيِّنَةٍ﴾ الطلاق: ١.

***"Msiwatoe kwenye nyumba zao wala wao wasitoke isipokuwa tu watakapofanya uchafu (zinaa) ulio dhahiri".*** Sura Attalaq: 1.

# NAMNA YA KUTEKELEZA UMRA

Muislam anapotaka kufanya Umra ni wajibu kwake kufuata mambo yafuatayo:

**1)** Kwenda kwenye mojawapo ya Mikati (vituo) za maeneo[1] ambayo Mtume (s.a.w) ameya ainisha na kuwawekea watu wa kila muelekeo Mikati yao inayowahusu. Mikati ni tano:

**a) Dhulhulaifa**. Hii ni Mikati ya watu wa Madina na watu wasiokuwa wa Madina ambao wanapitia hapo. Hivi sasa mahali hapo panaitwa **Aabaar Ali.**

**b) Juhfah.** Hii ni Mikati ya watu wa Sham na wanaokwenda Hija kupitia hapo kutokea Misri na Morocco. Mwenye kukusudia Hija atatia (atahirimia) mahali panapoitwa Rabigh, mahali ambapo ni kabla ya Juhfah kuelekea upande wa baharini.

**c) Karnulmanaazil.** Hii ni Mikati ya watu wa Najdi na wanaopitia Najdi. Hivi sasa mahali hapo panaitwa **Asseil Alkabiir.**

**d) Yalamlam.** Hii ni Mikati ya watu wa Yemen, Tihama na India. Sehemu hii ipo kusini mwa mji wa Makka, na hivi sasa inaitwa **Saadiya.**

**e) Dhaatu Irki.** Hii ni Mikati ya watu wa Iraq na watu wengine wa mashariki. Hivi sasa mahali hapo panaitwa **Dhwariiba.**

Haijuzu kwa mtu aliyekusudia Makka na kukusudia kuhiji au kufanya Umra kuzipita sehemu hizo bila ya kuhirimia (kutia Nia). Ni sawa aliyepita awe mtu wa hapo au asiyekuwa mtu wa hapo.

---

(1) Mikati za maeneo ni maeneo yanayo uzunguka mji wa Makka na ambayo Mtume (s.a.w.) ameya ainisha. Haifai kwa anayekusudia kuhiji au kufanya Umra kuyapita maeneo hayo bila ya kuhirimia (kutia nia).

❖ Ama mtu ambaye makazi yake ni baada ya Mikati hizi za maeneo, kama vile maeneo ya Qudaid, Usfaan, Marri Dhahran au Jeddah, yeye Mikati yake ni hapo hapo anapoishi. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Anayeishi ndani ya humo, basi – atahirimia – hapo anapoishi"***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

❖ Yule ambaye ni katika wakazi wa Makka atakwenda sehemu ya karibu zaidi ya mipaka ya Mji Mtukufu wa Makka, kama vile Tan-iim na kuhirimia hapo.

**2)** Mwenye kufanya Umra akifika kwenye Mikati atavua nguo zake zilizoshonwa, atanyoa nywele zake za sehemu za siri na za kwenye kwapa, ataoga, atajitia manukato kichwani, kwenye ndevu na mwilini. Haidhuru ikibaki athari ya manukato baada ya kuhirimia, ila tu anatakiwa aepuke kuzitia manukato nguo zake.

Ama mwanamke, yeye ataoga hata kama yumo kwenye Hedhi au Nifasi, ila tu hatakiwi kujitia manukato.

**3)** Baada ya kuoga na kujitia manukato, atavaa nguo za Ihramu. Nguo za Ihramu kwa mwanaume ni shuka ambayo ataivaa upande wa nusu ya chini ya mwili wake, na nguo ya kujitanda ambayo ataitupia upande wa nusu ya juu ya mwili wake. Inashurutiwa nguo hizi zisiwe zemeshonwa. Ama mwanamke, yeye anaruhusiwa kuvaa nguo yoyote atakayo ila tu asiviweke wazi viungo vyake na asijipambe. Pia ajiepushe kufunika uso na viganja vyake, isipokuwa akihofia fitina, hapo itajuzu kwake kufunika uso wake bila ya kujitia Nikabu.

**4)** Baada ya mwenye kufanya Umra kuvaa mavazi ya Ihramu, atasali hapo Mikati ikiwa wakati ni wa sala ya faradhi. Ikiwa sio hivyo, atasali rakaa mbili za suna na kuhirimia baada ya rakaa mbili hizo.

**5)** Akimaliza kusali, atapanda kipando chake na kuhirimia Umra huku akisema:

**(لَبَّيكَ اللَّهمَّ لبَّيك، لبَّيكَ لا شريكَ لكَ لبَّيك، إنَّ الحَمْدَ والنِّعْمَةَ لكَ والمُلْك لا شريكَ لكَ)**

Mwanamume atasoma dua hiyo ya Talbiya kwa sauti ya juu. Ama mwanamke yeye atasoma Talbiya kwa kiwango atakachoweza kujisikizisha yeye mwenyewe tu. Hapa, Muislam atakuwa ameshaingia kwenye kuhirimia ikiwa ndiyo nguzo ya mwanzo katika nguzo za Umra.

**6)** Mwenye kuhirimia iwapo atahofia kukumbwa na kikwazo au kizuizi chochote kinachoweza kumzuia kukamilisha ibada yake, inajuzu kusema, baada ya Talbiya ya Umra, maneno haya:

(فإنْ حَبَسَني حابِسٌ فمَحِلِّي حيثُ حَبَسْتَنِي)

(kikinizuwa cha kunizuwia pahala pangu pa kutokea kwenye kuhirimia ni hapo uliponizuwia).

Iwapo jambo lolote liatamkwaza au kumzuiwa asiweze kukamilisha ibada itajuzu kwake kutoka kwenye kuhirimia, na hatakuwa na kosa lolote.

Inatakikana kwa mwenye kuhirimia kusoma sana dua ya Talbiyah, wakati akiwa kwenye safari yake ya kuelekea Makka na atakatisha pale tu atakapoanza kufanya Tawafu.

**7)** Mwenye kuhirimia Umra atakapofika Makka ni suna kwake kuoga kabla ya kuingia Makka na kutawadha kwa ajili ya kutufu. Atakapoingia Msikiti Mtukufu atatanguliza mguu wake wa kulia, na kusema:

(بسم اللَّه، والصَّلاة والسَّلام على رسول اللَّه، اللَّهمَّ اغْفِر لي ذُنوبي، وافْتَح لي أبوابَ رَحْمَتِكَ، أَعوذُ باللَّه العَظيم، وبِوَجْهِهِ الكَريم، وبِسُلْطانِهِ القَديم، مِنَ الشَّيْطان الرَّجيم).

**8)** Baada ya hapo, mwenye kuhirimia Umra ataelekea kwenye Jiwe Jeusi. Atalishika kwa mkono wake wa kulia na kulibusu. Ikiwa haitakuwa rahisi kwake kulibusu atalishika na kubusu mkono wake. Ikiwa hakuweza kulishika atalielekea jiwe hilo na kuliashiria kwa mkono wake, huku akisema: (بسم اللَّه، واللَّه أكبر)

Halafu ataiweka Alkaabah na Jiwe Jeusi upande wake wa kushoto ili aanze kuizunguka Alkaaba mizunguko saba ya Tawafu akianzia kwenye Jiwe Jeusi.

Tawafu hii ndio nguzo ya pili katika nguzo za Umra. Atauanza mzunguko wa Tawafu kwenye Jiwe Jeusi, na kumalizia kwenye Jiwe Jeusi. Atafanya hivyo mara saba.

**9)** Ni suna kwa mwanaume mwenye kufanya Umra kuvaa Ihramu kwa mtindo wa rubega anapoanza kutufu. Rubega ni kuliacha wazi bega lake la kulia na kuiweka sehemu ya katikati ya nguo yake ya kujitanda chini ya kwapa lake la kulia, na ncha zake mbili ataziweka juu ya bega lake la kushoto. Akimaliza kutufu mara saba atairejesha nguo yake ya kujitanda kwenye hali yake kabla ya kuvaa rubega.

**10)** Ni suna kwa mwanaume mwenye kufanya Umra kwenda mwendo wa haraka haraka pamoja na hatua za karibu karibu katika mizunguko yake mitatu ya mwanzo katika kutufu. Katika mizunguko yake iliyobaki atatembea mwendo wake wa kawaida.

**11)** Inapasa kwa mwenye kufanya Umra kujiepusha kutufu ndani ya Hijri. Hijri ni jengo lenye umbo la upinde lililojengwa mbele ya Alkaaba, kwa sababu jingo hilo ni sehemu ya Alkaaba. Yeyote atakayepita baina ya jingo hilo na baina ya Alkaaba atakuwa hajatufu kuizunguka Alkaaba.

**12)** Mwenye kufanya Umra akifika kwenye Kona ya Yamani (Ruknu Yamani) katika kutufu, ni suna kwake kuishika na kuibusu. Kona ya Yamani ni kona iliopo kabla ya Jiwe Jeusi. Ikiwa hakuweza kuishika kwa sababu ya msongamano, ataipita bila ya kuibusu wala kuiashiria.

**13)** Mwenye kufanya Umra anapokuwa kwenye sehemu iliopo baina ya Kona ya Yamani na Jiwe Jeusi katika kutufu atasema:

﴿رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِى ٱلْءَاخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ﴾ البقرة: ٢٠١.

***"Mola wetu Mlezi, tupe duniani mema, na Akhera mema, na utulinde na adhabu ya Moto".*** Sura Albaqarah: 201.

**14)** Akifika kwenye Jiwe Jeusi atalishika na kulibusu, kwa kadiri itakavyomuwia wepesi kufanya hivyo, na kusema: (بسم اللَّه، واللَّه أكبر). Halafu ataanza mzunguko wa pili na kufanya kama alivyofanya kwenye mzunguko wa kwanza, mpaka atakapomaliza mizunguko yote saba.

**15)** Mwenye kufanya Umra anapokuwa kwenye kutufu kwake anaweza kumtaja Allah Mtukufu na kumuomba, kusoma Qur'ani na aepuke mazungumzo ya kipuuzi na kuzungumza mambo ya kidunia.

**16)** Ni wajibu kwa mwenye kufanya Umra kufuatisha baina ya mizunguko yake na asitenganishe baina yake kwa chochote kile. Ikiwa atatenganisha na mtengano ukawa mkubwa, usiokuwa wa sala, basi atawajibika kurejea kutufu upya.

Ni juu ya mwenye kufanya Umra kulinda Udhu wake wakati wa kutufu. Iwapo Udhu utatenguka atawajibika kutia Udhu upya. Ikiwa muda aliouhitaji kwa ajili ya Udhu ni mfupi atakamilisha Tawafu yake kutokea pale alipofikia.

**17)** Mwanamke mwenye Hedhi na mwenye Nifasi watajiepusha kutufu Alkaaba, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) kwa bibi Aisha, Allah amuwiye radhi, pale alipopata Hedhi kwamba: ***"Fanya kama anavyofanya mwenye kuhiji isipokuwa tu usitufu Alkaaba mpaka utakapotoharika".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Wawili hawa wanatakiwa kuahirisha Tawafu mpaka watakapotoharika.

**18)** Mwenye kufanya Umra akimaliza mizunguko yake saba ataelekea kwenye Maqaam Ibrahim. Hili ni jengo lililopo mbele ya Alkaaba. Atasoma kauli yake Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿وَٱتَّخِذُواْ مِن مَّقَامِ إِبْرَٰهِـۧمَ مُصَلًّى﴾ البقرة: ١٢٥.

***"Na alipo kuwa akisimama Ibrahim pafanyeni pawe pa kusalia".*** Sura Albaqarah: 125.

Atasali rakaa mbili nyuma ya Maqaam Ibrahim ikiwa wepesi kwake kufanya hivyo. Ikishindikana atasali rakaa hizo mahali popote ndani ya Haram. Katika rakaa ya kwanza baada ya sura Alfaatiha atasoma: ﴿قُلْ يَـٰٓأَيُّهَا ٱلْكَـٰفِرُونَ﴾ yote, na kwenye rakaa ya pili baada ya sura Alfaatiha atasoma:﴿قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ﴾ yote.

**19)** Akimaliza kusali atarejea kwenye Jiwe Jeusi ili alishike ikiwa itakuwa wepesi kwake.

**20)** Baada ya hapo, mwenye kufanya Umra atatoka kwa ajili ya kwenda kwenye sehemu ya kussayi (kutembea) ili atembee baina ya Swafa na Marwa mara saba. Hii ni nguzo ya tatu katika nguzo za Umra. Ataanza kutembea kuanzia Swafa. Akiikaribia Swafa atasoma:

﴿ إِنَّ ٱلصَّفَا وَٱلۡمَرۡوَةَ مِن شَعَآئِرِ ٱللَّهِۖ فَمَنۡ حَجَّ ٱلۡبَيۡتَ أَوِ ٱعۡتَمَرَ فَلَا جُنَاحَ عَلَيۡهِ أَن يَطَّوَّفَ بِهِمَاۚ وَمَن تَطَوَّعَ خَيۡرٗا فَإِنَّ ٱللَّهَ شَاكِرٌ عَلِيمٌ ﴾ البقرة: ١٥٨.

***"Hakika vilima vya Safaa na Marwa ni katika alama za Mwenyezi Mungu. Basi anaye hiji kwenye Nyumba hiyo au akafanya Umra, si kosa kwake kuvizunguka. Na anaye jitendea mwenyewe kheri basi bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye shukrani na Mjuzi".*** Sura Albaqarah: 158.

Halafu atapanda kilima cha Swafa, ataelekea Kibla, atanyoosha mikono yake na kusema:

**(لا إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الحَمْدُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيءٍ قَدِيرٌ، لا إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ، أَنْجَزَ وَعْدَهُ، وَنَصَرَ عَبْدَهُ، وَهَزَمَ الأَحْزَابَ وَحْدَهُ).**

Atakariri uradi huu mara tatu, na anaweza kuomba anachokitaka.

**21)** Baada ya kumaliza kuomba dua, atateremka kwenye kilima cha Swafa akielekea Marwa, akitembea kwa miguu. Akifika kwenye alama mbili mistari miwili ya kijani atakwenda mwendo wa matiti (mwendo wa mbiombio) kulingana na uwezo wake. Mwanamke hatatembea mwendo wa matiti. Akifika kwenye alama ya pili atarejea mwendo wake wa kawaida mpaka afike Marwa. Akiwa kwenye Saayi atakuwa akiomba dua, akimdhukuru Allah Mtukufu na kusoma Qur'ani.

**22)** Mwenye kufanya Umra akifika kilima cha Marwa, atakipanda, ataelekea Kibla, atatoa Takbira, atanyanyua mikono miwili kwa kuomba dua na kusema yale aliyokuwa akiyasema kwenye Swafa. Kwa kufanya hivi, atakuwa amekamilisha mzunguko wake wa kwanza.

**23)** Halafu baada ya hapo atateremka kilima cha Marwa akienda Swafa. Atatembea kawaida sehemu ya kutembea, atatembea matiti

akifika kwenye sehemu ya alama mbili za kijani mpaka afike Swafa. Kwa kufanya hivyo atakuwa ameshamaliza mzunguko wake wa pili. Atafanya kama alivyofanya kwenye mzunguko wa mwanzo. Atafanya namna hii mpaka atakapokamilisha mizunguko saba; akianzia Swafa na kumalizia Marwa kiasi kwamba, kutembea kwake kutoka Swafa kwenda Marwa ni mzunguko mmoja na kurejea kwake kuelekea Swafa ni mzunguko mwingine.

**24)** Baada ya kumaliza mara saba za kutembea baina ya Swafa na Marwa, mwenye kufanya Umra atanyoa kichwa chake. Akiwa ni mwanaume, atanyoa nywele zake zote au atapunguza kwa kukata nywele kwenye sehemu zote za kichwa. Mwanamke atapunguza nywele zake tu kwa kukata kwenye ncha ya nywele zake kiasi cha ncha ya kidole (sentimita 2). Kunyoa nywele zote ni bora zaidi kwa mwanaume kuliko kupunguza, kwa sababu Mtume (s.a.w.) aliwaombea dua njema wanalionyoa nywele zote mara tatu na waliopunguza aliwaombea mara moja tu. Iwapo wakati wa Hija upo karibu na Umra yake hii ni kwa ajili ya Hija, inapendekezwa kwake kupunguza nywele ili aweze kunyoa wakati wa Hija.

**25)** Baada ya kunyoa au kupunguza nywele, mwenye kufanya Umra atakuwa ameshakamilisha ibada ya Umra na amali zake. Atavua nguo za Ihramu na kuvaa nguo zake zilizoshonwa, anaweza kujitia manukato na kufanya kila kilichokuwa kikikatazwa wakati akiwa kwenye Ihramu, kama vile manukato, kukutana na mke au mume wake kimwili na kuondoa nywele na kucha.

## NAMNA YA KUHIJI

### KWANZA: Aina za Hija

Kuna njia tatu za kutekeleza Hija, na kila njia inaitwa **Nusuki**[1]**.** Njia hizo ni hizi zifuatazo:

**a. Ifradi.** Ifradi ni Mwenye kutaka kuhiji kunuwia Hija tu, kwa kusema: **(لبَّيكَ حَجّاً)**. Nusuki hii haitanguliwi na utekelezaji wa Umra kabla yake, na pia mwenye kuinuwia halazimiki kuchinja mnyama mwisho wa Hija yake.

**b. Kirani.** Kirani ni Mwenye kutaka kuhiji kunuia kuchanganya Hija na Umra kwa pamoja kwa nia moja, kwa kusema kwenye kuhirimia kwake kwamba: (لبيك حَجّاً وعُمْرة).

Kwa maana hiyo, atatenda ibada za Umra kama ilivyotangulia kubainishwa, ila tu hatokata chochote katika nywele zake wala kutoka kwenye Ihramu yake. Atabakia kwenye kuhirimia kwake mpaka atakapomaliza kikamilifu matendo ya Hija. Mwisho wake atalazimika kuchinja mnyama.

**c. Tamatui.** Tamatui ni Alhaji kunuwia Umra katika miezi ya Hija, halafu atoke kikamilifu kwenye kuhirimia kwake, na baade ahirimie Hija siku ya tarehe nane ya mwezi wa Mfungotatu, kwa sharti kwamba asitoke nje ya Makka na kurejea kwao. Akifanya hivyo, Tamatui yake itabatilika na kulazimika kufanya Umra nyingine.

Nusuki bora zaidi kati ya hizi ni Tamatui, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa**: *“Lau kama ningejua, nisingechunga mnyama wa kuchinja, na ningetoka kwenye Ihramu pamoja na watu (wengine) pale walipotoka kwenye Ihramu”.*** Hadithi hii

---

(1) Nusuki ni njia ambayo Alhaji anatekelezea vitendo vya Hija kwa kutumia njia hiyo.

imepokewa na Bukhari na Muslim.

## PILI: Matendo ya Hija katika siku ya mwezi nane ya Dhulhija (Siku ya Tarwiya)

**1)** Alhaji akishamaliza kufanya Umra yake na kuingia kwenye siku ya mwezi nane wa Dhulhija (Mfungotatu), ikiwa alinuwia Kirani atakuwa amebaki kwenye Ihramu yake baada ya kutekeleza Umra na hatajivua kwenye Ihramu. Ikiwa alinuia kufanya Tamatui atahirimia hapo hapo pahala alipo baada ya kuoga, kuondoa nywele zake za sehemu za siri na za kwapa, kujitia manukato, kuvaa mavazi ya Ihramu na kuesma kuwa: (لبَّيك حَجّاً)

Ikiwa atahofia kukumbwa na pingamizi au kikwazo chohote kile kitakachoweza kumfanya asiweze kukamilisha Hija yake, anatakiwa kuweka sharti kwa kusema kwamba:

(وَإِنْ حبسنِي حابِسٌ فَمَحلِّي حَيْثُ حَبَستَنِي).

***"Na iwapo kitanizuiwa chochote cha kunizuia, kutoka kwangu kwenye Ihramu ni hapohapo uliponizuia".***

Ama aliyenuia Ifradi, atahirimia Hija kwenye Mikati kwa sababu yeye hana Umra.

**2)** Alhaji baada ya kuhirimia kwake atakwenda Mina wakati wa Dhuha (Asubuhi). Huko atasali sala ya Adhuhuri, Alasiri, Magharibi na Isha kila sala kwa wakati wake. Sala za rakaa nne atazisali kwa kupunguza na kusali rakaa mbili mbili.

**3)** Mwenye kuhiji atalala hapo Mina mpaka alfajiri ya siku ya Arafa. Inamtosha kupitisha sehemu kubwa tu ya usiku hapo Mina.

## TATU: Matendo ya Hija katika siku ya tisa ya Dhulhija (Siku ya Arafa)

**1)** Jua litakapochomoza siku ya mwezi tisa, ambayo ndiyo siku ya Arafa, Alhaji ataondoka Mina kuelekea Arafa. Atafikia Namirah na kubaki hapo mpaka wakati wa zawali, iwapo hilo litakuwa jepesi kwake.

Alhaji kuwepo Arafa ni nguzo ya pili katika nguzo za Hija baada ya kuhirimia, na ndio nguzo kubwa kwenye Hija, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Hija ni Arafa, na atakayekuja kabla ya sala ya Alfajiri kwenye usiku wa –mkusanyiko (Muzdalifa) Hija yake imetimia".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Tirmidhiy, Nasai na Ibnimaja.

**2)** Baada ya jua kuhama kutoka usawa wa kati, mwenye kuhiji atasali Adhuhuri na Alasiri kwa pamoja kwa kupunguza na kwa kutanguliza sala ya Alasiri na kuisali pamoja na Adhuhuri kwa Adhana moja na Iqama mbili.

**3)** Baada ya kumaliza kusali, mwenye kuhiji ataingia Arafa na kubaki hapo mpaka jua litakapozama huku akisali, akimtaja Allah, akimnyenyekea kwa kumuomba, akinyanyua sauti yake, akielekea Kibla na kusoma sana uradi huu:

**(لا إِلَهَ إِلاَّ اللَّهُ وَحْدَهُ لا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ المُلْكُ وَلَهُ الحَمْدُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيءٍ قَدِيرٌ)**

Inajuzu kwa mwenye kuhiji kupumzika kwa kulala, kuzungumza na wenzake mazungumzo yenye manufaa au kusoma vitabu vyenye faida.

**4)** Jua likishazama siku ya mwezi tisa, mwenye kuhiji ataelekea Muzdalifa(1). Akifika atasali Magharibi na Isha kwa kukusanya na kupunguza; kwa Adhana moja na Iqama mbili. Anatakiwa asisali Magharibi na Isha mpaka afike Muzdalifa, ila ikiwa atachelea kutoka kwa wakati wa sala ya Isha kabla ya kufika, kwa sababu ya msongamano.

Mwenye kuhiji hatakiwi kujishughulisha na kuokota vijiwe mara tu baada ya kufika Muzdalifa kabla ya kusali, bali analazimika kwanza kujishughulisha na kusali. Anaruhusiwa kuokota vijiwe mahali popote pale.

**5)** Mwenye kuhiji atakuwepo usiku Muzdalifa na kubaki hapo mpaka Alfajiri. Kwa kuwepo Muzdalifa usiku sio lazima kulala, bali

---

(1) Muzdalifa: Ni eneo lililopo kwenye njia baina ya Arafa na Mina kusini mashariki ya Mina na huitwa (Almash-ar Alharaam).

kunapatika kwa kubaki kwake Muzdalifa usiku. Inajuzu kwa wenye nyudhuru kuondoka Muzdalifa baada ya nusu ya usiku, kama vile wazee na wagonjwa wasioweza kuhimili msongamano. Pia inajuzu kuondoka na wanaofuatana nao. Ama kwa asiyekuwa na udhuru atabaki mpaka alfajiri.

### NNE: Matendo ya Hija katika siku ya kumi (Siku ya Kuchinja):

**1)** Mwenye kuhiji akimaliza kusali alfajiri siku ya mwezi kumi, ataelekea Mash-ari Haraam (Msikiti wa Muzdalifa). Hapo atamuomba Allah na kutoa Takbira mpaka kutakapo pambazuka. Kupamabazuka ni kuisha kwa hali ya giza na kuwa kweupe kabla ya kuchomoza kwa jua. Ikiwa haikuwa wepesi kwake kwenda Mash-ari Haraam atamuomba Allah, kumdhukuru na kutoa Takbira hapo hapo alipo.

**2)** Kukisha pambazuka vizuri, mwenye kuhiji ataanza kwenda Mina kabla ya kuchomoza kwa jua. Afikapo kwenye bonde la Muhassir lililopo baina ya Muzadalifa na Mina, atatembea mwendo wa haraka haraka, kwa sababu bonde hili ndio mahali ambapo Allah alimuangamiza Abraha na jeshi lake pale walipotaka kuivunja Alkaaba.

Mwenye kuhiji anaruhusiwa kuokota vijiwe mahali popote pale.

**3)** Mwenye kuhiji akifika Mina, atakwenda kwenye Jamrat Aqabah (Mnara wa kutupia mawe wa Akaba). Huu ni mnara wa mwisho kuelekea Makka. Atautupia mnara huu vijiwe saba vyenye ukubwa wa mfano wa harage. Atautupia kwa mfululizo, kijiwe kimoja baada ya kingine, huku akitoa Takbira pamoja na urushaji wa kila kijiwe.

**4)** Mwenye kuhiji akimaliza kurushia vijiwe Jamrat Aqabah atachinja kichinjo chake, ikiwa yeye ni mwenye kufanya Tamatui au Kirani. Ama anayefanya Ifradi, yeye hatakuwa na kichinjo chochote. Jambo bora zaidi ni mtu kuchinja mnyama yeye mwenyewe. Ikiwa hakuweza inajuzu kwake kumuwakilisha mtu mwengine amchinjie.

**5)** Baada ya kuchinja kichinjo chake, mwenye kuhiji akiwa ni mwanaume atanyoa nywele zote za kichwa chake au kuzipunguza. Kunyoa ni bora zaidi. Ama mwanamke, atapunguza nywele zake kwa kiwango cha ukucha (kama ilvyotangulia kuelezwa kwenye Umra).

**6)** Inajuzu kwa mwenye kuhiji kutanguliza au kuahirisha matendo ya siku ya kumi na asiwe na kosa lolote. Kama atatanguliza kuchinja kabla ya kurushia viviwe Jamarati inafaa, au kama atatanguliza kurushia viviwe Jamarati kabla ya kuchinja pia itafaa na kadhalika.

**7)** Mwenye kuhiji (Alhaji) akishafanya matendo mawili katika yale matendo ya Hija ya siku ya mwezi kumi, atakuwa ameshatoka kwenye Ihramu Utokaji Mdogo[1]. Kwa sababu hiyo, itakuwa halali kwake kufanya yale yote aliyokuwa amezuiwa kuyafanya baada ya kuhirimia, isipokuwa tu maingiliano ya kimwili ya mume na mkewe au mke na mumewe.

**8)** Baada ya kumaliza kufanya matendo ya Hija pale Mina, Alhaji ataelekea Makka kwa ajili ya kutufu Tawafu Ifadha. Tawafu hii ni nguzo ya tatu katika nguzo za Hija. Atatufu Alkaaba mara saba. Halafu atafanya Saayi kwa kutembea baina ya Swafa na Marwa ikiwa yeye ni mwenye kufanya Tamatui, na pia kama bado alikuwa hajafanya Saayi baina ya Swafa na Marwa alipotufu Tawafu Quduum (Tawafu ya kuingia Makka). Kwa kufanya hivyo, Alhaji atakuwa ametoka kwenye Ihramu Utokaji Mkubwa. Kwa maana hiyo, itakuwa halali kwake kufanya kila kitu kilichokuwa haramu kwa sababu ya Ihramu, hata maingiliano ya kimwili baina ya mume na mkewe au mke na mumewe.

**9)** Baada ya Tawafu Ifadha na kufanya Saayi, mwenye kuhiji atarejea Mina ili abaki hapo kwa kuwepo siku tatu za Tashrik[2] na kurushia vijiwe Jamarati zote tatu.

## TANO: Matendo ya Hija katika siku za Tashriki

Siku za Tashriki ni siku tatu baada ya siku ya kuchinja; siku ya mwezi kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu za mwezi wa

---

(1) Tahallul ndogo ni kwa Mweneykuhiji kuruhusiwa kufanya yale yote aliyokuwa akizuwiwa kufanya baada ya kuhirimia, kkama vile kuvaa nguo zilizoshonwa, kukata kucha, kukata nywele, kujitia manukato ila tu bado anaharamishiwa kukutana na mkewe au mumewe kimwili au kuchezeana naye.

(2) Ayyami –siku za–Tashriiq ni siku ya mwezi kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu za mwezi wa Dhul Hijah ,nazo zimeitwa hivyo kwasababu walikuwa wakiani ka nyamma za dhahaya kwa kuziweka juani ili kuzikausha.

Dhulhija (Mfungotatu). Hizi ni siku za kula na kunywa ambazo haifai kufungwa, ila tu kwa mweneye kuhiji ambaye alikuwa na wajibu kuchinja na hakuweza kuchinja. Kwa ufupi, matendo ya siku za Tashriki ni kama ifuatavyo:

**1)** Baada ya Alhaji kuwepo usiku wa mwezi kumi na moja Mina, atabaki hapo mpaka wakati wa Zawali (wakati wa Adhuhuri). Baada ya zawali, atakwenda kwenye Jamarati tatu. Atairushia vijiwe Jamrat Ndogo ambayo iko karibu na Majid Khaif vijiwe saba mfulululizo; kimoja baada ya kingine, na kutoa Takbira wakati wa kurusha kila kijiwe. Atakwenda mbele kidogo upande wa kulia na kuomba dua ndefu anayoitaka ikiwa itakuwa wepesi kwake.

**2)** Halafu ataelekea moja kwa moja kwenye Jamrat ya Kati na kuirushia vijiwe saba kwa mfulululizo akitoa Takbira wakati wa kurusha kila kijiwe. Halafu atasogea kidogo upande wa kushoto na kuelekea Kibla na kuomba dua ndefu ikiwa wepesi kwake.

**3)** Mwenye kuhiji atakuwepo Mina usiku wa mwezi kumi na mbili. Ifikapo adhuhuri katika siku ya mwezi kumi na mbili Dhulhija, atafanya kama alivyofanya mwezi kumi na moja; atarushia vijiwe Jamarati tatu. Kama ana haraka, ataondoka Mina kabla ya kuzama kwa jua, na ataelekea Makka kwa ajili ya Tawafu Wadai (Tawafu ya Kuaga kwa ajili ya kuondoka Makka). Kama magharibi itamkuta akiwa bado yuko Mina bila ya udhuru wowote, atawajibika kubaki Mina mpaka mwezi kumi na tatu, ambayo ndiyo siku ya mwisho wa Siku za Tashriki, na kwa sababu hiyo, atazirushia vijiwe Jamarati tatu kama alivyofanya siku mbili kabla yake.

**4)** Baada ya kurushia vijiwe Jamarati katika siku za Tashriki na iwapo atataka kuondoka Makka, ni wajibu kwake kwenda Makka ili akatufu Tawafu Wadai (Tawafu ya Kuaga) mizunguko saba. Baada ya kufanya hayo, atasali rakaa mili na baada ya hapo ataondoka Makka. Hatakiwi kuchelewa kuondoka kwa sababu ya kutembea madukani, kufanya biashara au kufanya ziara, vinginevyo atalazimika kufanya Tawafu Wadai upya. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***“Kamwe mmoja wenu yeyote asiondoke (Makka) mpaka wakati wake wa mwisho uwe ni kukutana na Nyumba***

***(Tukufu)”.*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Kama akichelewa kuondoka kwa sababu ya msongamano au kungojea wenzake au kujitafutia mahitaji ya njiani kwa ajili ya safari yake, hatakuwa na makosa na hatalazimika kufanya Tawafu nyengine (ya kuaga).

Iwapo mwanamke amepatwa na Hedhi au Nifasi kabla ya kuondoka, na ikawa haiwezekani kwa msafara wake kumngojea, itajuzu kwake kuondoka kabla ya kutufu Tawafu Wadai.

***Kwa kufanya hayo, mwenye kuhiji atakuwa ameshamaliza ibada ya Hija.***

## SITA: Mambo yaliyokatazwa kwa kuhirimia

Haya ni mambo ambayo haijuzu kwa mwenye kufanya Hija au Umra kuyatenda wakati akiwa katika Ihramu. Kuyatenda mambo hayo kunasababisha kutoa fidia(1), na mengine yanaharibu Hija yenyewe. Mambo hayo yaliyokatazwa ni haya yafuatayo:

**1) Kuondoa nywele** kwa njia yoyote ile; iwe kwa kunyoa au kunyonyoa. Pia ni sawa iwe yeye mwenyewe ndiye aliyeondoa nywele hizo au mtu mwengine ndiye aliyeziondoa. Aidha ni sawa nywele zilizo ondolewa ziwe nyingi au kidogo. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿وَلَا تَحۡلِقُواْ رُءُوسَكُمۡ حَتَّىٰ يَبۡلُغَ ٱلۡهَدۡيُ مَحِلَّهُۥ﴾ البقرة: ١٩٦.

***“Na msinyoe vichwa vyenu mpaka mnyama wa kuchinja afike kwenye mahala pake”.*** Sura Albaqara:196.

Zinaingia katika hukumu hii nywele zote za mwili.

❖ Aliyenyoa kichwa chake bila ya udhuru wowote atakuwa na makosa na atalazimika kutoa fidia. Ama mwenye kunyoa kichwa

(1) Ni kile kinachotolewa na mwenye kufanya Hija miongoni mwa chakula au kichinjo, kwa sababu ya kutenda kitu kilichoharamishwa kwenye Hija, nayo hutofautiana kutokana na aina ya kosa lenyewe.

chake kwa udhuru, kama vile maradhi au kero, hatakuwa na makosa, isipokuwa tu atawajibika kutoa fidia, ambayo ni kufunga siku tatu au kuwapa chakula masikini sita au kuchinja mbuzi au kondoo. Atachagua kufanya mojawapo kati ya haya mambo matatu.

❖ Inajuzu kwa mwenye kuhirimia kukuna nywele zake, kuzichana na kuziosha, hata kama hilo litasababisha nywele zake kidogo kudondoka, ila tu inampasa afanye hivyo kwa upole.

**2) Kukata kucha.** Haijuzu kwa mwenye kuhiji kukata kucha baada ya kuhirimia Hija au Umra. Ni suna kukata kucha kabla ya kuhirimia. Ama baada ya kuhirimia inakuwa haramu kufanya hivyo, kwa mujibu wa makubaliano ya maulamaa wote, kwa sababu kufanya hivyo ni miongoni mwa aina fulani za kujiburudisha jambo ambalo ni kinyume na malengo ya kuhirimia. Allah Mtukufu amesema kuwa**:**

﴿ثُمَّ لْيَقْضُوا۟ تَفَثَهُمْ﴾ الحج: ٢٩.

***"Kisha waondoshe taka zao".*** Sura Alhajj :29.

Amesema Ibniabbas, Allah amuwiye radhi yeye na mzazi wake, kwamba: *"**Taka ni kutoka kwenye Ihramu, kunyoa kichwa, kuvaa nguo na kukata kucha".***

**3) Kufinika kichwa** kwa kukigandanisha na kitu. Haijuzu kwa mwenye kuhirimia akiwa mwanaume kufinika kichwa chake kwa kitu kitakachokamatana na kichwa. Ni sawa iwe kofia, shali, kilemba au kuweka mtandio wake juu ya kichwa chake na mfano wa hayo yanayohesabika kuwa ni kufinika kichwa. Ama atakapoweka kitu juu ya kichwa akiwa hakusudii kufunika kichwa, kama kubeba mzigo, begi au mwavuli hatakuwa na kosa.

Katika yanayoruhusiwa kwa mwenye kuhiji ni kujifunika kwa paa la gari au hema. Haya hayahesabiwi kuwa ni katika yaliyokatazwa kwenye kuhirimia.

Haijuzu kwa mwanamke kufinika uso wake ila atakapohofia fitina. Hapo, atafinika uso wake lakini bila ya kutumia Barakoa (Nikabu).

**4) Kuvaa nguo zilizoshonwa.** Msingi katika kuhirimia ni kuvaa

Izari (Msuli) na Ridai (nguo ya kujitanda) na kujiepusha na nguo zilizoshonwa ambazo zimeshonwa kwa ajili ya kufunika kiungo husika, kama vile gauni, shati, suruali, kanzu, glavu, viatu vya buti, soksi n.k.

Ama makubadhi (sandali/sandals) pamoja na kuwa yameshonwa ila sio katika vitu vilivyokatazwa kwa sababu ya kushonwa. Sheria imeruhusu kuvaa makubadhi. Hata hivyo, haijuzu kuvaa makubadhi yanayofinika vifundo viwili vya miguu kama buti.

Kwa upande wa mwanamke, yeye anaruhusiwa kuvaa atakacho isipokuwa tu glavu, Barakoa au kitu kinachoonesha kiwiliwili.

**5) Manukato.** Haijuzu kwa mwenye kuhirimia kujitia manukato kwenye mwili wake au kwenye nguo zake za kuhirimia. Ama manukato ambayo ameyatia kwenye mwili wake kabla ya kuhirimia na athari yake ikabaki hayana ubaya. Ama ikiwa manukato yako kwenye nguo za kuhirimia atawajibika kuyaosha.

**6) Kuwinda.** Haijuzu kwa mwenye kuhirimia kuwinda mnyamapori yoyote anayeliwa, kama vile paa, sungura na ndege. Pia haijuzu kutoa msaada katika kumuwinda kwa kuashiria au kutoa taarifa za mahali walipo wanyamapori. Atakapowinda au kuwindiwa na mtu mwengine kwa ajili yake, haitajuzu kwake kula nyama hiyo, kwa sababu nyama hiyo kwake ni katika hukumu ya mzoga.

Iwapo mtu asiyekuwa mwenye kuhirimia atawinda na akawa hakukusudia kumuwindia mwenye kuhirimia, itajuzu kwa mwenye kuhirimia kula nyama hiyo.

Inajuzu kwa mwenye kuhirimia kuvua baharini na kula bila ya kizuizi chochote.

**7) Kuoa.** Haijuzu kwa mwenye kuhirimia kufunga ndoa wala mtu mwengine kumuolea kwa niaba yake, hata kama huyo mwenye kumuolea sio mwenye kuhirimia. Iwapo atafunga ndoa yeye mwenyewe au mtu mwengine kumuolea, akidi ya ndoa hiyo haitafungamana na itakuwa batili.

**8) Kukutana kimwili mume na mkewe.** Hili ni katazo kubwa sana,

kwa sababu mwenye kuhirimia akikutana na mkewe kimwili kabla hajafanya Utokaji Mdogo (Tahaluli ya Kwanza) Hija yake itabatilika. Ikiwa mkewe ni mwenye kuhirimia pia, naye Hija yake pia itaharibika, na watawajibika kukamilisha Hija yao na kutoa fidia ambayo ni kuchinja ngamia kwa kila mmoja wao na kugawa nyama yake kwa masikini wa Mji Mtukufu (wa Makka) na kurejea kuhiji kwenye mwaka unaokuja.

Ama ikiwa kukutana kimwili huko ni baada ya Tahaluli Ndogo na kabla ya Tahaluli Kubwa, Hija itaharibika na kuwalazimu kutoa fidia ambayo ni kuchinja mbuzi au kondoo na kugawa nyama yake kwa fukara wa Mji Mtukufu (wa Makka).

**9) Kuchezeana mke na mume kwa** kubusiana, kushikanashikana au kukumbatiana, kwa sababu hayo yote ni katika vitangulizi vya tendo la kujamiiana, na linaingia katika uchafu alioukataza Allah Mtukufu kwenye kauli yake isemayo kuwa:

﴿فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي ٱلۡحَجِّ﴾ البقرة: ١٩٧.

"***Kusiwe na uchafu wala majadiliano kwenye Hija".*** Sura Albaqara: 197.

# SHERIA MAALUMU KWA MWANAMKE WA KIISLAMU

## KWANZA: Sheria za Hedhi, Nifasi na Istihadha

### 1) Sheria za Hedhi:

**a. Maana ya Hedhi.** Hedhi ni damu inayotoka kwenye tumbo la uzazi la mwanamke anapofikia balehe, na halafu inakuwa kawaida yake katika nyakati maalumu.

**b. Wakati wake.** Hedhi huanza kuanzia mwanamke anapofikia umri wa miaka tisa ya mwezi muandamo. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Bibi Aisha, Allah amuwiye radhi, isemayo kwamba: ***"Binti akifika umri wa miaka tisa, basi huyo ni mwanamke".*** Hadithi hii imepokewa na Tirmidhiy na Bayhaqiy.

Kwa kawida Hedhi hukatika kwa mwanamke kufikia umri wa miaka hamsini, kwa mujibu wa kauli ya Bibi Aisha, Allah amuwiye radhi, isemayo kwamba: ***"Mwanamke anakapofika umri wa miaka hamsini hutoka kwenye mipaka ya (kupata) Hedhi".*** Hadithi hii imetajwa na Ahmad. Hedhi inaweza kuendelea baada ya umri wa miaka hamsini. Kwa hiyo, mwanamke kama ataona damu kwa namna yake ya kabla ya miaka hiyo hamsini, hiyo ni damu ya Hedhi.

**c. Muda wake.** Muda wa chini wa Hedhi ni siku moja, na wingi wake ni siku kumi na tano. Aamesema Atwaa, Allah amuwiyr radhi, kwamba: ***"Mimi nimewaona wenye kupata Hedhi siku moja, na mwenye kupata Hedhi siku kumi na tano".*** Aghalabu ya muda wa Hedhi nyingi ni siku sita au saba, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) alipomwambia Hamna Binti Jahshi kwamba***: "Jichukulie kuwa unapata Hedhi siku sita mpaka saba, kwenye elimu ya Allah na uoge…".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Abudaudi na Tirmidhiy.

**d. Mambo yanayoharamishwa kwa mwenye Hedhi.**

Yanaharamishwa mambo kadhaa kwa mwenye Hedhi. Miongoni mwa mambo hayo ni haya yafuatayo:

- **Kujamiiana (kwa mke na mumewe),** kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿فَٱعْتَزِلُوا۟ ٱلنِّسَآءَ فِى ٱلْمَحِيضِ وَلَا تَقْرَبُوهُنَّ حَتَّىٰ يَطْهُرْنَ﴾ البقرة: ٢٢٢.

***"Waepukeni wanawake (wakiwa) kwenye Hedhi na msiwasogelee mpaka watakapotoharika".*** Sura Albaqara:222.

- **Kumpa Talaka.** Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah kuwa*:*

﴿فَطَلِّقُوهُنَّ لِعِدَّتِهِنَّ﴾ الطلاق: ١

*"Na* ***wapeni alaka kwa (mujibu wa) hesabu zao (za Hedhi)".*** Sura Attalaaq:1.

- **Kusali.** Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Hedhi ikija, acha kusali".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

- **Kufunga saumu.** Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: **"Hivi si mmoja wenu anapopata Hedhi hafungi wala hasali? Kina mama Swahaba wakasema: Ndio".** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

- **Kutufu**. Hii inatokana na kauli ya Mtume (s.a.w.) kwa Bibi Aisha pale alipopata Hedhi kwamba: ***"Fanya kila anachokifanya mwenye kuhiji isipokuwa tu usitufu Nyumba Tukufu mpaka utakapotoharika".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

- **Kugusa Msahafu.** Hii inatokana na kauli ya Allah Mtukufu inayosema kwamba:

﴿لَّا يَمَسُّهُۥٓ إِلَّا ٱلْمُطَهَّرُونَ﴾ الواقعة: ٧٩

***"(Kitabu hicho cha Qur'ani) Hakiguswi ila na wenyekujitoharisha***

***tu”.*** Sura Alwaaqia: 79.

- **Kukaa msikitini.** Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***“Siuhalalishi msikiti kwa mwenye Janaba wala mwenye Hedhi*”.** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi. Ibnikhuzaima amesema kuwa ni sahihi. Wanazuoni wengine wamesema kuwa ni dhaifu.

**e. Mambo ambayo ni wajibu kwa sababu ya Hedhi.** Mwanamke anapopata Hedhi, hiyo ni alama kuwa amebalehe, na ni wajibu kwake kuoga damu itakapokatika. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: *“**Aacha kusali kwa** siku **kiasi cha siku ambazo ulikuwa ukipata Hedhi, halafu oga na sali.**”*. Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**f. Alama ya kutwaharika kwa mwanamke mwenye Hedhi.**

- Damu ya Hedhi ikikatika kiasi kwamba mwanamke akiweka pamba kwenye kipindi cha Hedhi haibadiliki, atakuwa tayari ametwaharika.

- Ikiwa ataona umanjano na weusi kwenye kipindi cha Hedhi, hiyo ni Hedhi., kwa mujibu wa nukuu ya Alqamah akimnukuu mama yake kwamba: *“**Wanawake walikuwa wakipeleka kwa Aisha chombo ndani yake mkiwa na pamba yenye maji maji ya umanjano. Aisha alikuwa akiwaambia kuwa: Msifanye haraka mpaka muone maji meupe”.*** Hadithi hii imepokewa na Malik, na Bukhari akaiweka kwenye Muallaqaat**.** Maji meupe ni maji meupe yanayokuja baada ya Hedhi ikiwa ni ishara ya kuwa mwanamke ametoharika Hedhi.

- Ama majimaji ya rangi ya manjano na ya kahawia katika kipindi cha Tohara ni Twahara na mwanamke hatakiwi kuizingatia kuwa ni Hadhi, kwa mijubu wa kauli ya Ummuatiyah, Allah amuwiye radhi, aliposema kuwa: ***“Tulikuwa hatuzingatii umanjano na ukahawia baada ya Tohara ni chochote (katika Hedhi)”.*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi na Bukhari bila ya neno (baada ya Tohara).

**g. Mamabo ambayo mwenye Hedhi anatakiwa kuyalipa ya baada ya kutoharika kwake:**

Mwenye Hedhi anatakiwa kulipa saumu baada ya kutwaharika, na hatakiwi kulipa sala. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Muadha, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, alipomuuliza Aisha, Allah amuwiye radhi, kwamba: ***"Inakuwaje, mwenye Hedhi analipa saumu na halipi sala? Aisha akasema: Ilikuwa ikitupata hali hiyo, wakati wa Mtume wa Allah, na tulikuwa tukiamrishwa kulipa saumu na hatukuwa tukiamrishwa kulipa sala".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Iwapo mwenye Hedhi atatoharika kabla ya kutua kwa jua, itamlazimu kusali Adhuhuri na Alasiri ya siku hiyo. Wakati wowote atakapotoharika kabla ya kuchomoza kwa alfajiri, itamlazimu kusali Magharibi na Isha ya usiku huo.

**2) Sheria za Mustahadha[1]:**

**a. Maana ya Istihadha.** Istihadha ni utokaji wa damu mfululizo katika wakati usiokuwa wa kawaida, kwa sababu ya ugonjwa na hitilafu katika mshipa uliopo katika sehemu ya chini ya mfuko wa uzazi. Mwanamke ambaye damu yake imevuka siku kumi na tano, huyo atakuwa na damu ya Istihadha, na kamwe damu hiyo haiwezi kuwa Hedhi.

**b. Hali za Mustahadha.** Mustahadha ana hali nyingi:

**Ya Mwanzo:** Ni kwamba Mustahadha anayo kawaida ya mpangilio kabla ya kupata Istihadha, akijua idadi ya siku zake na wakati wake katika mwezi. Huyu ataifanyia kazi kawaida hiyo, kwa maana kwamba ataacha kusali na kufunga katika zile siku za kawaida yake. Ni sawa ameweza kutofautisha kati ya damu hiyo na damu ya Hedhi au la. Siku zilizozidi siku za kawaida yake, itakuwa ni Istihadha. Hii ni kwa mujibu wa ujumla wa kauli ya Mtume (s.a.w.) alipomwambia Ummuhabiba, Allah amuwiye radhi, kwamba: ***"Kaa (usisali na usifunge) kiasi cha siku za Hedhi yako zilizokuwa zikukuzuwia (kusali na kufunga hapo awali) na (kisha) oga na sali".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

---

(1) Hali ya kuendelea na hedhi nayo ni maradhi.

**Ya pili**: Ni kwamba Mustahadha hakuwa na kawaida maalumu au alikuwa nayo lakini ameisahau. Ikiwa damu yake inataofautika kwa maana kwamba, baadhi yake ni nyeusi, nzito na inatoa harufu mbaya na nyingine ni nyepesi na nyekundu, na hiyo nyeusi ikawa haizidi wingi wa Hedhi (ambao ni siku kumi na tano), na haipungui uchache wake (ambao ni siku moja), Mustahadha huyo atakuwa ni mpambanuzi (anao uwezo wa kutofautisha) na kwa maana hiyo, ataacha kusali kipindi cha Hedhi yake nyeusi, na kisha ataoga na kusali. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Fatma Binti Kaisi, Allah amuwiye radhi, aliponukuliwa akisema kuwa: ***"Nilimuuliza Mtume (s.a.w.) kuwa: Ewe Mtume wa Allah, Mimi napata Hedhi mfululizo na sitohariki. Je, niache kusali? Mtume akasema: Hapana! Hakika, huo ni mshipa na sio Hedhi. Kwa hiyo, ikija Hedhi, acha kusali. Hedhi ikiondoka, jioshe damu na sali".*** Hadithi hii imepokewa Bukhari na Muslim. Na katika matamshi mengine ya Hadithi hiyo imenukuliwa kwamba, Mtume (s.a.w.) alisema kuwa: ***"Kama damu ni ya Hedhi ni nyeusi inayotoa harufu mbaya. Basi (kama iko hivyo) acha kusali. Kama damu hiyo ni nyingine (ambayo sio nyeusi na haitoi harufu mbaya) tawadha, kwa sababu huo ni mshipa tu".*** Hadithi hii imepokewa na Nasai.

**Ya tatu:** Ni kwamba Mustahadha hana kawaida maalumu na hawezi kutofautisha na amekwazika. Huyu, atakaa siku sita au saba katika kila mwezi atakazokuwa akizipitiliza. Halafu ataoga, atasali na kufunga, baada ya kuosha pahali pa damu na kuweka kitu kinachozuwia kuchuruzika kwa damu. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) alipomwambia Hamnah Binti Jahshi kuwa: ***"Hakika hilo ni shambulizi miongoni mwa mashambulizi ya shetani. Chukulia kuwa ni Hedhi siku sita mpaka saba, na Allah ndiye ajuae. Halafu oga".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Abudaudi na Tirmidhy.

**c. Sheria za Mustahadha.** Mustahadha ana sheria kadhaa zinazomhusu. Muhimu zaidi ya sheria hizi ni kwamba, ni wajibu kwake kutawadha kila wakati wa sala unapofika. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Fatma Binti Abihubaish ambayo ndani yake kuna maneno ya Mtume (s.a.w.) yasemayo kuwa: ***"Halafu tawadha kwa***

***kila sala".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

**3) Sheria za Nifasi.**

**a. Maana ya Nifasi.** Nifasi ni damu inayotoka kwenye uke wa mwanamke kwa sababu ya kujifungua.

**b. Muda wake.** Hakuna ukomo wa uchache wa Nifasi. Ama urefu wa muda wake ni siku arubaini. Ikizidi hapo, sio damu ya Nifasi na itakuwa Istihadha. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Ummusalamah, Allah amuwiye radhi, aliyenukuliwa akisema kuwa: *"**Mwanamke mwenye Nifasi wakati wa Mtume (s.a.w.) alikuwa akikaa siku arubaini".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Abudaudi, Tirmidhiy na Ibnimaja.

**c.** Y**anayoharamishwa kwa sababu ya Nifasi.** Yanakuwa haramu kwa sababu ya Nifasi yale mambo yote ambayo ni haramu kwa sababu ya Hedhi. Sheria za mwanamke mwenye Nifasi ni sawa na sheria za mwanamke mwenye Hedhi.

## PILI: Hijabu ya mwanamke na mavazi yake.

Miongoni mwa mafundisho makubwa na muhimu ambayo Allah amemuamrisha mwanamke ni Hijabu (stara) ambayo Allah ameifanya ni nembo ya hadhi yake, anuani ya usafi wake na kielelezo cha wema wake. Kwa sababu hii, imekuwa muhimu kwa wanawake kujua sheria na taratibu zianazohusiana na Hijabu.

**1) Maana ya Hijabu:**

**Hijabu katika Sheria** ni nguo pana, isiyobana, yenye kusitiri mwili wote wa mwanamke, isiyo onesha ngozi yake, isiyo ainisha sehemu zake za kuvutia na isiyo acha wazi sehemu yoyote ya mwili wake.

Kwa hiyo, mwanamke mwenye kuvaa Hijabu ni yule aliyesitiri mwili wake na kuficha sehemu zake za kufitinisha (kuvutia) isipokuwa tu zile sehemu ambazo Allah ameruhusu kudhihirishwa na ambazo ni uso na viganja, ikiwa patakuwa na salama, kama walivyosema hivyo

wanazuoni wengi, Allah awarehemu. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا﴾ النور: ٣١.

***"Na wasidhihirishe mapambo yao ila tu yaliyodhihiri katika hayo".*** Sura Annuur: 31. Imenukuliwa kwa Abdallah Bin Omar, Allah amuwiye radhi yeye na mzazi wake, akisema kuwa: ***"Mapambo yaliyodhihiri ni uso na viganja viwili".*** Hadithi hii imepokewa na Bayhaqiy.

Jambo bora zaidi ni kwa mwanamke kusitiri uso wake, kwa mujibu wa kauli ya Mtume wa Allah isemayo kuwa: ***"Mwanamke mwenyekuhirimia havai Nikabu wala havai glavu".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari. Kwa maana hii, mwanamke asiyekuwa mwenye kuhirimia ni sheria kwake kuvaa Nikabu na kuficha uso.

**2) Hukumu ya Hijabu.**

Hijabu ni wajibu kwa mwanamke Muislamu aliye fikia umri wa balehe. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿يَا أَيُّهَا النَّبِيُّ قُل لِّأَزْوَاجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَاءِ الْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِن جَلَابِيبِهِنَّ ذَٰلِكَ أَدْنَىٰ أَن يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَيْنَ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا﴾ الأحزاب: ٥٩.

***"Ewe Mtume, waambie wake zako na mabinti zako na wake wa Waislamu kwamba, wajigubike nguo zao. Kufanya hivyo ni kujiweka karibu zaidi katika kujulikana na hivyo wasiudhiwe, na Allah ni mwingi wa kusamehe, mwenye kurehemu".*** Sura Al-ahzaab: 59.

Amesema Ummusalama, Allah amuwiye radhi, kuwa: ***"Ilipoteremka aya hii "wajigubike nguo zao", wanawake walitoka kama kwamba kuna kunguru juu ya vichwa vyao, na juu yao wakiwa wanavaa nguo nyeusi".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi na Ibni Abihatim.

**3) Umuhimu wa Hijabu na mazuri yake.**

Mwanamke kujilazimisha kuvaa Hijabu ni ibada ambayo kwayo mwanamke wa Kiislamu anajiweka karibu na Mola wake. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ﴾ الأحزاب: ٣٦.

***"Na haiwi kwa Muumini mwanaume wala muumini mwanamke kuwa na hiari pale Allah na Mtume wake wanapoamua jambo katika mambo yao".*** Sura Al-ahzaab: 36. **Kwa hiyo, H**ijabu sio kawaida ya kijamii ambayo jamii inarithiana, bali ni ibada na ni suala la kisheria ambalo ni wajibu kufuatwa.

**4) Masharti ya Hijabu.**

Wanazuoni wametaja masharti ya Hijabu ili iwe ya kisheria na ili mwanamke awe ametekeleza amri ya Allah Mtukufu.

**Sharti la kwanza:** Hijabu iwe inasitiri mwili mzima, kwa maana kwamba kisiwe wazi kiungo chochote katika mwili. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ قُل لِّأَزۡوَٰجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَآءِ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ يُدۡنِينَ عَلَيۡهِنَّ مِن جَلَٰبِيبِهِنَّۚ ذَٰلِكَ أَدۡنَىٰٓ أَن يُعۡرَفۡنَ فَلَا يُؤۡذَيۡنَۗ وَكَانَ ٱللَّهُ غَفُورٗا رَّحِيمٗا﴾ الأحزاب: ٥٩.

***"Ewe Mtume, waambie wake zako na mabinti zako na wake wa Waislamu kwamba, wajigubike nguo zao. Kufanya hivyo ni kujiweka karibu zaidi katika kujulikana na hivyo wasiudhiwe, na Allah ni mwingi wa kusamehe, mwenye kurehemu".*** Sura Al-ahzaab:59.

Mtume (s.a.w.) aliposema kuwa: ***"Yeyote mwenye kuburura nguo yake kwa majivuno Allah hatamuangalia (kwa jicho la huruma) Siku ya Kiyama. Ummusalama aliuliza: Sasa wanawake waifanyeje mikia ya nguo zao? Mtume akasema: Waiachilie kiasi cha shubiri. Ummusala akasema: Kwa kufanya hivyo miguu yao itakuwa wazi. Mtume (s.a.w.) akasema: Waiachie kiasi cha dhiraa, wasizidishe zaidi ya hapo".*** Hadithi hii imepokewa na Tirmidhiy na Nasai. Hivyo Hijabu inayotakiwa na sheria ni ile inayositiri sehemu zote za mwili, na kamwe sio Hijabu ile nguo inayofinika kichwa tu na kuonesha wazi wazi kila kitu katika sehemu ya chini ya mwili.

**Sharti la pili:** Hijabu iwe nzito, isiwe nyepesi na isiyo onesha mwili, kwa sababu lengo la Hijabu ni kusitiri. Iwapo nguo haisitiri haiitwi Hijabu. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Aina mbili (za watu) ni katika watu wa motoni, bado sijawaona: Wanaume wenye***

***bakora kama mikia ya ng'ombe ambazo kwazo wanawapiga watu, na wanawake waliovaa nguo (lakini) wako uchi, wenye kuyumba, wenye kuyumbisha. Vichwa vyao ni kama nundu za ngamia zilizoinama. Hawataingia peponi wala hawatapata harufu yake, na harufu yake inapatikana kutokea umbali wa masafa kadhaa".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. Maana ya ***"wamevaa wako uchi"*** ni kwamba, wamevaa nguo nyembamba zinazo onesha rangi ya mwili au fupi zinazo onesha baadhi ya mwili au zenye kubana zinazo ainisha wazi wazi mwili kama vile yuko uchi au yuko karibu na kuwa uchi. Kwa hiyo, yeye kwa jina amevaa lakini kwa uhalisia yuko uchi. Maana ya ***"wenye kuyumba"*** ni kwamba, wameacha kumtii Allah Mtukufu, wameacha kujisitiri na kuwa na haya jambo ambalo ni la lazima kwao na pia katika kutembea kwao wanayumbayumba kwa madaha kwa lengo la kutia mshawasha. Maana ya ***"wenye kuyumbisha"*** ni kwamba, wanawayumbisha wenzao kwa kuwafundisha kutembea uchi kwa kutumia njia tofauti na pia wanaziyumbisha nyoyo za wanaume kwa vitendo vyao. Maana ya ***"vichwa vyao ni kama nundu za ngamia"*** ni kwamba, wanazifuma nywele zao na kuzipiga fundo la mduara juu kama nundu za ngamia wanaoyumbayumba.

Imam Malik katika kitabu chake cha Muwattai amenukuu kwamba, Hafsa Binti Abdulrahman aliingia kwa Aisha, Allah amuwiye radhi, akiwa amejitanda mtandio mwepesi. Aisha aliuchana mtandio huo na kumvalisha mtandio mwingine mzito.

**Sharti la tatu:** Vazi lenyewe lisiwe la mapambo, lisiwe la kumeremeta au kufumwa na kutiwa nakshi na urembo kwa kutumia rangi zinazo vutia machoni. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا﴾ النور: ٣١.

***"Na wasidhihirishe mapambo yao isipokuwa yale tu yaliyodhihiri"***. Sura Annuur: 31.

Vazi lenyewe likiwa ni urembo, basi haifai kulivaa, na haliitwi Hijabu, kwa sababu Hijabu ni ile inayositiri na kuzuia kuonekana kwa mapambo kwa wanaume wa pembeni.

Pia amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: **"Msiwazuie vijakazi vya Allah (wanawake) (kwenda kwenye) misikiti ya Allah, na watoke wakiwa hawakujipamba".** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi. Maana ya ***"wakiwa hawakujipamba"*** ni kwamba, wasijitie manukato wala wasijipambe.

Ikiwa wanawake wanatakiwa wawe hivi pale wanapokwenda msikitini na kwenye ibada, basi kwenye safari nyingine hali hii inastahiki zaidi kuzingatiwa.

Kutokea hapa, ni wajibu kwa mwanamke Muislamu mwenye kuvaa Hijabu kujiepusha kutumia vipodozi anatokapo nyumbani kwake, kwa sababu kufanya hivyo ni kudhihirisha mapambo ambayo amekatazwa kuyaonesha wasiokuwa maharimu zake, na pia kufanya hivyo ni kuvutia wanaume. Hakuna tofauti katika hilo ikiwa vipodozi ni hafifu au vikali.

**Sharti la nne:** Vazi liwe pana, sio lenye kubana, lisioneshe taswira ya sehemu za siri wala lisioneshe sehemu za mvuto.

**Sharti la tano:** Vazi lisiwe limetiwa manukato au kufukizwa, kwa sababu hilo linahemua hisia za wanaume. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Mmoja wenu (nyinyi wanawake) anapokwenda msikitini asijitie manukato".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. Ikiwa hii ni hukumu ya mwanamke anayekwenda msikitini, sasa vipi kwa yule anayekwenda sehemu nyingine?

**Sharti la sita:** Vazi lisiwe linafanana na vazi la wanaume. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, isemayo kuwa: ***"Mtume wa Allah amemlaani mwanaume anayevaa vazi la mwanamke na mwanamke anayevaa vazi la mwanaume".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad na Abudaudi. Maana ya laana ni kunyimwa rehema za Allah Mtukufu.

**Sharti la saba:** Vazi lisiwe la fahari ambalo linakusudiwa umashuhuri na kujifaharisha mbele za watu, na kuwavutia watu kwa sababu ya umashuhuri wake au thamani yake au kwamba ni vazi ambali si la kawaida iliyo zoeleka kwa watu nchi husika. Hii ni kwa

mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.): ***"Yeyote yule ambaye anavaa vazi la umashuhuri duniani, Allah atamvisha vazi la udhalili Siku ya Kiyama".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad na Ibnimaja.

## TATU : Vazi la mwanamke katika sala.

Ni wajibu kwa mwanamke katika sala kufunika mwili wake wote ila uso na viganja, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa : ***'Allah haikubali sala ya mwanamke mwenye kubalehe bila ya ushungi'.*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi, Tirmidhiy na Ibnimaja.

Ushungi ni nguo inayofunika kichwa na shingo.

Imenukuliwa kwa Ummusalama, Allah amuwiye radhi, akisema kuhusu mwanamke anayesali akiwa amevaa Dera (gauni lisilokuwa na marinda) na ushungi bila ya kuvaa nguo ya kujifunga kiunoni kwamba**:** ***'(Inafaa kufanya hivyo) Iwapo Dera ni refu linalofunika miguu yake'.***

Ni wajibu kwa mwanamke kujibana katika kurukuu na kusujudu badala ya kujitanua, kuiweka sambamba miguu yake na kuifanya iwe kwenye upande mmoja badala ya kukaa kikao cha Tawaruki na Iftirashi, kwa sababu kufanya hivyo ni stara zaidi kwake.

## NNE : Sheria za urembo wa mwanamke.

### 1) Mambo ya maumbile halisi:

Inapendekezwa kwa mwanamke kuyadumisha mambo ya maumbile halisi yanayomhusu na ambayo Mtume (s.a.w.) amehimiza kuyapatiliza, kupitia kauli yake isemayo kuwa: ***'Mambo ya maumbile halisi ni matano au mambo matano ni katika maumbile halisi: Jando, kunyoa nywele za sehemu za siri, kunyonyoa nywele za kwapa, kukata kucha na kupunguza masharubu'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Inampasa mwanamke apatilize kunyoa nywele za sehemu za siri, nywele za kwapa na kukata kucha kila zinapokuwa ndefu, kwa

sababu kufanya hivyo ni usafi na urembo. Asiache kufanya hivyo zaidi ya siku arubaini, kwa mujibu wa kauli ya Anas, Allah amuwiye yardhi, aliyenukuliwa kusema kuwa : ***'Mtume wa Allah (s.a.w.) ametuwekea muda kwenye kukata masharubu na kukata kucha na kunyoa nywele za siri na kunyonyoa nywele za kwapa kwamba, tusiziache zaidi ya siku arubaini'.*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi, Tirmidhiy, Nasai na Ibnimaja.

**2) Kupaka hina, kutia wanja na kutia rangi nywele:**

Inapendekezwa kwa mwanamke, hasa aliyeolewa, kupaka hina mikono na miguu yake, kutia wanja na mfano wake awapo nyumbani kwake na sio anapotoka nje. Imenukuliwa kwa Aisha, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***'Mwanamke mmoja aliashiria, nyuma ya sitara, mkononi mwake akiwa na barua akitaka kumkabidhi Mtume (s.a.w.). Mtume (s.a.w.) akakamata mkono wake akasema: Sijui ni mkono wa mwanaume au wa mwanamke? Yule mwanamke akamwambia: Bali ni wa mwanamke. Mtume akamwambia: Lau kama ungekuwa mwanamke ungelizibadilisha kucha zako'*** akimaanisha kuwa, angelizibadilisha kwa kutia hina**.** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi na Nasai.

Lakini mwanamke hatakiwi kutia rangi kucha kwa kutumia kitu kinachaganda na kuzuia maji kufikia kwenye ngozi wakati wa kujitoharisha, kama vile rangi za kucha. Kama atafanya hivyo atalazimika kukitoa kitu hicho kilichoganda wakati wa kujitoharisha.

Imenukuliwa kwa Ibniabbas, Allah amuwiye radhi yeye na mzazi wake, akisema kuwa: ***'Hakika, miongoni mwa wanja wenu bora zaidi ni Ithmid, kwa sababu inatakatisha macho na kuotesha nywele'.*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi, Tirmidhiy, Nasai na Ibnimaja. **Ithmid** ni jiwe jeusi linalokaribia kuwa jekundu, hutumika kama wanja.

Inafaa kwa mwanamke kutia rangi nywele za kichwa chake kwa hina au kitu kingine, na hasa akiwa na mvi. Lakini ni makuruhu kutia rangi nyeusi, kwa sababu Mtume (s.a.w.) amekataza kujitia rangi nyeusi. Imenukuliwa kwa Jabir Bin Abdallah, Allah amuwiye radhi,

akisema kuwa: ***'Abuquhafa alipelekwa kwa Mtume (s.a.w.) siku ya ukombozi wa mji wa Makka huku kichwa na ndevu zake ni mfano wa Thaghama kwa weupe. Mtume akasema: Zibadilisheni hizi (ndevu na nywele) kwa kitu na jiepusheni rangi nyeusi'***. Hadithi hii imepokewa na Muslim. **Thaghama** ni mmea wenye maua na matunda meupe ambao ndevu nyeupe zinafananishwa na mmea huo.

**3) Kupunguza nywele na kuzinyoa:**

Inafaa kwa mwanamke kunyoa nywele za kichwa chake na kuzipunguza, kwa sababu jambo limefanywa na wake wa Mtume (s.a.w.). Imenukuliwa kwa Abusalama Bin Abdulrahman, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***'Wake wa Mtume (s.a.w.) walikuwa wakipunguza (nywele za) vichwa vyao mpaka huwa kama Wafrah'.*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. **Wafra** ni nywele za kichwa zinapofika kwenye njewe za masikio.

Lakini haifai kwa mwanamke kupunguza nywele kwa lengo la kuwaiga makafiri au wanaume, kwa sababu imethibiti kwamba Muislamu, kwa jumla, amekatazwa kujifananisha na makafiri, na pia mwanamke wa Kiislamu amekatazwa kujifananisha na wanaume. Imenukuliwa kwa Ibniabbas, Allah amuwiye radhi yeye na mzazi wake, akisema kuwa: ***"Allah amewalaani wanaume wanaojifananisha na wanawake na wanawake wanaojifananisha na wanaume"***. Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

Pia haijuzu kwa mwanamke kunyoa nywele zake ila kwa dharura tu.

**4) Kuunganisha nywele:**

Haijuzu kwa mwanamke kuunganisha nywele na kuziongezea kwa nywele nyingine, ni sawa nywele hizo ziwe za kweli au za bandia kama vile wigi, kwa sababu kufanya hivyo ni katika udanganyifu. Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***'Allah amemlaani muunganishaji nywele na muunganishwaji'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**5) Kuchora tattoo, kunyoa nyusi na kuchonga meno:**

Haifai kwa mwanamke kuchora tattoo katika sehemu yoyote ya

mwili wake wala kutoa nyusi zake wala kuchonga meno yake na kuyatenganisha, kwa lengo la kutaka kuifanya sura yake iwe nzuri, kwa sababu kufanya hivyo ni kubadilisha uumbaji wa Allah. Mtume (s.a.w.) amemlaani mwanamke anayefanya hayo. Imenukuliwa kwa Ibnimasoud, Allah amuwiye radhi yeye na mzazi wake, akisema kuwa: ***'Allah amewalaani wanawake wanaochora tattoo na wanaotaka kuchorwa, na wanawake wanaonyoa nyusi na wanaotaka kunyolewa, na wanawake wanaochonga meno kwa kutaka uzuri wanaobadilisha uumbaji wa Allah'.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim, na matamshi haya ni ya Muslim.

**Kuchora tattoo** ni kutoboa mkono au uso kwa sindano au kwa kitu kingine na kuijazia ile sehemu iliyotobolewa kwa wanja au kitu kingine.

**Kunyoa nyusi** ni kuondoa nyusi zote au baadhi yake kwa kunyoa au kunyonyoa au kwa madawa (kemikali).

**Kuchonga meno** ni kuyatenganisha meno kwa kuyakereza kwa kerezo na mfano wake ili kuwe na mwanya mdogo kati yake kwa ajili ya kutaka uzuri.

Ama iwapo meno yamekaa vibaya na yanahitaji kurekebishwa au yameshambuliwa na ugonjwa na mwanamke akawa anahitaji kuirekebisha hali hiyo, hakuna ubaya.

### TANO: Sheria za mwanamke kutoka nyumbani mwake na mahusiano yake na watu kando:

Mwanamke anapotoka nje ya nyumba yake, ni lazima achunge sheria na maadili yafuatayo:

**1)** Awe mwenye kujistiri kwa kuvaa Hijabu kwa namna iliyokwisha elezwa. Asiwe amejipamba kwa mikufu wala vipodozi na mfano wake. Pia asiwe mwenye kujitia manukato. Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Musiwazuie vijakazi vya Allah misikiti ya Allah, na watoke (waende misikitini) wakiwa hawakujitia manukato".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi.

**2)** Ayazuie macho yake yasiangalie kisichokuwa halali yake. Allah amemuamrisha mwanamke kufanya hivyo kama alivyowaamrisha wanaume. Amesema***:***

﴿قُل لِّلْمُؤْمِنِينَ يَغُضُّوا۟ مِنْ أَبْصَٰرِهِمْ وَيَحْفَظُوا۟ فُرُوجَهُمْ ۚ ذَٰلِكَ أَزْكَىٰ لَهُمْ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ خَبِيرٌۢ بِمَا يَصْنَعُونَ ۝٣٠ وَقُل لِّلْمُؤْمِنَٰتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَٰرِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ﴾ النور: ٣٠-٣١.

***"Na waambie waumini wanaume wazuie macho yao na wahifadhi tupu zao. Kufanya hivyo ni utakaso zaidi kwao. Hakika, Allah anayajua sana wanayoyafanya. Na waambie waumini wanawake wazuie macho yao na wahifadhi tupu zao".*** Sura Annuur: 30-31.

**3)** Awe na tahadhari wakati wa mazungumzo na wanaume wasiokuwa maharimu zake asilegeze sauti yake. Pia wakati wa kutembea asidunde miguu yake, kwa sababu kufanya hivyo ni kushawishi na kuamsha mihemuko ya wanaume. Allah Mtukufu amawakataza wanawake kufanya hivyo kwa kusema kuwa:

﴿فَلَا تَخْضَعْنَ بِٱلْقَوْلِ فَيَطْمَعَ ٱلَّذِى فِى قَلْبِهِۦ مَرَضٌ وَقُلْنَ قَوْلًا مَّعْرُوفًا﴾ الأحزاب: ٣٢.

***"Msilainishe kauli akatamani yule ambaye kwenye moyo wake kuna maradhi, na semeni maneno mema".*** Sura Ali-ahzaab: 32.

Na akasema Allah kuwa:

﴿وَلَا يَضْرِبْنَ بِأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِينَ مِن زِينَتِهِنَّ﴾ النور: ٣١

***"Na kamwe wasidunde miguu yao ili yajulikane mapambo yao waliyoyaficha".*** Sura Annuur: 31.

**4)** Ajiepushe kusongamana na wanaume, hasa kwenye masoko na mfano wake, pia ajiepushe kukaa faragha na mwanaume ambaye sio maharimu wake. Amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Yeyote yule ambaye anamuamini Allah na Siku ya Mwisho, kamwe asikae faragha na mwanamke ambaye hana udugu naye wa kuto oana (maharimu), kwa sababu wa tatu wao atakuwa shetani".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad.

Baadhi ya wanawake na mawalii (walezi) wao wanazembea kwenye aina za kukaa faragha na michanganyiko pamoja na kuwepo kwa shaka,

kama vile kukaa faragha na dereva, daktari, mtumishi na kukaa faragha pia kuchanganyika na ndugu wasiokuwa maharimu. Jambo hili ni hatari sana kuliko jambo jingine. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***"Jihadharini kuingia kwa wanawake. Mtu mmoja katika Ansaar akasema: Ewe Mtume wa Allah, unamuonaje shemeji? Mtume akasema: Shemeji ni kifo".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Shemeji ni ndugu wa kiume wa mume. Maana ya ***"Shemeji ni kifo"*** ni kawamba, shemeji anatakiwa kuogopwa sana kuliko mtu mwengine kama ambavyo kifo kinaogopwa sana kuliko kitu kingine.

**5)** Anatakiwa asipeane mkono na mwanaume ambaye sio miongoni mwa maharimu zake, kwa sababu katika kufanya hivyo kuna mtihani. Kwa sababu hiyo, Mtume wa Allah (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Hakika, mimi sipeani mikono na wanawake".*** Hadithi hii imepokewa na Malik, Nasai na Ibnimaja. Pia Mtume aliwaambia Swahaba wake kuwa: ***"Kwa yakini kabisa, mmoja wenu kuchomwa na sindano ya chuma (msumari) katika kichwa chake ni bora kuliko kumshika mwanamke asiyekuwa halali yake".*** Hadithi hii imepokewa na Tabarani. Hakuna tofauti katika hilo baina ya kupeana mikono kwa kuwepo kitu kinachuzuwia kugusana, kama vile glavu na mfano wake au kutokuwepo, kwa sababu hali zote hizo zinasababisha majaribu.

# VYAKULA NA VINYWAJI VILIYVO HARAMISHWA

Sharia ya kiislamu Imetilia umuhimu mkubwa vyakula vya Mwanadamu na vinywaji vyake,

Ikamrusu kutumia kila kilicho kizuri (katika vyakula na vinywaji) chenye manufa kwa mwili wake au akili yake au tabia yake, na ikamkataza kila kilicho kibaya chenye kudhuru mwili wake au akili yake au tabia yake, Na haya yote hayajawekwa na sharia tukufu ya kiislamu ispokuwa kwa ajili ya usalama wa nafsi za watu na kulinda tabia za watu na kuweka sawa mienendo ya watu; kwa sababu vyakula vizuri(vilivyo halalishwa) vina athari kubwa katika tabia ya mwanadamu na mwenendo wake, na vyakula vibaya (vilivyo haramishwa) vina athari mbaya kwa mwanadamu.

Na miongoni mwa vitu ambavyo Sharia ya kiislamu imekuja kuviharamisha katika vyakula na vinywaji ni vifuatavyo:

## 1) Nyamafu /Mzoga

Nyamafu/ Mzoga (Maiti) kila mnyama wa nchi kavu ambae ni halali kuliwa amekufa kabla ya kuchinjwa kisharia,

Na makusudio ya kuchinja kisharia ni: Kuchinjwa mnyama ambae ni halali kuliwa ,mwenye uwezekano wa kuchinjwa kwa kukata koo la mnyama na mishipa miwili ya shingoni inayopitisha damu (mariy' u na widaji) au kuchoma kisu katka koromeo (chini ya shingo najuu yakifua) kama inavofanyika hivi sasa wakati wakuchinja ngamia, au kumjeruhi (katika viungo vyake) inaposhindikana kumdhibiti, ama atapigwa kwa pigo lolote lenye kumtoa roho katika sehemu yoyote katika mwili wake, na lazima hilo pigo liwe kutoka kwa muislamu au Ahalu kitabi (mayahudi na manaswara), au kwa kumtuma mnyama mwindaji ama ndege mwindaji aliefundishwa kuwinda.

Ikiwa mnyama atakufa bila kupatikana hatua hizi, akafa kwa kujinyonga ama kuzama katika maji au kupigwa kwa jiwe au fimbo na

mfano wa vitu hivi, (basi huyo mnyama atakuwa nyamafu) na ni harumu kula nyama yake (maiti) kwa kauli ya Mwenyezimungu mtukufu:

﴿حُرِّمَتۡ عَلَيۡكُمُ ٱلۡمَيۡتَةُ﴾ المائدة: ٣

***"Mmeharamishiwa nyinyi kula nyamafu, maiti"*** Surutul al maaidah 3.

Ama maiti ya samaki ni halali kuliwa kwa ushahid wakauli ya mtume (s.a.w.) kuhusiana na bahari ***"bahari ni twahara maji "masafi" yake na nihalali nyamafu yake"maiti kuliwa""*** Hadithi imepokelewa na Imam Ahmad.

**2) Damu inayomwagika:**

Damu ni haramu kwa ushahidi wa kauli ya Mwenyezimungu mtukufu:

﴿حُرِّمَتۡ عَلَيۡكُمُ ٱلۡمَيۡتَةُ وَٱلدَّمُ﴾ المائدة: ٣

***"mmeharamishiwa nyinyi nyamafu"maiti" na damu"*** al maida 3.

Na amesema allah mtukufu:

﴿قُل لَّآ أَجِدُ فِي مَآ أُوحِيَ إِلَيَّ مُحَرَّمًا عَلَىٰ طَاعِمٖ يَطۡعَمُهُۥٓ إِلَّآ أَن يَكُونَ مَيۡتَةً أَوۡ دَمٗا مَّسۡفُوحًا﴾

الأنعام: ١٤٥

***"Sema: Sioni katka yale niliofunuliwa mimi kitu kilicho haramu kwa mlaji kukila ispokuwa kiwe ni nyamafu"maiti" au damu inayo mwagika"*** Suratul Al- anaam 145.

Ama damu isiyo mwagika ile inayobaki katika nyama ni ruhusa kuliwa na imetolewa katika hukumu ya uharamu wa damu, aina mbili (damu za halali) Ini na Bandama, kwa ushahidi wa kauli ya Mtume rehema na Amani ziwe juu yake, (s.a.w.) ***"Tumehalilishiwa sisi maiti za aina mbili na damu za aina mbili, ama maiti za aina mbili samaki na nzige, na ama damu za aina mbili ini na bandama"*** Hadithi imepokelewa na Imam Ahmad na Ibni maajah.

**3) Nguruwe:**

Nguruwe ni haramu kuliwa kwa makubaliano ya Wanazuoni wote, kwa dalili ya aya takatifu:

﴿حُرِّمَتۡ عَلَيۡكُمُ ٱلۡمَيۡتَةُ وَٱلدَّمُ وَلَحۡمُ ٱلۡخِنزِيرِ﴾ المائدة: ٣

***"Mmeharimishiwa nyinyi nyamafu maiti na damu na nyama ya Nguruwe)"*** Suratul Al maaida 3.

Na inavofahamika hakika ya huyu mnyama (Nguruwe) ni mchafu na pia anaishi katika uchafu na nijisi, na pia nguruwe hula vyakula vichafu vya najisi bali vyake vizuri na anavyovipenda Zaidi ni najisi na vichafu vichafu tu; ndiomana nyama yake imekusanya maradhi mengi kama ilivyothibiti katka tafiti za kidaktari za zama hizi, na kwa kuongezea nyama ya nguruwe ina minyoo ya (hatari) yenye kuuwa.

**4) Kila mnyama mwitu mwenye meno ya kushambulia:**

Mfano simba, mbwa mwitu, mbwa, chui, dubu, nyani na wengineo wanaofanana na hawa, ni haramu kuliwa.

Kwa mujibu wa hadith ya abuo hurayrah – radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie -amesema Mtume (swalla allahu alayhi wasallam ***"Ameharamisha kula kila mnyama mwitu mwenye kutia meno (kushambulia kwa meno)"*** Hadithi imepokelewa na Imam Muslim.

**5) Kila ndege mwenye kutumia makucha:**

kama mfano wa kipanga,kunguru, na aina nyinginezo mfano wa hawa ndege,

kwa hadiyth ya ibn abbaas radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie amesema: (Amekataza mtume kula kila mnyama mwitu mwenye meno ya kushambulia ,na kila ndege mwenye kutumia makucha ) Hadithi imepokelewa na Imam Muslim.

**6) Punda wa mjini (punda wa kufugwa):**

Ni haramu kula nyama ya punda wa mjini (wa kufugwa) kwa

hadith ya abby thaalabah al-khushany radhi za Mwenyezi Mungu zimfikie amesema (ameharamisha mtume -rehema na Amani zimfikie -kula nyama ya punda wa mjini (wakufugwa) al-bukhaariy na muslim"

Na vilevile haramu kula nyama ya wanyama ambao waliozaliwa baina ya mnyama alie halalishwa (kuliwa) na alie haramishwa (kuliwa) mfano farasi, alie zaliwa baina ya farasi na punda dume; kwa sababu ya mmoja ya wazazi wake ni haramu kuliwa nayeye atafata hukumu yake (ya uharamu)

### 7) Wadudu, Nyoka, Nge, Panya, na Mende:

Na mfano wa hawa ni haramu kula kwa sababu wadudu hawa ni miongoni mwa uchafu, na pia wanamadhara na hatari kwa afya ya mwanadamu, na usalama wake, amesema Mwenyezi Mungu mtukufu:

﴿وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيۡهِمُ ٱلۡخَبَٰٓئِثَ﴾ الأعراف: ١٥٧

***"Na anawahalalishia vizuri na anawaharamishia vibaya"*** Suratu Al-aaraf. 157.

### 8) Kila kilichohukumiwa na sharia kuwa ni najisi (uchafu)

Kwa mfano, mkojo kinyesi matapishi, na mfano wa hivi, ni haramu kutumia (kula na kunywa) kwa sababu ni uchafu na vina madhara, amesema Mwenyezi Mungu mtukufu:

﴿وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيۡهِمُ ٱلۡخَبَٰٓئِثَ﴾ الأعراف: ١٥٧

***"na anawaharamshia vibaya"*** Al-araaf 157".

### 9) Pombe na madawa ya kulevya:

Na mfano wake, kila vyenye kulewesha vina vvyo ondosha akili ya mtu na kumtoa katika uhalisia wake.

Amesema Mwenyezi Mungu mtukufu:

﴿إِنَّمَا ٱلۡخَمۡرُ وَٱلۡمَيۡسِرُ وَٱلۡأَنصَابُ وَٱلۡأَزۡلَٰمُ رِجۡسٞ مِّنۡ عَمَلِ ٱلشَّيۡطَٰنِ فَٱجۡتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمۡ تُفۡلِحُونَ﴾

المائدة: ٩٠

***"Hakika ya ulevi na kamari na kuabudu masanamu, na kupiga ramli ni uchafu katika kazi ya shetani, basi jiepusheni navyo,ili mpate kufanikiwa"*** Al-maaidah 90".

Na amesema Mtume rehema na Amani zimfike: ***"kila kilevi ni haramu, na kila kilevi ni pombe"*** Hadithi imepokelewa na Imam An-nasai.

**10) Vinaruhusiwa kutumiwa katika vile vilivyo tajwa uharamu wake:**

Ikipatikana dharura kubwa ya kutumia (chakula na kinywaji vilivyo haramishwa)

Itaruhusiwa kwa ajili ya dharura tu, kwa mfano mtu kuhofia kufa, kwa kukosa chakula, ispokuwa akapata vyakula vilivo haramishwa au kinywaji kilicho haramishwa) itaruhusiwa wakati huo,kula (au kunywa) vyakula vilivyo haramishwa, kiwango cha kujikinga na kufa na madhara.

**11) Sumu za aina yoyote:**

Ni haramu kutumia sumu, kwa sababu ya madhara yake, na kwakuwa sumu inamuangamiza mtu (anapotumia) na amesema allah mtukufu:

﴿وَلَا تَقْتُلُوٓاْ أَنفُسَكُمْ﴾ النساء: ٢٩

***"na wala msijiuwe"*** an nisaa 29.

﴿وَلَا تُلْقُواْ بِأَيْدِيكُمْ إِلَى ٱلتَّهْلُكَةِ﴾ البقرة: ١٩٥

***"na wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizi" Suratul Al-baqara 195.***

Na amesema Mtume rehema na Amani zimfikie ***"Na yeyote atakae kunywa sumu, akajiuwa mwenyewe (kwa sumu iyo) basi mtu huyo atakuwa anakunywa sumu yake hiyo,katika moto wa jahannamu, akiishi humo milele"*** Hadithi Imepokelewa na Imam Al-bukhari na Muslimu.

# MLANGO WA NNE

# UHUSIANO WA

# MUISLAMU MPYA

# NA JAMII

## Utangulizi

Mwenye kuyatafakari maandiko ya sheria ya Kiislamu atagundua kuwa, kutofautiana katika mitazamo ya binadamu na itikadi zao ni suala la kimaumbile linalo fungamana na matakwa na hekima za Allah. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ النَّاسَ أُمَّةً وَاحِدَةً وَلَا يَزَالُونَ مُخْتَلِفِينَ ۝١١٨ إِلَّا مَن رَّحِمَ رَبُّكَ وَلِذَٰلِكَ خَلَقَهُمْ﴾ هود: ١١٨ - ١١٩.

***"Lau kama Mola wako angetaka, angewafanya watu umma mmoja. Na (watu) hawatoacha kutofautiana, isipokuwa tu wale aliowarehemu Mola wako. Na kwa hilo aliwaumba".*** Sura Hud: 118-119.

Uislamu kwa kuzingatiwa kwake kuwa ni dini ya mbinguni na ni sheria ya Mungu, inatambua tofauti hiyo na kuichukulia kwamba jambo halisia, hasa ukitia maanani kwamba kupatikana uongofu kwa watu wote ni jambo gumu. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ﴾ يوسف: ١٠٣

***"Na watu wengi, hata ukiwa na ari kubwa, si wenye kuamini".*** Yusuf: 103.

Kwa sababu hii, Uislamu umewawekea wafuasi wake misingi na mifumo ambayo inaratibu mahusiano yao na watu wengine, inawatunzia misingi yao na mafundisho yao na kuyalinda yasitetereke na yasiharibike, ukitilia maanani kwamba heshima ya Muislamu na hadhi yake ina nafasi ya kwanza katika kutunzwa na kulindwa. Pia Uislamu unatia maanani kwamba, huruma, kuvumiliana, kutenda wema na kufanya uadilifu kwa viumbe wote ni sehemu isiyokubali kujitenga ya maisha ya kijamii ya dini hii tukufu.

Katika maelezo yafuatayo, tutayaweka wazi masuala kadhaa yatakayomfafanulia Muislamu mpya na kumuanishia misingi ya mahusiano yake na watu wasiokuwa Waislamu wanaomzunguka;

wawe ndugu wa karibu au watu wengine. Hayo yatafanyika kupitia vipengele vifuatavyo:

- Uhusiano wa kifamila.

- Uhusiano wa kifedha.

- Uhusiano wa kijamii na kibinadamu.

## UHUSIANO WA WANANDOA BAADA YA WOTE WAWILI KUWA WAISLAMU AU MMOJA WAO

Katika jamii yoyote ile, familia inazingatiwa kuwa ndio tofali la mwanzo na msingi wa mwanzo katika kuijenga jamii hiyo. Familia inapata umuhimu wake mkubwa kwamba, ni mfumo muhimu wa kijamii kwa sababu jamii ndiyo inayoitegemea katika kulea na kuwapa malezi watu wake, kwa kufanya yale yanayoiletea jamii nguvu, maendeleo na kukua.

Kwa kuangalia umuhimu huu mkubwa na jukumu nyeti la maisha ya kijamii ambayo jengo lake ni mahusiano ya ndoa, Uislamu umejitwisha jukumu muhimu la kuratibu uhusiano wa ndoa hadi kufikia kiwango cha juu sana, na kufanya hima ya kuhakikisha kuwa zinakuwepo sababu zinazo chochea uhusiano huo kuwa endelevu na wa kudumu.

Kwa kuwa Uislamu unawaita watu wote kuingia kwenye dini hii na kufuata mwongozo wake ulio nyooka, umetia maanani kwamba wale wanaoingia katika dini wanaweza kuwa na mikataba na mahusiano madhubuti ya kifamilia baina yao na baina ya watu wengine, na kwamba si jambo jepesi kukatisha na kuvunja mahusiano na mikataba hiyo. Kwa sababu hiyo, Uislamu umeuwekea taratibu mkataba na uhusiano huu na kufafanua mipaka yake. Mume na mke ambao sio Waislamu na ambao wamo katika mahusiano ya ndoa kabla ya kusilimu, ama watasilimu wote kwa wakati mmoja, au mmoja wao atamtangulia mwenzake. Sasa je, ni ipi hukumu ya ndoa yao katika hali hizi?

### KWANZA: Kusilimu kwa wanandoa kwa pamoja.

Wanazuoni wote wamekubaliana kwamba mke na mume watakaposilimu kwa pamoja katika wakati na kikao kimoja, Uislamu unaikubali ndoa yao waliyoifunga kabla ya Uislamu, iwapo tu hakuna pingamizi inayozuia kudumu kwa ndoa hiyo. Ni sawa kusilimu kwao kumefanyika kabla au baada ya kukutana kimwili.

Watu wengi wakati wa Mtume (s.a.w.) walisilimu na alizithibitisha ndoa zao walizozifunga kabla ya kusilimu kwao, na kamwe hakuwauliza kuhusu namna walivyozifunga au kwa kiasi gani masharti yalikamilika.

Ama ndoa iliyofungwa kabla ya kusilimu kwao ikiwa ni katika zile ambazo hazifai kudumu, kwa sababu ya nasaba au kunyonya, ndoa hiyo itakuwa batili wanapoingia katika Uislamu, kama vile mtu kumuoa mwanamke ambaye ni katika maharimu zake: kama mama yake au binti yake au dada yake au mke wa baba yake, au mtu akaowa mwanamke ambaye baina yake na baina ya mwanamke huyo kulikuwepo unyonyeshaji kama vile mama aliyemnyonyesha au dada yake wa kunyonya.

Ama mwenye kusilimu akiwa na zaidi ya wake wanne, atachagua wanne tu kati yao, na waliobaki atatengana nao, kwa sababu Uislamu hauruhusu zaidi ya wake wanne kwa wakati mmoja. Imenukuliwa kwa Abdallah Bin Omar, Allah amuwiye radhi yeye na mzazi wake, akisema kuwa: ***"Ghaylani alisilimu akiwa na wake kumi. Mtume wa Allah (s.a.w.) akamwambia kuwa: Kaa na wanne na achana na waliobaki".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Tirmidhiy, Ibnimaja na Ibnihibban.

Na mfano mwengine wa hali kama hiyo ni lau kama mtu alikuwa ameoa madada wawili. Atachagua mmoja wao na kutengana na mwengine, kwa sababu Uislamu hauruhusu kuwakusanya dada wawili katika ndoa, kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿وَأَن تَجۡمَعُواْ بَيۡنَ ٱلۡأُخۡتَيۡنِ﴾ النساء: ٢٣.

***"Na (mmeharamishiwa) kuwakusanya dada wawili (katika ndoa)".*** Sura Annisai: 23.

**PILI: Kusilimu kwa mmoja kati ya wanandoa**

Sura ya pili ya mke na mume wasiokuwa Waislamu ni kuingia kwa mmoja wao katika Uislamu kabla ya mwengine. Zinachipuka kutokana na sura hii hali kadhaa:

**Hali ya kwanza:** Ni kusilimu kwa mmoja wa wanandoa ambao

ni Watu wa Kitabu (Wakristo na Wayahudi) baada ya kufunga ndoa na kabla ya kukutana kimwili. Katika hali hii, ndoa yao waliyoianzisha kabla ya Uislamu itakubaliwa, kwa sababu Uislamu, kimsingi, unaruhusu kuoa Watu wa Kitabu, na kwa maana hiyo, inajuzu ndoa hii kuendelea kuwepo. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَٱلۡمُحۡصَنَٰتُ مِنَ ٱلۡمُؤۡمِنَٰتِ وَٱلۡمُحۡصَنَٰتُ مِنَ ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡكِتَٰبَ﴾ المائدة: ٥.

***"Na (mmehalalishiwa kuoa) wanawake wenye kuhifadhiwa (na maovu) miongoni mwa waumini wanawake, na (pia mmehalalishiwa kuoa) wanawake wenye kuhifadhiwa (na maovu) miongoni mwa wale waliopewa kitabu".*** Sura Almaida: 5.

Ama mke ambaye ni Mtu wa Kitabu akisilimu kabla ya mumewe baada ya kufunga ndoa na kabla ya kumuingilia kimwili, ndoa yake kwa mume huyo itavunjika hapo hapo. Hakuna tofauti katika hilo baina ya kuwa mume ni Mtu wa Kitabu au sio Mtu wa Kitabu, kwa sababu katu haijuzu kwa mwanaume ambaye sio Muislamu kumuoa mwanamke Muislamu, kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿فَإِنۡ عَلِمۡتُمُوهُنَّ مُؤۡمِنَٰتٖ فَلَا تَرۡجِعُوهُنَّ إِلَى ٱلۡكُفَّارِۖ لَا هُنَّ حِلّٞ لَّهُمۡ وَلَا هُمۡ يَحِلُّونَ لَهُنَّ﴾ الممتحنة: ١٠.

***"Na (hao wanawake wa Kiislamu wahamiaji) mkiwajua kuwa ni waumini basi msiwarejeshe kwa makafiri. Wao (wanawake Waislamu) sio halali kwao (makafiri), na wao (makafiri) hawawi halali kwao (wanawake Waislamu)".*** Sura Almumtahina:10.

**Hali ya pili: Ni kusilimu kwa mmoja wa wanandoa ambao sio Watu wa Kitabu, au mmoja ni Mtu wa Kitabu na mwengine sio Mtu wa Kitabu, baada ya kufunga ndoa na kabla ya kumuingilia mke:**

Ikiwa mume ameslimu, sawa awe Mtu wa Kitabu au asiwe Mtu wa Kitabu, kabla ya mkewe ambaye sio Mtu wa Kitabu, na ikawa kuingia kwake katika Uislamu ni baada ya kufunga ndoa na kabla ya kumuingilia mkewe, basi hali hiyo itafanya iwe wajibu kwake kutengana na mkewe tangu wakati aliposilimu, kwa sababu kimsingi Muislamu haijuzu kwake kuoa mwanamke ambaye sio Mtu wa

Kitabu. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿وَلَا تُمۡسِكُواْ بِعِصَمِ ٱلۡكَوَافِرِ﴾ الممتحنة: ١٠.

***"Na msiwaweke kwenye hifadhi (ya ndoa zenu) wanawake makafiri".*** Sura Almumtahinah:10.

❖ Ikiwa kusilimu kwa mmoja wa wanandoa ni kabla ya kukutana kimwili na ikawa wajibu kutengana, katika kupewa nusu ya mahari, iwapo mume ndiye aliyeingia kwenye Uislamu, hali hii mke anastahiki kwa sababu utengano umetokea kwa sababu yake.

❖ Ama ikiwa mke ndiye aliyeingia kwenye Uislamu, basi hatostahiki cho chote kile katika mahari, kwa sababu utengano umetokea kwa sababu yake.

**Hali ya tatu:** Ni kusilimu kwa mmoja wa wanandoa baada ya kukutana kimwili. Katika picha hii, suala litakuwa katika moja ya hali zifuatazo:

**1) Mume kusilimu wakati mke ni Mtu wa Kitabu.**

Ikiwa mume atasilimu kabla ya mkewe ambaye ni Mtu wa Kitabu, na ikawa kusilimu kwake ni baada ya kumingilia kimwili, ndoa iliyofungwa kabla ya Uislamu itakubaliwa, kwa sababu kimsingi inajuzu kwa Muislamu kumuoa mwanamke Mtu wa Kitabu. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَٱلۡمُحۡصَنَٰتُ مِنَ ٱلۡمُؤۡمِنَٰتِ وَٱلۡمُحۡصَنَٰتُ مِنَ ٱلَّذِينَ أُوتُواْ ٱلۡكِتَٰبَ﴾ المائدة: ٥.

***"Na (mmehalalishiwa kuoa) wanawake wenye kuhifadhiwa (na maovu) miongoni mwa waumini wanawake, na (pia mmehalalishiwa kuoa) wanawake wenye kuhifadhiwa (na maovu) miongoni mwa wale waliopewa kitabu".*** Sura Almaida: 5.

**2) Mume kusilimu wakati mke sio Mtu wa Kitabu.**

Ikiwa mume atasilimu kabla ya mkewe ambaye sio Mtu wa Kitabu, na ikawa kusilimu kwake ni baada ya kukutana na mkewe huyo kimwili, atatengana naye, ila tu kubakia kwa ndoa baina yao na

kumalizika kwake kutategemea kumalizika kwa Eda. Ikiwa mke huyo atasilimu kabla ya kumalizika kwa Eda ambayo ni Hedhi tatu kwa yule mwenye kupata Hedhi au miezi mitatu kwa asiyepata Hedhi au kujifungua kwa mwenye ujauzito, ndoa yao ya nyuma itakubaliwa na uwanandoa utabakia kuwepo baina yao. Iwapo mke hakusilimu mpaka Eda ikamalizika, mtengano utapatikana baina yao kuanzia pale mume alipoingia kwenye Uislamu. Abusufiani Bin Harb alisilimu kabla ya mkewe Hindu Binti Utbah ambaye naye alisilimu baada yake kwa siku kadhaa. Mtume (s.a.w.) aliithibitisha ndoa yao ya awali.

**3) Kusilimu kwa mke wakati Mume sio Muislamu** (Mtu wa Kitabu au sio Mtu wa Kitabu)

Iwapo mke ameslimu wakati mume sio Muislamu, sawa awe Mtu wa Kitabu au sio Mtu wa Kitabu, na kusilimu kwake kukawa ni baada ya kuingiliana kimwili, itakuwa wajibu kwa mwanamke huyo kutengana na mumewe, na haijuzu kwake kuruhusu mume huyo astarehe naye, ila tu kubakia kwa ndoa baina yao kutategamea kumalizika kwa Eda yake. Iwapo mume atasilimu kabla ya kumalizika kwa Eda, watathibitishiwa ndoa yao ya mwanzo. Na iwapo hakusilimu mpaka Eda ikamalizika, utengano utakuwa umepatikana na mke atakuwa ametengana na mumewe kikamilifu kwa kumalizika kwa Eda yake. Imenukuliwa kwa Daudi Ibni Kardusi akisema kuwa: ***"Mtu mmoja katika kabila la Banitaghlib anaye itwa Abadi Bin Nuuman Bin Zur'a alikuwa na mke wa kabila la Banitamim, na Abadi alikuwa Mkristo. Mkewe alisilimu na yeye akakataa kusilimu. Omar akawatenganisha baina yao".*** Hadithi hii imepokewa na Ibniabishaiba. Pia imenukuliwa kwa Ibniabbas, Allah amuwiye radhi yeye na mzazi wake, akisema kuwa: ***"Iwapo mwanamke Mkristo atasilimu kabla ya mumewe kwa muda, mwanamke huyo atakuwa haramu kwa mumewe huyo".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

Baadhi ya wake wa Swahaba walisilimu kabla ya waume zao, na waume hao wakasilimu baada yao katika kipindi cha Eda zao. Mtume alizithibitisha ndoa zao na hakuwafungisha ndoa mpya, kama ilivyo tokea kwa Swafuwan Bin Umayya na Ikrima Bin Abijahli.

❖ **Iwapo mwanamke ataslimu kabla ya mumewe, ni wajibu kumfahamisha mumewe juu ya kusilimu kwake. Pia inapendekezwa kwake kumvuta memewe kwenye Uislamu kwa maneno mazuri, na kumuwekea wazi kwamba, kutokubali kwake kusilimu katika kipindi cha Eda yake, kutalazimisha kutengana naye.** Haya yamepokewa na Ibniabishaiba.

# MAHUSIANO YA MUISLAM MPYA NA WATOTO WAKE

## KWANZA: Ufuasi wa dini wa watoto baada ya wazazi kusilimu:

Iwapo mtoto yuko chini ya umri wa balehe au akiwa mwendawazimu, anawafuata wazazi wake katika dini ambayo wao wanaifuata. Wakiwa Wayahudi na yeye anakuwa Myahudi kama wao, wakiwa Wakristo na yeye anakuwa Mkristo kama wao na wakiwa Waislamu na yeye anakuwa Muislamu kama wao. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) inayosema kuwa: ***"Kila mtoto huzaliwa akiwa katika maumbile halisi. Wazazi wake ndio wanaomfanya awe Myahudi au Mkristo au Mmajusi".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Wazazi wawili wanaposilimu au mmoja wao, mtoto aliyekuwa bado hajabalehe au mwendawazimu anakuwa Muislamu kwa kumfuata mzazi mwenye dini bora zaidi miongoni mwao na ambayo ni dini ya yule aliyesilimu. Ikiwa aliyesilimu ni baba, mwanawe anamfuata na anakuwa Muislamu kama yeye. Ikiwa mama ndiye aliyesilimu, basi mtoto anamfuata mama katika dini yake na kuwa Muislamu, kwa sababu Uislamu siku zote uko juu, wala haukaliwi juu. Pia Uislamu ndio dini ambayo Allah anairidhia kwa waja wake.

Ama wazazi wawili wakisilimu baada ya mtoto kubalehe au mwendawazimu kurudi kwenye akili zake timamu, sheria haitamhukumu kwamba ni Muislamu ila tu atakapokubali yeye mwenyewe kuufuata Uislamu. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) inayosema kwamba: ***"Hakuna mtoto anayezaliwa isipokuwa kwamba yupo katika umbile halisi (la Uislamu) mpaka ulimi wake utakapotamka kumsemea".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

## PILI: Ulezi wa watoto baada ya kusilimu.

Wanazuoni wote wamekubaliana kwamba, wazazi wawili watakaposilimu kwa pamoja, malezi ya watoto yatakuwa yao wote

kwa pamoja.

Ama mmoja wa wazazi anaposilimu kabla ya mwengine, akisilimu mke (mama) kabla ya mumewe (baba), malezi ya mtoto yatakuwa kwa mama na sio kwa baba. Akisilimu baba kabla ya mama, malezi ya mtoto yatakuwa kwa baba na sio kwa mama.

Malezi ya mtoto yanakuwa kwa mzazi Muislamu kati wa wazazi wawili, kwa sababu mtoto kuishi na mzazi ambaye sio Muislamu kuna madhara ya wazi kwa mtoto, kutokana na kwamba aghalabu mtoto anaathirika na dini ya mlezi wake, na hivyo hupelekea kutoka kidogo kidogo katika Uislamu.

Aidha, ulezi ni aina fulani ya utawala kwa mtoto, na ni jambo lilokwishaamuliwa na sheria kwamba hakuna utawala wa kafiri kwa Muislamu. Imenukuliwa kwa ***"Rafiu Bin Sinani kwamba, yeye alisilimu na mkewe akakataa kusilimu. Mwanamke akenda kwa Mtume s.a.w. (kwenda kushtaki) na kumwambia: (Huyu ni) Mwanangu. Rafiu naye akamwambia (Mtume): (Huyu ni) Mwanangu. Wakati huo mtoto huyo wa kike alikuwa amesha achishwa kunyonya au karibu kuachishwa. Mtume (s.a.w.) akamwambia Rafiu: Kaa upande huu. Pia akamwambia mkewe: Kaa upande huu. Rafiu akasema: Na Mtume akamuweka mtoto baina yao, kisha akawaambia: Muiteni. Mtoto akenda kwa kwa mama yake. Mtume (s.a.w.) akasema: Ewe Mola wangu, muongoze. Hapo, mtoto akapinda na kwenda kwa baba yake, na akamchukua"***. Hadithi hii imepokewa na Abudaudi na Nasai.

Mtoto alipokwenda upande wa mama yake mwanzoni, Mtume (s.a.w.) alimuombea uongofu akapinda na kwenda kwa baba yake, kwa sababu kuwepo kwake kwa kafiri ni kinyume na mwongozo wa Allah Mtukufu alioutaka. Wanazuoni wa Taabiina, Allah awarehemu, wamelitamka wazi suala hili. Hasan Albasriy amesema kuhusu mtoto mdogo kwamba ***"Awe pamoja Muislamu katika wazazi wake".*** Ameyapokea haya Bukhari. Imenukuliwa kwa Ibrahimu Al-nakhai akisema kuhusu Wakristo wawili waliokuwa na mtoto mdogo na mmoja wao akasilimu kwamba: ***"Mwenye ubora zaidi kati yao kuwa na mtoto ni Muislamu".*** Ameyapokea haya Bukhari.

## TATU: Uwalii (usimamizi) katika ndoa.

Ni katika mambo yaliyokwisha amuliwa katika sheria kwamba, mwanamke hawezi kusimamia kujiozesha yeye mwenyewe, na anatakiwa kusimamiwa na Walii wake, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) inayosema kuwa: ***"Mwanamke yeyote aliye olewa bila ya idhini ya Walii wake, ndoa yake ni batili. Mtume alikakariri kusema hivyo mara tatu".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Abudaud, Tirmidhiy, Nasai na Ibnimaja.

Lakini mwanamke anaposilimu na Walii wake akawa sio Muislamu, haitasihi Walii huyo kuwa walii wa binti yake kwenye ndoa baada ya kusilimu kwa mwanamke huyo, kwa sababu Uislamu umeukataa uwalii (usimamizi) wa makafiri kwa Waislamu, pale Allah Mtukufu aliposema kuwa:

﴿وَلَن يَجْعَلَ ٱللَّهُ لِلْكَٰفِرِينَ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ سَبِيلًا﴾ النساء: ١٤١.

***"Na kamwe Allah hatojaalia makafiri kuwa na njia yoyote ile (ya utawala na usimamizi) juu ya Waislamu".*** Sura Annisaa: 141.

Mtume (s.a.w.) amebainisha wazi ubora na utukufu wa Uislamu juu ya dini nyingine kwa kauli yake isemayo kuwa: ***"Uislamu uko juu wala haukaliwi juu".*** Hadithi hii imepokewa na Tabaraniy.

Kwa hiyo, hawezi kusimamia jambo la mwanamke Muislamu isipokuwa walii wake Muislamu tu. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿وَٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَآءُ بَعْضٍ﴾ الأنفال: ٧٣

***"Na waliokufuru ni Mawalii wao kwa wao".*** Sura Al-anfaal: 73.

Kwa hiyo, Walii wa mwanamke wa Kiislamu anatakiwa awe ndugu wa karibu ambaye ni Muislamu. Ikiwa hakupatikana Muislamu katika ndugu zake wa karibi, Walii wake atakuwa kiongozi wa Kiislamu au anayemuwakilisha, kama vile Kadhi au kiongozi wa kijamii. Ikwa hakupatikana, atampa mamlaka ya kusimamia ndoa yake mwanaume katika Waislamu.

Vile vile si sahihi kwa Muislamu mwanaume kuwa Walii wa binti

yake ambaye sio Muislamu, kwa sababu hana haki ya kumsimamia. Aya ya Qur-ani imeweka wazi kuwa, wasiokuwa Waislam uwalii wao huwa wao kwa wao. Zaidi ya hivyo, ongeza kuwa uwalii umejengeka juu ya uhusiano wa kurithiana baina ya mababa na watoto, na Sheria imekata uhusiano huu ikiwa kutakuwepo tofauti za kidini, hivyo uwalii nao utakatika.

## NNE: Usimamizi na usia kwa watoto:

Miongoni mwa sheria ambazo huathirika kutokana na tofauti za kidini baina ya mababa na watoto ni usimamizi wa baba ambaye sio Muislamu kwa watoto wake ambao ni Waislamu.

Iwapo patahukumiwa kwamba watoto ni Waislamu, na baba akawa sio Muislamu, baba huyu hana uwalii (usimamizi) juu ya mali za watoto wake iwapo wana upungufu au wendawazimu au wasiokomaa kiakili. Uwalii utahama na kwenda kwa ndugu wa karibu Muislamu au mtu ambaye Kadhi atamteua kuwa msimamizi wa mambo yao, kwa sababu jambo la Muislamu halisimamiwi ila tu na Muislamu kama yeye, ikiwa masharti mengine yaliyobaki yatakuwepo. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu inayosema kuwa:

﴿وَٱلۡمُؤۡمِنُونَ وَٱلۡمُؤۡمِنَٰتُ بَعۡضُهُمۡ أَوۡلِيَآءُ بَعۡضٖ﴾ التوبة: ٧١.

***"Na waumini wanaume na waumini wanawake ni mawalii wao kwa wao".*** Sura Attauba: 71.

Ama mtu ambaye sio Muislamu, hana uwalii na usimamizi wa kumtawalia Muislamu, kwa mujibu wa kauli ya Allah inayosema kuwa:

﴿وَلَن يَجۡعَلَ ٱللَّهُ لِلۡكَٰفِرِينَ عَلَى ٱلۡمُؤۡمِنِينَ سَبِيلًا﴾ النساء: ١٤١.

***"Na kamwe Allah hatojaalia makafiri kuwa na njia yoyote (ya utawala na usimamizi) juu ya Waislamu".*** Sura Annisaa: 141.

Aidha, haijuzu kwa baba, akiwa Muislamu au sio Muislamu, kumuusia mtu ambaye si Muislamu juu ya watoto wake Waislamu baada ya kufa kwake, kwa sababu usia ni aina ya uwalii, na Sheria imeukataa uwalii na utawala wa asiyekuwa Muislamu kwa Muislamu.

## UHUSIANO WA MUISLAM MPYA NA WAZAZI WAKE, NDUGU NA MAHARIMU ZAKE WENGINE:

### KWANZA: Kuwafanyia wema na hisani wazazi ambao sio Waislamu:

Miongoni mwa mambo muhimu sana ambayo yanaipa dini yetu tukufu sifa ya kipekee ni wito wake wa kuwataka Waislamu kuwa na tabia njema na maadili mazuri katika kuishi na watu wote. Muislamu ambaye anajinasibu na dini hii anatakiwa kuwa wa mwanzo katika kuyaonesha maadili na tabia hizi kwa vitendo. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَقُولُوا۟ لِلنَّاسِ حُسْنًا﴾ البقرة: ٨٣.

***"Na waambieni watu maneno mazuri".*** Sura Albaqara: 83. Pia Allah amesema kuwa:

﴿وَجَـٰدِلْهُم بِٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ﴾ النحل: ١٢٥

***"Na jadiliana nao kwa njia iliyo nzuri zaidi".*** Sura Annahli: 125.

Mtume (s.a.w.) ameuusia umati wake kujipamba kwa maadili haya akasema, akitoa maelekezo, kuwa: ***"Unga udugu na yule aliye kukata, na mpe aliyekunyima na msamehe aliyekudhulumu".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad.

Hakuna yeyote mwenye haki zaidi ya kufanyiwa wema na hisani kuliko wazazi ambao wao ndio sababu, baada ya Allah Mtukufu, ya kuja kwa mwanadamu hapa duniani. Ni kwa sababu hiyo ndiyo Allah ameinyanyua hadhi na nafasi yao na kuufanya wema na hisani wanayofanyiwa wazazi iko katika katika daraja ya baada ya daraja ya kumwamini Allah Mtukufu. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿وَٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا۟ بِهِۦ شَيْـًٔا ۖ وَبِٱلْوَٰلِدَيْنِ إِحْسَـٰنًا﴾ النساء: ٣٦.

***"Na muabuduni Allah na msikishirikishe naye kitu chochote".*** Sura Annisaa:36. Na Allah pia amesema kuwa:

﴿وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعۡبُدُوٓاْ إِلَّآ إِيَّاهُ وَبِٱلۡوَٰلِدَيۡنِ إِحۡسَٰنًا﴾ الإسراء: ٢٣.

***"Na Mola wako ameshaamua kuwa usiabudu chochote isipokuwa yeye (Allah tu) na wafanyieni wazazi".*** Sura Al -israa: 23.

Utukufu wa Uislamu umedhihiri wazi pale ulipousia kuwatendea wema wazazi hata kama sio Waislamu. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَوَصَّيۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ بِوَٰلِدَيۡهِ حَمَلَتۡهُ أُمُّهُۥ وَهۡنًا عَلَىٰ وَهۡنٖ وَفِصَٰلُهُۥ فِي عَامَيۡنِ أَنِ ٱشۡكُرۡ لِي وَلِوَٰلِدَيۡكَ إِلَيَّ ٱلۡمَصِيرُ ١٤ وَإِن جَٰهَدَاكَ عَلَىٰٓ أَن تُشۡرِكَ بِي مَا لَيۡسَ لَكَ بِهِۦ عِلۡمٞ فَلَا تُطِعۡهُمَاۖ وَصَاحِبۡهُمَا فِي ٱلدُّنۡيَا مَعۡرُوفٗا﴾ لقمان: ١٤-١٥.

***"Na Tumemuusia mwanadamu (kuwafanyia wema) wazazi wake. Mama yake amemchukulia ujauzito tabu juu ya tabu. Na kuachishwa kwake kunyonya ni katika miaka miwili. (Tumemuusia) kwamba: Nishukuru mimi na (pia washukuru) wazazi wako. Kwangu mimi tu ndio marejeo. Na ikitokea wakakufanyia kila juhudi ili uvishirikishe nami (katika kuabudu) vitu ambavyo huvijui, usiwatii na ishi nao duniani kwa wema".*** Sura Luqman :14-15. Pia Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿وَوَصَّيۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ بِوَٰلِدَيۡهِ حُسۡنٗاۖ وَإِن جَٰهَدَاكَ لِتُشۡرِكَ بِي مَا لَيۡسَ لَكَ بِهِۦ عِلۡمٞ فَلَا تُطِعۡهُمَآ﴾ العنكبوت: ٨.

***"Na Tumemuusia mwanadamu kuwafanyia mazuri wazazi wake na ikitokea wanakufanyia juhudi ili uvishirikishe nami vitu usivyovijua, usiwatii".*** Sura Al-ankabuut: 8.

Imenukuliwa kwa Asmaa Binti Abubakar, Allah awawiye radhi, akisema kuwa: ***"Mama yangu alikuja (kwangu) yeye pamoja na baba yake na yeye (akiwa) ni kafiri katika wakati wa Wakuraishi na muda wao pale walipoingia mkataba wa amani na Mtume (s.a.w.). Nikamtaka ushauri Mtume (s.a.w.) na kusema: Hakika, mama yangu amekuja akiwa mhitaji. Je, nimuunge (kwa kumtekelezea mahitaji yake)? Mtume akasema: Ndio. Muunge mama yako".*** Hadithi hii

imepokewa na Bukhari na Muslim.

Kuwatendea wema wazazi, hata kama sio Waislamu, ni wajibu kwa watoto wao Waislamu. Kwa hiyo, watoto wanatakiwa wasikatae kuwafanyia wema wazazi wao, kuwatii, kuwafanyia hisani na kuwahudumia. Pia wanatakiwa wasiwatukane na kuwaudhi. Haifai kuwafanyia hivyo kwa kisingizio cha kwamba wao sio Waislamu. Uharamu wa kuwatii umebanwa katika Uislamu katika hali ya wazazi kuwaamrisha watoto wamuasi Allah Mtukufu, kama vile kuwataka wauache Uislamu, au waache kutekeleza faradhi na mambo ya wajibu ambayo Uislamu umeamrisha kuyatekeleza, au kufanya mambo ya haramu ambayo Uislamu umeyaharamisha, kama vile kulewa, kula nyama ya nguruwe, kuzini na mambo mengine ya haramu ambayo Allah Mtukufu ameyakataza. Kanuni kuu katika dini ya Allah, kama alivyoibainisha Mtume wa Allah inasema kwamba: ***"Hakuna kumtii kiumbe katika kumuasi Muumba".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad na Tabarani.

Miongoni mwa mambo makubwa sana ambayo kwayo Muislamu atakuwa anawafanyia wema wazazi wake ni kuwarai na kuwahubiria waingie katika Uislamu kwa kutumia njia nzuri, mahusiano mema na kuwafafanulia uzuri wa dini ya Kiislamu kupitia tabia zake yeye mtoto, kufuata kwake mafunzo ya Uislamu, maadili yake na taratibu zake.

## PILI: Kuwafanyia wema na hisani ndugu ambao sio Waislamu:

Ni katika ustahamilivu wa Uislamu kwamba umemuamrisha Muislamu kuunga udugu wa ndugu na jamaa zake na kuwafanyia hisani hata kama sio Waislamu. Allah Mtukufu, akiwapa maelekezo waja wake waumini, amesema kuwa:

﴿ وَٱعۡبُدُواْ ٱللَّهَ وَلَا تُشۡرِكُواْ بِهِۦ شَيۡـٔٗاۖ وَبِٱلۡوَٰلِدَيۡنِ إِحۡسَٰنٗا وَبِذِي ٱلۡقُرۡبَىٰ وَٱلۡيَتَٰمَىٰ وَٱلۡمَسَٰكِينِ
وَٱلۡجَارِ ذِي ٱلۡقُرۡبَىٰ ﴾ النساء: ٣٦.

***"Na muabuduni Allah na msikishirikishe naye kitu chochote, na (watendeeni) wazazi wenu wawili hisani na pia ndugu".*** Sura Annisaa: 36.

Na amesema Allah Mtukufu akibainisha tabia za Mtume (s.a.w) katika kujipendekeza kwa ndugu zake hata kama sio Waislamu kwamba:

﴿قُل لَّآ أَسۡـَٔلُكُمۡ عَلَيۡهِ أَجۡرًا إِلَّا ٱلۡمَوَدَّةَ فِي ٱلۡقُرۡبَىٰ﴾ الشورى: ٢٣.

***“Sema (uwaambie) kuwa: Mimi sikuombeni malipo isipokuwa tu upendo katika udugu”.*** Sura Ash-shuura:23.

Imenukuliwa katika Hadithi kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***“Hakika familia ya fulani sio wapenzi wangu. Kwa hakika kabisa, kipenzi changu ni Allah na waumini wema, lakini (familia hiyo ya fulani) wana udugu (na mimi). Nina uunga udugu huo kwa wema unaostahiki”.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Ni wajibu kwa Muislamu kuwa na mahusiano mazuri na ndugu zake, awe na mawasiliano nao hata kama wao watamtenga. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) isemayo kuwa: ***“Muungaji udugu hatakiwi kuwa mwenye kulipiza (kisasi), na lakini muungaji udugu (wa kweli) ni yule ambaye udugu wake ukikatwa yeye anauunga”.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

Ni wajibu wake kujipendekeza kwao kwa njia nzuri na kuwafanyia mema ili kuwashawishi na kuwavuta katika dini ya Kiislamu.

Ni wajibu wake pia kumsaidia masikini na mwenye shida miongoni mwa ndugu zake hao, kwa sababu yote haya ni katika kufanya wema na hisani aliyoiamrisha Allah. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿لَّا يَنۡهَىٰكُمُ ٱللَّهُ عَنِ ٱلَّذِينَ لَمۡ يُقَٰتِلُوكُمۡ فِي ٱلدِّينِ وَلَمۡ يُخۡرِجُوكُم مِّن دِيَٰرِكُمۡ﴾ المتحنة: ٨.

***“Allah hakukatazeni (kuwafanyia wema na uadilifu) wale ambao hawajakupigeni vita katika Dini na hawajakutoeni katika nchi zenu”.*** Sura Almumtahina:8.

Mtume (s.a.w.) alipewa zawadi ya nguo. Nguo moja moja akampa Omar Ibni-khataab, Allah amuwiye radhi. Omar naye akampa zawadi nguo hiyo kaka yake miongoni mwa watu wa Makka kabla ya kusilimu.

Ni wajibu wa Muislamu kujua kwamba kuunga udugu ni chanzo

cha kheri kwake hapa duniani na kesho akhera. Allah humbarikia muungaji udugu umri wake na riziki zake, na uungaji huo unakuwa sababu ya yeye kuingia Peponi. Imenukuliwa kwa Abu-ayoub Al-ansaary, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa, mtu mmoja alisema ***"Ewe Mtume wa Allah, nifahamishe amali itakayoniingiza peponi. Mtume wa Allah akasema: Muabudu Allah na usikishirikishe naye kitu chochote, simamisha Sala, toa zaka na unga udugu".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Imenukuliwa kwa Anas, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa Mtume wa Allah (s.a.w.) amesema kwamba: "**Yeyote anayependa kuongezewa katika riziki zake na athari yake ichelewe kuondoka, aunge udugu wake".** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Muislamu hatakiwi kusahau kwamba lengo lake kubwa ni kuwaokoa ndugu zake na familia yake isipate ghadhabu za Allah na adhabu yake. Kwa maana hiyo, anatakiwa kuwa na hima ya kuwavuta waingie katika Uislamu kila anapopata fursa. Allah amemuusia Mtume wake (s.a.w.) ailinganie familia yake na ndugu zake wa karibu. Amesema kuwa:

﴿وَأَنذِرْ عَشِيرَتَكَ ٱلْأَقْرَبِينَ﴾ الشعراء: ٢١٤.

***"Na waonye ndugu zako wa karibu".*** Sura Ash-shuaraa: 214. Ameusiwa hivyo huku akitakiwa, katika kuwahuburia ndugu zake, kutumia lugha na mawaidha mazuri. Allah amesema kuwa:

﴿ٱدْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلْحِكْمَةِ وَٱلْمَوْعِظَةِ ٱلْحَسَنَةِ ۖ وَجَٰدِلْهُم بِٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ﴾ النحل: ١٢٥.

***"Lingania (ita watu) kwenye njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mazuri, na jadiliana nao kwa njia ambayo ni nzuri".*** Sura Annahli: 125.

## MAHUSIANO YA KIFEDHA KWA MUISLAMU

### KWANZA: Huduma

Huduma ni chakula, kinywaji, mavazi na malazi anayotoa mtu, bila ya ubadhirifu, kwa ajili ya kuwahudumia wazazi wake, mke wake na watoto wake.

Huduma hii ni wajibu kwa mtoaji, hata dini yake inatofautiana na dini ya anayepewa huduma hiyo. Allah ameeleza kuhusu wazazi aambao sio Waislamu kwamba:

﴿وَإِن جَٰهَدَاكَ عَلَىٰٓ أَن تُشۡرِكَ بِي مَا لَيۡسَ لَكَ بِهِۦ عِلۡمٞ فَلَا تُطِعۡهُمَاۖ وَصَاحِبۡهُمَا فِي ٱلدُّنۡيَا مَعۡرُوفٗا﴾

لقمان: ١٥.

***"Na ikitokea wakakufanyia kila juhudi ili uvishirikishe nami (katika kuabudu) vitu ambavyo huvijui, usiwatii na ishi nao duniani kwa wema".*** Sura Luqman: 15. Ni katika kuwa nao kwa wema kuwahudumia, kwa sababu haiwezekani mtu akawa anaishi maisha mazuri, wakati wazazi wake wanaishi kwenye maisha magumu na ya ufukara.

Na hali ni hiyo hiyo kuhusu na watoto. Huduma zao kwa baba yao ni wajibu hata kama sio Waislamu. Hii ni kwa sababu huduma ni mahusiano na ni msaada, mambo ambayo ni miongoni mwa haki za udugu. Allah Mtukufu amuewekea udugu haki na kubainisha kuwa ukafiri hauifuti haki hiyo, kama ilivyo elezwa katika aya iliyotangulia.

Na katika yanayotilia nguvu wajibu wa huduma pamoja na tofauti za dini, ni maelezo yaliyopo kwenye Hadithi ya Asmaa, Allah amuwiye radhi, pale alipomtaka idhini Mtume wa Allah (s.a.w.) kumsaidia mama yake. Mtume alimjibu kuwa: ***"Muunge mama yako".***

Amesema Imam Alkhattaabiy kuwa: ***"Kwenye Hadithi hii limo fundisho kwamba udugu wa kafiri unaungwa kwa mali n.k kama***

***unavyoungwa udugu wa Muislamu. Kutokana na Hadithi hiyo, tunapata fundisho kwamba ni wajibu kumhudumia baba kafiri na mama kafiri, hata kama mtoto ni Muislamu".*** Fat-hulbaari: 234/5.

Muhammad Bin Hassan anasema kuwa: ***"Ni wajibu kwa mtoto Muislamu kuwahudumia wazazi wake Dhimmiy (wasiokuwa Waislamu wanaoishi katika nchi ya Kiislamu kwa kukubali kufuata taratibu za utawala wa Kiislamu). Allah Mtukufu amesema kuwa:***

﴿وَصَاحِبۡهُمَا فِي ٱلدُّنۡيَا مَعۡرُوفٗاۖ﴾ لقمان: ١٥.

***"Na ishi nao duniani kwa wema". Sura Luqman: 15. Sio katika kuishi na wazazi kwa wema kwamba, mtoto anajivinjari na neema za Allah na kuwaacha wazazi wake wakifa kwa njaa. Wajukuu, mababu na mabibi kwa upande wa baba na upande wa mama ni sawa na baba na mama katika suala hili. Kustahiki kwao kupata huduma kwa kuzingatia uzazi ni sawa na kustahiki kwa baba na mama".*** Almabsuut: 105/4.

Katika wale walio wajibu kwa Muislamu kuwahudumia ni mke Dhimmiy (Mkristo au Myahudi), kwa sababu huduma ni sheria katika sheria za ndoa sahihi. Kumuoa mwanamke Mkristo au Myahudi ni katika mambo ambayo Uislamu umeyaruhu na kuyakubali. Muktadha wa ruhusa hii ni kuwepo kwa wajibu wa kumhudumia.

Ama mke ambaye sio Mkristo au Myahudi, na huyu ni ambaye hafuati dini ya mbinguni, ni kwamba haijuzu kwa Muislamu kubaki naye kwenye ndoa, kwa mujibu wa kauli ya Allah isemayo kuwa:

﴿وَلَا تُمۡسِكُواْ بِعِصَمِ ٱلۡكَوَافِرِ﴾ الممتحنة: ١٠.

***"Na msiwaweke kwenye hifadhi (ya ndoa zenu) wanawake makafiri".*** Sura Almumtahinah:10. Ikiwa ndoa imebatilika, yatabatilika pia masuala mengine yanayotokana nayo likiwemo suala la wajibu wa huduma.

## PILI: Mahari

Ikiwa mtu amemtolea mahari mkewe kabla ya Uislamu, baadae mke na mume wakasilimu, na ikawa mwanamke ameshapokea mahari

yake kabla ya kusilimu, mume hatodaiwa mahari nyengine badala yake baada ya kusilimu, hata kama mahari ambayo mwanamke aliipokea ni haramu kuitwa mahari, kama vile nguruwe au pombe.

Ama iwapo mwanamke bado hajapokea mahari yake, hapo itakuwa wajibu kubadilisha mahari hiyo ambayo ni haramu. Anatakiwa ampe mahari mengine yanayofanana na mahari wanayopewa wanawake wengine kama yeye, kwa sababu Uislamu haukubali kwa mwanamke wa Kiislamu kupewa mahari haramu.

Ikiwa amekabidhiwa baadhi ya mahari na baadhi kubaki kwenye dhima ya mume, atastahiki kupewa sehemu iliyobaki katika mahari yake.

## TATU: Mirathi

Kurithiana baina ya ndugu ni katika sheria ambazo Uislamu umekuja kuziwekea kanuni na kuzipangilia. Allah Mtukufu amewatengea watu fulani katika ndugu fungu katika mali ya ndugu yao aliyefariki, kwa mujibu wa misingi na kanuni maalumu.

Wanazuoni wamebainisha kuwa kustahiki kwa ndugu kupata urithi wa mali iliyowachwa na ndugu yake anayemrithi, hakutakuwepo ila tu baada ya kukamilika kwa masharti yake na kukosekana kwa pingamizi zake. Miongoni mwa masharti muhimu sana ni kuwa na dini moja kwa mrithi na mrithiwa. Kutokea hapo, sheria imeamua kwamba tofauti ya dini ni pingamizi la kurithiana baina ya ndugu, sawa mrithi awe ni Muislamu au kafiri, au mrithiwa awe ni Muislamu au kafiri. Imenukuliwa kwa Usama Bin Zaid, Allah amuwiye radhi, akisema kwamba, amesema Mtume (s.a.w.) kuwa: ***"Muislamu hamrithi kafiri na kafiri hamrithi Muislamu".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Pia imenukuliwa kwa Abdillahi Bin Amri, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa amesema Mtume wa Allah (s.a.w.) kwamba: ***"Hawarithiani watu wenye dini mbili tofauti".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi, Tirmidhiy na Ibnimaja.

## NNE: Mali iliyochumwa kabla ya Uislamu

Mali iliyochumwa na mtu ambaye sio Muislamu kabla ya kusilimu

kwake, ikiwa aliichuma kwa njia halali kama vile biashara ya bidhaa halali, au kwa ujuzi wa kazi iliyo halali au kwa njia zisizokuwa hizo na ambazo, kimsingi, ni halali katika Uislamu, mali hii ni halali tu bila ya mjadala wowote.

Mikataba na makubaliano ambayo yalifanyika kabla ya kusilimu kwake na muda wake ukawa unaendelea mpaka baada ya kusilimu, mikataba hiyo itakuwa ni mikataba sahihi, na zitatekelezwa athari zake zinayopelekea kustahikia kwa thamani (malipo) kwa muuzaji, na kuwajibika kukabidhi bidhaa kwa mnunuzi.

Ama ikiwa mtu ameichuma mali kwa njia haramu, kama vile mikataba ya riba, kamari, biashara ya vitu vilivyoharamishwa, kama kuuza nguruwe, pombe na madawa ya kulevya, ikiwa mtu aliingia makubaliano haramu na kupokea kilichopelekea makubaliano hayo kabla ya kuingia kwenye Uislamu, atasamehewa alichochukua hata kama ni haramu. Haitomlazimu kuitoa mali iliyo haramu kutoka kwenye msingi wa mali yake, kwa sababu hayo yalitokea kabla ya kusilimu kwake. Uislamu unafuta yaliyofanyika kabla yake, kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿قُل لِّلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ إِن يَنتَهُواْ يُغۡفَرۡ لَهُم مَّا قَدۡ سَلَفَ﴾ الأنفال: ٣٨.

***"Sema uwaambie waliokufuru kwamba: Wakikanyika (na kuacha ukafiri) watasamehewa (madhambi yao) yaliyopita".*** Sura Al-anfaal: 38.

Pia amesema Allah kuhusu wale wanaofanya miamala ya riba kwamba:

﴿فَمَن جَآءَهُۥ مَوۡعِظَةٞ مِّن رَّبِّهِۦ فَٱنتَهَىٰ فَلَهُۥ مَا سَلَفَ﴾ البقرة: ٢٧٥.

"***Basi yule ambaye yamemfikia mawaidha kutoka kwa Mola wake na kwa sababu hiyo, akakanyika (akaacha), basi ni haki yake kilichopita (alichokichuma huko nyuma)".*** Sura Albaqara: 275.

Na iwapo uingiaji katika makubaliano haramu ni kabla ya Uislamu, na mtu akawa amesilimu kabla ya kupokea haki inayotokana na makubaliano hayo, itakuwa sio halali kwake kuendelea na makubaliano hayo ya haramu. Makubaliano hayo yanahesabiwa kuwa yamevunjika.

Kama atakuwa ameshapokea sehemu ya haki, na sehemu nyingine hajapokea, atakubaliwa alichokwisha pokea na sehemu ambayo hajapokea itatoweka. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَذَرُواْ مَا بَقِىَ مِنَ ٱلرِّبَوٰٓاْ﴾ البقرة: ٢٧٨.

***"Enyi mlioamini, muogopeni Allah na acheni kilichobaki katika riba".*** Sura Albaqara: 278.

Na imenukuliwa katika Hadithi kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Na riba ya Kijahiliya (zama za kabla ya Uislamu) imefutwa".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. Mtume (s.a.w.) ameibatilisha riba ya Kijahiliya baada ya kuingia kwenye Uislamu, na hakugusia iliyokuwa kabla ya Uislamu na hakuamrisha kurejeshwa kwake. Hiyo ina maana kwamba riba hiyo inabaki kuwa milki ya aliyeichuma na kupokea thamani yake.

Imenukuliwa kwa Ibniabbas, Allah amuwie radhi yeye na mzazi wake, akisema kuwa amesema Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Kila ugawaji uliofanyika katika Ujahilia, utabaki hivyo kama ulivyogawiwa. Na kila ugawaji uliokutwa na Uislamu unatakiwa uwe kwa mujibu wa ugawaji wa Kiislamu".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi, Tirmidhiy na Ibnimaja.

## MAHUSIANO YA KIJAMII NA KIBINADAMU

### KWANZA: Kupenda na kunusuru (kutetea).

Pamoja na kwamba Uislamu unawahimiza wafuasi wake kufanya wema na uadilifu, katika mahusiano yao ya kuishi na viumbe wa Allah, vyovyote itakavyokuwa mielekeo yao na dini zao, ila tu umesisitiza kwamba uhusiano huo unapaswa usimfikishe Muislamu kwenye uvukaji mipaka katika mahusiano baina yake na baina ya mtu ambaye sio Muislamu, na kumfikisha hatua ya kupendana kwa undani, kunusuru na kutetea. Kupendana kwa undani hakutakiwi kuwepo isipokuwa tu kwa wale ambao Allah amutafahamisha katika kauli yake inayosema kwamba:

﴿ إِنَّمَا وَلِيُّكُمُ ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ﴾ المائدة: ٥٥.

***"Hakika, si vingine ispokuwa kwamba, kipenzi chenu ni Allah na Mtume wake na walioamini tu".*** Sura Al-maida:55.

Ama wasiokuwa hao, hakuna kuwapenda mapenzi ya undani (kusafiana nia). Aamesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿لَّا يَتَّخِذِ ٱلْمُؤْمِنُونَ ٱلْكَٰفِرِينَ أَوْلِيَآءَ مِن دُونِ ٱلْمُؤْمِنِينَ﴾ آل عمران: ٢٨.

***"Waumini wasiwafanye makafiri vipenzi badala ya waumini (wenzao)".*** Sura Aal-imraan: 28. Pia amesema Allah akiwaambia Waislamu kwamba:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَتَّخِذُواْ ٱلْيَهُودَ وَٱلنَّصَٰرَىٰٓ أَوْلِيَآءَۘ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَآءُ بَعْضٍۚ وَمَن يَتَوَلَّهُم مِّنكُمْ فَإِنَّهُۥ مِنْهُمْ﴾ المائدة: ٥١.

***"Enyi mlioamini, msiwafanye Wayahudi na Wakristo vipenzi. Wao kwa wao ni vipenzi. Na yeyote atakayewafanya vipenzi, huyo ni miongoni mwao".*** Sura Almaaida: 51. Pia Allah amesema kuwa:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَتَّخِذُواْ عَدُوِّي وَعَدُوَّكُمۡ أَوۡلِيَآءَ تُلۡقُونَ إِلَيۡهِم بِٱلۡمَوَدَّةِ وَقَدۡ كَفَرُواْ بِمَا جَآءَكُم مِّنَ ٱلۡحَقِّ﴾
الممتحنة: ١.

***"Enyi mliaomini, msiwafanye maadui zangu na maadui zenu kuwa vipenzi mnaokutana nao kwa mapenzi ya ndani ilhali wameikufuru haki iliyokujieni".*** Sura Almumtahina: 1.

Mapenzi ambayo Allah ameyakataza yako aina mbili:

**Kwanza: Mapenzi ambayo ni ukafiri.** Haya ni mapenzi ambayo yanapelekea kuwapenda wasiokuwa Waislamu kwa ajili ya dini yao, au kusaidiana nao kwa ajili ya dini yao na kusaidia katika kuifanya dini yao hiyo kuwa juu kuiko dini ya Kiislamu. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿لَّا تَجِدُ قَوۡمٗا يُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِ يُوَآدُّونَ مَنۡ حَآدَّ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَلَوۡ كَانُوٓاْ ءَابَآءَهُمۡ أَوۡ أَبۡنَآءَهُمۡ أَوۡ إِخۡوَٰنَهُمۡ أَوۡ عَشِيرَتَهُمۡ﴾ المجادلة: ٢٢.

***"Hutowapata watu wanaomuamini Allah na Siku ya Mwisho (siku ya Kiama) wanawapenda mapenzi ya dhati wale wanaompiga vita Allah na Mtume wake, hata kama ni baba zao au watoto wao au ndugu zao au jamaa zao".*** Sura Almujaadala: 22.

Kwa hiyo, ni wajibu kwa Muislamu kujitenga na maadui wa Allah na maadui wa dini yake, hata kama ni ndugu zake, ikiwa ni kumuiga Mtume wa Allah Ibrahim, Allah amfikishie amani, katika tangazo lake la kuwatenga maadui wa Allah. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿قَدۡ كَانَتۡ لَكُمۡ أُسۡوَةٌ حَسَنَةٞ فِيٓ إِبۡرَٰهِيمَ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥٓ إِذۡ قَالُواْ لِقَوۡمِهِمۡ إِنَّا بُرَءَٰٓؤُاْ مِنكُمۡ وَمِمَّا تَعۡبُدُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ كَفَرۡنَا بِكُمۡ وَبَدَا بَيۡنَنَا وَبَيۡنَكُمُ ٱلۡعَدَٰوَةُ وَٱلۡبَغۡضَآءُ أَبَدًا حَتَّىٰ تُؤۡمِنُواْ بِٱللَّهِ وَحۡدَهُۥٓ﴾ الممتحنة: ٤.

***"Hakika, umekuwa mfano mzuri kwenu (wa kuiga) kwa Ibrahimu na wale waliokuwa pamoja naye, pale walipowaambia watu wao kwamba: Hakika, sisi ni wenye kujitenga nanyi na (pia sisi ni wenye kujitenga na) hivyo mnavyoviabudu badala ya Allah. Tumekukataeni, na umedhihiri wazi baina yetu na baina yenu uadui na chuki milele mpaka mtakapomuamini Allah peke yake".*** Sura Almumtahina: 4.

**PILI: Mapenzi ambayo ni haramu.** Mapenzi haya ni pale inapokuwa kuwapenda watu ambao sio Waislamu ni kwa ajili ya maslahi ya kidunia, pamoja na kuwa Muislamu anawachukia makafiri na kuwapenda Waislamu na kutamani wawe na nguvu na wawe juu, lakini kuwapenda kwake makafiri kumeingia moyoni mwake kwa sababu ya maslahi ya kidunia ya pamoja. Kwa mfano: Mtu anajipendekeza kwa maadui wa Allah ili wamsaidie kupata kazi fulani, au kuwafanyia ujasusi kwa faida yao kwa tamaa ya kupata pesa nyingi wanazotoa. Aina hii ya upendo hata kama haimtii mtu katika ukafiri, ila ni maasi mazito na ni dhambi kubwa.

Ama Muislamu ikimtokea kupata madhara au kulazimishwa na wasiokuwa Waislamu kufanya jambo dhidi ya Uislamu, na akahofia usalama wake, usalama wa dini yake na usalama wa heshima yake, lakini uadui wake kwa makafiri hao umejikita ndani ya nafsi yake, hatakuwa na kosa wala dhambi, kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿لَّا يَتَّخِذِ ٱلْمُؤْمِنُونَ ٱلْكَـٰفِرِينَ أَوْلِيَآءَ مِن دُونِ ٱلْمُؤْمِنِينَ ۖ وَمَن يَفْعَلْ ذَٰلِكَ فَلَيْسَ مِنَ ٱللَّهِ فِى شَىْءٍ إِلَّآ أَن تَتَّقُوا۟ مِنْهُمْ تُقَىٰةً﴾ آل عمران: ٢٨.

***"Walioamini wasiwafanye makafiri vipenzi wao wa undani badala ya waumini (wenzao). Na mwenye kufanya hivyo, hana chochote kwa Allah (katika imani) ila tu kama mtajikinga nao (kwa kuhofia kukudhuruni)".*** Sura Aal-imraan:28. Maana ni kwamba: Kama mtahofia usalama wenu, mali zenu au heshima zenu, kutakuwa hakuna ubaya kuwaonesha urafiki wa nje tu kwa maneno, madamu nyoyo zenu zimetulizana kwenye imani. Amesema Allah Mtukufu kuwa:

﴿مَن كَفَرَ بِٱللَّهِ مِنۢ بَعْدِ إِيمَـٰنِهِۦٓ إِلَّا مَنْ أُكْرِهَ وَقَلْبُهُۥ مُطْمَئِنٌّۢ بِٱلْإِيمَـٰنِ وَلَـٰكِن مَّن شَرَحَ بِٱلْكُفْرِ صَدْرًا فَعَلَيْهِمْ غَضَبٌ مِّنَ ٱللَّهِ وَلَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ﴾ النحل: ١٠٦.

***"Yeyote aliyemkufuru Allah baada ya kumuamini kwake (atapata adhabu kali), isipokuwa yule aliyelazimishwa (kufanya ukafiri) ilhali moyo wake umetulizana kwenye imani. Na lakini wale ambao wamekunjua vifua (vyao) kwa (kuuridhia), hao itawashukia ghadhabu za Allah na watapata adhabu kubwa".*** Sura Annahli: 106.

Hayaingii katika mapenzi yaliyokatazwa yale mapenzi ya kimaumbile yaliyopo baina ya Muislamu na asiyekuwa Muislamu, kwa sababu ya udugu au ukwe, kama kuwapenda wazazi au mke ilimradi tu yasivuke na kufikia kuipenda dini yake au kuipenda batili aliyo nayo au mapenzi hayo kumshawishi kutenda maovu.

Uislamu haukatazi kufanya mahusiano na wasiokuwa Waislamu kwa kufanya kibiashara, kukodisha, kuazimana, kuuza na kununua. Haya yote hayaingii kamwe katika mlango wa Kupenda na Kutenga. Maisha ya Mtume (s.a.w.) na Swahaba wake, Allah awawiye radhi, yamejaa matukio yanayo onesha kuwa wao walikuwa wakihusiana na wasiokuwa Waislamu kwa kuuziana, kununuliana, kuazimana, kukodishana na miamala mingine ya kibiashara.

## PILI: Uadilifu na utendaji haki:

Allah Mtukufu amewaamrisha waja wake kufanya uadilifu katika mambo yao yote ya maisha yao. Allah amesema kuwa:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُونُواْ قَوَّٰمِينَ بِٱلْقِسْطِ شُهَدَآءَ لِلَّهِ وَلَوْ عَلَىٰٓ أَنفُسِكُمْ أَوِ ٱلْوَٰلِدَيْنِ وَٱلْأَقْرَبِينَ ﴾ النساء: ١٣٥.

***"Enyi mlioamini, kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mkiwa mashahidi wa Allah hata kama ushahidi huo utakuwa dhidi ya nafsi zenu au wazazi na ndugu wa karibu sana".*** Sura Annisaa: 135.

Pia Allah metoa angalizo kwamba, kuwachukia watu na kuwa uhasama nao hakutakiwi kumfanye Muislamu afanye dhulma. Anatakiwa awe muadilifu hata kwa maadui zake. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿ يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُونُواْ قَوَّٰمِينَ لِلَّهِ شُهَدَآءَ بِٱلْقِسْطِ ۖ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَـَٔانُ قَوْمٍ عَلَىٰٓ أَلَّا تَعْدِلُواْ ۚ ٱعْدِلُواْ هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ ﴾ المائدة: ٨.

***"Enyi mlioamini, kuweni watekelezaji uadilifu, mashahidi wa Allah. Na kuwachukia watu kusikuchukueni mkaacha kufanya uadilifu. Kuweni waadilifu. Huko ndio kuwa karibu zaidi na uchaji".***

Sura Almaida: 8.

﴿لَّا يَنْهَىٰكُمُ ٱللَّهُ عَنِ ٱلَّذِينَ لَمْ يُقَـٰتِلُوكُمْ فِى ٱلدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُم مِّن دِيَـٰرِكُمْ أَن تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوٓا۟ إِلَيْهِمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُقْسِطِينَ﴾ الممتحنة: ٨.

Na amesema Allah kuwa: "***Allah hakukatazeni kuwafanyia wema na uadilifiu wale ambao hawakupigeni vita kwa sababu ya dini wala hawakutoeni katika nchi zenu. Hakika, Allah anawapenda waadilifu".*** Sura Almumtahina: 8.

## TATU: Kuheshimu mikataba na makubaliano.

Uislamu unasisitiza kwamba kuheshimu ahadi, mikataba na makubaliano ni miongoni mwa misingi mikubwa sana ambayo dini ya Kiislamu inasimamia. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَوْفُوا۟ بِٱلْعُقُودِ﴾ المائدة: ١.

***"Enyi mlioamini, tekelezeni ahadi".*** Sura Almaida:1.

Pia amesema kuwa:

﴿وَأَوْفُوا۟ بِٱلْعَهْدِ ۖ إِنَّ ٱلْعَهْدَ كَانَ مَسْـُٔولًا﴾ الإسراء: ٣٤.

***"Na tekelezeni ahadi. Hakika, ahadi itauliziwa".*** Sura Al-israa: 34.

Pia Allah Mtukufu ameliweka wazi suala la kuheshima ahadi na mikataba hata pamoja na wasiokuwa Waislamu. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿إِلَّا ٱلَّذِينَ عَـٰهَدتُّم مِّنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ثُمَّ لَمْ يَنقُصُوكُمْ شَيْـًٔا وَلَمْ يُظَـٰهِرُوا۟ عَلَيْكُمْ أَحَدًا فَأَتِمُّوٓا۟ إِلَيْهِمْ عَهْدَهُمْ إِلَىٰ مُدَّتِهِمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُتَّقِينَ﴾ التوبة: ٤.

***"Isipokuwa wale makafiri mliowekeana ahadi halafu wakawa hawajakuvunjieni chochote (katika ahadi yenu), na hawakumsaidia yeyote yule dhidi yenu. Basi wakamilishieni ahadi yao mpaka kufikia muda wao. Hakika, Allah anawapenda wachamungu".*** Sura Attauba: 4. Pia Allah amesema kuwa:

﴿ إِلَّا ٱلَّذِينَ عَـٰهَدتُّمْ عِندَ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ ۖ فَمَا ٱسْتَقَـٰمُوا۟ لَكُمْ فَٱسْتَقِيمُوا۟ لَهُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُتَّقِينَ ﴾ التوبة: ٧.

***"Isipokuwa wale ambao mliwekeana nao ahadi kwenye Msikiti Mtukufu (wa Makka). Watakapokuwa na msimamo kwenu (katika kuheshimu ahadi na makubaliano) na nyie kuweni na msimamo kwao (katika kuheshimu ahadi na makubaliano). Hakika, Allah anawapenda wachamungu".*** Sura Attauba:7.

Maisha ya Wema wa umma huu waliotangulia, Allah awarehemu, yamejaa matukio yanayo onesha kuheshimu kwao ahadi na makubaliano walioafikiana na watu ambao sio Waislamu. Hudhaifa Ibnil-yamani wakati makafiri walipomteka yeye na baba yake, na wakataka kuwaachia huru, waliwawekea sharti kwamba waende Madina, na wasiende Badri kwa Mtume (s.a.w.) na Swahaba wake. Waliahadi kuwa watatekeleze ahadi. Hudhaifa na baba yake yake walikwenda kwa Mtume (s.a.w.) na kumpa habari hiyo. Mtume aliwaambia kuwa: ***"Ondokeni. Sisi tunatakiwa kutimiza ahadi yao, na sisi tunamuomba msaada Allah dhidi yao".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. Tazama namna Mtume (s.a.w) alivyowahimiza Swahaba wako hao kuheshimu makubaliano na kuyatekeleza.

Imenukuliwa kwa Saf-wan Bin Amri na Said Bin Abdulaziz kwamba: ***"Warumi walifanya suluhu na Muawiya kwamba awape mali, na Muawiyah akachukua (mateka) kama rahani kutoka kwao, na mateka akawaweka Balabak. Lakina Warumi walivunja ahadi. Muawiya na watu wake hawakutaka kuhalalisha kuwaua mateka waliokuwa mikononi mwao, bali walwaachia huru, na kwa kufanya hivyo, Muawiya na watu wake waliwashinda Warumi na kusema: Kutekeleza ahadi kwa waliovunja ahadi ni bora kuliko kuvunja ahadi kwa kuvunja ahadi".*** Kitabu cha Al-am-waal cha Abu-ubaid, Uk. 175.

Muislamu ameamrishwa kutovunja ahadi wala kutokuwa na hadaa kwenye ahadi, makubaliano na mikataba yake, madamu hakuna uvunjaji wa sharia ya Allah na dini yake. Kanuni hapa inasema: ***"Hakuna kumtii kiumbe katika kumuasi Muumba".*** Imenukuliwa kwa Aisha, Allah

amuwiye radhi, akisema kuwa Mtume (s.a.w.) amesema kwamba: ***"Sharti lolote lisilokuwemo kwenye kitabu cha Allah ni batili hata yakiwa masharti elfu moja".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Ikiwa mkataba na makubaliano aliofunga mtu kabla ya kusilimu kwake una jambo la haramu, kama vile mkataba wenye riba au mkataba wa biashara vilevi au nyama ya nguruwe au mambo mengine yaliyokatazwa na Uislamu, mkataba huo utakuwa batili kisheria na haitakuwa sahihi kuutekeleza, ila tu mtu kama atalazimishwa kwa nguvu kufanya hivyo.

## NNE: Kutembeleana na kupeana zawadi

Miongoni mwa malengo makubwa sana ya kutembeleana na kupeana zawadi ni kupatikana kwa upendo na kudumisha mshikamano baina ya wanaotembeleana na wanaopeana zawadi. Kwa kuwa upendo na mshikamano huu unahusika na Waislamu, Uislamu umeliwekea sharti suala la kutembeleana na kupeana zawadi baina ya Muislamu na mtu ambaye sio Muislamu. Sharti lenyewe ni hili: Ni lazima lengo liwe ni kulainisha nyoyo za wasiokuwa Waislamu wavutike kwenye Uislamu na kuwahubiria dini ya Allah. Ama ikiwa kutembeleana na kupeana zawadi ni kwa lengo la kujiliwaza tu na kujipendekeza, Muislamu anatakiwa aache kufanya hivyo, kwa kuwa hilo linasababisha madhara mengi, yakiwemo haya yafuatayo:

**1)** Muislam anaweza kuathirika na tabia na tamaduni za wasiokuwa Waislamu, zikiwemo kutokuwa na woga wa kufanya mambo ya haramu na kutojiheshimu, mambo ambayo yana athari mbaya katika dini na tabia za Muislamu.

**2)** Jambo hilo linaweza kuzalisha ndani ya moyo (wa Muislamu) aina fulani ya kuipenda dini yao, na kwa sababu hiyo, likamdhoofishia kuipinga dini batili.

**3)** Jambo hilo linaweza kusababisha upinzani na kutoridhika na sheria za Allah zinazo wahusu wasiokuwa Waislamu, na hasa kwa mtu ambaye analinganisha baina ya tabia za wasiokuwa Waislamu

na maendeleo yao makubwa na baina ya hali waliyonayo Waislamu hivi sasa.

kwa kuzingatia madhara hayo, Mtume (s.a.w.) amemkataza Muislam kuchanganyika na wasiokuwa Waislamu kwa kusema kuwa: ***"Usimfanye rafiki isipokuwa Muislamu tu, na asile chakula chako isipokuwa mchamungu tu".*** Hadithi hii imepokuwa na Ahmad, Abudaudi na Tirmidhi.

Hii haimaanishi kwamba Muislamu anatakiwa ampige pande (amsuse) asiyekuwa Muislamu moja kwa moja. Hakuna ubaya baina ya Muislamu na asiyekuwa Muislamu kutembeleana na kupeana zawadi kwa maslahi ya kidini au hata ya kidunia ambayo sheria inayakubali, kama mgeni ambaye sio Muislamu amefikia kwa Muislamu, au Muislamu kumhubiria asiyekuwa Muislamu aingie kwenye dini ya Allah (s.w.) na kumuongoza kwenye haki, au kama baina ya Muislamu na asiyekuwa Muislamu kuna mahusiano ya kibiashara yanayosababisha kutembeleana na kupeana zawadi. Saidi Ibnilmusayyib, akimnukuu baba yake, amesema kwamba: ***"Kifo kilipomfika Abutalib, Mtume (s.a.w.) aliingia nyumbani kwake akiwa pamoja na Abujahli na Abdallah Bin Abi-umayyah. Mtume (s.a.w.) akamwambia: "Ewe ami yangu, sema: Laa Ilaaha Illa-llah (Hakuna anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Allah tu, (na) nitakutetea kwa hilo mbele ya Allah. Abujahli na Abdallah Bin Abi-umayyah wakamwambia Abutalib: Ewe Abutalib, hivi unataka kuacha mila (dini) ya Abdulmuttalib? Mtume (s.a.w.) akamwambia ami yake: "Nitakuombea msamaha madamu sijakatazwa. Allah Mtukufu akateremsha aya hii:***

﴿مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَن يَسۡتَغۡفِرُواْ لِلۡمُشۡرِكِينَ وَلَوۡ كَانُوٓاْ أُوْلِي قُرۡبَىٰ مِنۢ بَعۡدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُمۡ أَنَّهُمۡ أَصۡحَٰبُ ٱلۡجَحِيمِ﴾ التوبة: ١١٣.

***"Haitakikani kwa Mtume na wale walioamini kuwaombea msamaha makafiri hata kama ni ndugu (zao) baada ya kuwa imewabainikia kuwa wao ni watu wa motoni". Sura Attauba: 113".*** Hadithi hii imepokewa na na Bukhari na Muslim.

Imenukuliwa kwa Anas, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa:

***"Alikuwepo kijana wa Kiyahudi akimuhudumia Mtume (s.a.w.). Kijana huyo aliugua, na Mtume (s.a.w.) akenda kumjuilia hali. Mtume alikaa mbele ya kichwa chake na kumwambia: Silimu (Ingia katika Uislamu). Kijana akamuangalia baba yake, ambaye wakati huo alikuwa mbele yake. Baba akamwambia: Mtii Abalqaasim (Baba Kasimu = Mtume s.a.w.). Kijana akasilimu. Mtume (s.a.w) aliondoka huku akisema:*** (الحمد لله الذي أنقذه من النار) ***Shukurani kwa Allah ambaye amemuokoa kijana asiingie motoni".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari.

Mtume (s.a.w.) alimruhusu Asmaa Binti Abubakar, kama ilivyotangulia kuelezwa, kumkaribisha mama yake kafiri. Omar alimpa kaka yake kafiri zawadi ya nguo aliyopewa na Mtume (s.a.w.).

Inajuzu kwa Muislamu kupokea zawadi kutoka kwa asiyekuwa Muislamu, iwapo zawadi hiyo haijakwenda kinyume na sheria, kama vile msalaba, kichinjo kilichochinjwa kwa ajili ya asiyekuwa Allah, kwa sababu Mfalme wa Misri Mkristo alimpa zawadi Mtume (s.a.w.), na Mtume aliipokea.

## TANO: Kula na kunywa.

Katika mambo ambayo Muislamu anatakiwa kuyachunga wakati wa mahusiano yake na wasiokuwa Waislamu ni kwamba, asiwafanye marafiki wa kushirikiana nao kwenye kula na kunywa mpaka ikawa ndio kawaida yake. Hii ni kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) inayosema kwamba: ***"Usimfanye rafiki isipokuwa Muislamu tu, na asile chakula chako isipokuwa mchamungu tu".*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Abudaudi na Tirmidhi.

Ama asiyekuwa Muislamu akiwa mgeni wa Muislamu, au Muislamu akiwa mgeni wa asiyekuwa Muislamu, hakuna ubaya kumpa chakula na kinywaji au yeye kupewa chakula na kinywaji kinachotokana na ukarimu wake, ikiwa chakula na kinywaji hicho hakina vitu viliyoharamishwa na Uislamu. Amesema Mtume (s.a.w.): ***"Yeyote Mwenye kumuamini Allah na Siku ya Mwisho, amkirimu mgeni wake".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Kumkirimu mgeni ni jambo lililoamrishwa kisheria, hata kama mgeni sio Muislamu kwa sababu, katika kumkirimu mgeni huyo kuna wito wa kumuita kwenye Uislamu na kumuelekeza kwenye kheri, ili aelewe mazuri na mema ya dini hii na tabia nzuri zilizomo.

Ujumbe wa Thaqiif ulimjia Mtume (s.a.w.) Madina na wao wakiwa makafiri. Mtume aliwakirimu na kuwalingania kwenye Uislamu mpaka wakasilimu. Pia Mtume (s.a.w.) alialikwa chakula na mwanamke wa Kiyahudi. Alikubali mwaliko huo na kula chakula chake, katika kisa mashuhuri cha kondoo aliyetiwa sumu.

Mfano wa hilo pia ni lau kama Muislamu amealikwa kwenye Walima (karamu), na kwenye karamu hiyo wamejumuika watu ambao sio Waislamu. Hakuna ubaya kula pamoja nao, kwa sababu yeye hakukusudia kufanya nao urafiki, isipokuwa kilichowakusanya ni chakula, kama vile linavyowakusanya soko na sehemu nyingine za mijumuiko ya umma.

Kwa ufupi, cha kuzingatia ni kwamba kinachokatazwa katika kula na kunywa na watu ambao sio Waislamu ni ule urafiki, mshikamano na uswahiba endelevu kwenye hilo. Ama hali na mazingira ya mpito, hakuna ubaya kufanya hivyo, na hakuna pingamizi katika kushirikiana nao kwenye kula na kunywa.

Katazo hili la kula na wasiokuwa Waislamu ni katika suala la kulinda dini ya Muislamu asije akaathirika na ada, tabia, utamaduni na mwenendo wa wasiokuwa Waislamu au kuathirika kwa kuvutiwa na dini yao.

## SITA: Kusalimiana

Inafaa kwa Muislamu kuanza kumsalimia mtu ambaye sio Muislamu kwa kutumia maamkizi ambayo sio ***(Assalaamu Alaykum* السلام عليكم*)***, kama vile kumwambia ***Karibu au Ahlan wa Sahlan (umefika kwako na jisikie vyema)***, na matamshi mengine kama hayo. Hii ni kwa mujibu wa kauli iliyothibiti kunukuliwa kwa Mtume (s.a.w.) kwamba: ***"Msianze kuwasalimia Wayahudi na Wakristo kwa salamu (Assalaamu Alaykum* السلام عليكم*)".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim. Mtume (s.a.w.) alikuwa akizianza barua

zake anazowapelekea wafalme na watawala kwa kusema: ***"Amani iwashukie wenye kufuata mwongozo السلام على من اتَّبَعَ الهُدَى".***

Inajuzu kwa Muislamu kujibu maamkizi ya Salamu ikiwa atasalimiwa yeye kwanza na mtu ambaye sio Muislamu. Hii ni kwa mujibu wa ujumla wa kauli ya Allah Mtukufu isemayo kuwa:

﴿وَإِذَا حُيِّيتُم بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوا۟ بِأَحْسَنَ مِنْهَآ أَوْ رُدُّوهَآ﴾ النساء: ٨٦.

***"Na mkiamkiwa kwa maamkizi yoyote basi rejesheni maamkizi (hayo) kwa maamkizi mazuri zaidi ya hayo, au rejesheni hayo hayo".*** Sura Annisaa:86.

Imenukuliwa kwa Abu-uthman Annahdi akisema kuwa: ***"Abumusa alimuandikia barua Dihkaan akimsalimu kwa Salaam kwenye barua yake. Akaulizwa: Unamsalimaje kwa Salaam Dikani wakati yeye ni kafiri? Abumussa akajibu: Yeye ameniandikia barua na kunisalimia kwa Salaam na mimi nimemjibu".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari kwenye kitabu Al-adabul Mufrad.

Iwapo kwenye baraza (mkusanyiko wa watu) wamechanganyika Waislamu na wasiokuwa Waislamu, itajuzu kuanza kusalimia kwa Salaam na kuwakusudia Waislam kwa Salaam yako hiyo. Hii inatokana na Hadithi iliyothibiti kunukuliwa kwa Usama Bin Zaid, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: ***"Mtume wa Allah (s.a.w.) alipanda punda na Usama yuko nyuma yake, wakienda kwa familia ya Baniharith Bin Alkhazraj kumjulia hali Saad Bin Ubada, kabla ya vita vya Badri. Walikwenda mpaka wakapita kwenye baraza la watu waliokuwa wamekaa, akiwepo humo Abdalla Bin Ubayyi Bin Saluul. Hiyo ilikuwa kabla ya kusilimu kwa Abdalla Bin Ubayyi Bin Saluul. Kwenye baraza hiyo kulikuwa kuna mchanganyiko wa Waislamu na washirikina wanao abudu masanamu na Wayahudi pia walikuwepo. Katika Waislamu alikuwepo Abdalla Bin Rawaaha. Vumbi la punda lilipolifunika baraza, lile Abdalla Bin Ubayyi alifunika pua yake kwa mtandio wake na kusema: Msitutie mavumbi. Mtume wa Allah (s.a.w) aliwasalimia kwa Salaam, alisimama, aliteremka, aliwahubiria na kuwaita kwenye dini ya Allah na kuwasomea Qur'ani".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

## WAJIBU NA MAJUKUMU YA KIDINI

### KWANZA: Msamaha wa majukumu ya Kiislamu yaliyothibiti kabla ya mtu kuingia katika Uislamu.

Umma wa Kiislamu umekubaliana kuwa asiyekuwa Muislamu atakaposilimu, halazimishwi kulipa ibada za wajibu zilizompita kabla ya kusilimu, ni sawa ibada hizo zilikuwa ni sala, funga, zaka au Hija. Allah Mtukufu amesema kuwa:

﴿قُل لِّلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ إِن يَنتَهُواْ يُغۡفَرۡ لَهُم مَّا قَدۡ سَلَفَ﴾ الأنفال: ٣٨.

***"Wambie waliokufuru (kuwa): Ikiwa wataacha (ukafiri) watasamehewa (madhambi yao) yaliyopita".*** Sura Al-anfaal:38.

Mtume (s.a.w.) hakumuamrisha yeyote aliyesilimu kulipa cho chote katika mambo ya faradhi, kwa sababu Uislamu unafuta madhambi yaliyotokea kabla yake, kama Mtume (s.a.w) alivyomwambia hivyo Amri Ibnil-as pale alipokwenda kwa Mtume akiwa amesilimu na kuweka sharti kwamba lazima asamehewe dhambi zake. Mtume (s.a.w) alimwambia: ***"Hivi wewe hujui kuwa Uislamu unavunja yaliyokuwa kabla yake?".*** Hadithi hii imepokewa na Muslim.

Ni katika ukamilifu wa fadhila za Allah kwa waja wake kwamba, anaposlimu hupewa thawabu kwa matendo yake mema aliyoyafanya kabla ya kusilimu kwake. Imenukuliwa kwa Abusaid Alkhudriy, Allah amuwiye radhi, akisema kwamba amesema Mtume (s.aw) kuwa: ***"Mja anaposilimu na Uislamu wake ukawa mzuri, Allah humuandikia kila jambo zuri alilokuwa amelifanya kabla (ya kusilimu) na hufutiwa kila jambo baya alilokuwa amelitenda kabla (ya kusilimu kwake)".*** Hadithi hii imepokewa na Nasai.

Imenukuliwa kwa Hakiim Bin Hizaam, Allah amuwiye radhi, akisema kuwa: "Nilisema (kumwambia Mtume) kuwa: Ewe Mtume wa Allah, unoanaje ibada nilizokuwa nilizafanya katika Ujahili

(wakati wa kabla ya Uislamu) ikiwa ni pamoja na sadaka, kuwaachia huru watumwa na kuunga udugu. Je, kuna thawabu zozote katika hayo? Mtume wa Allah akasema: ***"Umesilimu ukiwa nazo kheri zote ulizozifanya huko nyuma".*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

**PILI: Wajibu wa kufuata sheria za Kiislamu na mafundisho yake.**

Ni wajibu kwa kila mwenye kuingia katika dini ya Kiislamu, awe mwanamke au mwanaume, kufuata sheria za Kiislamu, mafunzo na maadili yake. Ni wajibu wake kutekeleza kila faradhi katika faradhi za Allah Mtukufu, kama vile sala za faradhi, funga ya mwezi wa Ramadhani ikiwa hana udhuru uanomzuwia kufunga, kutoa zaka kwa kumiliki kiwango kinachowajibika kutolewa zaka na kupitiwa na mwaka, kuhiji nyumba tukufu ya Allah akiwa na uwezo, kukamatana na kuvaa Hijabu akiwa ni mwanamke na mambo mengine ya wajibu.

Pia ni wajibu kwake kujiepusha na mambo yaliyoharamishwa na kukatazwa. Anatakiwa asiwadhuru watu wengine kwa kuwauwa, kuwavunjia heshima zao kwa kufanya zinaa au ulawiti, kula mali zao kwa dhuluma kwa njia ya rushwa, wizi na kula riba. Pia anatakiwa kutoidhuru akili yake kwa kutumia vilevi au madawa ya kulevya na mambo mengine yaliyoharamishwa na sheria ya Kiislamu, kama alivyosema Allah Mtukufu kuwa:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ إِذَا جَآءَكَ ٱلۡمُؤۡمِنَٰتُ يُبَايِعۡنَكَ عَلَىٰٓ أَن لَّا يُشۡرِكۡنَ بِٱللَّهِ شَيۡـٔٗا وَلَا يَسۡرِقۡنَ وَلَا يَزۡنِينَ وَلَا يَقۡتُلۡنَ أَوۡلَٰدَهُنَّ وَلَا يَأۡتِينَ بِبُهۡتَٰنٖ يَفۡتَرِينَهُۥ بَيۡنَ أَيۡدِيهِنَّ وَأَرۡجُلِهِنَّ وَلَا يَعۡصِينَكَ فِي مَعۡرُوفٖ فَبَايِعۡهُنَّ وَٱسۡتَغۡفِرۡ لَهُنَّ ٱللَّهَۚ إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٞ رَّحِيمٞ﴾ الممتحنة: ١٢.

***"Ewe Mtume, wakikujia waumini wa kike wakakupa ahadi ya Kiapo cha Utii juu ya kwamba hawatokishirikisha na Allah kitu chochote, hawatozini, hawatoua watoto wao, hawatopeleka uongo (kwa kupeleka mtoto wa uwongo kwenye ukoo) watakao uzusha baina ya mikono yao na miguu yao na kamwe hawatokuasi kwenye wema. Kwa hivyo, wakubalie ahadi ya utii kuwa pamoja nao, na waombee msamaha. Hakika, Allah ni Mwingi wa msamaha, mwenye***

***kurehemu”.*** Sura Almumtahina: 12.

Miongoni mwa sheria ambazo Muislamu mpya anatakiwa kuzichunga pia mwanzo wa kusilimu kwake ni hizi zifuatazo:

**a- Kuoga.**

Sheria inamtaka mwenye kutaka kuingia katika uwislamu kuoga.. Amenukuu Abuhuraira, Allah amuwiye radhi, kwamba ***“Thumama Bin Uthaal, Allah amuwiye radhi, alisilimu. Mtume (s.a.w.) aliwaambia Swahaba kuwa: Mpelekeni kwenye ukuta wa Bani Fulani na mumuamrishe aoge”.*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad.

Imenukulia pia kwa ***“Kaisi Bin Aasim alisilimu, Mtume akamuamrisha aoge kwa maji na kunazi”.*** Hadithi hii imepokewa na Ahmad, Tirmidhi na Nasai.

**b- Kutahiriwa.**

Kutahiriwa ni kuondosha ngozi ya ziada iliyoko kwenye kichwa cha dhakari. Kwa Muislamu mpya, ni wajibu kutahiriwa ikiwa hakuwa ametahiriwa kabla ya kusilimu, kwa sababu nembo na Uislamu na ni katika maumbile ya asili, na pia nayo ni mila ya Mtume Ibrahimu, Allah ampe amani. Mtume (s.a.w.), ametupa habari za Mtume Ibrahimu kuhusiana na hilo kwa kusema: ***“Mtume Ibrahimu, Allah ampe amani, alitahiriwa akiwa na umri wa miaka thamanini”.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim.

Ama ikiwa mtu hakuweza kutahiriwa kutokana na kuhofia kupata madhara kwa sababu ya uzee wake au maradhi, au kushauriwa na daktari muaminifu kuwa kutamsababishia kuvuja damu nyingi itakayoathiri maisha yake, hakutokuwa na ubaya wa kuacha kutahiriwa.

**c- Kujifunza sura Alfaatiha.**

Sura Alfaatiha ni nguzo katika nguzo za sala. Sala haiwi sahihi isipokuwa tu kwa kuisoma sura hii, kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w.) inayosema kuwa: ***“Ambaye hakusoma Sura Alfaatiha, hana sala”.*** Hadithi hii imepokewa na Bukhari na Muslim. Kwa

sababu hii, ni wajibu kwa Muislamu mpya kufanya haraka kujifunza kusoma Sura Alfaatiha kwa matamshi ya lugha ya Kiarabu.

Kama hakuweza kujifunza Sura Alfaatiha haraka, itamtosha kusoma: ***Subhanallah, walhamdu lillah, walaa ilaaha illallah, Allahu Akba***r mpaka hapo atakapojifunza Sura Alfaatiha kwa ukamilifu. Hii ni kwa mujibu wa Hadithi ya Rifaa Bin Raafii kwamba Mtume wa Allah alimwambia kuwa: ***"Tawadha kama alivyokuamrisha Allah Mtukufu, na utoe Shahada, usimame, useme Allahu Akbar. Ikiwa unayo Qur'ani isome. Ikiwa huna Qur'ni soma Subhanallah, Alhamdu Lillaah, Allahu Akbar".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaud na Tirmidhi.

**d- Kujifunza kutawadha.**

Udhu ni sharti la kusihi kwa sala, kwa mujibu wa kauli ya Allah Mtukufu inayosema kuwa:

﴿يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِذَا قُمۡتُمۡ إِلَى ٱلصَّلَوٰةِ فَٱغۡسِلُواْ وُجُوهَكُمۡ وَأَيۡدِيَكُمۡ إِلَى ٱلۡمَرَافِقِ وَٱمۡسَحُواْ بِرُءُوسِكُمۡ وَأَرۡجُلَكُمۡ إِلَى ٱلۡكَعۡبَيۡنِ﴾ المائدة: ٦.

***"Enyi mlioamini, mnaposimama kwenda kwenye sala osheni nyuso zenu na mikono yenu mpaka kwenye viungio, na mpanguse (kwa maji) vichwa vyenu, na muoshe miguu yenu mpaka kwenye nguyu (vifundo)".*** Sura Almaaida: 6.

Na Mtume (s.a.w.) amebainisha kwamba sala bila ya Udhu haikubaliwi. Imenukuliwa kwamba Mtume (s.a.w.) amesema kuwa: ***"Hakika sala ya yeyote katika watu haikamiliki mpaka atawadhe na aufanye vyema Udhu".*** Hadithi hii imepokewa na Abudaudi.

**e- Kufunga Mwezi wa Ramadhani.**

Mtu anapoingia kwenye Uislamu ndani ya mwezi wa Ramadhani, na ikiwa kusilimu kwake ni baada ya kuchomoza kwa Alfajiri, hapo atajizuia na yanayofunguza saumu, na atanuia kufunga kuanzia siku inayofuata na kumalizia siku zilizobakia za mwezi wa Ramadhani. Ama kusilimu kwake kukiwa kabla ya kuchomoza kwa Alfajiri, itamlazimu kufunga mchana unaofuatia na siku zilizobakia, mpaka mwezi wa Ramadhani utakapomalizika. Na katika hali zote hizo,

hatolazimika kulipa siku ambazo bado alikuwa hajasilimu.

**f- Wajibu wa Zakatulfitri.**

Mtu anapoingia kwenye Uislamu kabla ya kuzama kwa jua katika siku ya mwisho wa mwezi wa Ramadhani, itamlazimu kutoa Zakatulfitri, ikiwa atakuwa na ziada ya chakula chake na familia yake usiku na mchana wa siku ya Idi.

Ama atakapoingia kwenye Uislamu baada ya kuzama kwa jua katika siku ya mwisho wa mwezi wa Ramadhani, haitomlazimu kutoa Zakatulfitri.

***MWISHO WA KITABU***

# Yaliyomo

TAMKO LA IDARA .......... 3
UTANGULIZI .......... 5
KITABU KILICHOPO MIKONONI MWETU .......... 9

**MLANGO WA KWANZA**
**HAKIKA YA DINI**
**KWA ALLAH NI UISLAMU**

KWANZA: UISLAMU NI DINI YA MAUMBILE .......... 15
PILI: UISLAMU NI NINI? .......... 17
TATU: UISLAMU NI DINI YA MITUME WOTE.......... 18
NNE: NGUZO ZA UISLAMU .......... 21
NGUZO YA KWANZA.......... 21
NGUZO YA PILI: Kusimamisha sala .......... 23
NGUZO YA TATU: Kutoa Zaka .......... 24
NGUZO YA NNE: Kufunga Ramadhani .......... 25
NGUZO YA TANO: Kuhiji nyumba takatifu ya Allah .......... 26
TANO: UHUSIANO BAINA YA UISLAMU NA DINI NYINGINE ZA MBINGUNI ZILIZOTANGULIA .......... 27

**MLANGO WA PILI**
**ITIKADI YA MUISLAMU**

KUZIFUNGAMANISHA NYOYO KWA ALLAH .......... 33
KWANZA: MOYO WA MUISLAMU BAINA YA HOFU, MATARAJIO NA KUPENDA .......... 33
PILI: MOYO WA MUISLAMU NA HISIA ZA UTUKUFU WA ALLAH (S.W.) .......... 35
**TAWHID NA AINA ZAKE** .......... 53
KWANZA: ALLAH NI NANI? .......... 53
PILI: MAANA YA TAWHID .......... 54
TATU: AINA ZA TAWHID .......... 54
NNE: FADHILA ZA TAWHID .......... 58
TANO: MAANA YA TAMKO LA TAWHID .......... 59
SITA: MASHARTI YA TAMKO LA TAWHID .......... 60
SABA: MAMBO YANAYOTENGUA TAWHID .......... 62
NANE: AINA ZA SHIRKI .......... 63
- AINA YA KWANZA: SHIRKI KUBWA .......... 63
- AINA YA PILI: SHIRKI NDOGO .......... 64

TISA: UTAMBULISHO WA DHAMBI KUBWA NA TOFAUTI BAINA YAKE NA BAINA YA DHAMBI NDOGO .......... 65
KUMI: HUKUMU YA MWENYE KUFANYA DHAMBI KUBWA .......... 66
**NGUZO YA PILI: KUAMINI MALAIKA** .......... 67
KWANZA: UTAMBULISHO WA MALAIKA .......... 67
PILI: WAJIBU WA KUAMINI MALAIKA .......... 67
TATU: SIFA ZA MALAIKA .......... 69
NNE: IDADI YA MALAIKA .......... 74
TANO: MAJINA YA MALAIKA .......... 74
SITA: KAZI ZA MALAIKA .......... 76
SABA: UHUSIANO YA MWANADAMU NA MALAIKA .......... 79
NANE: MATUNDA NA FAIDA ZA KUAMINI MALAIKA .......... 82
NGUZO YA TATU: KUAMINI MITUME, (Allah awafikishie Amani) .......... 83
KWANZA: MAANA YA KUAMINI MITUME .......... 84
PILI: HUKUMU YA KUAMINI MITUME .......... 84
TATU: IDADI YA MITUME NA MANABII .......... 85
NNE: MANABII NA MITUME WA ALLAH NI BINADAMU ..........86
TANO: KUZIDIANA DARAJA BAINA YA MITUME .......... 88
SITA: DINI YA MITUME NI MOJA NA SHERIA ZAO NI TOFAUTI .......... 89
SABA: KAZI NA MAJUKUMU YA MITUME .......... 90
NANE: SIFA ZA MITUME .......... 95
TISA: MIUJIZA YA MITUME .......... 98
KUMI: WAHYI .......... 100
KUMI NA MOJA: WAJIBU WETU KWA MITUME .......... 100
**MUHAMMAD BIN ABDALLAH** (Allah ampe rehema na Amani) **NABII WA MWISHO** ..........105
BAADHI YA TABIA ZA MTUME (s.a.w.) .......... 108
BISHARA ZA MANABII WALIOPITA KUMBASHIRI MTUME .......... 110
MIUJIZA YA MTUME .......... 125
SIFA MAHUSUSI ZA MTUME .......... 127
HAKI ZAKE KWA UMMA WAKE .......... 130
**NGUZO YA NNE: KUAMINI VITABU** .......... 135
KWANZA: MAANA YA VITABU .......... 135
PILI: HUKUMU YA KUAMINI VITABU .......... 138
TATU: NAMNA YA KUAMINI VITABU .......... 138
NNE: WATU WA KITABU NA UPOTOSHAJI WA MANENO YA ALLAH .......... 140
TANO: SIFA MAHUSUSI ZA KUIAMINI QUR'ANI.......... 141
**NGUZO YA TANO: KUAMINI SIKU YA MWISHO** .......... 145

KWANZA: MAANA YA SIKU YA MWISHO ..................................................... 146
PILI: MAJINA YA SIKU YA MWISHO ............................................................ 146
TATU: WAJIBU WA KUAMINI SIKU YA MWISHO ......................................... 147
NNE: ALAMA ZA KIYAMA ......................................................................... 147
TANO: MTIHANI WA KABURINI ................................................................ 148
SITA: ADHABU ZA KABURINI NA NEEMA ZAKE ......................................... 149
SABA: KUPULIZWA KWA PARAPANDA ....................................................... 150
NANE: KUFUFULIWA NA KUKUSANYWA ..................................................... 151
TISA: MATUKIO YA KUTISHA YA SIKU YA KIYAMA .................................. 152
KUMI: HESABU NA MALIPO ...................................................................... 154
KUMI NA MOJA: MIZANI ......................................................................... 156
KUMI NA MBILI: HODHI ......................................................................... 157
KUMI NA TATU: SIRATI .......................................................................... 157
KUMI NA NNE: DARAJA ........................................................................... 158
KUMI NA TANO: PEPO NA WASIFU WAKE ................................................. 159
KUMI NA SITA: MOTO NA WASIFU WAKE ................................................... 160
KUMI NA SABA: FAIDA ZA KUAMINI SIKU YA MWISHO ............................... 161
**NGUZO YA SITA: KUAMINI QADARI** ......................................................... 163
**DHAMBI ZILIZOHADHARISHWA NA UISLAMU** ........................................ 167
YA KWANZA: UCHAWI ........................................................................... 167
1) Maana ya uchawi ................................................................................. 167
2) Aina za uchawi .................................................................................... 167
3) Hukumu ya uchawi na kujifunza uchawi ............................................... 167
4) Hukumu ya kwenda kwa wachawi .......................................................... 169
PILI: UTABIRI, RAMLI NA UNAJIMU .......................................................... 170
1) Utambulisho wake ................................................................................ 170
2) Hukumu ya Utbiri, Ramli na Unajimu ...................................................... 171
3) Vitendo ambavyo vinaingia katika Utabiri, Unajimu na Ramli .................. 171
HIRIZI NA AZIMA ................................................................................... 173
1) Maana ya hirizi .................................................................................... 173
2) Hukumu ya kuvaa hirizi ........................................................................ 173
3) Baadhi ya aina za hirizi ........................................................................ 174
NNE: KUAMINI NUKSI NA UCHURO ............................................................ 175
1) Maana ya Nuksi ................................................................................... 175
2) Aina za kuamini Nuksi .......................................................................... 175
3) Hukumu ya kuamini Nuksi .................................................................... 175
4) Tiba ya tatizo la kuamini mikosi ............................................................ 176
**TANO: KUMUOMBA MWENGINE BADALA YA ALLAH** ............................. 177

SITA: KUTAFUTA BARAKA KWENYE MAKUMBUSHO ............................ 180
1) Maana ya kutafuta Baraka .................................................................... 180
2) Aina za kutafuta Baraka ........................................................................ 180
3) Hukumu ya kutafuta baraka kuliko katazwa ........................................ 181
SABA: KUHAMA KWA ROHO ................................................................ 183
1) Maana ya kuhama kwa roho ................................................................ 183
2) Hukumu ya kuamini kuhama kwa roho ............................................... 183
NANE: KUOGOPA MAJINI NA MASHETANI ........................................ 184
TISA: KUSHEREHEKEA NA KUSHIRIKI SIKUKUU ZISIZOKUWA ZA WAISLAMU ........................................................................................ 188

## MLANGO WA TATU
## IBADA ZA MUISLAMU

SHERIA ZA TOHARA .............................................................................. 193
KWANZA: MAANA YA TOHARA ........................................................... 193
PILI: VIGAWANYO VYA MAJI ............................................................... 194
TATU: SHERIA ZA VYOMBO ................................................................. 195
NNE: TARATIBU ZA KWENDA CHOONI NA KUJISAFISHA ........................... 197
TANO: SHERIA ZA UDHU ...................................................................... 199
1) Maana ya Udhu ..................................................................................... 199
2) Hukumu ya kutawadha .......................................................................... 199
3) Fadhila za Udhu ..................................................................................... 200
4) Faradhi za Udhu .................................................................................... 200
5) Suna za Udhu ......................................................................................... 201
6) Namna ya kutawadha ............................................................................ 201
7) Mambo yanayotengua Udhu ................................................................. 203
SITA: SHERIA ZA KUPAKA MAJI KHOFU (VIATU) NA MFANO WAKE ................ 203
1) Maana ya kupaka maji viatu wakati wa kutia Udhu ............................ 203
2) Hukumu ya kupaka maji khofu ............................................................. 203
3) Muda wa kupaka maji khofu ................................................................ 203
4) Masharti ya kupaka maji khofu ............................................................ 204
5) Namna ya kupaka maji khofu ............................................................... 204
6) Yanayobatilisha kupaka maji Khofu ..................................................... 204
7) Kupaka maji kichacha ........................................................................... 205
SABA: SHERIA ZA KUOGA .................................................................... 205
1) Maana ya kuoga ..................................................................................... 205
2) Hukumu ya kuoga .................................................................................. 205
3) Mambo yanayowajibisha kuoga ........................................................... 206

4) Majosho ya Suna ........................................................................................ 206
5) Faradhi za kukoga ........................................................................................ 207
6) Suna za kuoga ........................................................................................ 207
7) Namna ya kuoga ........................................................................................ 208
8) Mambo yaliyo haramu kwa mwenye Hadathi Kubwa ........................................ 209
NANE: SHERIA ZA KUTAYAMAMU ........................................................................ 209
1) Maana ya Kutayamamu ........................................................................................ 209
2) Hukumu ya kutayamamu ........................................................................................ 209
3) Ni nani aliyewekewa sheria ya kutayamamu? ........................................................ 210
4) Faradhi za kutayamamu ........................................................................................ 210
5) Suna za kutayamamu ........................................................................................ 211
6) Namna ya kutayamamu ........................................................................................ 211
7) Mambo yanayobatilisha kutayamamu ........................................................................ 211
8) Hukumu ya aliyekosa vitoharisho vya maji na mchanga ........................................ 212
SHERIA ZA SALA ........................................................................................ 213
KWANZA: Maana ya Sala ........................................................................................ 213
PILI: Hukumu ya sala ........................................................................................ 213
TATU: Faida za sala ........................................................................................ 213
NNE: Idadi ya sala za faradhi na nyakati zake ........................................................ 214
TANO: Je, ni watu gani walio na wajibu wa kusali? ................................................ 215
SITA: Masharti ya kusihi kwa sala ........................................................................ 216
SABA: Nguzo za sala ........................................................................................ 218
NANE: Suna za sala ........................................................................................ 220
TISA: Namna Ya kusali ........................................................................................ 223
KUMI: Mambo yanayobatilisha sala ........................................................................ 226
KUMI NA MOJA: Sijida ya Kusahau ........................................................................ 227
SHERIA ZA MAZISHI ........................................................................................ 231
KWANZA: Hali ya Muislamu wakati wa kuugua na wakati wa kifo ...................... 232
PILI: Kuosha maiti ........................................................................................ 234
TATU: Kumvisha sanda maiti ........................................................................................ 237
NNE: Kumsalia maiti ........................................................................................ 238
TANO: Ubebaji wa Jeneza na uzikaji wa maiti ........................................................ 240
SITA: Rambirambi (mkono wa pole) ........................................................................ 243
SHERIA ZA ZAKA ........................................................................................ 245
KWANZA: Maana ya Zaka ........................................................................................ 245
PILI: Hukumu ya Zaka ........................................................................................ 245
TATU: Hekima ya kuwekwa kwa Zaka katika sharia ................................................ 246
NNE: Masharti ya kuwajibika kwa zaka ........................................................................ 246

TANO: Mali ambazo ni wajibu kutolewa zaka na viwango vyake ……………….. 247
SITA: Utoaji wa Zaka ........................................................................................ 253
SABA: Zaka ya Deni ........................................................................................ 256
SHERIA ZA SAUMU ........................................................................................ 257
KWANZA : Maana ya saumu ........................................................................... 257
PILI: Uzuri wa Saumu ........................................................................................ 257
TATU: Hukumu ya kufunga mwezi wa Ramadhani ............................................ 259
NNE: Kuingia kwa mwezi wa Ramadhani .......................................................... 259
TANO: Nani ana wajibu wa kufunga saumu ya Ramadhani? …………………… 260
SITA: Nguzo za saumu ...................................................................................... 260
SABA: Nyudhuru zinazoruhusu kutofunga katika Ramadhani ................................... 261
NANE: Suna za funga na maadili yake ............................................................... 264
TISA: Mambo yanayoruhusiwa katika saumu ...................................................... 266
KUMI: Mambo yanayobatilisha saumu ............................................................... 267
KUMI NA MOJA: Mambo yaliyo makuruhu katika saumu .................................. 269
KUMI NA MBILI: Zakatulfitri ............................................................................. 270
KUMI NA TATU: Funga za hiari ........................................................................ 272
KUMI NA NNE: Siku ambazo ni makuruhu kufunga ......................................... 274
KUMI NA TANO: Siku ambazo ni haramu kufungwa ......................................... 275
SHERIA ZA HIJA NA UMRA............................................................................. 277
KWANZA: Maana ya Hija na Umra ................................................................... 277
PILI: Masharti ya kuwajibika kwa Hija na Umra ................................................. 278
NAMNA YA KUTEKELEZA UMRA ................................................................. 281
NAMNA YA KUHIJI ........................................................................................ 289
KWANZA: Aina za Hija .................................................................................... 289
PILI: Matendo ya Hija katika siku ya mwezi nane ya Dhulhija (Siku ya Tarwiya).. 290
TATU: Matendo ya Hija katika siku ya tisa ya Dhulhija (Siku ya Arafa) .............. 290
NNE: Matendo ya Hija katika siku ya kumi (Siku ya Kuchinja) ........................................ 292
TANO: Matendo ya Hija katika siku za Tashriki .................................................. 293
SITA: Mambo yaliyokatazwa kwa kuhirimia ....................................................... 295

**SHERIA MAALUMU KWA MWANAMKE WA KIISLAMU** ........................ 299
KWANZA: Sheria za Hedhi, Nifasi na Istihadha .................................................. 299
PILI: Hijabu ya mwanamke na mavazi yake ......................................................... 304
TATU : Vazi la mwanamke katika sala ................................................................ 309
NNE : Sheria za urembo wa mwanamke .............................................................. 309
TANO: Sheria za mwanamke kutoka nyumbani mwake na mahusiano yake
na watu kando .................................................................................................... 312

**VYAKULA NA VINYWAJI VILIYVO HARAMISHWA** ............................ 315
1) Nyamafu /Mzoga ............................ 316
2) Damu inayomwagika ............................ 317
3) Nguruwe ............................ 317
4) Kila mnyama mwitu mwenye meno ya kushambulia ............................ 317
5) Kila ndege mwenye kutumia makucha ............................ 317
6) Punda wa mjini (punda wa kufugwa) ............................ 317
7) Wadudu, Nyoka, Nge, Panya, na Mende ............................ 318
8) Kila kilichohukumiwa na sharia kuwa ni najisi (uchafu) ............................ 318
9) Pombe na madawa ya kulevya ............................ 318
10) Vinaruhusiwa kutumiwa katika vile vilivyo tajwa uharamu wake …….…….. 319
11) Sumu za aina yoyote ............................ 319

## MLANGO WA NNE
## UHUSIANO WA MUISLAMU MPYA
## NA JAMII

Utangulizi ............................ 323
**UHUSIANO WA WANANDOA BAADA YA WOTE WAWILI KUWA WAISLAMU AU MMOJA WAO** ............................ 325
KWANZA: Kusilimu kwa wanandoa kwa pamoja ............................ 325
PILI: Kusilimu kwa mmoja kati ya wanandoa ............................ 326
MAHUSIANO YA MUISLAM MPYA NA WATOTO WAKE ............................ 331
KWANZA: Ufuasi wa dini wa watoto baada ya wazazi kusilimu ............................ 331
PILI: Ulezi wa watoto baada ya kusilimu ............................ 331
TATU: Uwalii (usimamizi) katika ndoa ............................ 333
NNE: Usimamizi na usia kwa watoto ............................ 334
**UHUSIANO WA MUISLAM MPYA NA WAZAZI WAKE, NDUGU NA MAHARIMU ZAKE WENGINE** ............................ 335
KWANZA: Kuwafanyia wema na hisani wazazi ambao sio Waislamu ............................ 335
PILI: Kuwafanyia wema na hisani ndugu ambao sio Waislamu ............................ 337
**MAHUSIANO YA KIFEDHA KWA MUISLAMU** ............................ 341
KWANZA: Huduma ............................ 341
PILI: Mahari ............................ 342
TATU: Mirathi ............................ 343
NNE: Mali iliyochumwa kabla ya Uislamu ............................ 343
**MAHUSIANO YA KIJAMII NA KIBINADAMU** ............................ 347
KWANZA: Kupenda na kunusuru (kutetea) ............................ 347
PILI: Uadilifu na utendaji haki ............................ 350

TATU: Kuheshimu mikataba na makubaliano ........................................................ 351
NNE: Kutembeleana na kupeana zawadi ................................................................ 353
TANO: Kula na kunywa ........................................................................................ 355
SITA: Kusalimiana ................................................................................................ 356
**WAJIBU NA MAJUKUMU YA KIDINI** ............................................................. 359
KWANZA: Msamaha wa majukumu ya Kiislamu yaliyothibiti kabla ya mtu kuingia katika Uislamu ......................................................................................... 359
PILI: Wajibu wa kufuata sheria za Kiislamu na mafundisho yake .......................... 360

إدارة الإفتاء

وزارة الأوقاف والشئون الإسلامية

دولة الكويت

# الملخص المفيد في أحكام المسلم الجديد

النسخة السواحلية

تأليف

وحدة البحث العلمي

بإدارة الإفتاء